

**TATHMINI YA USIMILISHO WA RIWAYA NA HADITHI FUPI KWA
WANAFUNZI WA SEKONDARI NCHINI KENYA**

TASNIFU YA UZAMIFU

CHUO KIKUU CHA KENYATTA

IDARA YA KISWAHILI

TITUS M. KAUI

C82/21411/2011

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KATIKA IDARA YA KISWAHILI ILI
KUTOSHELEZA MAHITAJI KATIKA SHAHADA YA UZAMIFU YA CHUO
KIKUU CHA KENYATTA**

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa na yeyote katika

Chuo Kikuu chochote kwa madhumuni ya kutuzwa shahada yoyote.

TITUS MUSYOKA KAUI

C82/21411/2011

Tasnifu hii imetolewa kwa Chuo Kikuu kwa idhini yetu kama wasimamizi.

PROF. GEOFFREY KITULA KING'EI

IDARA YA KISWAHILI

CHUO KIKUU CHA KENYATTA

DKT. RICHARD MAKHANU WAFULA

IDARA YA KISWAHILI

CHUO KIKUU CHA KENYATTA

TABARUKU

Kwa wapenzi wote wa fasihi na lugha ya Kiswahili.

Shukrani

Nawamimonia shukrani sufufu wasimamizi wangu, Prof. G.K. King'ei na Dkt. R.M. Wafula, kwa jitihada walizofanya kuisahihisha tasnifu hii hadi ikafikia kiwango hiki cha ufanisi. Shukrani nyingine ni kwa mke wangu mpendwa, Hellen, na wanangu, Evan na Jayden, kwa uvumilivu waliodhihirisha na hata kunitia moyo hali ilipokuwa ngumu. Sitasahau kuwashukuru marafiki, wasomi, wasimilishaji, waelekezi, waigizaji, walimu, na wanafunzi walionifaa nyanjani na kwingineko nilipokuwa nikiufanya utafiti huu. Na kwa taadhima na unyenyekevu, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema zake katika kila hatua niliyopiga kuiandika tasnifu hii.

Vifupisho

BBC:	British Broadcasting Corporation
CHAKINA:	Chama cha Kiswahili cha Chuo Kikuu cha Nairobi
K.C.S.E:	Kenya Certificate for Secondary Education
K.I.C.D:	Kenya Institute of Curriculum Development
K. Y. K:	Kabla ya Yesu Kristo
Mhr:	Mhariri
SCAFM:	School of Creative Arts Films and Media
SPSS:	Statistical Package for Social Sciences
T.Y:	Tafsiri yangu
Taz:	Tazama
U.k:	Ukurasa
Whr:	Wahariri

Orodha ya Majedwali

Jedwali 5.1: Kutathmini Usahihi wa Maigizo	134
Jedwali 5.2: Matatizo ya Usimilisho wa Riwaya	135
Jedwali 6.1: Idadi ya Maonyesho katika Hadithi Fupi Teule	171
Jedwali 6.2: Lafudhi Zilizotumika katika Maigizo ya Hadithi Fupi	177
Jedwali 6.3: Lafudhi ya Kiluhya	178
Jedwali 6.4: Lafudhi ya Kikamba	179
Jedwali 6.5: Kutathmini Usahihi wa Maigizo	197
Jedwali 6.6: Matatizo ya Usimilisho wa Hadithi Fupi	198

Maelezo ya Istilahi

Akala: Viatu vinavyotengenezwa kutokana na maganda ya magurudumu ya gari yaliyozeeka.

Analojia: Usimilisho unaokengeuka zaidi ukilinganishwa na matini chasili kiasi cha kuonekana kama kazi nyingine tofauti ya kisanaa. Hata hivyo, msimilishaji huisimilisha kazi yake hivyo kimakusudi.

Fasiri mpya: Usimilisho unaofuata muundo wa matini chasili lakini ukisheheni mabadiliko ya kimakusudi kutegemea ubunifu wa msimilishaji.

Similisho: Matini inayoandaliwa kutokana na ugeuzaji wa matini chasili. Pia, matini lengwa.

Tafsiri sisisi: Usimilisho unaohifadhi sifa za matini chasili na kuziwasilisha kiuaminifu katika similisho.

Usimilisho: Hali ya kuipa matini, inayopatikana katika utanzu fulani wa fasihi, sifa za matini nyingine katika utanzu tofauti wa fasihi.

Yaliyomo

Ungamo.....	ii
Tabaruku.....	iii
Shukrani	iv
Vifupisho.....	v
Orodha ya Majedwali.....	vi
Maelezo ya Istilahi Muhimu.....	vii
Yaliyomo.....	viii
Ikisiri	xviii
Abstract	xix

SURA YA KWANZA

MSINGI WA UTAFITI

1.0 Utangulizi	1
1.1 Usuli wa Utafiti	1
1.2 Suala la Utafiti	4
1.3 Maswali ya Utafiti	6
1.4 Malengo ya Utafiti.....	6
1.5 Sababu za Kuchagua Mada.....	7
1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti.....	8

1.7 Kiishilio	10
---------------------	----

SURA YA PILI

YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA NA MISINGI YA NADHARIA

2.0 Utangulizi	11
2.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada.....	11
2.2 Misingi ya Nadharia.....	18
2.2.1 Nadharia ya Usimilisho.....	18
2.2.2 Nadharia ya Ugizaji	22
2.3 Kiishilio.....	25

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.0 Utangulizi.....	26
3.1 Mbinu Changamano za Utafiti.....	26
3.2 Mahali pa Utafiti.....	27
3.3 Uteuzi wa Sampuli.....	28
3.4 Ukusanyaji wa Data.....	31
3.4.1 Maktabani.....	31
3.4.2 Nyanjani.....	31
3.4.3 Vifaa na Mbinu za Utafiti.....	31

3.4.3.1 Matumizi ya Kamera.....	32
3.4.3.2 Matumizi ya Daftari na Kalamu.....	32
3.4.3.3 Matumizi ya Hojaji.....	32
3.4.3.4 Matumizi ya Mahojiano.....	33
3.4.3.5 Matini za Masimilisho.....	33
3.4.3.6 Uchunzaji na Utazamaji.....	34
3.5 Uchanganuzi wa Data	34
3.6 Uwasilishaji wa Data.....	35
3.7 Kiishilio.....	36

SURA YA NNE

DHANA, SABABU ZA KUSIMILISHA NA HISTORIA YA USIMILISHO

4.0 Utangulizi.....	37
4.1 Dhana ya Usimilisho	37
4.1.1 Usimilisho kama Tafsiri	38
4.1.2 Usimilisho kama Mwingiliano wa Matini	40
4.1.3 Usimilisho kama Mwingiliano wa Njia za Mawasiliano.....	43
4.1.4 Usimilisho Halisi	45
4.2 Sababu za Kusimilisha Matini za Fasihi	42
4.3 Historia ya Usimilisho	56

4.3.1 Usimilisho katika Fasihi ya Kimagharibi	58
4.3.2 Usimilisho katika Fasihi ya Kiswahili	68
4.4 Kiishilio	60

SURA YA TANO

MBINU NA MATATIZO YA USIMILISHO WA RIWAYA

5.0 Utangulizi	81
5.1 Mbinu za Usimilisho katika Matini	82
5.1.1 Usimulizi	84
5.1.1.1 Uziada	85
5.1.1.2 Udondoshaji	86
5.1.1.3 Maelezo na Ubunifu katika Usimulizi	87
5.1.1.4 Dhima ya Usimulizi katika Usimilisho wa Riwaya	88
5.1.2 Mazungumzo	93
5.1.3 Udondoshaji	97
5.1.4 Mshindilio	100
5.1.5 Ubunaji wa Maelezo ya Jukwaani	101
5.1.6 Ufaraguzi wa Msuko	105
5.2 Mbinu za Usimilisho Jukwaani	107
5.2.1 Matumizi ya Msimulizi	108

5.2.2 Utendaji	112
5.2.3 Mazungumzo	113
5.2.4 Matumizi ya Jukwaa	119
5.2.4.1 Matumizi ya Pazia	119
5.2.4.2 Matumizi ya Sauti	120
5.2.4.3 Matumizi ya Muziki	121
5.2.4.4. Mandhari	123
5.2.4.5 Uangazaji	124
5.2.5 Uteuzi wa Wahusika	126
5.2.5.1 Maleba	126
5.2.5.2 Lugha	129
5.2.5.3 Maumbile	130
5.2.6 Uigizaji wa Mbinu za Utunzi	131
5.3 Matatizo ya Usimilisho wa Riwaya	132
5.3.0 Uwasilishaji wa Data Kuhusu Matatizo ya Usimilisho wa Riwaya	133
5.3.1 Data Kutokana na Hojaji za Walimu	133
5.3.1.1 Tathmini ya Usomaji wa Riwaya	133
5.3.1.2 Kutathmini Kiwango cha Usahihi wa Similisho	133
5.3.1.3 Kutathmini Umuhimu wa Usimilisho wa Riwaya	

kwa Wanafunzi.....	134
5.3.1.4 Kutambua Matatizo ya Usimilisho wa Riwaya	135
5.3.1.5 Njia za Kuboresha Usimilisho wa Riwaya	135
5.3.2 Data Kutokana na Hojaji na Mahojiano na Wasimilishaji	136
5.3.2.1 Mwaka wa Kuanza Kusimilisha	136
5.3.2.2 Kiwango cha Elimu	137
5.3.2.3 Ujuzi wa Kusimilisha	137
5.3.2.4 Malalamishi ya Hadhira	138
5.3.2.5 Matatizo ya Usimilisho	138
5.3.2.6 Utatuzi wa Matatizo ya Usimilisho	139
5.3.3 Matatizo Yaliyotokana na Mbinu za Usimilisho	140
5.3.3.1 Udondoshaji wa Maudhui Muhimu	140
5.3.3.2 Usawiri wa Wahusika	142
5.3.3.3 Ubunaji wa Muundo wa Tamthilia	142
5.3.3.4 Usawiri wa Mandhari	148
5.3.3.5 Uigizaji wa Mbinu	150
5.3.4 Matatizo Yaliyotokana na Wasimilishaji	152
5.3.4.1 Matini Zilizotumia Lugha Ngumu na Tata	153
5.3.4.2 Utegemezi Uliokithiri wa Mazungumzo	153

5.3.4.3 Kutia Chumvi katika Matukio ya Riwaya	154
5.3.4.4 Tatizo la Fedha	155
5.4 Kiishilio	157

SURA YA SITA

MBINU NA MATATIZO YA USIMILISHO WA HADITHI FUPI

6.0 Utangulizi	158
6.1 Mbinu za Usimilisho wa Matini za Hadithi Fupi.....	158
6.1.1 Mazungumzo	159
6.1.2 Usimulizi	164
6.1.3 Matumizi ya Muundo wa Kitamthilia	168
6.1.3.1 Muundo wa Mazungumzo	169
6.1.3.2 Muundo wa Sehemu	170
6.2 Mbinu za Usimilisho wa Hadithi Fupi Jukwaani	173
6.2.1 Matumizi ya Mtambaji	174
6.2.2 Mazungumzo	177
6.2.3 Uteuzi wa Waigizaji	180
6.2.3.1 Mavazi	182
6.2.3.2 Umbo	184
6.2.3.3 Lugha	185

6.2.4 Matumizi ya Jukwaa	185
6.2.4.1 Matumizi ya Sauti	185
6.2.4.2 Matumizi ya Muziki	187
6.2.4.3 Usawiri wa Mandhari	188
6.2.4.4 Matumizi ya Pazia	189
6.2.4.5 Uangazaji.....	190
6.2.5 Utendaji	192
6.2.6 Ugizaji wa Mbinu	194
6.3 Matatizo katika Usimilisho wa Hadithi Fupi	196
6.3.0 Uwasilishaji wa Data Kuhusu Usimilisho wa Hadithi Fupi	196
6.3.1 Data Kutokana na Hojaji za Walimu	196
6.3.1.1 Kutathmini Usomaji wa Hadithi Fupi.....	197
6.3.1.2 Kutathmini Usahihi wa Maigizo	197
6.3.1.3 Umuhimu wa Usimilisho wa Hadithi Fupi kwa Maandalizi ya KCSE.....	198
6.3.1.4 Utambuzi wa Matatizo ya Usimilisho wa Hadithi Fupi	198
6.3.1.5 Utatuzi wa Matatizo ya Usimilisho wa Hadithi Fupi	199
6.3.2 Matatizo Yaliyotokana na Mbinu za Usimilisho	201
6.3.2.1 Udondoshaji	201

6.3.2.2 Miundo Potovu ya Kitamthilia	202
6.3.3 Tatizo Lililotokana na Wasimilishaji	205
6.3.3.1 Matini Ngumu Kusimilika	205
6.4 Kiishilio	208

SURA YA SABA

HITIMISHO

7.0 Utangulizi	209
7.1 Muhtasari	209
7.2 Matokeo na Mchango wa Utafiti	211
7.3 Matatizo ya Utafiti	215
7.4 Mapendekezo	216
Marejeleo	218
Kiambatisho 1.....	231
Hojaji ya Walimu Kuhusu Riwaya	231
Kiambatisho 2.....	232
Hojaji ya Walimu Kuhusu Hadithi Fupi.....	232
Kiambatisho 3.....	233
Hojaji ya Wasimilishaji	233
Kiambatisho 4.....	236

Mwongozo wa Mahojiano na Wasimilishaji	236
Kiambatisho 5.....	237
Picha Kuonyesha Utendaji, Usawiri wa Wahusika, na Mandhari (<i>Siku Njema</i>)	237
Kiambatisho 6	238
Picha Kuonyesha Usawiri wa Mandhari na Wahusika (<i>Siku Njema</i>)	238
Kiambatisho 7	239
Picha Kuonyesha Usawiri wa Mandhari, Wahusika, na Utendaji (<i>Utengano</i>).....	239
Kiambatisho 8	240
Picha Kuonyesha Usawiri wa Wahusika, Mandhari, na Utendaji (<i>Utengano</i>)	240
Kiambatisho 9	241
Kibali cha Kufanya Utafiti	241

Ikisiri

Tanzu za riwaya na hadithi fupi kimsingi huandikwa ili kusomwa, bali siyo kuigizwa. Kwa muda wa miaka kumi na mitano hivi wasimilishaji wamefanya juhudi kuigiza tungo za kinathari za fasihi ya Kiswahili. Hali ya kuziigiza tungo za kinathari hutokana na ugeuzaji wa vipengele fulani vya kinathari ili vichukue umbo la kitamthilia. Lengo la uchunguzi huu lilikuwa kutathmini usimilisho wa riwaya na hadithi fupi kwa wanafunzi wa sekondari nchini Kenya. Uchunguzi ulidhamiria kubainisha dhana, historia, mbinu na matatizo ya usimilisho, na kupendekeza njia za kuyatatua matatizo hayo. Uchanganuzi umebainisha kwamba riwaya na hadithi fupi husheheni sifa za kitamthilia ambazo huwa msingi wa usimilisho. Aidha, imebainika kwamba mchakato wa kuubadilisha muundo wa kinathari na kuufanya wa kitamthilia huandamana na changamoto ambazo kama hazishughulikiwi ipasavyo zinaweza kuzalisha matatizo ya usimilisho. Uchanganuzi wa data uliongozwa na nadharia changamano iliyohulutisha misingi ya nadharia ya usimilisho na ya uigizaji. Mkabala wa nadharia ya usimilisho ulioongoza uchunguzi huu huhimiza usimilisho ufanywe kama tafsiri, pale maana ya matini chasili huhamishwa kwa usahihi iwezekanavyo. Hii ni kwa sababu usimilisho wa tungo zinazotahiniwa katika mtihani wa KCSE hutarajiwa kuwa na usahihi wa matini chasili. Misingi ya nadharia ya uigizaji ilitumika kutathmini ufaafu wa mbinu zilizotumika kusimilisha matini ya riwaya na hadithi fupi kwa muundo wa kitamthilia. Tasnifu hii imetumia mbinu changamano za utafiti ambapo mikakati ya kijarabati na kimaelezo imetumika kukusanya, kuchanganua, na kuwasilisha data. Utafiti ulifanywa katika magatuzi ya Nairobi na Kitui ukihusisha vikundi vinne vya uigizaji. Vikundi hivyo vilisimilisha riwaya za *Utengano* na *Siku Njema*, na diwani za hadithi fupi za *Mayai Waziri wa Maradhi* na *Hadithi Nyingine* na *Damu Nyeusi* na *Hadithi Nyingine*. Uchunguzi umebaini kwamba mbinu zilizotumika kusimilisha riwaya na hadithi fupi kuwa matini za kitamthilia zilikuwa za kimwingiliano matini. Kutegemea stadi za wasimilishaji katika matumizi ya mwingiliano matini, usimilisho ulijitokeza kama aminifu ama uliokengeuka kwa matini chasili. Riwaya na hadithi fupi zilizohakikiwa masimilisho yake zilidhihirisha uwepo wa sifa za kitamthilia ambazo ndizo kiini cha ubunaji wa mbinu za usimilisho. Fauka ya haya, tungo za kidrama na kinathari hubuniwa kwa sifa fulani za kimfanano ambazo huifanya rahisi kwa msimilishaji kuigeza utanzu mmoja kuwa mwingine. Hizi ni sifa za mwingiliano matini. Katika mjadala wa mwingiliano matini, utafiti huu umebainisha kwamba, matini zinaweza kuingiliana na zikadumisha sifa zake asilia, kinyume na inavyodaiwa na wahakiki wa mwingiliano matini.

Abstract

Novel and short story genres of written literature are created to be read, but not to be dramatized as is the case with the play. For a period of about fifteen years adapters have made effort to dramatize swahili prose texts. The dramatization of prose texts is made possible through transforming features of prose into features of drama. The purpose of this study was to evaluate adaptation of novels and short stories for secondary school students in Kenya. The study objectives were to explain the concept of adaptation, discuss history, stylistic devices and problems in adaptation. Further, the study was aimed at identifying the problems associated with adaptation and recommending possible ways of facing those challenges. The study has found out that novels and short stories use some dramatic features which make it possible to adapt them. The process of transforming prose structure into play has many challenges, which if not addressed appropriately can result in foiled adaptations. This research was guided by an eclectic approach where by it combined aspects of adaptation theory and performance theory. The foundations of adaptation theory which guided this research emphasized on faithful adherence to the original texts. These foundations were appropriate in analyzing the selected texts which were examinable in KCSE. The product was expected to demonstrate faithfulness to the original text. The foundations of performance theory were used to evaluate the appropriateness of stylistic devices used in transforming prose into drama. The research adopts both qualitative and quantitative methods in collection, analysis, and presentation of data. The study was carried out in two counties namely, Nairobi and Kitui, and involved four theatre groups. The groups adapted *Utengano* and *Siku Njema* novels and two anthologies of short stories, *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* and *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*. The research revealed that the main devices of style which were used to adapt the novels and short stories into dramatic pieces were intertextual in nature. Depending on how the adapters were adept at applying intertextuality, they were less or more faithful to the original text. It further demonstrated that, novels and short stories possess features of drama contrary to views held by many scholars. That, contrary to adaptation critics' view that faithful adaptations are unattainable, the research has shown that faithful adaptations are indeed inevitable in some transformations. Through intertextuality the thesis found out that texts and genres can cross their borderlines and still retain their original features.

SURA YA KWANZA

MSINGI WA UTAFITI

1.0 Utangulizi

Sura ya kwanza inafafanua kwa kina usuli wa utafiti pamoja na kubainisha suala linalotafitiwa. Maswali na malengo yaliyouongoza utafiti yanabainishwa. Aidha, sura hii inazieleza sababu mbalimbali za kuchagua mada na upeo na mipaka ya utafiti.

1.1 Usuli wa Utafiti

Waasisi wa nadharia ya uhakiki mpya kama vile T. S. Eliot (1933), I. A. Richards (1929), John Crowe Ransom (1941) na William Empson (1930), wanadai kwamba tanzu za fasihi ni bainifu kimipaka na hujitegemea. Msingi mkuu katika maoni yao ni kuwa, uchunguzi wa kazi yoyote ya fasihi haufai kutoka nje ya mipaka yake iliyobainishwa. Historia ya fasihi kote ulimwenguni imebainisha kinyume cha mtazamo huo. Wachanganuzi kama vile Michel Foucault, Roland Barthes, Umberto Eco, Jacques Derrida na wengineo, wameeleza kwamba, haiwezekani kuipata kazi asilia ya fasihi kwa ambavyo uasilia ni dhana ya kinasibu ambayo ni ngumu kueleza maana yake. Kauli hii inashadidia ukweli kuwa tanzu za fasihi zina mipaka nyumbufu inayoweza kuvunjwa ama kusongezwa na kuruhusu mwingiliano wa tanzu. Huu ndio mtazamo unaoendelezwa na wananadharia wa usemezano na mwingiliano-matini kwamba, matini za fasihi huingiliana na kutegemeana.

Kwa muda, kumekuwepo na mbinu mbalimbali zinazotumika na waandishi ili kupata mahusiano baina ya tanzu za fasihi. Njia moja ambayo imeenziwa sana ni usimilisho. Hii ni hali ya kuipa matini, inayopatikana katika utanzu fulani wa fasihi, sifa za matini nyingine katika utanzu tofauti wa fasihi. Historia ya fasihi inaonyesha kuwa fani hiyo imekuwepo ulimwenguni tangu asili ya fasihi. Huko Ugiriki, waandishi maarufu wa tamthilia kama vile Sophocles na Euripides walijenga mawazo yao kutokana na visasili, ngano na tenzi za Kigiriki zilizokuwa zimezoeleka katika jamii.

Maendeleo ya usimilisho yameibua aina nyingine mpya ya fani hiyo inayovuka mipaka iliyozoeleka ya fasihi. Huu ni usimilisho unaohusisha tungo za fasihi kugeuzwa kuwa filamu. Usimilisho wa aina hii umekita mizizi yake katika mataifa yaliyostawi kiuchumi. Kazi za kirasimi zilizoenziwa na wengi kama za Shakespeare zimekuwa zikisimilishwa ili kutengeneza filamu za kutazamwa na hadhira pana. Hata hivyo, usimilisho wa aina hii hauonekani kufanyiwa kazi za kimasimulizi katika fasihi ya Kiswahili. Usimilisho ambao umeanza kushamiri katika fasihi ya Kiswahili ni ule unaohusisha uigizaji jukwaani wa kazi za kinathari. Aina hii ya usimilisho imejikita zaidi katika uigizaji wa riwaya na hadithi fupi zinazotahiniwa katika mtihani wa kitaifa wa kidato cha nne.

Ingawa kusimilisha tanzu za fasihi kulianza katika enzi ya Sophocles, usimilisho wa vitabu vya kutahiniwa shuleni hauna historia ndefu. Huu umechipuka na kukulia nchini Kenya kama njia moja ya kuwasaidia wanafunzi na walimu kuvifahamu vitabu hivyo vinavyotahiniwa katika mtihani wa KCSE. Katika usimilisho huu, vikundi mbalimbali hushiriki kuigiza riwaya na hadithi fupi, shuleni na kwenye kumbi za thieta. Kuanzia mwaka 2008 hadi 2013, riwaya ambayo imekuwa ikiigizwa ni *Utengano*, na diwani ya hadithi fupi ya *Mayai*

Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine imeigizwa kutoka mwaka wa 2005 hadi 2012. Riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* na diwani ya hadithi fupi *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, zimeteuliwa na taasisi ya K.I.C.D. kufundishwa na kutahiniwa, na usimilisho wake umejitokeza mwaka wa 2014 na 2013, kwa usajali huo.

Uigizaji wa vitabu vinavyotahiniwa hujumuisha pia tamthilia na kwa nadra sana ushairi. Baadhi ya vikundi vimeanza majaribio ya kuigiza tanzu za fasihi simulizi. Usimilisho wa kazi za kimasimulizi huashiria kuwepo na sifa fulani za kimaigizo katika tungo hizo. Sifa hizo za kimwingiliano tanzu ndizo hutumika katika ubunaji wa mbinu za kuzisimilisha riwaya na hadithi fupi.

Waandishi wa fasihi kama Msokile (1993) na Ntarangwi (2004) wamebainisha wazi kwamba, tungo za kinathari hazisheheni sifa za kiutendaji sawa na ilivyo katika utungo wa tamthilia. Usimilisho wa riwaya na hadithi fupi umethibitisha madai yao na kubainisha kuwa kuwepo kwa sifa kadha za kiutendaji kunaziwezesha tungo hizo kuigizwa. Fauka yake, kazi za kimaigizo zinaweza kuhadithiwa kama masimulizi. Historia ya fasihi ya Kiswahili imeonyesha kuwa tendi maarufu kama *Utendi wa Fumo Liyongo* zilisimilishwa kuwa masimulizi ya kuhadithiwa. Hata hivyo, imebainika wazi kuwa usimilisho wa tungo katika tanzu za fasihi ya Kiswahili ni wa upande mmoja tu. Kazi za kinathari, riwaya na hadithi fupi, zimekuwa zikisimilishwa kuwa drama ya kuigizwa jukwaani, lakini hamna ithibati ya kuonyesha tungo za kitamthilia zikigeuzwa kuwa tungo za kinathari. Aidha, historia ya ushairi wa Kiswahili haionyeshi tungo za kimasimulizi zikisimilishwa kuwa tendi. Hali ya kuendelea kwa usimilisho huu wenye upendeleo ni ithibati ya kudhihirisha kuwepo na njia za uwasilishaji wa tanzu za fasihi zenye umaarufu kuliko nyingine. Katika muktadha wa fasihi ya

Kiswahili, uigizaji na utambaji, ni njia za uwasilishaji wa tanzu za fasihi ambazo zimekuwa zikivutia hadhira kubwa. Kwa sababu hiyo, usimilisho umedhihirika kuegemezwa kwa njia hizo za uwasilishaji wa tanzu.

Utafiti huu ulichochea na mwingiliano huu wa tanzu za fasihi na ulidhamiria kuchunguza mbinu za usimilisho wa riwaya na hadithi fupi. Kwa kuwa usimilisho huo hudhamiria kuwasilisha yaliyomo kwenye vitabu hivyo kwa usahihi ili kutosheleza haja ya mtihani wa fasihi, utafiti huu ulilenga pia kutathimini ufaafu wa mbinu hizo. Matokeo ya utafiti huu yanaingiza mawazo ya kinadharia katika usimilisho wa tungo za kinathari kwa minajili ya mtihani wa KCSE ambayo yanaweza kuuboresha mchakato huo.

1.2 Suala la Utafiti

Tanzu za fasihi andishi zinazotahiniwa katika mtihani wa kidato cha nne hujumuisha ushairi, tamthilia, riwaya na hadithi fupi. Ili kuwasaidia wanafunzi kupata kiwango cha juu cha uelewa, katika miongo kadha vikundi vya uigizaji vimejitokeza kuigiza kazi ambazo hazikuandikwa kuigizwa. Riwaya ambazo zimeigizwa ni kama vile *Kiu, Walenisi, Siku Njema, Mwisho wa Kosa, Utengano* na *Kidagaa Kimemwozea* (kuanzia 2014). Kwa upande wa hadithi fupi kuna *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* pamoja na diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* ambayo ilituliwa mwaka wa 2012.

Hata hivyo, ingawa maigizo hayo hudhamiriwa kuinua viwango vya uelewa wa kazi hizo kwa wanafunzi na walimu, mchakato mzima wa usimilisho hukumbwa na matatizo mbalimbali. Taasisi ya Ukuzaji Mitaala ya Kenya (K.I.C.D.) katika ukaguzi wake wa kuteua kikundi bora wanachoweza kutumia kunasia maigizo ya tungo hizo ilibaini kuwa, baadhi ya maigizo ya vikundi hivyo hayatimizi ubora

unaotarajiwa. Ili kuufanya usimilisho wa kikundi kinachochaguliwa kukaribia kitabu kinachoigizwa, wasimilishaji wa K.I.C.D. hushirikiana na kikundi hicho kuiboresha matini ya similisho pamoja na uigizaji wake. Mwandishi Cahir (2006) anasema kuwa, mchakato wa usimilisho unaweza kukumbwa na matatizo kutegemea matini inayosimilishwa na mbinu zinazotumika kuisimilisha. Matatizo hayo yanayouzingira mchakato wa usimilisho huyafanya maigizo hayo kukosa kutimiza lengo lake na kutinga uwasilishaji wa ujumbe uliomo kwenye tungo za kinathari. Usimilisho wa vitabu vya kutahiniwa hutakiwa kufanywa kwa uaminifu kwa matini chasili ili kuwasaidia wanafunzi kujibu maswali ya mtihani wa fasihi.

Kuna haja ya kuuchanganua utaratibu mzima wa usimilisho wa matini za kinathari na maigizo yake ili kubainisha mbinu zinazotumiwa kuzisimilisha tungo hizo pamoja na matatizo yanayoandama uteuzi wa mbinu zenyewe. Katika usimilisho na uigizaji huo, kuna vipengele vya fani na maudhui vya matini chasili ambavyo huachwa na vingine huongezewa. Aidha, uchanganuzi huu ni muhimu kufanywa ili kudhihirisha kuwa tungo za kinathari husheheni sifa za kitamthilia ambazo huziruhusu kuigizika, kinyume na maoni ya wanafasihi wengi.

Utafiti huu ulihusu ubainishaji wa mbinu za usimilisho wa kazi za kinathari kuwa maigizo, utathmini wa mbinu hizo, na ufafanuzi wa matatizo yanayokumba utaratibu huu mzima. Katika kutekeleza azimio hili kuu, utafiti huu umeelekeza jinsi ya kuufanikisha usimilisho wa tungo za kinathari zinazotahiniwa. Kazi za kinathari zilizohakikiwa ni riwaya ya *Siku Njema* na *Utengano*, na hadithi fupi ni diwani ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* na *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*.

1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na malengo manne ya utafiti yafuatayo:

- I. Kueleza dhana ya usimilisho, historia ya usimilisho wa fasihi na sababu za kusimilisha.
- II. Kuainisha na kutathmini mbinu zinazotumika kuzisimilisha na kuziigiza riwaya na hadithi fupi.
- III. Kubainisha matatizo yanayokumba mchakato wa usimilisho wa riwaya na hadithi fupi.
- IV. Kuonyesha jinsi ya kuyatatua matatizo ya usimilisho wa riwaya na hadithi fupi.

1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu ulidhamiria kuchunguza na kujibu maswali yafuatayo:

- I. Kwa
nini usimilisho wa tungo za fasihi?
- II. Je,
ni ipi historia ya usimilisho wa kazi za fasihi ulimwenguni?
- III. Je,
ni mbinu zipi zinazotumiwa kuzisimilisha riwaya na hadithi fupi?
- IV. Kun
a matatizo yapi yanayokumba mchakato wa usimilisho wa riwaya na hadithi fupi?

V.

Je,

matatizo ya usimilisho wa riwaya na hadithi fupi yanaweza kutatuliwa vipi?

1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Usimilisho ni fani maarufu katika fasihi ya ulimwengu. Ukweli wa fasihi kuhusu fani hii unahitaji kutafitiwa katika upana wake. Mada kuhusu usimilisho wa riwaya na hadithi fupi ni muhimu katika usomi wa sasa. Wahakiki wa mwanzo katika fasihi kama vile Aristotle na wengine walivishughulikia vitanzu vya fasihi kama vilivyokuwa na mipaka bainifu isiyoweza kuvunjwa. Baada ya kuasisiwa kwa nadharia ya mwingiliano matini, usomi unaohusu jinsi tanzu za fasihi zinavyoingiliana umeongezeka na kupata umaarufu. Usomi kuhusu mwingiliano huo wa tanzu ni mjadala muhimu wa kiakademia usioweza kupuuzwa. Hii ni sababu kuu iliyoelekeza kuchaguliwa kwa mada ya usimilisho wa kazi za kinathari ili kuonyesha kuwapo kwa sifa za kimaigizo katika tungo hizo. Utafiti huu umebainisha mbinu za kimwingiliano matini zinazotumika kuugeza utungo wa kimasimulizi kuwa wa kidrama na matatizo yanayotokana na uteuzi wa mbinu hizo.

Riwaya na hadithi fupi teule zinazosimilishwa ni sehemu ya karatasi ya fasihi katika mtihani wa somo la Kiswahili (KCSE) inayochangia asilimia arobaini ya mtihani huo. Usimilisho na uigizaji wa vitabu umekuwa kama sehemu mojawapo ya usomaji wake mbali na kusaidia wanafunzi kuimarisha kumbukumbu zao

katika matukio na masuala katika vitabu hivyo. Uchaguzi kuhusu mada hii ulibainika kuwa muhimu kwani uchunguzi wake umeweza kuarifu zaidi kuhusu jinsi usimilisho huu hufanywa, matatizo yanayouathiri, na jinsi unavyoweza kuboreshwa.

Mada hii, aidha, ilichochea na uchipuzi wa vikundi mbalimbali katika kumbi za thieta na vingine ambavyo huzuru shule hadi shule vikiigiza vitabu hivyo. Vingi vyake huwa na idhini kutoka wizara ya elimu, kupitia maafisa wake wa kukadiria ubora. Kwa hivyo, ilikuwa muhimu kuchunguza ili kubaini iwapo usimilisho wa vikundi hivyo umeafiki viwango vinavyotarajiwa katika usimilisho wa vitabu teule vya mtihani wa KCSE. Utafiti kuhusu mada hii umebainisha kuwa, usimilisho dhaifu hudengua yale wanafunzi na walimu wamesoma kitabuni na kuathiri kwa njia hasi uelewa wa vitabu teule vya fasihi.

Khamis (2008:8) anaonyesha umuhimu wa nadharia katika uelezaji wa matatizo ya kitaaluma. Akimnukuu Masinjila (1992:2), anasema kuwa ni vigumu kupata muktadha usioelekezwa na nadharia. Hii ilituelekeza kufikiria kuwa, usimilisho na uigizaji wa riwaya na hadithi fupi unaongozwa na nadharia fulani. Mada hii, basi, ilikuwa muhimu kwa vile imeonyesha misingi ya kinadharia inayofuatwa katika uigizaji wa tungo za kimasimulizi. Pia, imedhihirisha upungufu wa nadharia changamano iliyotumika katika ufafanuzi wa vipengele mbalimbali vya usimilisho. Kwa sababu hiyo, tasnifu hii imetoa mchango katika nadharia changamano kwa kupendekeza misingi mbadala inayoweza kutumika katika ubunaji na uhakiki wa masimilisho.

1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulijikita katika kutathmini usimilisho wa riwaya na hadithi fupi za Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Kenya. Kiini cha uchunguzi huu kilikuwa kubaini mbinu zinazotumika kuzisimilisha tungo za kinathari, utathmini wa mbinu hizo, na ufafanuzi wa matatizo yanayotinga uwasilishaji wa ujumbe kama alivyodhamiria mwandishi wa matini chasili. Fauka ya haya, utafiti huu ulidhamiria kuelekeza kuhusu jinsi ya kuyatatua matatizo hayo. Aidha, utafiti huu umejadili dhana ya usimilisho, sababu za kusimilisha, na historia ya usimilisho wa kazi za fasihi ulimwenguni.

Uchunguzi huu ulihusisha tungo zinazotahiniwa katika shule za upili. Hizo ni tungo ambazo zilikuwa zikiigizwa mwakani 2013, video ya riwaya ya *Siku Njema* ambayo ilikuwa imenaswa na Taasisi ya Ukuzaji Mitaala ya Kenya (K.I.C.D.), na video za Diwani ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* kutoka vikundi teule. Mtafiti alichunguza sampuli ya vikundi vinne pamoja na kikundi cha uigizaji kilichokuwa kimenaswa na K.I.C.D. Katika vikundi hivyo, mtafiti alichagua vikundi viwili kutoka miongoni mwa vile vinavyofanyia maigizo yake shuleni, kisha akachagua vingine viwili kati ya vikundi vinavyoigizia kwenye kumbi za thieta. Vikundi vinne vilivyoteuliwa kuchunguzwa ni *Fanaka Theatre Group, Jicho Four, Planets Theatre* na *Nairobi Theatre Group*. Uchaguzi wa vikundi namna hiyo ulikuwa muhimu na ulimwezesha mtafiti kubaini mbinu mbalimbali zinazotumika katika usimilisho wa kazi za kinathari. Aidha, ulimwezesha mtafiti kuyatambua matatizo katika usimilisho wa kazi za kimasimulizi yanayotokana na uchaguzi wa maeneo ya kuigizia. Kama ilivyobainika, kumbi za thieta zimetengenezwa kwa ajili ya maigizo na majukwaa yake huwa na vifaa muhimu vya uigizaji, jambo lililofanya mbinu za uigizaji katika majukwaa hayo kuwa tofauti na mbinu zilizopatikana

kwenye majukwaa ya shule. Hata hivyo, utafiti ulibaini kwamba, wasimilishaji katika majukwaa ya shule hutumia mbinu za kifaraguzi kuziba upungufu unaotokana na majukwaa hayo.

1.7 Kiishilio

Sura hii imebainisha na ikafafanua vipengele vya kimsingi katika utafiti. Vipengele vya kimsingi vilivyobainishwa na vikafafanuliwa ni usuli wa utafiti, suala la utafiti, sababu za kuchagua mada, na upeo na mipaka ya utafiti. Pia, sura hii imeyabainisha maswali na malengo yaliyouongoza utafiti.

SURA YA PILI

YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA NA MISINGI YA NADHARIA

2.0 Utangulizi

Sura ya kwanza imeshughulikia vipengele vya kimsingi katika utafiti. Sura ya pili inachambua kazi mbalimbali zilizoandikwa kuhusu mada. Kazi zilizoandikwa kuhusu mada zinashughulikiwa kwa misingi mitatu: usimilisho wa tungo za kimasimulizi kuwa filamu, tahakiki za riwaya na hadithi fupi, na tafiti zinazohusu maigizo. Aidha, sura hii imeshughulikia misingi ya nadharia iliyouongoza utafiti.

2.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Usimilisho wa riwaya na hadithi fupi kwa minajili ya kuigizwa jukwaani haujatafitiwa sana. Tafiti nyingi zilizofanywa zinahusu usimilisho wa tanzu za kinathari kuigizwa kama filamu. Kwa sababu ya uchangamano na urefu wake, riwaya ndiyo utanzu unaosimilishwa sana kuwa filamu.

Tafiti kuhusu usimilisho wa riwaya na hadithi fupi kuwa filamu zinaainishwa katika makundi mawili makuu. Kundi la kwanza ni tafiti za wahakiki ambao

wanachunguza uaminifu wa masimilisho kwa matini chasili. Tahakiki zao zinakashifu filamu zinazokosa kuwasilisha yaliyomo kwenye matini chasili kama yanavyosomeka na kufasiriwa na wasomaji. Mtazamo wa kundi hili ulivuma zaidi katika karne ya 19 na unapatikana katika tafiti za watu kama vile Giddings na Erica (2000).

Kundi la pili ni la wahakiki wenye mtazamo kuwa, masimilisho yanapaswa kutathminiwa kama kazi za kisanaa zinazojisimamia na kujitegemea. Kulingana na wahakiki hawa, haifai kuilazimisha filamu kufanana na kitabu kinachosimilishwa, kwani hilo huenda likawa silo lengo asilia la msimilishaji. Mtazamo wa kundi hili unaonekana kupata uungwaji mkono na wengi wanaolitaftia eneo la usimilisho. Watafiti kama vile Wagner (1975), McFarlane (1996), Stam (2005) na Andrew (1984) wamejajadili mitazamo hii katika kazi zao. Tafiti zao zinapinga uwezekano wa kupatikana similisho aminifu kwa matini chasili.

Utafiti wao unahusiana na huu kwani tafiti zote zinalenga usimilisho wa tungo za kinathari. Kwa hivyo, uliandaa msingi imara katika utafiti wetu hasa upande wa kinadharia. Ingawa mfanano ulidhihirika baina ya tafiti hizi, kuna tofauti kubwa inayobainika. Tafiti zilizorejelewa zimejikita katika usimilisho wa filamu ilhali utafiti huu ulihusu usimilisho wa drama inayoigizwa jukwaani. Zaidi yake, usimilisho huu ulitarajiwa kuonyesha kiwango fulani cha uaminifu kwa matini zinazosimilishwa, kwani hivyo ni vitabu vinavyotahiniwa shuleni.

Utafiti uliokaribiana na huu katika kuangazia usimilisho ni wa Kiai (1996), aliyechunguza usimilisho katika sajili ya lugha. Utafiti wake ulichanganua usemi unaotumika katika vipindi vya redio vinavyohusu kilimo na afya vikiwalenga

wakulima wa mashamba madogo madogo. Kiai alijikita katika kuchunguza mitindo inayotumika kusimilisha matini za kisayansi ili ziafiki msimbo wa mawasiliano unaotumika na zieleweke na hadhira inayolengwa. Uchanganuzi wake ulijikita katika viwango vya leksia na mtindo. Dhamira ya utafiti wa Kiai ina ukuruba sana na utafiti wetu. Tafiti zote zinachunguza usimilisho unaolenga kukuza viwango vya uelewa wa matini fulani. Baadhi ya mbinu za kiisimu alizozibainisha Kiai zinahusiana na mbinu zilizobainishwa katika usimilisho wa tungo za kinathari. Hata hivyo, utafiti huu ni tofauti na wa Kiai (1996), kwa vile utafiti wake ulihusu usimilisho katika viwango vya kiisimu ilhali utafiti huu unahusu usimilisho katika matini za fasihi.

Ingawa usimilisho wa kinathari katika fasihi ya Kiswahili bado ni mchanga, kuna tafiti ambazo ni muhimu kwa utafiti huu. Hizi ni tafiti ambazo zimehakiki riwaya na hadithi fupi kama tanzu, na zile ambazo zimechunguza maigizo kwa ujumla.

Tafiti ambazo zimefanywa katika utanzu wa hadithi fupi zimejikita katika vipengele vya fani na maudhui. Baadhi ya tahakiki muhimu katika utanzu huo ni tahakiki ya Mohochi (1995) aliyeangalia fani katika hadithi fupi kwa jumla. Tahakiki nyingine ni ya Mbuthia (2005) ambaye alichunguza vipengele vya fani na maudhui katika hadithi fupi za Kiswahili. Aidha, Mulewa (2008) alichunguza kipengele cha wahusika katika fani. Wengine walioandika kuhusu hadithi fupi ni kama Mohamed (1995), Kezilahabi (1983), King'ei na Kisovi (2005), Wamitila (2002, 2003, na 2008), na Mbatiah (2000).

Utafiti huu ulihusiana kwa kiasi fulani na tafiti zilizotajwa. Tafiti zote zimelenga kuhakiki vijenzi vikuu vya hadithi fupi, ambavyo ni maudhui na fani. Usimilisho wa hadithi fupi hulenga kuvihamisha vijenzi hivyo kutoka kwa matini ya

kinathari hadi matini ya kidrama. Hata hivyo, utafiti huu unatofautiana na tahakiki zilizorejelewa. Tahakiki zilizotajwa zilishughulikia vipengele vya hadithi fupi ya Kiswahili kama utanzu unaojitegemea. Utafiti huu umeuchunguza utanzu wa hadithi fupi kama utanzu unaoweza kusheheni sifa za kimaigizo kama tamthilia.

Kinyume na hali ilivyo katika utafiti wa hadithi fupi, utanzu wa riwaya umefanyiwa utafiti mwingi unaozaga katika vipengele vyake muhimu. Waandishi mbalimbali wameushughulikia utanzu huo kwa kina huku wakichambua vipengele vyake vikuu. Hawa ni kama vile Mohamed (1983 na 1995), Msokile (1993), Wamitila (2002, 2003, na 2008), Mazrui na Syambo (1992), Kezilahabi (1983), Ntarangwi (2008), na Njogu na Chimerah (1999), miongoni mwa wengine. Suala lililotafitiwa katika utafiti huu lilitokana na pengo lililoachwa na tafiti zao. Aidha, tafiti hizo zilikuwa muhimu katika kuongoza utafiti huu kwani ndizo zilizotoa maelezo ya kutegemewa na mtafiti kuhusu riwaya.

Mbali na vitabu, kuna tasnifu nyingi zilizofanywa katika utanzu huo. Tasnifu nyingi zilijikita katika uchunguzi wa maudhui na fani katika riwaya ya Kiswahili. Tahakiki zilizochunguza fani ni za watafiti kama vile: Muindi (1990), Mayaka (1991), Kamau (1992), Ndung'u (1996), Gaita (1998), Anaye (2004), Musee (2007), Mavisi (2007) na Musembi (2008), miongoni mwa nyingine. Watafiti waliohakiki maudhui katika riwaya wanajumuisha Mbatiah (1999), Kimani (2003) na Kavuria (2008), miongoni mwa wengine.

Kama ilivyodhihirika, tafiti kuhusu maudhui na fani katika riwaya ya Kiswahili ziliichunguza riwaya kama utanzu huru unaojisimamia. Ingawa utafiti huu

ulivihakiki vipengele vya fani na maudhui, lengo la kufanya hivyo lilikuwa kuchunguza namna vipengele hivyo vilivyowasilishwa katika masimilisho ya riwaya. Isitoshe, mtafiti aliichunguza riwaya kama matini ya fasihi yenye uwezo wa kushirikisha sifa za kimaigizo kama tamthilia.

Mbali na vipengele vya maudhui na fani, kuna tafiti za riwaya zilizojikita katika udhihirishaji wa sifa fulani za kiisimu ama kinadharia. Mathalan, utafiti wa Osore (1994) ulichunguza sifa za kiisimu katika riwaya za Suleiman Mohamed. Utafiti huu ulihusiana na wa Osore kwa vile riwaya na masimilisho yake yaliyohakikiwa yalisheheni sifa za kiisimu alizozibaini. Hata hivyo, tafiti hizi zilitofautiana kimalengo kwani nia ya utafiti huu ilihusu udhihirishaji wa namna masimilisho yalivyowasilisha maudhui na fani ya riwaya husika.

Tafiti zilizojikita katika udhihirishaji wa nadharia za uhakiki ni kama vile: Bakari (2008), Magaju (2008) na Osore (2008). Utafiti huu, ingawa ulitumia nadharia tofauti, ulidhamiria kudhihirisha namna nadharia ya uigizaji na usimilisho zinavyotumika kusimilisha na kuigiza kazi za kinathari zinazotahiniwa. Hata hivyo, tafiti hizo zilijikita katika udhihirishaji wa nadharia moja mahsus, ilhali utafiti huu ulitumia mseto wa nadharia kutimiza lengo lake.

Waandishi mbalimbali waliyashughulikia maigizo kwa mikabala tofauti tofauti. Wengi wao walijihusisha na maigizo kama kipera cha fasihi simulizi. Kwa kufanya hivyo, walichunguza maigizo katika jamii mbalimbali za Kiafrika. Tafiti za baadhi ya watafiti zilishughulikia dhima ya maigizo katika jamii husika. Mathalan, Chesaina (1977) alitafitia dhima ya maigizo ya nyimbo katika jamii ya Waembu na Wambeere katika mawasiliano. Utafiti mwingine ni wa Kerr (1995) aliyetafiti kuhusu maigizo ya *Kote- Hon* katika jamii ya Bamana huko Mali.

Utafiti wa Kerr unakaribiana na wa Mlacha (2000), aliyetafitia dhima ya maigizo ya *Mwindiki* katika kabila la Nguu huko Tanzania. Matti (1996) naye alitafiti kuhusu nyiso katika jamii ya Watharaka. Utafiti wa Matti (1996) unakaribiana sana na ule uliofanywa na Mutwiri (2005), kuhusu utendakazi wa nyiso katika jamii ya Watigania. Uchunguzi wa aina hiyo ndio unaopatikana katika kazi ya Mutegi (2010). Mutegi alitafiti kuhusu maigizo katika fasihi simulizi kwa kurejelea mifano ya *Kirarire* katika nyimbo za tohara za Wameru. Katika utafiti wake, Mutegi alionyesha umuhimu wa maigizo katika utanzu wa nyimbo.

Ilibainika kuwa baadhi ya watafiti tayari wameweza kuhusisha maigizo na elimu ya kisasa. Gituku (1990) alishughulikia maigizo ya kienyeji ya watoto nchini Kenya na dhima yake katika ufundishaji. Kutokana na utafiti wake, alipata kwamba maigizo hayo yanaweza kutumika ili kuboresha ufundishaji katika shule za msingi. Utafiti wa Gituku ulikaribiana sana na ule uliofanywa na Bigambo (1987) aliyetafiti kuhusu uigizaji katika muktadha wa majaribio ya ufundishaji. Bigambo alipata kuwa maigizo yana nafasi ya kuupa ufundishaji uhai na hivyo kuwa kivutio kwa wanafunzi.

Tafiti hizo ambazo ziliyashughulikia maigizo kwa mujibu wa dhima yake zina uhusiano na utafiti huu. Maigizo ya riwaya na hadithi fupi yana dhima muhimu katika ufundishaji wa vitabu vinavyotahiniwa vya fasihi. Kwa hivyo, utafiti huu ulilenga kutathmini utendakazi wake katika ufundishaji. Hata hivyo, utafiti huu ulitofautiana na tafiti hizo. Pale ambapo usuli wa tafiti hizo ni fasihi simulizi, utafiti huu ulijikita katika fasihi andishi katika tanzu za riwaya na hadithi fupi. Zaidi yake, utafiti huu ulihusu usimilisho wa tungo za kinathari kuwa matini za kidrama na maigizo yake.

Dhana ya uigizaji katika tungo za kinathari imeshughulikiwa na waandishi wachache. Kati yao ni Msokile (1993) aliyeeleza kuwa, riwaya (pia hadithi fupi) iwapo itaigizwa basi itabidi ibadilishwe kwanza na kuchukua muundo na mtindo wa tamthilia. Kauli ya Msokile inaashiria kuwepo na mbinu zinazotumika kuibadilisha kazi ya kinathari kuwa tamthilia. Hata hivyo, Msokile hazionyeshi mbinu hizo za usimilisho, pengo linalojazwa na utafiti huu. Mwandishi mwingine aliyelishughulikia suala hili ni Wamitila (2002) alipoelezea sifa zinazokamilisha msuko wa tamthilia. Mwandishi huyu alisema kuwa, riwaya inayofikiriwa kuigizwa ni lazima ifuate kaida za uigizaji kama kuwa na msuko wenye wasifu fulani tu. Hili wazo lake lilikuwa muhimu katika utafiti huu, kwani liliarifu kuhusu kuwepo kwa kaida fulani zinazotawala usimilisho wa tungo za kinathari. Licha ya kwamba Wamitila alitaja kaida hizo na kuonyesha moja, hakupiga hatua mbele kuonyesha kaida nyinginezo na ufaafu wake katika kuiwasilisha dhamira ya mwandishi. Utafiti huu umelijaza pengo hilo kwa kudhihirisha kwamba riwaya na hadithi fupi husheheni kaida fulani mahsusi za kitamthilia ambazo huwezesha kuigizika kwake.

Mbali na waandishi waliotajwa, suala hili liliendelezwa na Ochenja (2008) aliyetafiti kuhusu maigizo kama mbinu ya maudhui katika kijiriwaya cha Ken Walibora – *Ndoto ya Amerika (2001)* na riwaya ya mwandishi huyo *Kufa Kuzikana (2003)*. Ochenja, kupitia utafiti wake, alibainisha kuwa riwaya hizi zina sifa za kitamthilia. Utafiti huu wa Ochenja (2008) unakaribiana na utafiti huu kwa vile sifa alizobainisha ndizo msingi wa usimilisho katika tungo za kinathari. Hata hivyo, tafiti hizi zinatofautiana sana. Utafiti wa Ochenja ulijikita katika uchunguzi wa umatini wa kidrama katika riwaya na jinsi unavyotumika na waandishi kuwasilisha maudhui yao. Madhumuni hayo ni tofauti na yale

yaliyoongoza utafiti huu ambao ulilenga kuchunguza jinsi umatini wa kidrama unavyotumika kuzisimilisha tungo za kinathari. Fauka yake, utafiti huu umevijadili vikwazo vinavyokumba uhamishaji wa sifa hizo za kitamthilia kutoka riwaya husika kwa matini ya kidrama.

2.2 Misingi ya Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia changamano iliyoundwa kutokana na nadharia ya usimilisho na ile ya uigizaji. Uteuzi wa nadharia jinsi hiyo ulitokana na malengo ya utafiti ambayo yaliazimia kubaini jinsi matini za kimasimulizi husimilishwa na kuigiziwa wanafunzi na walimu.

2.2.1 Nadharia ya Usimilisho

Ili kutimiza malengo ya utafiti yaliyohusu kuziainisha na kuzitathmini mbinu za usimilisho, kuyabainisha matatizo katika mchakato huo, na kueleza njia za kuyatatua, utafiti huu ulitumia nadharia ya usimilisho ili kuchanganua na kueleza mbinu, matatizo, na suluhu ya matatizo hayo. Misingi ya kinadharia iliyouongoza uchanganuzi na uelezaji huo ilitokana na mkabala wa nadharia hii unaohimiza usimilisho ufanywe kwa uaminifu wa matini chasili. Hii ni kwa sababu riwaya na hadithi fupi teule ni tungo zilizokuwa zikitahiniwa katika mtihani wa KCSE na zilitakiwa kusimilishwa kwa usahihi.

Nadharia ya usimilisho ina msingi wake katika uigizaji wa filamu. Ni muhimu kudhihirisha kwamba kuna uhusiano mkubwa baina ya usimilisho wa kifilamu na ule wa kidrama. Hili linatokana na mchakato wa usimilisho. Katika mchakato huo, kazi ya kinathari hufasiriwa na kugeuzwa kuwa matini ya drama

iliyoandikwa. Hatua inayofuata huwa ni kuigeuza drama hiyo kuwa sanaa ya maonyesho, ambapo inaweza kuigizwa kama filamu ama mchezo wa kuigiza. Kwa ambavyo utafiti huu ulihusisha uchanganuzi wa uigizaji wa masimulizi ya riwaya na hadithi fupi jukwaani, mtafiti aliyatumia mawazo ya kinadharia ambayo yalilenga mchakato wenyewe.

Nadharia hii iliwekewa msingi na kazi yake George Bluestone –*Novels into Film* (1957). Bluestone alichanganua filamu sita akidhamiria kubainisha mabadiliko yaliyofanywa kwa kazi asilia na waandishi wa filamu hizo. Kutokana na utafiti wake alihitimisha kwa kauli ambayo ilikuwa muhimu kwa nadharia hii, kwamba, usimilisho wa kazi moja hadi nyingine huzalisha kazi nyingine huru inayojitawala. Kulingana na mawazo yake, haiwezekani kazi inayosimilishwa ikailanda similisho lake, kwani wasimilishaji huongeza, huondoa na pia kubatilisha vijisehemu vya kazi asilia.

Maoni ya Bluestone (1957) yaliendelezwa na wahakiki Andrew (1984), Goodman (1976), na Starrs (2006). Wahakiki hawa wanahoji kuwa, ni vigumu kuibuka na similisho sahihi ama amanifu kwa matini chasili.

Kutegemea kiwango cha usahihi kwa matini chasili, usimilisho unaweza kuzalisha aina tatu za similisho: tafsiri sisisi, fasiri mpya na analojia. Katika tafsiri sisisi, mtunzi hulenga kuwasilisha kazi inayofanana na matini ya kinathari inayosimilishwa. Fasiri mpya ni aina ya similisho ambapo matini chasili inafuatwa lakini usimilisho ukisheheni mabadiliko ya kimakusudi katika elementi fulani. Mazingira, vipindi vya wakati na vimalizio huenda vikabadilishwa ili kuzalisha kazi tofauti lakini inayoonyesha mfanano na matini chasili. Analojia ni dhana iliyobuniwa na Wagner (1995) kurejelea aina ya usimilisho ambao

unakengeuka zaidi kutoka kwa matini chasili, kiasi cha kuzalisha kazi nyingine mpya ya sanaa. Kulingana na Wagner, kazi hiyo haiwezi kuhukumiwa kama ukiushi wa kazi asilia kwa vile mtunzi wake hadhamirii kuiwasilisha matini chasili.

Maoni ya Bluestone (1957) na ya wafuasi wake yalidhihirisha upungufu katika uchunguzi wa usimilisho uliodhamiriwa kuinua viwango vya uelewa wa kazi za kinathari miongoni mwa wanafunzi na walimu. Masimilisho yaliyoandaliwa na wasimilishaji yalitarajiwa kuwakilisha asilimia mia moja ya kiwango cha uaminifu kwa matini chasili. Utafiti ulibaini kwamba zipo mbinu mahsusi, kama vile usimulizi, ambazo hudhamiriwa kuwasilisha sifa za riwaya na hadithi fupi ambazo zinaweza kupotea katika usimilisho wake. Kwa namna hiyo, inawezekana kubuni masimilisho aminifu kwa matini chasili.

Kwa kuzingatia msingi huu, mtafiti aliyachanganua masimilisho ya vitabu teule kwa mikabala ya nadharia hii inayosisitiza usahihi wa similisho kwa matini chasili. Mihimili iliyotumika ilitokana na mawazo ya Jakobson (1963) na Linda Hutcheon (2013). Kulingana na Lhermite (2005), Jakobson aliutazama usimilisho kama tafsiri baina ya mifumo ya sauti (intersemiotic translation). Kama tafsiri, dhima kuu ya usimilisho huwa ni mawasiliano; kuuwasilisha ujumbe jinsi ulivyo katika matini chasili hadi kwa matini lengwa. Naye Hutcheon (2013), anaitazama hadithi kama kiungo cha msingi katika usimilisho. Wasimilishaji huisimilisha hadithi ya matini kwa njia tofauti tofauti kama vile usimuliaji, utendaji na mtagusano.

Kutokana na mawazo ya wahakiki hao wawili, mihimili miwili ilizuka ambayo iliongoza uchanganuzi wa mbinu za usimilisho:

Kwanza, msimilishaji hutakiwa kuhamisha vipengele vya maana ya matini chasili kwa matini lengwa kama vinavyobainishwa na mwandishi wake. Kwa hivyo, hana budi kuzingatia mtazamo wa mtunzi kuhusu wahusika na uhusika wao, maudhui, hali ya usimuliaji, mandhari, mbinu, na kadhalika, ili vipengele hivi viwasilishe maana kama alivyokusudia mwandishi.

Pili, kiungo muhimu cha usimilisho ni hadithi. Katika usimilisho majadiliano ya hadithi hupotea, lakini visawe vya vipengele mbalimbali vya hadithi hutafutwa katika mifumo tofauti ya ishara. Baadhi ya vipengele hivi ni kama vile maudhui, matukio, wahusika na uhusika, mitazamo, muktadha, ishara, jazanda, matokeo, na kadhalika. Kwa mujibu wa Hutcheon (2013), wahusika ni muhimu katika hadithi ikizingatiwa namna wanavyokua kisaikolojia na hata jinsi hadhira inavyowahusisha na matini chasili. Mwandishi huyu akimnukuu Hamon (1977: 264) anaongeza kuwa, vihadithi katika hadithi vinaweza vikafupishwa na hata msuko wake kufaraguliwa. Aidha, mwendo wa hadithi unaweza kuumbwa upya, muda ukafinywa ama kunyambuliwa. Hata hivyo, haiwezekani kuubadilisha mtazamo wa hadithi, kwa ambavyo kufanya hivyo kunaweza kuzalisha hadithi mpya.

Mihimili hii iliufaa utafiti huu katika kuchanganua mbinu zilizotumika kusimilisha vitabu teule vya kinathari. Aidha, iliarifu kuhusu makosa yaliyofanywa katika harakati za kusimilisha matini hizo. Mtafiti alitumia mihimili ya nadharia hii katika hatua mbili muhimu za kusimilisha tungo za kinathari. Katika hatua ya kwanza, mtafiti alizisoma matini chasili teule na kisha masimilisho yake na kuchunguza jinsi usimilisho ulivyokuwa umefanywa. Hatua ya pili mtafiti alichunguza namna masimilisho hayo yalivyoigizwa jukwaani.

Huu ndio usimilisho wa mwisho, ambao pia ndio matokeo ya mchakato mzima wa usimilisho.

2.2.2 Nadharia ya Ugizaji

Msingi katika nadharia ya drama ulijengwa na mawazo ya Aristotle aliyeanisha vipengele sita ambavyo ni muhimu katika muundo wa tamthilia, hasa tanzia. Vipengele hivi ni msuko (mythos), wahusika (ethos), dhamira (theme), uteuzi na matumizi ya maneno (lexis), nyimbo (melopoeia) na maonyesho (opsis). Mawazo haya yamepanuliwa na wahakiki wengine waliochangia katika nadharia hii.

Upanuzi wa mawazo haya ya kirasimi umeenda sambamba na ukuzaji wa drama katika miktadha mbalimbali ya kitamaduni. Kwa sababu hii, drama katika fasihi ya jamii nyingi za kilimwengu inaweza kudhihirisha tofauti katika sifa zake bainifu.

Drama ya fasihi ya Kiswahili imezalika katika umahuluti wa fasihi ya Kimagharibi na fasihi simulizi ya Kiafrika. Kutokana na ukweli huu, wahakiki mbalimbali wamejadili nadharia ya ugizaji kwa kuegemea usanifu wake katika muktadha wa fasihi ya Kiswahili. Baadhi yao ni Hussein (1983), Mlama (1983), Syambo na Mazrui (1992), Mohamed (1995) na Wamitila (2002 na 2008). Hussein (1983) alifafanua jinsi vigezo sita vya Ki-Aristotle vilivyozingatiwa na kukiukwa katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili. Katika uchanganuzi wake, Hussein (1983) analinganisha tamthilia ya Kiyunani na ile ya Kiswahili. Majadiliano kama hayo yanadhihirika katika makala ya Mlama (1983) ambaye anajadili vigezo vya tamthilia ya Ki-Tanzania. Wahakiki wanaoshughulikia

nadharia ya uigizaji ya Kiswahili, kwa namna wazi na isiyo wazi, wanaonekana kuuzingatia umahuluti uliopo baina ya drama ya Kiswahili na drama ya Kimagharibi.

Kutokana na maoni ya wahakiki hawa wa drama ya Kiswahili, utafiti huu unaweza kudondoa mihimili ya nadharia ya uigizaji ya Kiswahili ambayo ilisaidia kuchanganua maigizo ya masimilisho ya Kiswahili.

Mihimili miwili ya kwanza iliyouongoza utafiti huu ilitokana na maelezo ya Wamitila (2008) kuhusu misingi ya drama ya Kiswahili. Kwanza, drama ya Kiswahili huhusisha uwasilishaji wa kisimulizi. Matukio ya drama huwasilishwa kiutendaji na kwa namna ya usimulizi. Kuna aina tatu za usimulizi katika drama:

- I. Usimulizi katika maelekezo ya jukwaani.
- II. Matumizi ya msimulizi kusimulia matukio.
- III. Mazungumzo ya wahusika.

Mhimili huu uliufaa utafiti huu katika uelezaji wa usimulizi uliodhihirika katika uigizaji wa masimilisho na ubunaji wake. Aidha, mazungumzo ya wahusika yalihakikiwa kwa mujibu wa mhimili huu. Ilibainika kwamba, usimulizi, maelekezo ya jukwaani, na mazungumzo ni mbinu muhimu katika usimilisho wa riwaya na hadithi fupi.

Pili, drama hukamilishwa na msuko na hadithi. Wahakiki wengi hubainisha hadithi kama mpangilio wa matukio kiwakati, na msuko kama mfuatano wa matukio kiusababishi. Hadithi huelezwa kama msingi wa drama. Kuna kanuni tatu zinazodhibiti uwasilishaji wa matukio ya hadithi:

- I. Kanuni ya mpishano/mfuatano: Katika kanuni hii, mbinu rejeshi huepukwa na tukio moja hufuatwa na jingine pasipo kuingiliwa na chochote katikati.
- II. Kanuni ya mshindilio: Mambo mengi katika hadithi hushindiliwa katika kipindi kifupi sana cha wakati.
- III. Kanuni kuhusu vikwazo vya kithieta na kijamii. Kanuni hii hukataza uwasilishaji wa matukio yanayokiuka matarajio ya maadili ya kijamii.

Mhimili huu ulitumika kuelezea mbinu mbalimbali zilizotumika kuvisimilisha vipengele vya msuko na hadithi. Aidha, mhimili huu ulitufaa katika uelezeaji wa namna vipengele hivyo vilivyoigizwa na matatizo yaliyobainika kuhusiana na uwasilishaji wake.

Tatu, ngoma na muziki huchukua nafasi kubwa katika drama ya Kiafrika. Kwa kawaida ngoma na muziki huashiria mwanzo wa tendo la kidrama au kuongeza kiwango cha hisia katika tendo fulani. Aidha, kipengele hiki cha uigizaji kinaweza kutumika ili kushadidia ujumbe unaoendelezwa na tukio fulani la kidrama. Kwa mujibu wa Hussein (1983), Aristotle alipendekeza nyimbo ziimbwe katika sehemu ya mwisho ya tamthilia. Uigizaji wa drama ya Kiswahili umepitia mabadiliko na hali na hisia katika uigizaji zinaweza kuchangiwa pia na sauti za nyuma ya jukwaa, sauti zilizorekodiwa, mingurumo, ngoma, vilio na vicheko.

Uhakiki wa nyimbo na muziki katika maigizo ya kinathari ulifanywa kwa kuzingatia maelekezo ya mhimili huu wa tatu. Aidha, mhimili huu ulisaidia uelezaji wa sauti nyingine za jukwaani na tathmini yake.

Nne, wahusika ni sehemu nyingine muhimu katika drama. Hawa ndio huigwa na waigizaji jukwaani. Wahusika wa tamthilia huhitajika wabainishwe kiumri, kihulka, kiitikadi, kisura, misingi yao ya kiuchumi na kijamii pamoja na lugha wanayoitumia. Kwa ambavyo drama hukosa maelezo mengi kuhusu wasifu wa wahusika, Mohamed (1995) anashauri kuwa, mwongozaji wa tamthilia pamoja na watendaji wake, lazima wawe na kipawa na uzoefu mkubwa wa kubuni mambo na miondoko ambayo itasaidia kuweka wazi wasifu, tabia na saikolojia ya wahusika wakati wa utendaji. Huu ulibainika kuwa mhimili muhimu ulioongoza kueleza na kutathmini mbinu zilizotumika kuwasawiri na kuwateua waigizaji katika masimilisho na uigizaji wake. Usimilisho wa riwaya na hadithi fupi ulipania kuwasawiri na kuwateua wahusika na waigizaji waliobeba wasifu wa wahusika asilia wa tungo hizo.

Tano, maonyesho ni kipengele kingine muhimu katika uigizaji. Maonyesho hujumuisha matayarisho ya jukwaani na chochote katika jukwaa kinachosaidia ufanisi katika igizo. Kwa mujibu wa Syambo na Mazrui (1992), vipengele muhimu vya maonyesho ni aina ya jukwaa, mandhari, maleba, na umulikaji wa jukwaa. Mhimili huu ulikuwa nguzo katika uchanganuzi wa namna uigizaji wa masimilisho ulivyoandaliwa na vikundi mbalimbali vilivyoigiza vitabu teule vya kinathari.

2.3 Kiishilio

Sura ya pili imeshughulikia kazi mbalimbali zilizoandikwa kuhusu mada na misingi ya nadharia. Tasnifu katika sura hii imekuwa kubainisha kwamba, suala kuhusu uigizaji wa riwaya na hadithi fupi zinazotahiniwa halijatafitiwa na haja ya

kulichunguza ili kubaini mbinu za usimilisho na ufaafu wake, pamoja na kutambua matatizo yanayokumba mchakato huo.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.0 Utangulizi

Sura ya pili imeshughulikia yaliyoandikwa kuhusu mada na misingi ya nadharia iliyouongoza utafiti. Sura ya tatu inashughulikia mbinu za utafiti. Vipengele vinavyofafanuliwa katika sura hii ni mbinu changamano za utafiti, mahala pa utafiti, uteuzi wa sampuli, na ukusanyaji, uwasilishaji na uchanganuzi wa data.

3.1 Mbinu Changamano za Utafiti

Kimsingi kuna mbinu za kitakwimu na mbinu za kistahilifu. Utafiti huu ulitumia mtindo wa mbinu changamano ambapo mbinu za kitakwimu zilitumika pamoja na mbinu za kistahilifu. Kulingana na Creswell (2010), mtindo wa mbinu changamano za utafiti hurejelea ujumuishaji wa mikakati mbalimbali ya kinaelezo na kijarabati katika utafiti mmoja. Johnson (2007) anaeleza kwamba mtindo wa mbinu changamano za utafiti umeanza kuzoeleka kama njia ya tatu ya kufanya utafiti. Awali utafiti ulitarajiwa kutumia mtindo mmoja wa kutafiti; ama mbinu ya kinaelezo au ile ya kijarabati. Creswell (2010) anahoji kuwa, mtindo wa mbinu changamano hauna maana ya mchanganyiko wa kiholela, bali unahusu matumizi ya mikakati zaidi ya kutafiti katika ukusanyaji wa data, ambayo

haiwezi kupatikana kwa kutumia mtindo mmoja wa mbinu za utafiti. Mtafiti hutumia mikakati ya ziada katika utafiti wake ili kumwezesha kupata taswira kamilifu kuhusu tabia na tajriba ya binadamu. Kutokana na utambuzi kwamba mbinu zote za utafiti huwa na upungufu, watafiti huchukulia kuwa mapendeleo katika mbinu moja yanaweza kupunguzwa ama kuondolewa na matumizi ya mbinu ile nyingine.

Katika utafiti huu, mtafiti alichanganya mbinu za kimaelezo na kijarabati katika hatua ya kukusanya data na uchanganuzi wa data hiyo. Hata hivyo, mtindo wa mbinu ya kimaelezo ndio uliokuwa msingi katika uchunguzi huu. Kwa kutumia mbinu ya kimaelezo, mtafiti aliainisha na akaelezea mbinu na matatizo katika usimilisho wa riwaya na hadithi fupi. Aidha, mbinu za kimaelezo kama kusoma na kuhakiki matini za similisho, upigaji picha, uchunzaji na mahojiano zilitumika katika ukusanyaji wa data iliyochanganuliwa. Mtafiti alijumuisha mbinu za kijarabati kwa nia ya kumwezesha kubaini tathmini ya walimu na wasimilishaji kuhusu usimilisho wa tungo za kinathari kwa wanafunzi wanaotahiniwa katika kidato cha nne. Watafitiwa waliteuliwa kwa njia isiyo na mapendeleo kisha wakakabidhiwa hojaji wajaze. Uchanganuzi wa data hiyo ulifanywa kwa kuzingatia mbinu za kijarabati.

3.2 Mahali pa Utafiti

Utafiti kuhusu tathmini ya usimilisho wa riwaya na hadithi fupi kwa wanafunzi wa sekondari nchini Kenya ulifanywa katika magatuzi mawili: Nairobi na Kitui. Katika gatuzi la Kitui, mtafiti aliyatazama maigizo ya vikundi viwili teule katika shule za upili za Kisasi na Ikanga, na kukusanya data akitumia mbinu mbalimbali alizokuwa ameteua. Katika gatuzi la Nairobi, vikundi viwili vilitafitiwa katika

kumbi za *Kenya National Theatre* na *Liberty Hall*. Gatuzi la Nairobi lilikuwa muhimu kwani ndilo linalochukuliwa kuwa kitovu cha uigizaji huo. Fauka ya hili, gatuzi hilo lina majumba ya kisasa ya kuigizia yanayoruhusu matumizi ya mbinu mbalimbali za usimilisho jukwaani. Mtafiti aliliteua gatuzi la Kitui kwa vile alikuwa ameyazuru maigizo hayo kabla katika eneo hilo, na kuona jinsi yalivyokuwa yakitofautiana na yale yanayoigizwa katika kumbi za thieta. Kwa hivyo, utafiti ulikuwa umeazimia kuchunguza ulinganifu na tofauti za usimilisho katika majumba rasmi ya kuigizia na majukwaa huria ya shule.

3.3 Uteuzi wa Sampuli

Kwa ambavyo utafiti huu ulichanganya mbinu za kimaelezo na kijarabati, uteuzi wa sampuli yake ulifanywa kwa kuzingatia data iliyotarajiwa na namna ilivyotakiwa kuchanganuliwa. Utafiti huu ulihitaji sampuli za aina tano. Sampuli kuhusu riwaya na hadithi fupi zilizokuwa zimesimilishwa, vikundi vya uigizaji, maeneo ya utafiti, wasimilishaji na walimu.

Uteuzi wa sampuli ya vikundi vya uigizaji ulifanywa kwa kutumia mbinu kusudio. Mtafiti alibuni utaratibu mahsusi uliomwongoza katika uteuzi huo. Kwanza, mtafiti alichunguza historia ya usimilisho miongoni mwa vikundi vya uigizaji, huku akibaini wazi umri wa kila kikundi katika uigizaji wa tungo za kinathari. Pili, aliainisha vikundi hivyo katika kategoria mbili zikijumuisha vikundi vinavyoigizia katika gatuzi la Nairobi na vile vinavyoigizia nje ya gatuzi hilo. Kisha, mtafiti alichagua vikundi viwili kutoka kila kategoria ambavyo vilionekana kuwa na historia ndefu ya usimilisho wa kazi za kinathari. Mbinu hiyo ilituwezesha kuteua vikundi vinne vya uigizaji. Uchaguzi wa vikundi vilivyokuwa na historia ndefu ya uigizaji wa masimilisho ulituwezesha

kubainisha mbinu mbalimbali ambazo zilikuwa zikitumika na kuzoeleka na vikundi hivyo. Aidha, wasimilishaji hao walikuwa na tajriba pana iliyohitajika katika kubainisha matatizo ya usimilisho na jinsi yanavyoweza kutatuliwa.

Mbinu kusudio ilitumika kwa mara nyingine kuteua maeneo mawili ya ukusanyaji wa data nyanjani. Maeneo hayo yalikuwa magatuzi ya Kitui na Nairobi. Baada ya kuyateua magatuzi hayo mawili, mtafiti alifuata utaratibu ambao umeelezewa na kuteua sampuli ya vikundi vilivyokuwa vikiigiza masimilisho yake katika magatuzi hayo. Kwa kuzingatia utaratibu huo wa uteuzi wa vikundi na maeneo, sampuli ilituliwa ifuatavyo:

Katika gatuzi la Nairobi, vikundi vilivyoteuliwa ni *Fanaka* na *Jicho Four*. Maigizo ya vikundi hivyo yalikuwa katika kumbi za *Kenya National Theatre* na *Liberty Hall*. Vikundi vilivyoteuliwa kutafitiwa katika gatuzi la Kitui ni *Planets Theatre* na *Nairobi Theatre Group*. Maigizo ya vikundi hivyo yalikuwa katika shule za upili za Ikanga na Kisasi. Filamu ya riwaya ya *Siku Njema* iliyoandaliwa na K.I.C.D iliwakilisha taasisi hiyo kwa ushirika na kikundi kilichokuwa kimerekodiwa.

Wa aidha, mbinu kusudio iliongoza uteuzi wa tungo za kinathari zilizochunguzwa. Tungo zilizochaguliwa ni zile zilizokuwa zikiigiziwa wanafunzi na vikundi hivyo katika mwaka wa 2013. Hata hivyo, matini za masimilisho na video za diwani ya hadithi fupi ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* iliyoigizwa mwakani 2012 zilichaguliwa na kuchunguzwa. Matini na video hizo ni zile zilizotokana na vikundi teule. Aidha, kwa kutumia mbinu kusudio, filamu ya riwaya ya *Siku Njema* iliyoandaliwa na K.I.C.D ilichaguliwa. Uteuzi wa filamu hiyo ulidhamiriwa kuchunguza iwapo kuna

vigezo mahsusi vinavyozingatiwa na taasisi hiyo inapochagua similisho bora la kunaswa katika filamu. Utafiti huu ulibaini kwamba, ingawa vigezo hivyo sio dhahiri, usimilisho wa K.I.C.D na kikundi kishiriki una usahihi wa hali ya juu ukilinganishwa na vikundi vilivyokuwa vikitafitiwa.

Kwa kuzingatia utaratibu huo ulioelezwa wa kuteua vitabu, riwaya ya *Utengano* (S.A. Mohamed) na *Siku Njema* (K. Walibora) ziliteuliwa. Katika utanzu wa hadithi fupi, diwani ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (Mhr.K.Wamitila) na *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* (Wahr.K.Walibora na S.A.Mohamed) zilichaguliwa. Dhamira ya kuteua sampuli ya aina hiyo ilikuwa ni kutaka kubaini namna mtindo wa mwandishi unavyoathiri mbinu za usimilisho.

Katika uteuzi wa sampuli ya walimu na wasimilishaji, utafiti huu ulitumia mbinu kusudio. Mtafiti aliwateua walimu waliokuwa wamewapeleka wanafunzi kuyatazama maonyesho hayo ya vitabu kushiriki katika sampuli ya wahojiwa. Walimu walikuwa muhimu kuhojiwa kwa vile wana ujuzi na tajriba pana kuhusu fasihi na utahini wake. Isitoshe, walimu ndio huvialika vikundi hivyo kwa kuzingatia vigezo fulani wanavyovijua. Kwa vile idadi yao ilikuwa ndogo, mtafiti aliwahoji na kuwapa hojaji walimu wote wa Kiswahili waliokuwa wamehudhuria maigizo hayo. Mtafiti aliteua msimilishaji mmoja kutoka kila kikundi. Kwa ujumla sampuli ya wasimilishaji wanne na walimu kumi na tisa ilichaguliwa. Maonyesho ya hadithi fupi yalijumuisha walimu tisa na yale ya riwaya yakawa na walimu kumi. Hojaji ya wasimilishaji iliwataka wajibu maswali kuhusiana na tanzu zote mbili, na kwa hivyo walihojiwa mara moja tu.

Sampuli ya wahojiwa ishirini na watatu (23) iliufaa utafiti huu katika kubaini matatizo ya usimilisho na jinsi yanavyoweza kutatuliwa. Maoni ya walimu na

wasimilishaji ni muhimu na yakishirikishwa pamoja usimilisho unaweza kuwa na manufaa zaidi kwa walengwa wake. Dhima ya msimilishaji wa vitabu vinavyotahiniwa ni sawa na ya mwalimu anayewafundisha wanafunzi vitabu hivyo. Data iliyokusanywa kutokana na sampuli hiyo inakubalika, kwani kulingana na Lune (2010), sampuli ya mbinu kusudio huwa ni ndogo. Hii ni kwa sababu wahojiwa walioteuliwa ni wale waliokuwa na tajriba na ujuzi wenye data iliyokusudiwa katika mahojiano na hojaji.

3.4 Ukusanyaji wa Data

Mtafiti alikusanya data maktabani na nyanjani. Maeneo hayo yote yalizua data muhimu iliyochanganuliwa.

3.4.1 Maktabani

Maktabani mtafiti alizisoma riwaya na hadithi fupi husika na kuzichambua ndipo apate uelewa wa yale yaliyotarajiwa kusimilishwa. Data iliyokusanywa kutoka vitabu hivyo ililinganishwa na yaliyomo katika masimilisho na maigizo yake. Vitabu vilivyosomwa maktabani ni riwaya za *Utengano* na *Siku Njema*, na diwani za hadithi fupi za *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* na *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*.

3.4.2 Nyanjani

Nyanjani mtafiti aliyatazama maigizo hayo shuleni na katika kumbi za thieta za umma. Katika gatuji la Kitui, mtafiti aliyazuru maigizo ya vikundi viwili vilivyokuwa vikiigiza katika shule mbili tofauti. Kumbi za thieta, *Kenya National Theatre* na *Liberty Hall*, zilitembelewa na mtafiti ili kukusanya data kuhusu maigizo ya vikundi viwili vilivyokuwa vimeteuliwa katika gatuji la Nairobi.

3.4.3 Vifaa na Mbinu za Utafiti

Data iliyochanganuliwa katika utafiti huu ilikusanywa kwa vifaa na mbinu mbalimbali. Mugenda (2008) anafafanua mbinu kama namna ambavyo kifaa fulani hutumiwa ili kukusanya habari fulani. Vifaa vya utafiti vilivyotumiwa ni kama vile kamera, kalamu na daftari, mwongozo wa mahojiano na hojaji. Mbinu za utafiti zilizotumiwa ni mahojiano, uchunzaji, na uchanganuzi wa masimilisho.

3.4.3.1 Matumizi ya Kamera

Data iliyohusu namna uigizaji wa riwaya na hadithi fupi ulivyofanywa ilikusanywa kwa kamera za kunasa na kupiga picha. Mtafiti aliyapiga picha matukio muhimu katika uigizaji wa masimilisho. Kwa vile haikuruhusiwa kunasa kila tukio la uigizaji, mtafiti aliyanaswa katika video matukio muhimu kwa malengo ya utafiti huu. Mandhari ya jukwaani yalipigwa picha ili kumwarifu mtafiti kuhusu namna vipengele vya uigizaji vilivyozingatiwa. Kwa ambavyo kamera zilizotumika zilikuwa na uwezo wa kunasa sauti, mtafiti alihitari kutumia kamera hizo kurekodi mazungumzo ya waigizaji na sauti za jukwaani.

3.4.3.2 Matumizi ya Daftari na Kalamu

Mtafiti alitumia daftari na kalamu kama vifaa muhimu vilivyotumika sambamba na kamera. Mambo muhimu ambayo hayakuweza kunaswa na kamera yaliandikwa. Namna maigizo yalivyokuwa yakianzishwa na kuhitimishwa ni jambo lililohitaji kunakiliwa kimaandishi. Mbinu ya kuandika ilitumika kunakili hoja muhimu katika mahojiano baina ya mtafiti na wahojiwa walimu na wasimilishaji.

3.4.3.3 Matumizi ya Hojaji

Hojaji zilizokuwa zimeandaliwa na mtafiti kwa dhamira ya kutaka kubaini matatizo ya usimilisho, jinsi ya kuyatatua, na maoni ya walimu na wasimilishaji kuhusu usimilisho wa riwaya na hadithi fupi, zilisambaziwa walengwa. Wasimilishaji ambao hawakuandamana na vikundi vyao walitumiwa hojaji zao kupitia barua pepe, njia waliotumia kurudisha majibu yao. Njia hii ilizua data nyingi kuhusu matatizo ya usimilisho na jinsi ya kuyatatua, hasa kutoka kwa walimu.

3.4.3.4 Matumizi ya Mahojiano

Mtafiti alipanga mahojiano na baadhi ya wasimilishaji na walimu waliokuwa wameteuliwa. Mahojiano baina ya mtafiti na wasimilishaji yalihusu ubainishaji wa viwango vyao vya elimu, ujuzi wao wa fasihi, na matatizo wanayopitia katika kusimilisha tungo za kinathari na jinsi wanavyoyatatua. Katika mahojiano hayo wasimilishaji walitakiwa kueleza kuhusu kazi ya usimilisho na historia yake nchini Kenya. Mahojiano na walimu yalilenga kubaini kasoro zilizodhihirishwa na usimilisho na maoni yao kuhusu umuhimu wake kwa wanafunzi wanaotahiniwa mtihani wa fasihi ya Kiswahili.

3.4.3.5 Matini za Masimilisho

Mtafiti alikusanya matini za masimilisho ya riwaya na hadithi fupi husika yaliyokuwa yameandaliwa. Masimilisho hayo ni yale yaliyokuwa yakiigizwa na vikundi hivyo. Mtafiti aliyasoma masimilisho hayo huku akiyalinganisha na matini chasili ili kubaini mbinu na matatizo yaliyodhihirishwa na utaratibu wa kusimilisha kazi za kinathari. Pia, masimilisho hayo yalilinganishwa na maigizo yake katika jaribio la kutaka kutambua iwapo waigizaji waliyazingatia jukwaani walipokuwa wakiyaigiza.

3.4.3.6 Uchunzaji na Utazamaji

Mbinu ya uchunzaji wa kutoshiriki ilitumiwa na mtafiti alipoyatembelea maigizo hayo ili kubaini jinsi uigizaji ulivyofanywa, kunasa, na kunakili data muhimu. Mtafiti alinunua na kutazama video ya riwaya ya *Siku Njema* iliyokuwa imeandaliwa na K.I.C.D. Aidha, alizikusanya video za diwani ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* na kuzitazama.

3.5 Uchanganuzi wa Data

Data iliyokusanywa nyanjani na maktabani ilichanganuliwa kwa misingi ya maswali, malengo, na nadharia za utafiti. Kiini cha uchanganuzi huu kilikuwa kubaini mbinu za usimilisho wa tungo za kinathari, matatizo yanayotinga ufanisi wa kusimilisha, na jinsi ya kuyatatua matatizo hayo. Misingi ya nadharia changamano ilitumika kufafanua mbinu na matatizo ya usimilisho. Fauka ya haya, nadharia changamano ilielekeza namna mbalimbali za kuyatatua matatizo yaliyobainika katika mchakato wa kusimilisha.

Uchanganuzi wa data ulifanywa kwa awamu mbalimbali. Kwanza, data iliyokusanywa maktabani ilisomwa kwa makini na kuchanganuliwa. Data hiyo ilihusisha riwaya na hadithi fupi teule. Awamu ya pili ilihusu uchanganuzi wa data iliyokusanywa nyanjani. Katika uchanganuzi mtafiti alizitazama video zilizonaswa katika maigizo pamoja na zile zilizokusanywa kutoka vikundi mbalimbali. Hojaji na data iliyonakiliwa nyanjani zilisomwa na hoja zake

muhimu kupangwa kwa mujibu wa maswali na vigezo vya uainishaji. Aidha, mtafiti aliyasoma na kuyachanganua masimilisho ya riwaya na hadithi fupi.

Baada ya utazamaji na usomaji huo, yaliyomo katika masimilisho na maigizo yalilinganishwa na yaliyomo katika matini chasili za riwaya na hadithi fupi teule. Kiini cha kufanya hivyo kilikuwa kubaini mbinu zilizotumika kusimilisha yaliyomo katika matini chasili kuwa matini ya kidrama na kisha namna matini ya kidrama ilivyowekwa jukwaani na kuigizwa. Matatizo yaliyotokea katika ugeuzaji wa matini moja kwenda matini ile nyingine yalibainishwa. Mtafiti aliziainisha mbinu kwa kuzingatia hatua mbili za usimilisho wa tungo za kinathari. Hatua moja ikihusu ugeuzaji wa matini ya kinathari kuwa matini ya kidrama, na nyingine ikiwa ni uwasilishaji wa matini ya kidrama jukwaani. Matatizo yaliyotambuliwa katika hatua hizo yalibainishwa na kuorodheshwa.

Data iliyopatikana kutokana na uchanganuzi wa mbinu na matatizo ya mchakato wa usimilisho ilifafanuliwa kimaelezo. Mawazo ya kinadharia yaliyokuwa yamekusanywa maktabani na mtandaoni yalitumiwa katika uelezaji wa matokeo ya uchanganuzi huo.

Uchanganuzi wa data kutoka kwa hojaji ulifanywa kwa mbinu ya kijarabati. Data kutoka kwa hojaji ilipangwa kulingana na maswali mbalimbali yaliyoulizwa na kisha ikachanganuliwa kwa takwimu za kueleza idadi marudio na asilimia. Uchanganuzi huo ulitekelezwa kwa kutumia programu ya tarakilishi ya SPSS. Data iliyochanganuliwa kijarabati ilihusu matatizo ya usimilisho yaliyobainishwa na wasimilishaji na walimu, njia za kuyatatua, na tathmini za makundi hayo mawili kuhusu usimilisho wa kazi za kinathari zinazotahiniwa.

3.6 Uwasilishaji wa Data

Data iliwasilishwa kwa njia ya kimaelezo na kijarabati. Njia ya kimaelezo ilitumika kuwasilisha mbinu zinazotumika kusimilisha tungo za kinathari na matatizo yanayouzingira mchakato wa usimilisho. Mbinu za kijarabati za uwasilishaji data zilizotumiwa ni kama vile majedwali na takwimu. Mtafiti alizitumia mbinu za kijarabati za uwasilishaji wa data ili kuwasilisha matatizo ya usimilisho yaliyotambuliwa na walimu na wasimilishaji, pamoja na maoni yao kuhusu usimilisho wa vitabu viteule vinavyotahiniwa.

3.7 Kiishilio

Sura ya tatu imeshughulikia mbinu za utafiti. Vipengele ambavyo vimefafanuliwa ni mbinu changamano za utafiti, mahala pa utafiti, uteuzi wa sampuli, na ukusanyaji, uwasilishaji na uchanganuzi wa data. Sura imefafanua vipengele hivyo kwa kuzingatia ufaafu wake katika kutathmini usimilisho wa riwaya na hadithi fupi zinazotahiniwa katika shule za sekondari nchini Kenya.

SURA YA NNE
DHANA, SABABU ZA KUSIMILISHA NA HISTORIA YA
USIMILISHO

4.0 Utangulizi

Sura iliyotangulia imeshughulikia mbinu za utafiti. Sura hiyo imefafanua muundo wa utafiti, mbinu changamano za utafiti, mahala pa utafiti, uteuzi wa sampuli, na ukusanyaji, uwasilishaji na uchanganuzi wa data. Sura ya nne ni mjadala kuhusu mitazamo mbalimbali katika fasiri ya dhana ya usimilisho kwenye muktadha wa kusimilisha na fasihi. Namna usimilisho unavyofasiriwa inaathiri mbinu zinazotumiwa, na kutegemea mtazamo uliotumika usimilisho unaweza kuhukumiwa kama uliofaulu ama kupungukiwa. Aidha, mjadala huu umepiga hatua katika kuchunguza na kueleza sababu zinazopelekea kusimilishwa kwa kazi za fasihi na historia ya usimilisho ulimwenguni. Katika historia ya fasihi ulimwenguni, usimilisho umeweza kuibua sura mbalimbali kutegemea miktadha ya utunzi na kipindi cha wakati. Usimilisho wa riwaya na hadithi fupi kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Kenya ni maendeleo katika usimilisho ulimwenguni.

4.1 Dhana ya Usimilisho

Ingawa fani ya usimilisho wa tungo za fasihi ina historia ndefu ulimwenguni, dhana ya usimilisho imekuwa ikialika fasiri mbalimbali kutegemea kinachosimilishwa, matokeo yake na mchakato husika. Hii ni dhana changamano

na yenye fasiri tata. Hutcheon (2012), anasema kuwa, utata huo unatokana na upana wa kimatumizi wa neno usimilisho. Neno hili limekuwa likitumika kurejelea mambo mawili tofauti: mchakato husika na matokeo yake.

Dhana ya usimilisho hudhihirika katika sura mbalimbali ambazo husaidia kuifasiri. Sura hizo zinazalika kutokana na mitazamo mbalimbali ya kinadharia inayoibuka katika jaribio la kueleza dhana hii. Kuna mikabala minne muhimu ambayo inaweza kusaidia kufasiri dhana ya usimilisho. Mikabala hiyo inafumbata dhana mbili zinazoibuliwa na usimilisho za ‘mchakato’ na ‘matokeo’. Katika sehemu inayofuata mikabala hiyo imejadiliwa, mmoja baada ya mwingine.

4.1.1 Usimilisho kama Tafsiri

Mkabala unaoutazama usimilisho kama tafsiri una usuli wake katika maoni ya Roman Jakobson ya mwaka wa 1963. Kulingana na Lhermitte (2005), Jakobson aliushughulikia usimilisho kama tafsiri baina ya mifumo ya sauti (intersemiotic translation). Tafsiri ya aina hiyo huhusu ubadilishaji wa mfumo fulani wa sauti kwa umbo lingine tofauti. Hali ya kuigeuza matini ya fasihi kuwa opera, muziki, mchoro wa rangi au hata filamu huchukuliwa kama tafsiri baina ya mifumo ya sauti. Kama anavyoeleza Lhermitte (2005), dhana ya usimilisho ilitumika mara ya kwanza kurejelea aina fulani ya tafsiri kabla ya kuanza kutumika kutaja ugeuzaji wa tungo za fasihi kuwa filamu (au tungo nyinginezo).

Maoni kama hayo yanafafanuliwa na Dean (2009), anayesema kuwa, usimilisho kwa kawaida ni tafsiri katika njia tofauti za mawasiliano na hujibainisha kupitia matumizi tofauti ya mbinu, malighafi muhimu, na kanuni za ubunifu. Ingawa fasiri ya Dean inahusu zaidi usimilisho wa tungo za fasihi kugeuzwa filamu,

mtazamo wake kuhusu fasiri ya dhana hii unajibainisha wazi. Kwa namna hiyo, dhana ya usimilisho inaweza kufasiriwa kama uhamishaji wa ujumbe kutoka njia moja ya mawasiliano kwenda njia nyingine tofauti.

Usimilisho na tafsiri ni dhana mbili zinazohusiana kimalengo na kidhima. Fani hizo mbili hulenga uhamishaji wa ujumbe kutoka matini moja hadi nyingine kwa namna ambavyo uasilia wake utadumishwa. Aidha, mchakato wa kutafsiri na kusimilisha hutokelezwa kwa namna inayohusiana sana. Hata hivyo, baadhi ya waandishi kama Lhermitte (2005) wana mtazamo kwamba usimilisho na tafsiri ni maumbo duni kwani hayawezi kuwasilisha ujumbe kama ulivyodhamiriwa kwa ukamilifu wake. Suala hili la uaminifu ama usahihi kwa matini chasili katika usimilisho limejadiliwa na waandishi wengi. Mtazamo wa utafiti huu umepingana na maoni hayo, kwani umebainisha misingi inayoweza kufuatwa kuafikia similisho lenye hadhi sawa na matini chasili.

Ingawa mkabala huu hutazama usimilisho kama tafsiri, kuna baadhi ya waandishi wanaopinga kuwapo na uhusiano wa kimalengo na kidhima kati ya fani ya usimilisho na tafsiri. Kati yao ni Graham (2006), anayesema kuwa hamna mkinzano wowote baina ya tafsiri na usimilisho kwa ambavyo fani zote mbili hutokeleza dhima tofauti. Mwandishi huyo anaishadidia hoja yake kwa kumrejelea Jean-Paul Sartre. Sartre analizungumzia similisho lake 'Trojan Women' alilolisimilisha kutoka kazi ya Mgiriki Euripides. Kulingana na Sartre, ilimbidi kuisimilisha kazi hiyo ili kuinua viwango vya upokezi wake, jambo ambalo halingewezekana iwapo angeitafsiri. Ni dhahiri kwamba Sartre anazifasiri dhana hizi mbili, usimilisho na tafsiri, kama tofauti kimaana, kimalengo na kidhima.

Inavyobainika ni kwamba, usimilisho unapochunguzwa kwa undani ni aina ya tafsiri. Aina hii ya tafsiri hutofautiana na aina nyingine kwa ambavyo inahusu uhamishaji wa ujumbe baina ya njia tofauti za mawasiliano. Dhima kuu ya tafsiri na usimilisho, katika muktadha huu, huwa ni mawasiliano. Katika fasihi, fani zote zinaweza kuambatana na ubunifu wa msimilishaji ama mtafsiri, ili kutekeleza lengo lake linaloweza kuwa tofauti na lile la mwandishi asilia wa matini. Usimilisho uliojadiliwa na tasnifu hii ulidhamiriwa kutekeleza malengo na dhima sawa na ile ya utungo uliosimilishwa.

4.1.2 Usimilisho kama Mwingiliano wa Matini

Baadhi ya waandishi wameufafanua mchakato wa usimilisho na matokeo yake kama mwingiliano wa matini mbalimbali. D'Angelo (2010) anasema kuwa, kila matini huhusiana na matini nyingine kwa njia ya urejeleaji, unukuzi, ukopaji, usimilisho, udokezi, uigaji wa kubeza (parodia), uigaji na njia nyinginezo. Mwandishi huyu anahoji kuwa usimilisho ni aina ya mwingiliano matini. Maoni yake yanatokana na kauli ya muasisi wa nadharia ya mwingiliano matini, Kristeva, aliyesema kuwa matini yoyote huundwa kama picha ya urejeleaji na, ni ufyonzaji na ugeuzaji wa matini nyingine.

Hayo ndiyo mawazo ya Dean (2009), anayeeleza kuwa, hadithi huibuka katika jamii, na kizazi cha wakati fulani cha jamii hiyo huzibadilisha hadithi za jadi ili ziweze kuafikiana na wakati uliopo, mazingira mapya, na mahitaji ya wakati huo pamoja na njia zake za uwasilishaji. Dean anamrejelea mtunzi maarufu wa drama, Mgiriki Aeschylus aliyesema hivi:

Michezo yangu ya kuigiza ni vipande vya mashairi ya Homer nilivyovikata na kuviunganisha. (T. Y) Dean (2009:1)

Kwa hivyo, Dean anauchukilia usimilisho kama mwingiliano matini wenye dhima ya kuzifanya mpya hadithi za jadi. Maoni kama hayo yalitolewa na Chan (2004), aliyehoji kuwa, usimilisho huhusisha uhamishaji wa vipengele vya matini chasili lakini huiweka matini ya similisho katika muktadha mpya wa kuifasiri. Kwa hivyo, matini ya similisho huchanganya chembe chembe za matini chasili na matini nyingine zinazopatikana katika muktadha wa matini lengwa.

Bluestone (1954) ni miongoni mwa wahakiki wa kwanza kuuzungumzia usimilisho kama mwingiliano wa matini. Mwandishi huyu aliuona utanzu wa riwaya kama mnyumbufu na ambao husimilisha makala, nyaraka, kumbukumbu, historia, dini, manifesto, ngano, tamthilia na mengineyo. Kulingana naye, mwingiliano wa matini katika tanzu za fasihi ni usimilisho wa aina yake. Katika hali hiyo, sifa za matini fulani hufinyangwa ili kuiwezesha kuingiliana na sifa za matini nyingine.

Dhana ya usimilisho kama mwingiliano wa matini pia imezungumziwa na Hutcheon (2013) katika jaribio lake la kuelezea nadharia ya usimilisho. Kwa mujibu wa Hutcheon (2013) usimilisho unapotazamwa kwa mkabala wa mchakato wa upokezi, ni aina ya mwingiliano matini. Masimilisho hupokelewa kama ufufuo wa tungo ambao husheheni tofauti. Katika msingi huu tunaweza kusema kuwa, watazamaji au wasomaji huzipokea kazi zilizosimilishwa kama zinazosemezana na matini nyingine katika mpito wa wakati. Fasiri yetu inaenda sambamba na maana ya mwingiliano matini anayotoa Hutcheon kuwa ni uhusiano wa semi katika matini za fasihi.

Ingawa usimilisho unaweza kutazamwa kama matokeo ya mwingiliano matini, kimatumizi dhana hizi mbili zinaweza kutofautiana. Kulingana na Oloruntoba-

Oju (2009), tafsiri ama similisho za tungo za kirasimi ambazo zimeibuka katika muktadha wa Kiafrika, zinafaa kurejelewa kama mwingiliano matini badala ya kutumia dhana za tafsiri na similisho. Kama anavyoelezea, tungo hizo huvyazwa na vichangizi mbalimbali katika muktadha wa Kiafrika, ambavyo ni tofauti na vile vilivyozalisha tungo asilia. Baadhi ya tungo za kirasimi anazorejelea ni tamthilia ya Sophocle, *Oedipus*, na ile ya John Gay, *The Beggar's Opera*. Wasimilishaji wa tamthilia hizo Soyinka, Sofola na Rotimi, wote kutoka Nigeria, walibuni matini mpya zilizokengeuka kutoka matini asilia za Kimagharibi. Ukengeushi huo kutoka matini asilia unadhihirika katika viwango vya maudhui, lugha, na uigizaji.

Mathalan, Wole Soyinka aliisimilisha tamthilia ya *The Beggar's Opera* na kuipa anwani *Opera Wonyosi*. Soyinka katika tamthilia yake anapigia tashtiti jamii za Kiafrika ambazo baada ya uhuru kutoka kwa wakoloni zilienzi maovu kama uimla na mapinduzi ya serikali ambayo yalileta umwagikaji wa damu. Inavyobainika ni kuwa, wasimilishaji hawa wa tungo za Kimagharibi iliwabidi kuzikengeusha tungo hizo ili ziwiane na maudhui yaliyojikita katika muktadha wao. Mwingiliano huo wa matini za Kiafrika na zile za Kimagharibi ndio kiini cha maoni ya mwandishi huyu kwamba tungo hizo zinaafiki zaidi kuonekana kama mwingiliano wa matini, wala sio similisho ama tafsiri.

Kama inavyobainika, usimilisho wa kazi za fasihi hufanyika katika miktadha mahsusi. Wasimilishaji huongozwa na muktadha wa matini lengwa katika jaribio lao la kuisimilisha matini ya fasihi. Katika msingi huu, inawezekana wakaisilimisha matini chasili kwa namna ambayo itaweza kusemezana na matini nyingine katika muktadha lengwa, ambazo zinafahamika na hupokelewa vizuri na hadhira. Katika jaribio la kuisilimisha matini kwa muktadha fulani wa

upokezi, mwingiliano wa matini ni hali isiyoweza kuepukika. Kutokana na hali hiyo, baadhi ya waandishi wanaoshughulikia fani ya usimilisho wamekuwa wakiuchunguza mchakato na matokeo yake kama mwingiliano matini. Hata hivyo, baadhi ya tungo, kama ilivyodhihirika, huonyesha mwingiliano matini wa kiwango cha juu kuliko nyingine.

Hali ya mwingiliano matini katika usimilisho wa riwaya na hadithi fupi iliweza kudhihirika. Baadhi ya masimilisho yaliyoigizwa yalijumuisha nyimbo maarufu na semi za kisiasa zilizopatikana katika miktadha lengwa. Hii ina maana kuwa usimilisho huu unaweza vilevile kuangaziwa kama mwingiliano wa matini.

4.1.3 Usimilisho kama Mwingiliano wa Njia za Mawasiliano

Wolf (1999) anaeleza mwingiliano wa njia za mawasiliano kama kushiriki kwa njia zaidi ya moja za mawasiliano katika uashiraji wa dhana fulani. Katika hali hiyo, njia mbalimbali za mawasiliano zinaweza kutumika pamoja katika uwasilishaji wa ujumbe. Mwingiliano wa njia za mawasiliano hushughulikiwa na waandishi wa taaluma za mawasiliano, fasihi, na hata filamu kama mwendelezo wa nadharia ya mwingiliano matini. Jinsi ambavyo matini ama semi huingiliana, hivyo ndivyo njia za mawasiliano zinavyoweza kuingiliana na kuathiriana.

Dhana ya mwingiliano wa njia za mawasiliano katika fasihi ni kongwe, ingawa matumizi ya istilahi ‘mwingiliano wa njia za mawasiliano’ imechipuka mwishoni mwa karne ya ishirini. Muller (1998) anahoji kuwa, dhana hii inapatikana katika mawazo ya Aristotle kuhusiana na dhana aliyoielezea ya ‘*ut pictura poesis*’ katika kitabu chake *Poetics*. Dhana ya Kilatini ‘*ut pictura poesis*’ ilitumika kwa maana ‘*kama ulivyo uchoraji, ndivyo pia ulivyo ushairi (T.Y.)*’. Mawazo hayo ya ‘*ut pictura poesis*’ yaliendelezwa pia na Horace katika kitabu chake cha *Ars*

Poetica. Aristotlele na Horace walinuia kuonyesha uhusiano uliopo baina ya ushairi na uchoraji. Sanaa ya ushairi na ya uchoraji, wakati huo, ilijengeka zaidi katika uigaji wa maumbile na pia tungo za fasihi za kirasimi. Kama inavyobainika, mwingiliano wa njia za mawasiliano unaohusisha tungo za fasihi una historia ndefu.

Kuhusiana na ukale huo Wolf (1999) anaonelea kuwa, uigizaji wa jukwaani (drama) na opera, kimsingi hudhihirisha matumizi ya njia tofauti za mawasiliano ambazo huingiliana. Drama inafumbata matumizi ya maneno, matendo, ishara, michoro, maleba, uangazaji na njia nyinginezo ambazo hutumika ili kuipitisha ujumbe. Fasihi huhusiana na njia nyingine za mawasiliano kama vile uchoraji, filamu na muziki. Matini ya fasihi inaweza kupatikana katika filamu na ile ya filamu ikapatikana katika ile ya fasihi. Vivyo hivyo, mwingiliano huu unaweza kuhusisha uchoraji na fasihi sawa na fasihi na muziki.

Punzi (2007) anafafanua dhana ya mwingiliano wa njia za mawasiliano kama hali ya ujumbe kuvuka mipaka inayotenga njia za mawasiliano. Katika mwingiliano wa njia za mawasiliano, kazi ya fasihi huwa katika hali ya mpito, yaani kazi hiyo huendelea kutafsiriwa kutoka njia moja ya mawasiliano kwenda nyingine. Kwa hivyo, kazi hiyo ya fasihi huishia kuwa na sura nyingi zinazoibainisha. Punzi anakiri kwamba hali ya kuvuka mipaka ya njia za mawasiliano, sawa na mipaka ya tanzu, ni jambo ambalo limekuwa likifanyika katika fasihi kwa muda mrefu.

Kama inavyobainika, mwingiliano wa njia za mawasiliano hurejelea hali ya kuigeuza matini ya fasihi kuwa umbo la kisanaa katika njia nyingine ya mawasiliano. Hata hivyo, mchakato unaohusika katika hali hizo kimsingi ni usimilisho, ingawa Punzi (2007) anaona neno hilo likiwa finyu kimaana. Hii ni

kwa kuwa usimilisho wa kazi za fasihi kuwa filamu huangaziwa sana kwa kigezo cha usahihi kwa kazi chasili. Kwa hivyo anapendekeza kuwa, dhana ‘mwingiliano wa njia za mawasiliano’ inaweza kutumika kama kabadala mwafaka cha dhana ‘usimilisho’ na ‘tafsiri baina ya mifumo ya sauti’, kwa vile dhana hizo mbili zimeonyesha upungufu katika uelezeaji wa dhana inayohusika katika ugeuzaji wa tungo za fasihi kuwa filamu.

Kutokana na maelezo haya imebainika kuwa, usimilisho wa tungo za fasihi andishi kwa njia za mawasiliano zisizotumia maandishi kwa kawaida huhusisha mwingiliano wa njia za mawasiliano. Matini ya riwaya inaweza kujumuisha vimatini vya filamu, drama, na hata muziki, ambavyo kimsingi ni njia za mawasiliano zinazojibainisha na kujisimamia. Ugizaji wa riwaya ama hadithi fupi kama filamu au mchezo wa jukwaani hudhihirisha matumizi ya njia mbalimbali za mawasiliano ambazo huingiliana kama vile picha zitembeazo, sauti, muziki, michoro, na njia nyinginezo. Usimilisho ulioangaziwa na utafiti huu ulitazamwa kama mwingiliano wa njia za mawasiliano katika hatua ya uigizaji. Mbinu mbalimbali za kimawasiliano zilitumika kuyaigiza masimilisho kama vile sauti, maleba, mafigu, mwangaza, pazia, na rangi, miongoni mwa nyingine.

4.1.4 Usimilisho Halisi

Licha ya kwamba usimilisho unaibua sura mbalimbali zinazoelekeza fasiri yake, baadhi ya waandishi hushikilia kuwa usimilisho ni fani inayojitegemea na kujibainisha. Mathalan, Hutcheon (2013) anaifasiri dhana hii ifuatavyo:

Usimilisho ni unyambulishaji ambao si wa hadhi duni, ni kazi ya pili (inayofuata) ambayo siyo ya daraja la pili (hafifu). Ni kazi yenye upekee wake. (T.Y.)

Kutokana na kauli hii ya Hutcheon, inabainika dhahiri kuwa anaangazia usimilisho kama fani ya kisanaa ambayo ni zao la kiubunifu linalofaa kuchunguzwa kwa utoshelevu wake pasipo na kulilinganisha na matini inayolizalisha.

Usimilisho unafaa kuangaziwa kama usanii unaofumbata ubunaji wa msanii pamoja na kuendeleza dhamira yake kuu kwa hadhira. Dhamira hiyo ya msimilishaji inaweza kwenda sambamba na ile ya mtunzi wa matini chasili, ingawa hamna hatia ya kisanaa iwapo msimilishaji atakaidi.

D'Angelo (2010) anashikilia mtazamo kuwa usimilisho ni fani yenye upekee wake ambayo hujibainisha kifani na kidhamira. Anaeleza kuwa, usimilisho huchukuliwa kama fasiri, mtazamo ambao ni dhahiri na asilia wa kazi ya fasihi. Hata kama usimilisho utajitokeza kama vipande vipande vya kazi fulani, huwa ni fani muhimu kwa ambavyo huweka kitabu katika mtandao wa kiubunifu na mawasiliano. D'Angelo anasema kuwa, usimilisho ukiangaziwa kama fasiri haulazimiki kuhifadhi tofauti ndogo za kitabu, ila unafaa kubakia kazi ya kisanaa inayojitegemea, yenye muwala, ubunifu dhahiri, na inayobeba maana. Hii ina maana kuwa, usimilisho hauna budi kuwa na usahihi ama uaminifu kwa mantiki inayobuniwa na mtazamo mpya katika kazi inayosimilishwa. Maoni yake yanatofautiana na ya wengi ambao wanahimiza usimilisho ufanywe kwa misingi inayohakikisha uaminifu kwa matini chasili. Kauli yake inawiana na ya Tomasulo (1997) anayehoji kuwa, usimilisho wa tungo za kifasihi, hasa wa kifilamu, haufai kuangaziwa kwa msingi wa usahihi ama uaminifu kwa matini chasili, bali unaweza kuangaziwa kwa ulinganifu wa maana ya vipengele husika. Mwandishi huyu anairejelea kauli ya mchanganuzi wa usimilisho McFarlane aliyesema kuwa:

Mjadala kuhusu usimilisho umezongwa na suala kuu la uaminifu ama usahihi (kwa matini asilia). (T.Y)

Ni maoni ya wachanganuzi wengi kwamba usimilisho unafaa kushughulikiwa pasipo na kuutathmini kwa jicho la uaminifu. Mchanganuzi Carroll (2006) anasema kuwa, usimilisho hudhihirisha hali ya kutaka kurejelea matini chasili na kwa namna hiyo huonyesha dalili za kurudia. Hata hivyo, usimilisho hata kama umefanywa kwa dhamira ya kuonyesha uaminifu kwa matini chasili, bado hubakia kuwa fasiri ya matini hiyo. Kwa hivyo, Carroll (2006) anadai kwamba, kila usimilisho ni mfano wa ukiushi wa uaminifu ama usahihi wa matini.

Kama inavyobainika, fasiri ya dhana ya usimilisho inafaa kutokana na upekee wa fani yenyewe pasipo na kujumuisha mambo mengine kutoka nje yake. Hii ni kwa sababu kuwa, lengo la msimilishaji linaweza likawa tofauti na lengo la mtunzi wa matini inayosimilishwa. Usimilisho unaweza kutazamwa kama ufasiri wa matini fulani ya fasihi ambapo tofauti zinaweza kujiri kulingana na jinsi ufasiri wenyewe ulivyotekelezwa. Kama msanii, msimilishaji ana uhuru wa kuingiza mtindo wake katika uwasilishaji wa similisho lake. Ni nadra msimilishaji kufaulu kuuwasilisha mtindo wa mwandishi kama ulivyo, hasa iwapo wawili hawa wanatoka tamaduni tofauti za jamii. Hali hiyo ya kuwepo na ugumu katika uwasilishaji wa similisho aminifu ndiyo inayopelekea wachanganuzi wengi wa usimilisho kuhimiza usimilisho uangaziwe kama kazi ya sanaa inayojitegemea na kujibainisha. Iwapo usimilisho utaangaziwa kwa 'heshima' yake unayostahiki, basi fikira za kuuona kama 'usaliti', 'ukiushi', 'maumbo duni', na 'uigaji' zitakoma. Kazi iliyosimilishwa inaweza kuangaziwa kama kazi nyingine ya kisanaa.

Hata hivyo, mtazamo wa kuuchunguza usimilisho kama uzalishaji wa kazi mpya ya kisanaa ulitofautiana na mtazamo ambao ulizingatiwa katika utafiti huu. Usimilisho haufanywi kila mara kwa dhamira moja pekee. Utafiti huu ulichunguza usimilisho uliodhamiriwa kuifasiri matini chasili kwa namna ilivyodhamiriwa walengwa wake na mwandishi. Kwa hivyo, ubunifu wa msimilishaji katika usimilisho wa jinsi hiyo ulichukua nafasi ya chini sana. Nafasi kuu katika usimilisho huu ilipewa uwasilishaji wa maudhi na fani katika sifa za kimuundo za matini lengwa.

4.2 Sababu za Kusimilisha Matini za Fasihi

Shughuli ya kusimilisha kazi za fasihi hufanywa kwa sababu mahsuszi zinazojulikana. Ingawa wasimilishaji hawaandiki msukumo uliowafanya kuzisimilisha matini fulani, wachanganuzi wa usimilisho wamejaribu kuelezea baadhi ya sababu hizo. Kutokana na uelezaji huo, imebainika kuwa, sababu za kusimilisha hutofautiana kutoka msimilishaji mmoja kwenda mwingine.

Usimilisho umekuwa ukifanywa kwa sababu za kitamaduni. Kila jamii huwa na kaida, thamani na amali, ambazo huhitaji kupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine ili kuendeleza utangamano na umoja wa jamii. Wasimilishaji wanaweza kuwa na madhumuni ya kuzisimilisha tungo zenye ukwasi wa vito hivyo vya utamaduni wa jamii, ili ziweze kuwanufaisha wanajamii kupitia njia tofauti. Katika utamaduni wa Wagiriki, baadhi ya tungo za kirasimi kama michezo ya kuigiza na mashairi zilisimilishwa kutoka kwa visasili, mighani na tanzu nyingine za fasihi simulizi ya jamii hiyo. Usimilisho huo wa Wagiriki ulifanywa kwa madhumuni ya kuwasilisha tungo maarufu za kitamaduni, ambazo ziliweza kutoa majibu kuhusu mambo mengi ambayo yalikuwa yakiisumbua jamii kuyatambua.

Kwa mfano, wasanii wengi wa Kigiriki walikisimilisha kisasili cha *Mfalme Edipode* kama hadithi, tamthilia, na hata ushairi. Kulingana na Edmunds (2006), kisasili cha *Mfalme Edipode* kilikuwa kikisimuliwa katika tanzu mbalimbali za fasihi simulizi katika karne ya tano (K.Y.M). Usimilisho wa kisasili hicho uliweza kugubika uasilia wake na kuibua mitindo yake mbalimbali. Kisa cha Edipode kilipata umaarufu mwingi duniani baada ya kusimilishwa katika tamthilia tatu za tanzia na Sophocles. Hizi ni *Oedipus the King*, *Oedipus at Colonus* na *Antigone*. Washairi maarufu wa Kigiriki kama Homer, Hesiod, Pindar, Aeschylus na Euripides, pia walikirejelea kisasili hicho katika mashairi.

Kisasili cha Edipode na tungo nyinginezo katika utamaduni wa Wagiriki, zilisimilishwa kupitisha maudhui yaliyokuwa yakienziwa katika utamaduni wa jamii hiyo. Aidha, tungo hizo zilichukuliwa na baadhi ya waandishi kama vielelezo bora vya utunzi katika utamaduni wao. Jambo hili linathibitishwa na hali ya wasimilishaji kujaribu wawezavyo kuvisimulia visa hivyo kwa usahihi kama vilivyopatikana katika tamaduni zao. Hata hivyo, mitindo ya waandishi ilitofautiana kutokana na fasiri, kumbukumbu, na ubunifu wao.

Usimilisho kwa dhima ya kuendeleza utamaduni wa jamii umejadiliwa vilevile na Hutcheon (2013). Mwandishi huyu anasema kuwa usimilisho wa riwaya katika runinga za Uingereza katika karne ya kumi na nane na kumi na tisa ulitegemea sana umaarufu wa kitamaduni wa riwaya hizo. Riwaya nyingi zilizosimilishwa ni zile za kirasimi zilizokuwa zimeenziwa zaidi katika utamaduni wake. Kwa ambavyo riwaya hizo zilichukuliwa kama mizani bora ya utunzi katika fasihi, wasimilishaji walidhamiria masimilisho yao yawe vimelea katika umaarufu huo.

Katika fasihi ya Kiswahili, usimilisho umefanywa kwa madhumuni ya kueneza tungo maarufu na kupitisha thamani muhimu za kitamaduni. Kwa mfano, utendi wa *Fumo Liyongo* katika jamii ya Waswahili umesimilishwa kama tamthilia. Awali, utendi huo ulisimuliwa kabla ya kuwekwa katika maandishi. Haya ni kwa mujibu wa tafiti mbalimbali. Hali ya kuutoa katika usimulizi na kuuweka katika maandishi ni usimilisho wa aina yake, kwa sababu unahusisha maamuzi kuhusu namna vipengele muhimu vya usimulizi vitakavyowasilishwa kimaandishi.

Utendi wa Fumo Liyongo ni maarufu sana katika fasihi ya Kiswahili; andishi na simulizi. Katika fasihi ya sasa utendi huo umesimilishwa kama mchezo wa kuigiza. Tamthilia ya *Kifo Kisimani* ni usimilisho uliokengeuka wa utendi wa *Fumo Liyongo*. Kisa kinachoigizwa kumhusu mhusika mkuu Mwelusi anayeshukiwa kuwa mchochezi wa umma dhidi ya utawala wa Mtemi Bokono, kinalandana na mkasa uliomfika Fumo Liyongo. Watawala Sultani Daudi Mringwari wa Pate na Mtemi Bokono wa Butangi wamesawiriwa kwa sifa zenye ukuruba sana. Daudi na Bokono wanatawala kwa hofu ya kupokonywa mamlaka yao. Hasimu wa Daudi ni Fumo Liyongo, huku Mwelusi akiwa adui mkuu wa Mtemi Bokono. Fumo Liyongo na Mwelusi wanapitia masaibu yanayofanana. Tanzania inayowakumba wawili hawa inafanana zaidi, kwani wote wanakufa kwa kusalitiwa na jamaa zao.

Mwandishi wa *Kifo Kisimani*, Kithaka Mberia, kwa makusudi ama pasipo kudhamiria, aliufanyia utendi huo usimilisho katika muktadha tofauti wa kitamaduni. Jamii ya Waswahili iliuenzi utendi huo kwa kuwa uliyasawiri mazingira yao na kupitisha maudhui yaliyotokana na utamaduni wao. Jamii inayolengwa na Kithaka Mberia ni pana mno na yenye tamaduni zinazotofautiana. Aidha, wakati katika muktadha wa kitamaduni umebadilika na

kupisha asasi mbalimbali za kijamii ambazo zilikosekana wakati wa kubuniwa kwa utendi huo. Huenda mwandishi wa *Kifo Kisimani* alidhamiria kuusimilisha utendi huo ili upate kueleweka na wasomaji wa tamaduni tofauti.

Kazi za fasihi huvyazwa na miktadha tofauti ya kitamaduni. Baadhi ya elementi za kitamaduni katika jamii za ulimwengu zimepata kukubalika na walimwengu, huku nyingine ikiwa ni vigumu kukubalika na wote. Hutcheon (2013) anaeleza kuwa, usimilisho unaweza ukafanywa kwa nia ya kushirikisha ama kuepusha kazi fulani ya fasihi katika au kutoka uhakiki wa kitamaduni. Kulingana naye, wasimilishaji wengi wa kifeministi, wanaopinga ushoga na vita, wameutumia usimilisho kueneza sera zao, hasa katika usimilisho unaoigizwa kwenye filamu. Kwa namna hiyo, usimilisho hutekelezwa ili kutimiza malengo mahsusi ya kitamaduni.

Katika usimilisho wa kazi za fasihi ya Kiswahili, usimilisho wa aina hiyo umeshuhudiwa. Mithalan, mtunzi Julius Nyerere aliisimilisha tamthilia ya *Merchants of Venice* ya Shakespeare kama *Mabepari wa Venisi* (1969). Tunairejelea kazi hiyo ya Nyerere kama similisho wala siyo tafsiri kwa sababu ilikengeuka zaidi kutoka kazi asilia na kuingiza dhamira mpya ya mtafsiri. Katika tamthilia ya *Mabepari wa Venisi*, itikadi ya msimilishaji kuhusu mfumo wa uzalishaji mali wa ubepari inadhihirika wazi. Dhamira ya Nyerere inatofautiana na ile inayoendelezwa na Shakespeare katika kazi yake. Kwa namna hiyo, inawezekana kusema kuwa usimilisho wa Nyerere ulinuiwa kukashifu ubepari ama kuishirikisha tamthilia hiyo katika uhakiki wa kitamaduni ili kueleweka vizuri katika jamii yake.

Usimilisho unaweza kutekelezwa ili kukidhi sababu za kiuchumi. Wasimilishaji hunuia kuzisimilisha kazi zinazovuma ili similisho zao zipate umaarufu. Ni kweli kwamba kazi zinazovuma huvutia mauzo ya juu katika soko la biashara. Usimilisho unaofanywa kwa misingi hiyo unaonekana kuwa na umaarufu katika taaluma ya utengenezaji wa filamu. Watengenezaji wa filamu huvutiwa sana na riwaya na hadithi fupi zinazopendwa na wengi, kwa kuwa jambo hilo huwahakikishia utazamaji mpana. Mchanganuzi wa masuala ya usimilisho Engelstad (2012) anasema kuwa, utengenezaji wa filamu ni shughuli ghali na inayohatarisha mtaji. Kwa sababu hiyo, watayarishi wa filamu huhitaji kuigiza matini inayowahakikishia soko pana. Ingawa msukumo wa kusimilisha unaweza kutofautiana miongoni mwa wasimilishaji, haikosi kwamba kila msimilishaji hutarajia kupata pato la kiwango fulani kutokana na kazi anayosimilisha. Hii ina maana kuwa, miongoni mwa sababu nyingi zinazopelekea usimilisho wa tungo za fasihi, msukumo wa kiuchumi hupewa nafasi kuu.

Usimilisho wa riwaya na hadithi fupi ambao uliangaziwa na utafiti huu ulidhihirisha msukumo wa kiuchumi. Mahojiano na wasimilishaji yalibaini kwamba, usimilisho na uigizaji ni kazi wanayoitegemea kuwapa riziki.

Katika fasihi ya ulimwengu, usimilisho hufanywa kwa madhumuni ya kuifanya kazi fulani ya fasihi kuiangazia hadhira fulani. Vitabu vya fasihi vilivyoandikiwa hadhira ya watu wazima vimekuwa vikisimilishwa ili viweze kusomwa na hadhira ya watoto. Hadithi katika misahafu zimepata pia kusimilishwa ili ziweze kufasirika kwa uwepesi na hadhira ya watoto. Mathalan, hadithi za Biblia zimesimilishwa kama vibonzo ama michoro inayorahisisha usomaji. Pia, katika kipindi cha ukoloni, uhaba wa vitabu uliwashurutisha waandishi kuvitafsiri vitabu vya Kiingereza na Kiarabu kwa Kiswahili ili vipate kusomwa na watoto

shuleni. Kairu (2005), anatoa mifano ya vitabu vilivyotafsiriwa ili vipate kusomwa na watoto wa Kiafrika kama vile *Mashimo ya Mfalme Suleimani* tafsiri ya *King Solomon's Mines* (Rider Haggard) na *Safari za Guliva* tafsiri ya *Gulliver's Travels* (Jonathan Swift). Kitabu cha *Alfu Lela Ulela* kilitafsiriwa kutoka lugha ya Kiarabu. Kulingana na Mpesha (1995), baadhi ya mashairi ya kikoloni yaliyokuwa yakikaririwa na watoto shuleni, yalikuwa yamefanyiwa mabadiliko katika vipengele vya wahusika na mandhari ili kuyafanya yakubalike na watoto.

Usimilisho hufanywa ili kutimiza sababu za kibinafsi. Hutcheon (2013) anahoji kuwa, uamuzi kuhusu kazi itakayosimilishwa huwa ni uchaguzi wa kibinafsi wa msimilishaji. Wasimilishaji, mbali na kuifasiri matini ya fasihi, huchukua msimamo fulani kuihusu. Msimamo unaochukuliwa na msimilishaji fulani ni wa kibinafsi kutegemea kile anapendelea hadhira yake inufaike nacho kutokana na kazi anayoisimilisha. Hali ya msimilishaji kuwa na msimamo wake kuhusu masuala yanayowasilishwa na mwandishi wa matini chasili, ni sababu mojawapo ya kuwepo na fasiri mbalimbali katika usimilisho wa matini moja ya fasihi. Maamuzi mengi yanayofanywa na msimilishaji ni ya kibinafsi na hutegemea kiwango chake cha ubunifu na uwezo wa kuifasiri matini ya fasihi.

Usimilisho umefanywa kama jaribio la kufufua kazi maarufu za fasihi. Katika fasihi ya Kiswahili, tungo mbalimbali za fasihi simulizi zimetwa kwenye maandishi. Hali ya kuhamisha matini ya fasihi simulizi kwa fasihi andishi ni usimilisho unaohusisha uhamishaji wa baadhi ya sifa za kisimulizi kwa sauti zilizoandikwa. Ishara tamkwa na vitendo, hubadilishwa na kuwasilishwa kwa maneno yaliyoandikwa. Kwa mfano, *Utendi wa Fumo Liyongo* ambao awali ulipatikana katika masimulizi, kama wasemevyo wahakiki wengi wa ushairi wa

Kiswahili, kabla ya kuandikwa na Mohamed Kijumwa mwaka wa 1913. Hali kadhalika, kuna *Utenzi wa Sundiata*, utenzi uliokuwako katika masimulizi ya jamii ya Wandinga katika nchi ya Mali kabla ya kuvumbuliwa kwa maandishi. Kulingana na Wamitila (2003), utendi huo unaifumbata historia ya jamii hiyo na una masimulio tofauti tofauti.

Sababu ya kuzisimilisha tungo kwa dhamira ya kuzifufua inaingiliana na sababu nyingine za kusimilisha ambazo zimekwisha kuzungumziwa katika sehemu hii. Ufufuaji huu unaweza ukawa kwa misingi ya kitamaduni, kisiasa, kisanaa na hata kiuchumi. Mara nyingi kazi za fasihi zinazofufuliwa husheheni mabadiliko katika vipengele vya fani na maudhui.

Mbali na sababu za kijamii na kiutamaduni, usimilisho umekuwa ukifanywa kwa misingi ya kisiasa. Hutcheon (2013) anahoji kuwa, wasimilishaji huongozwa na misukumo kadha wa kadha ya kisiasa kabla ya kuafikia kufanya usimilisho. Mathalan, watunzi wa drama za baada ya ukoloni na wanaopinga vita, wamekuwa wakitumia usimilisho kuwasilisha mitazamo yao ya kisiasa. Mwandishi huyu anadai kuwa, iwapo msimilishaji atakosa msukumo fulani wa kuisimilisha riwaya ama hadithi fupi fulani, huenda drama inayobuniwa iathirike pakubwa.

Usimilisho unaofanywa kwa misingi ya kisiasa umeshuhudiwa katika fasihi ya Kiswahili. Mtunzi Julius Nyerere aliisimilisha tamthilia ya *Merchants of Venice* ya Shakespeare kama *Mabepari wa Venisi (1969)*. Usimilisho huu ulifanywa ili kuuwasilisha mtazamo wa mtafsiri kuhusu ubepari ambao anausuta na kuukashifu. Kithaka wa Mberia katika utunzi wa tamthilia ya *Kifo Kisimani (2001)*, amedhihirisha taswira za usimilisho kwa malengo ya kisiasa kwa

kiwango kikubwa. Tamthilia hiyo inamuumba upya jagina Fumo Liyongo na kumfanya kuwa mwanasiasa (Mwelusi) anayetetea haki za wanyonge katika jamii. Majahili wa Fumo Liyongo wameumbwa kuwa viongozi wakandamizaji wanaowanyonya wanyonge na kuangamiza watetezi wa haki na usawa.

Aidha, tamthilia hiyo inapiga mwangwi kisa kuhusu mateso ya Yesu Kristo yanayosimuliwa katika Biblia. Utani unaofanyiwa Mwelusi na mapigo kutoka kwa makachero, yanasawiana na yale Yesu Kristo aliyopitia mbele ya askari wa Kiyahudi. Mwandishi Kithaka wa Mberia ameyapa mateso ya Yesu na kisa cha Fumo Liyongo mtazamo wa kisiasa.

Kwa muhtasari, sehemu hii imezishughulikia kwa kina sababu zinazopelekea kusimilishwa kwa kazi za fasihi. Kama ilivyobainika, usimilisho huongozwa na madhumuni mahsusi ya msimilishaji. Kuna sababu za kisanaa, kiutamaduni, kisiasa, kiuchumi, kibinafsi, na nyinginezo ambazo huwa ni msukumo katika sanaa ya kusimilisha. Hata hivyo, sababu ya kuisimilisha matini fulani ya fasihi hufahamika vizuri na msimilishaji mwenyewe.

Tungo zinazosimilishwa huteuliwa kwa uzingatifu wa vigezo fulani kama ilivyodhihirika. Kigezo cha maudhui na fani hutumika na wasimilishaji wanaosimilisha kutokana na misukumo ya kitamaduni, kisiasa na kibinafsi. Umaarufu wa utungo ni kigezo muhimu kwa wasimilishaji ambao hunuia kuteua tungo za kusimilisha kwa sababu za kiuchumi. Kama ilivyobainika, wasimilishaji hao huchagua vitabu vya fasihi ambavyo vimefanya vyema katika soko. Kigezo kingine muhimu katika uteuzi wa tungo za kusimilishwa ni kile cha usanifu. Tungo zilizosanifiwa vyema huwa mizani bora ya kuigwa na wasimilishaji. Hili hufanywa kwa nia ya kudhihirisha usanifu huo katika similisho linalozalishwa.

Utafiti huu ulidhamiria kuelezea sababu nyingine ya usimilisho, ambao hufanywa ili kuinua kiwango cha uelewa kwa wanafunzi kuhusu tungo za kinathari zinazotahiniwa katika mtihani wa kidato cha nne. Aidha, usimilisho huo hufanywa ili kuimarisha kumbukumbu zao kupitia hisi za kuona, kusikia na kushiriki katika matukio fulani ya maigizo. Mbali na sababu hizo za kiusomi, usimilisho huo hushirikisha sababu za kibinafsi na kiuchumi.

4.3 Historia ya Usimilisho

Sehemu hii imejadili historia ya usimilisho katika fasihi. Uelezaji wa historia duniani hukumbwa na changamoto zinazohusiana na ustawi wa jamii na hifadhi ya rekodi za kurejelewa. Jamii zilizostawi mapema ama zilizokuwa na nyenzo bora za kuhifadhi historia zimekuwa zikipendelewa katika usomaji ama uchunguzi wa historia. Fasihi ya Mwafrika ni moja kati ya taaluma zilizoathiriwa vibaya, kwani historia yake imekuwa ikihifadhiwa katika fasihi simulizi ya jamii na akilini mwa wanajamii. Historia hiyo imekuwa ikipitishwa kwa njia za kimasimulizi kwa muda mrefu. Hali hizo zimechangia changamoto zilizopo katika uangaziaji wa historia ya fasihi ya Mwafrika.

Wasomi wa Kimagharibi wamekuwa wakiipuuza fasihi simulizi ya Mwafrika, sawa na wanavyoipuuza historia na ustaarabu wake. Kiini chake kama ilivyotajwa, ni kule kukosekana kwa rekodi zilizohifadhiwa na zilizokuwa zimeandikwa. Mathalan, mwanafalsafa Hegel alipuuzilia mbali ustaarabu wowote uliopatikana barani Afrika kabla ya majilio ya wageni. Kwa maoni yake, Afrika halisi (sehemu ya kusini mwa jangwa la Sahara) haikuonyesha chembe chembe za historia hadi pale wageni walipoasisi ustaarabu wao katika eneo hilo.

Mulokozi (2003) ananukuu moja kati ya maandishi ya Friedrich Hegel yaliyonuiwa kuibeza historia ya Mwafrika na fasihi yake:

Afrika, tunavyoifahamu hasa, ni nafsi isiyo na Historia, ambayo haijaendelea, ambayo bado inaishi katika mazingira asilia ya kujikimu ... Historia ya Dunia imeanzia Mashariki kuelekea Magharibi, kwa vyovyote vile Ulaya ndiyo mwisho wa Historia, na Asia ndiyo mwanzo.
(Mulokozi, 2003, uk. 6)

Madai ya Hegel yalitumiwa na wengine na yakaathiri pakubwa utafiti wa fasihi na historia ya Mwafrika. Kutokana na ukosefu wa hati za maandishi, nyenzo muhimu ya kuipitisha historia ya jamii za Kiafrika ilikuwa fasihi simulizi. Kwa bahati mbaya, nyenzo hiyo ilikosa kutambuliwa na watafiti kama vile Hegel. Finnegan (1987) anaonyesha kuwa kasumba hizo za kuibeza fasihi simulizi ya Mwafrika ziliimarishwa na matumizi ya nadharia kama ile ya mageuko iliyoasisiwa na Charles Darwin. Waafrika kwa jicho la Wazungu, walionekana kama 'washenzi' waliopaswa 'kustaarabishwa'. Hali hiyo ya kuitelekeza fasihi simulizi iliathiri moja kwa moja historia ya fasihi ya Mwafrika. Hata hivyo, ni muhimu kutambua kuwa wageni hao ndio walioleta hati za maandishi na kuwezesha kuwekwa kwa rekodi muhimu za matukio.

Historia ya fasihi katika mataifa ambayo yalistawi mapema kama yale ya Kimagharibi, imehifadhiwa vyema na kuna kumbukumbu za miaka ya zamani ambazo zinaweza kurejelewa. Fasihi andishi ya Kimagharibi, hasa ya Wagiriki, inaonekana kuanza miaka ya jadi hata kabla ya kuzaliwa kwa Yesu Kristo. Trypanis (1981) anasema kuwa, mashairi ya Homer yanakisiwa kutungwa baina ya karne ya tano na ya nane kabla ya kuzaliwa kwa Kristo.

Tasnifu hii imejadili historia ya usimilisho katika muktadha wa fasihi ya Kimagharibi na ya Kiswahili. Fasihi ya Kimagharibi ni muhimu katika uchunguzi

wa historia ya usimilisho, kwani historia ya fasihi imethibitisha kuwa tungo za awali za fasihi zinapatikana miongoni mwa Wagiriki. Zaidi yake, fasihi ya Kimagharibi imeiathiri sana fasihi ya ulimwengu. Historia ya usimilisho katika fasihi ya Kiswahili ni muhimu katika utafiti huu kwani usimilisho uliochunguzwa ni sehemu yake.

4.3.1 Usimilisho katika Fasihi ya Kimagharibi

Chimbuko la usimilisho lipo katika fasihi simulizi ya ulimwengu. Hapo jadi, hata sasa, fasihi simulizi ilikuwa ikisimilishwa kupitia ufaraguzi ‘jukwaani’ na katika utunzi. Haya yalifanywa ili kuitimizia hadhira matakwa na mahitaji yake. Katika hali hiyo, fasihi simulizi ya watu wazima ilisimilishwa kwa madhumuni ya kuifanya iweze kutazamwa na kueleweka na hadhira changa katika jamii. Baadhi ya tungo maarufu za matanga zilisimilishwa na kutongolewa katika miktadha isiyo ya simanzi, nazo tungo zilizotongolewa kwenye miviga yenye furaha zikageuzwa kuwa tungo za maombolezi. Ni kweli kudai kuwa, kila muktadha wa utambaji huashiria mchakato wa usimilisho. Katika utambaji, simulizi moja linaweza kusimuliwa na watambaji tofauti katika miktadha, mitindo, na hadhira tofauti. Fani hii ya usimilisho katika fasihi simulizi inaonekana kuendelezwa, huku mbinu za kale zikibadilishwa na nafasi yake kuchukuliwa na zile za kisasa.

Huko Ugiriki, wasanii maarufu kama Euripides, Sophocles na Aeschylus, aghalabu walitunga michezo yao ya kuigiza kwa kusimilisha visasili na ngano za utamaduni wa jamii yao. Kulingana na Wiley (2002), Wagiriki katika miaka ya 400 K.Y.K waliyaigiza matatizo yaliyotokana na utamaduni wao jukwaani na kulifanya jukwaa kama ‘dhabahu’ la kutakasia kasoro za mila na itikadi. Majumba ya thieta yalikuwa kama sehemu ya utamaduni, na tungo za fasihi

simulizi zilisimilishwa michezo ya kuigiza iliyoakisi maudhui ya utamaduni wa Wagiriki.

Katika kipindi cha Urasimi wa Kigiriki uliotokea baina ya karne ya nne (K.Y.K) na karne ya nne (B.Y.K), kazi za kirasimi zilichota malighafi yake kutoka visa maarufu vya fasihi simulizi. Kama tulivyoona katika sura hii, kisasili cha *Mfalme Edipode* kilikuwa kikisimuliwa katika tanzu mbalimbali za fasihi simulizi katika karne ya tano (K.Y.M). Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (1999), kazi hizo za kirasimi zilichukuliwa kama mizani bora ya utunzi ambayo ilifaa kuigwa na wasanii chipukizi. Hii ina maana kwamba usanii wa fasihi simulizi ulikuwa mizani bora katika uvyazaji wa fasihi andishi ya jamii za ulimwengu. Njia bora ambayo ilitumika ili kuhifadhi ama kuhamisha mizani ya utunzi kutoka fasihi simulizi kwenda fasihi andishi ilikuwa usimilisho.

Historia ya fasihi ya Kimagharibi huonyesha kipindi cha ukame katika utunzi wa kazi za sanaa ya lugha. Kulingana na Wafula na Njogu (2007), kipindi cha giza kilichotokea huko Ulaya kilishuhudia kuadimika kwa tungo mpya katika fasihi baada ya kipindi cha urasimi. Wafula (1992:18) anasema hivi:

Baada ya kudidimia na kuporomoka kwa utamalaki wa Uroma na tawala za kimashariki zilizochipuka katika ujanibu wa mji wa Constantinople, Uropa kwa ujumla ilifunikwa gubigubi kwa giza la ushenzi na ujinga. Hakukuwa na uvumbuzi wa kisanaa au wa taaluma yoyote ile unaoweza kurejelewa.

Katika usimilisho, hamna ushahidi wowote wa tungo zinazosimilishwa katika kipindi hicho cha giza. Hata hivyo, kipindi cha urasimi mpya ambacho kilitokea kuanzia karne ya kumi na sita na kufikia kilele chake katika karne ya kumi na nane, kilifufua sanaa za urasimi mkongwe na usimilisho. Wahakiki maarufu kama Alexander Pope walihimiza utunzi kufanywa kwa njia ya kuiga tungo za

urasimi mkongwe. Kwa mujibu wa Wafula (1992), Pope aliamini kwamba uandishi mzuri ulitokana na mitindo na vipengele vilivyotumiwa, kuimarishwa na kuthaminiwa na watunzi maarufu wa kale. Mbali na kutunga kazi mpya, wasanii wa kipindi hicho walizitafsiri tungo maarufu za kipindi cha urasimi mkongwe zilizopatikana katika lugha ya Kiroma kwa lugha ya Kiingereza.

Ingawa fani ya usimilisho haidhihiriki moja kwa moja katika kipindi hicho, baadhi ya wahakiki wa usimilisho wanaichukulia hali ya kuiga ama kutafsiri tungo za utamaduni mmoja kwenda mwingine kama tendo la usimilisho. Madai haya yana mashiko kwani baadhi ya tungo zilizotafsiriwa, zilifanywa hivyo kwa misingi ya utamaduni pokezi wala sio utamaduni wa lugha chasili. Aidha, katika mtazamo wa kuuangazia usimilisho kama mwingiliano matini, msisitizo wa warasimi wapya kwa watunzi wajumuishe nukuu na marejeleo kutoka kwa tungo za magwiji wa jadi, unaafiki zaidi kuitwa usimilisho. Kwa hakika, usanii katika kipindi hicho cha urasimi mpya haukuwa na upya mwingi unaoweza kurejelewa katika misingi ya kisanaa. Hata hivyo, ni muhimu kutambua kwamba sayansi iliasisiwa katika kipindi hicho na ikazua athari katika utunzi wa kazi za fasihi. Kama anavyosema Wafula (1992), baadhi ya wanafasihi katika kipindi hicho walizua kanuni zilizoshabihiana na zile zilizokuwa zikitekelezwa katika sayansi.

Kulingana na Wiley (2002), huko Uingereza mnamo mwaka wa 1583 kulijengwa ukumbi wa thieta katika jiji la London ulioitwa *Shakespeare's New Globe Theatre*. Katika ukumbi huo, masimilisho ya Shakespeare kuhusu visa vya historia ya kale yaliigizwa na kupata umaarufu mkubwa. Jambo hilo, kulingana na Wiley, lilimfanya malikia wa Uingereza kumwalika Shakespeare katika makao yake, huku michezo yake ikiwa imevuma katika jiji zima. Katika ukumbi huo, hadithi zilizokuwa zikiigizwa huko Ugiriki zilisimilishwa, zikaundwa upya

na kusimuliwa tena na Shakespeare. Shakespeare alikuwa ameupa uhai usimilisho ambao ulikuwa umepatwa na utasa katika kipindi cha giza kwenye historia ya Ulaya. Usimilisho katika kipindi hicho ulikuwa na dhima kuu kijamii, ikitiliwa maanani kwamba uliweza kuisimulia upya historia ya jamii pamoja na kufufua visa vya kale ambavyo vilikuwa vimeanza kusahaulika na wanajamii.

Katika mataifa ya Kimagharibi, usimilisho ulioshamiri sana katika kipindi cha urasimi mpya ni ule wa matini kwa matini, pamoja na ule uliohusisha uigizaji wa jukwaani wa tungo zilizosimilishwa. Hata hivyo, katika karne ya kumi na tisa, aina hizo mbili za usimilisho zilionekana kugubikwa na usimilisho mwingine uliohusisha matini za fasihi kugeuzwa kuwa filamu. Usimilisho huo wa kifilamu ulichukua nafasi ya usimilisho wa jukwaani uliotegemea waigizaji na hadhira hai. Maendeleo hayo ya usimilisho yalichipuka punde baada ya teknolojia ya filamu kuvumbuliwa katika karne hiyo ya kumi na tisa. Filamu ilikuwa njia mpya ya mawasiliano iliyotumiwa na wasimilishaji kutekeleza azma yao ya kisanaa. Kwa mujibu wa Shepherd (2009), usimilisho wa kazi za fasihi ulipiga jeki taaluma hiyo mpya ya filamu katika siku zake za mwanzo. Kama anavyosema Shepherd, filamu maarufu zilizoigizwa zilisimilishwa kutoka vyanzo vya kifasihi. Mathalan, filamu ya *Nosferatu* (F.W.Murnau, 1922) na *Dracula* (Tod Browning, 1931), hizi mbili zikisimilishwa kutoka riwaya ya *Dracula* (1897) ya Bram Stokers. Pia, *Frankenstein* (James Whale, 1931), ikisimilishwa kutoka kazi ya Mary Shelley, *Frankenstein* (1818), na filamu ya *Gone with the Wind* (Victor Fleming, 1939) kutoka riwaya ya Margaret Mitchell, *Gone with the Wind* (1939).

Usimilisho wa kifilamu unaonekana kuangaziwa sana na wahakiki wa taaluma za fasihi na filamu, kiasi cha kupuuza usimilisho wa matini kwa matini na ule wa

kuigiziwa jukwaani. Karne ya ishirini ilishuhudia tafiti na tahakiki nyingi zilizoangazia filamu zilizokuwa zimeigizwa kutokana na vitabu vya fasihi.

Mnamo miaka ya 1940 na 1950, vituo vya televisheni vya Uingereza kama *Ealing* vilianza kusimilisha michezo ya kuigiza kutokana na matini za fasihi ya kirasimi. Hata hivyo, michezo hiyo ya kidrama haikuonyeshwa mara nyingi katika runinga hadi miaka ya sitini ya karne ya ishirini (SCAFM, 2008). Michezo ya drama ya kuonyeshwa kwenye televisheni ilitolewa kwa ufanisi sana na idhaa ya BBC mnamo 1967 walipotoa similisho la riwaya ya John Galsworthy, *The Forstye Saga*. Similisho hilo lilikuwa na ufanisi mkubwa na lilishinda tuzo la *Royal Television Award*, huku likitazamwa na hadhira ya watu milioni sita kati ya Januari hadi Julai 1967. Ingawa usimilisho huo ulikuwa na ufanisi mkubwa, watayarishi wa drama za televisheni katika miaka ya sitini ya karne ya ishirini, walitoa nafasi kwa drama za kisasa zilizokuwa zikiwalenga vijana. Mathalan, walitoa drama ya *The Avengers* (1961) na *Prisoner* (1967).

Kulingana na SCAF (2008), usimilisho wa drama za televisheni kutoka riwaya za zamani ulirejelewa katika miaka ya sabini, karne ya ishirini. Katika miaka hiyo, usimilisho ulilenga riwaya za karne ya kumi na tisa ambazo ziliivuta na kuishirikisha hadhira katika usimilisho. Kituo cha televisheni cha BBC kilipata sifa kimataifa kutokana na utengenezaji wa drama nzuri. Licha ya hatua hizo nzuri katika usimilisho wa drama za televisheni, uhuru wa kibiashara uliohalalishwa na serikali ya Margeret Thatcher wa Uingereza katika miaka ya themanini karne ya ishirini, ulihasiri utengenezaji wa filamu vibaya. Sekta ya utengenezaji wa filamu ilianza kuchukuliwa kama biashara na ilitakiwa kuwajibikia nguvu za kisoko kama biashara nyinginezo. Aidha, wawekezaji katika sekta ya filamu walitakiwa kulipa kodi kama wawekezaji wengine katika

sekta nyingine za uchumi. Fauka yake, shirika la kitaifa la kufadhili watengenezaji wa filamu lilibinafsishwa. Hatua hizo za serikali mpya ya Thatcher ziliathiri pakubwa sekta ya filamu, ijapokuwa watayarishi wa filamu katika televisheni walijizatiti na kuhimili misukumo hiyo hasi. Kutokana na ukosefu wa msaada wa serikali na sheria mpya za uwekezaji, sekta ya filamu nchini Uingereza iliathirika vibaya na kupoteza hadhi yake katika jamii.

Katika sekta ya elimu, idara ya filamu na taaluma ya fasihi zilichipuka nchini Uingereza na Marekani katika miaka ya sitini na sabini karne ya ishirini (Aragay, 2005). Taaluma ya filamu na fasihi ilirithi misingi iliyotawala uchunguzi wa fasihi wakati huo, ya uhakiki mpya na elimu huru ya binadamu. Usimilisho wa tungo za fasihi kuwa filamu ulianza kuhakikiwa kwa misingi ya nadharia hizo, na watayarishaji wa filamu wakatarajiwa kuitimiza. Kwa mujibu wa Cartmell na Whelehan (2007), utegemeaji wa filamu kwa tungo za fasihi ulionekana kama udhaifu katika kipindi cha nusu ya karne ya ishirini. Wahakiki walihimiza watayarishaji wa filamu kuitafsiri simulizi pamoja na mbinu za utunzi badala ya kuinakili yote jinsi ilivyowasilishwa na mwandishi wake. Hii ni kwa sababu utegemezi huo ungeifanya filamu kuchukuliwa kuwa ya hadhi ya chini ikilinganishwa na fasihi.

Katika mvutano huo, George Bluestone alichapisha matokeo ya utafiti wake kuhusu uigizaji wa fasihi katika filamu, *Novels into Film* (1957). Bluestone alianza kwa kuchunguza mfanano uliopo baina ya fasihi na filamu, na kuhitimisha kwa msisitizo kuwa, sanaa hizo mbili zinafaa kuhukumiwa kama tofauti na zinazojisimamia. Kauli yake iliwafanya wahakiki katika fani za fasihi na filamu kuanza kuifikiria upya mitazamo yao kuhusu usimilisho wa fani hizo. Kwa mujibu wa Blustone (1957), ni vigumu usimilisho kuzalisha kazi sawa na ile

inayosimilishwa. Kwa hivyo, haikuwa haki kulihukumu similisho (filamu) kama umbo duni kwa vile utoaji wa similisho sahihi ni jambo lisilowezekana. Kazi ya Bluestone ilikuwa muhimu katika uchunguzi wa usimilisho kwani ndiyo iliyotoa mwanga zaidi kuhusu usimilisho, hasa wa kifilamu.

Kwa mujibu wa Aragay (2005), usomi kuhusu filamu na fasihi ulishika kasi katika miaka ya sabini ya karne ya ishirini. Katika kipindi hicho, madai kwamba fasihi ndiyo utanzu mkuu (wenye hadhi) kuliko filamu yalitawala maoni ya wasomi wengi. Mhakiki wa similisho Geoffrey Wagner katika kitabu chake *The Novel and the Cinema* (1975), alichunguza jinsi masimilisho yalivyowasilisha fani na maudhui ya kazi chasili. Kutokana na uhakiki wake, Wagner (1975), aliainisha aina tatu za usimilisho kutegemea kiwango cha uaminifu kwa matini chasili. Hizi aina tatu alizirejelea kama tafsiri sisisi, fasiri mpya na analogia. Katika tafsiri sisisi, matini ya fasihi hugeuzwa moja kwa moja pasipo na mabadiliko yoyote makubwa. Katika hali hiyo, matini huwa imetafsiriwa moja kwa moja kutoka matini chasili. Kwa upande wa fasiri mpya, inawezekana msimilishaji akaifanyia matini mabadiliko ya kimakusudi na kuubadilisha mtazamo asilia wa mtunzi. Usimilisho wa analogia ni ule unaokengeuka zaidi kutoka matini chasili na kuibua tofauti kuu zinazolifanya similisho hilo kuonekana kama ni matini tofauti ya fasihi. Mara nyingine inaweza kuwa vigumu kubaini iwapo similisho hilo limetokana na matini nyingine.

Uainishaji wa Wagner uliongozwa na kigezo cha uaminifu wa similisho kwa matini chasili. Jambo hilo lilimfanya Wagner kukosa kuzingatia athari za mwingiliano matini na muktadha katika usimilisho. Matini inaweza kukosa kuwa aminifu kwa matini chasili, lakini ikawa aminifu kwa matini nyingine

inazoitikiana nazo katika muktadha wake. Uaminifu wa similisho kwa matini chasili hutegemea dhamira inayoongoza usimilisho.

Miaka ya kumalizia karne ya ishirini na mwanzoni mwa karne ya ishirini na moja, ilitawaliwa na mijadala kuhusu usimilisho aminifu kwa matini za fasihi. Mhakiki Beja (1979), alipuuzilia mbali matumizi ya maneno kama vile ‘usaliti’ na ‘uaminifu kwa matini’ ambayo yalitumika na wahakiki kupimia upokezi wa similisho. Beja alisisitiza kuwa msimilishaji alifaa kuongozwa na kile alichokiita ‘moyo wa kazi asilia’ ambacho ndicho alipaswa kuaminikia. Uhakiki uliosisitiza kigezo cha ‘uaminifu’ ulikashifiwa na Andrew (1980). Kulingana na Andrew (1980), mjadala kuhusu uaminifu katika usimilisho huchosha baadhi ya wahakiki na wasomi.

Mjadala kuhusu uaminifu ulifikia kileleni mwake baada ya kuchapishwa kwa kitabu cha McFarlane, *Novel to Film: An Introduction to the Theory of Adaptation* (1996). Kitabu hicho kilikuwa muhimu katika kuponda kigezo cha uaminifu katika upimaji wa similisho bora. McFarlane alihoji kuwa, uhakiki unaolenga kigezo cha uaminifu huegemezwa kwa dhana kuwa, matini ya fasihi huwa na maana moja sahihi inayopokezwa msomaji na ndiyo maana ambayo msimilishaji huifuata ama kuikiuka. Hii ni dhana iliyoenziwa sana na wana nadharia wa baada-umuundo. Mhakiki huyo alichunguza masimilisho akitumia mtazamo wa kinaratolojia. Mtazamo wa kinaratolojia ulimwezesha McFarlane (1996) kuangazia zaidi muundo wa similisho. Hata hivyo, hali hiyo ya kujikita katika muundo wa similisho ilimfanya mhakiki huyo kuzipuuza athari za kitamaduni na kiusanifu katika usimilisho. Kulingana na Stam (2005), mtazamo wa kinaratolojia ni muhimu sana katika uchunguzi wa mchakato wa usimilisho, lakini unapotumika pasipo na kuhusisha mitazamo mingine unaweza kupuuza

athari za muktadha na mwingiliano wa matini, pamoja na umahuluti wa usimilisho kama fani inayotumia njia kadha za mawasiliano.

Aragay (2005) anaeleza kuwa, umahulitishaji wa usimilisho na taaluma nyingine za usomi ulipata ufanisi mkubwa sana katika miaka ya tisini, karne ya ishirini. Wasomi kama Cattrysse (1992a na 1992b) walipendekeza kutumiwa kwa nadharia ya mifumo-mingi ya tafsiri (polysystems) katika uchunguzi wa mchakato wa usimilisho. Nadharia ya mifumo-mingi ya tafsiri huangazia namna matini lengwa inavyotenda kazi katika muktadha wake, na kuelezea jinsi na kwa nini mabadiliko ya mkazo hutokea katika mchakato wa kutafsiri. Nadharia hiyo inapotumika kuchunguza usimilisho, inaweza kupanua mitazamo na kuangazia zaidi ya kigezo cha uaminifu kwa matini chasili. Kwa mujibu wa Cattrysse (1992b), maswali yanayofaa kuulizwa kuhusu utendakazi wa similisho yanapaswa kubaini: iwapo similisho linajitokeza kama similisho na kwa nini; upokezi wa similisho hilo na hadhira pamoja na wahakiki, na jinsi unavyobadilika kiwakati na mahali; na, muhimu zaidi, uchunguzi wa mwingiliano matini katika usimilisho huo.

Kama inavyobainika, Cattrysse anahimiza mabadiliko katika mitazamo jadi ya uchunguzi wa similisho. Namna mabadiliko yalivyotokea katika uchunguzi wa tafsiri, pale msisitizo ulipotolewa kwa matini chasili na kuwekwa kwa mchakato wenyewe na matini lengwa, vivyo hivyo mabadiliko hayo yanapaswa kuendelezwa katika usimilisho. Kile kinachofaa kusisitizwa sio namna matini chasili ilivyowasilishwa kwa usahihi na msimilishaji, bali pia, vichangizi vya kimuktadha na kiusanifu vinavyoathiri usimilisho kwa ujumla na upokezi wake. Pamoja na hayo, Cattrysse anauweka usimilisho katika uchunguzi wa mwingiliano matini. Katika uchunguzi wa mwingiliano matini, masimilisho

yatafasirika kama kazi ambazo hazitokani na matini moja ama zinazofaa kuwa aminifu kwa matini yoyote ile. Kwa hakika, mtazamo wa Cattrysse unapingana na ule wa wanamaumbo ambao unasisitiza zaidi uaminifu ama usahihi katika harakati za kusimilisha matini za fasihi. Mtazamo huo unaungwa mkono na Naremore (2000), anayependekeza uchunguzi wa usimilisho utolewe kutoka masuala ya umbo ama muundo, na ulenge zaidi masuala ya muktadha (kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni, kiviwanda, na kielimu) na vichangizi vya mwingiliano matini. Hayo ndiyo maoni ya Stam (2000) anayependekeza uhakiki unaozingatia nadharia ya mwingiliano matini.

Katika mwongo wa kwanza wa karne ya ishirini na moja, usimilisho umeweza kuangaziwa kwa mujibu wa nadharia za kisasa. Nadharia kama vile naratolojia, upokezi wa msomaji, mwingiliano wa matini, usemezano, na mwingiliano wa njia za mawasiliano zimeweza kutumiwa na wachanganuzi mbalimbali wa usimilisho. Hayo ndiyo maendeleo ya juu katika fani ya usimilisho katika fasihi ya Kimagharibi.

Kwa kuhitimisha historia ya usimilisho katika fasihi ya Kimagharibi, imebainika kwamba, usuli wa usimilisho upo katika fasihi simulizi ya jamii za ulimwengu. Usimilisho ulikuwa na dhima kuu ya kuvyaza tanzu mbalimbali za fasihi andishi. Maendeleo ya kiusomi katika taaluma ya usimilisho yameibua mjadala mkubwa wa suala la uaminifu wa similisho kwa matini chasili. Uchunguzi umebaini kwamba hayo ni matokeo ya mitazamo na nadharia zinazotumika kuhakiki masimilisho. Wahakiki waliotumia nadharia ya uhakiki mpya walijifunga zaidi katika uaminifu wa matini, huku waliofuata nadharia za mwingiliano wa matini wakipinga kigezo cha uaminifu kwa matini.

Uchunguzi huu uliutazama usimilisho kama aina ya mwingiliano wa matini. Ingawa wahakiki wa mwingiliano matini hupinga uwezekano wa kuwepo na usimilisho aminifu ama sahihi, uchunguzi huu ulinuia kubainisha kwamba kuna uwezekano wa matini kuingiliana, lakini uaminifu kwa matini chasili ukadumishwa. Hiki ndicho kiini kinachotawala usimilisho wa riwaya na hadithi fupi zinazotahiniwa katika mtihani wa kidato cha nne.

4.3.2 Usimilisho katika Fasihi ya Kiswahili

Historia ya usimilisho katika fasihi ya Kiswahili imekumbwa na changamoto kutokana na ukosefu wa nyenzo za kuhifadhia tungo za jadi za fasihi hii, jambo linalofanya urejeleaji wake kuwa mgumu. Chimbuko la usimilisho huu, ingawa ni katika fasihi simulizi, linajidhihirisha wazi baada kuingia kwa wakoloni Afrika Mashariki. Kuingia kwa wakoloni katika Afrika Mashariki kulifungua ukurasa mpya katika usomi na uhifadhi wa rekodi muhimu za kurejelewa. Hati za kuandika ni moja kati ya michango iliyotokana na wageni waliozuru ukanda wa Afrika Mashariki.

Wakoloni wa kwanza kuingia Afrika Mashariki walikuwa Wareno katika karne ya kumi na tano. Hata hivyo, historia haionyeshi mchango wowote wa Wareno katika fasihi ya Kiswahili. Wakoloni wa Kireno waliondolewa Afrika Mashariki na Waarabu ambao walianzisha himaya yao katika ukanda wa pwani ya Afrika Mashariki. Utawala wa wakoloni Waarabu ulikuwa chini ya Seyyid Said aliyeufanya mji wa Unguja makao yake makuu baada ya kuyahamisha kutoka Muscat, Omani.

Wakoloni wa Kiarabu walikuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya fasihi ya Mwafrika. Waarabu walichangia katika fasihi ya Kiswahili kwa kuleta hati za Kiarabu ambazo zilitumika kuhifadhiwa katika maandishi baadhi ya kazi za fasihi simulizi. Kiango (2004:66) anatumia mchango huu:

... Waarabu waliwafundisha wenyeji kusoma na kuandika maandishi ya Kiarabu. Hali hii ilisaidia kuweka hazina ya msamiati pamoja na sanaa ya lugha ya Kiswahili kama vile hadithi, mashairi, tenzi na nyimbo katika maandishi kwa abjadi ya Kiarabu.

Hati hizo za Kiarabu zilitumiwa na baadhi ya watunzi kuandika tungo zao za fasihi andishi. Ni muhimu kutambua kuwa, fasihi andishi ya Kiarabu ilikuwa msingi katika utunzi wa tanzu andishi za fasihi ya Kiswahili. Massamba (2003:64) akiyarejelea maelezo ya Hichens (1941) anadokeza hivi:

... utungaji wa mashairi ya mizani ndefu ndefu ... una asili ya athari ya ki- Ajemi ... unahusiana sana na utungaji wa beti ambazo wanaarudhi wa ki- Ajemi waliita 'kasida' (mashairi yenye kina kimoja) na 'mathnawi' (mashairi yenye vina viwili) ... uliletwa kwenye pwani za Uswahilini na wahamiaji kutoka Uajemi katika karne ya 12. Waswahili baada ya kuuiga waliufanyia marekebisho kadha ambayo yaliweza kukidhi haja yao na kuweza kuingia katika mambo ya utungaji waliyoyazoea.

Maoni ya Massamba (2003) na Hitchens (1941) yanashadidia kuwepo na usimilisho wa ushairi wa Kiarabu katika ushairi wa Kiswahili. Marekebisho ama mabadiliko yanayotajwa kufanyiwa ushairi wa Kiarabu katika utunzi wa mashairi ya Kiswahili hayakufanywa kwenye ombwe tupu, bali yalilingozwa na mbinu mahsusuni. Usimilisho huo ulikuwa mahuluti, ukichanganya sifa za ushairi wa Kiarabu na zile za ushairi simulizi zilizokuwa zimezoeleka katika muktadha wa ushairi wa Kiswahili. Massamba (2003) anaongeza kuwa, tanzu za ushairi kama vile *Takhamisa* na *Khamziya* zimetokana na asili ya Kiarabu. Madai haya yanaungwa mkono na Abdilatifu Abdalla anayerejelewa na Kandoro (2003:122) akisema kuwa:

Asili ya utungo huu (takhmisa) kuingia pande za huku kwetu ilitokana na ‘takhmisa’ ya Kiarabu ijulikanayo kwa jina la ‘Madini’ na ambayo maudhui yake yalikuwa ni ya kidini.

Kulingana na Wamitila (2002), tungo nyingi za wakati huo zinafanana kidhamira na kifani. Baadhi yake zinachota malighafi yake kutoka visa, hurafa na migani ya Kiarabu au ni tafsiri za moja kwa moja. Katika mtindo, zinafanana kwa matumizi ya fomyula za fasihi simulizi, fomyula sawa za ufunguzi na mwisho wa utungaji, msuko na mgogoro wa msuko unaokaribiana, miongoni mwa sifa nyinginezo. Kwa kuchukua mtazamo kuwa mwingiliano matini na tafsiri ni sura nyingine za usimilisho, ni bayana kwamba katika kipindi hicho fasihi ya Kiarabu ilisimilishwa kwa madhumuni ya kuzalisha visa, mitindo na maudhui ya fasihi changa iliyoandikwa ya Kiswahili. Fasihi hiyo ya Kiarabu ilikuwa msingi muhimu katika kuasisi utunzi wa fasihi andishi ya Kiswahili.

Hata hivyo, ufanisi katika usimilisho ulionekana dhahiri baada ya kuingia kwa wakoloni Wazungu ambao walileta hati za kuandika za Kirumi. Mfano mzuri wa kazi iliyosimilishwa katika kipindi hicho ni *Utendi wa Fumo Liyongo* ulioandikwa na Mohamed Kijumwa mwaka wa 1913. Utenzi huu, kama ilivyobainika awali, ulikuwa ukisimuliwa kabla ya kutiwa katika maandishi. Uhamishaji wa utungo wa fasihi simulizi kuwa utungo wa fasihi andishi, umebainishwa na tasnifu hii kama usimilisho. Msimilishaji hufanya uteuzi muhimu kuhusu namna ya kuviwasilisha vipengele vya fasihi simulizi katika fasihi iliyoandikwa. Aidha, baadhi ya sifa za kisimulizi hupotea na nafasi yake kuchukuliwa na sifa za fasihi andishi.

Kwa mujibu wa Njogu na Chimera (1999), vitabu vilivyotokana na ngano za fasihi simulizi ni: *Swahili Tales as Told by Natives of Zanzibar* (1889)- Edward Steere na *Mazungumzo ya Alfu- Lela Ulela* (Juzuu 1-4) (1928)- kilichotafsiriwa

na Edwin Brenn na kuhaririwa na F. Johnson. Waandishi hawa wanaongezea kuwa, baada ya mwaka wa 1940 na kuendelea hadi miaka ya sitini, riwaya nyingi zilifuata mkondo wa ngano za fasihi simulizi. Sifa zilizohamishiwa riwaya hizo ni kama mianzo ya ‘paukwa pakawa...’, ‘hapo zamani za kale paliondokea...’ na kimaudhui, inasemekana kuwa riwaya nyingi zilikuwa na mambo ya mila na tabia kama njia ya kufunza maadili. Baadhi yake zilitokana na fasihi ya Kiarabu kama *Kisa cha Mwana wa Mfalme* (Mohamed Bin Suleiman, 1944), *Msafiri katika Nyumba ya Sultani* (David E. Diva, 1949), *Hadithi za Bibi Maahira* na *Bibi Maahira Tena – S.O.S. Baalawy* (1968).

Kama ilivyotanguliwa kusemwa katika historia hii, msingi wa usimilisho unapatikana katika fasihi simulizi ya ulimwengu. Ni dhahiri kuwa fasihi andishi ya Kiswahili, hasa utanzu wa riwaya na hadithi fupi, imefaidi sana kutoka kwa fasihi simulizi. Kipera cha ngano kilikuwa kama kielelezo cha utunzi wa kinathari miongoni mwa waandishi wengi. Hii ndio maana tungo za kinathari za fasihi andishi ya Kiswahili ziliathiriwa kimuundo na kimaudhui na ngano za fasihi simulizi. Hali hiyo ya kuziwasilisha ngano katika fasihi andishi pamoja na kuzitumia kama msingi wa utunzi wa fasihi andishi, inaashiria kuwepo kwa usimilisho wa kiwango fulani. Huu ni usimilisho uliokuwa umechochewa na haja mbili kuu. Kwanza, palikuwepo na haja ya kuwa na msingi bora wa kuigwa katika utunzi wa tungo za kinathari katika fasihi andishi ya Kiswahili. Haja hiyo ilitatuliwa kupitia tafsiri za tungo za kinathari kutoka fasihi ya Kiingereza na Kiarabu, pamoja na uigaji wa kisanaa wa ngano za fasihi simulizi ya Kiafrika. Pili, ni haja ya kutaka kutosheleza mahitaji ya vitabu vilivyokuwa vinasomwa shuleni nyakati hizo. Ili kutosheleza haja hiyo, wamishenari walikusanya ngano za fasihi simulizi na kuziandika, pamoja na kutafsiri vitabu vya fasihi ya kigeni

kwa Kiswahili. Kulingana na Mpesha (1995), baadhi ya mashairi ya kigeni yalifanyiwa mabadiliko upande wa wahusika na mahali ili kuyafanya yakubalike zaidi na watoto.

Kazi za fasihi ya kigeni ziliendelea kuathiri fasihi ya Kiswahili, hasa katika kipindi cha ukoloni. Mathalan, baadhi ya riwaya zilizotungwa katika kipindi hicho zilionekana kama similisho za kazi fulani za kigeni. Njogu na Chimera (1999) wanasema kuwa, baadhi ya riwaya ambazo zilifuata misingi ya kigeni ni zile zilizoiga maudhui ya upelelezi kama za Mohamed Said Abdulla. Hizi ni kama vile *Mzimu wa Watu wa Kale*, *Siri ya Sufuri*, na *Kisima cha Giningi*. Riwaya hizi za Mohamed Said Abdulla zinadaiwa na baadhi ya wahakiki wa fasihi kuwa zimeathiriwa na utunzi wa kigeni wa wakati huo, hasa kazi za Arthur Canon Doyle. Athari hizo zinadhihirika upande wa mtindo na maudhui.

Uigaji huo wa visa, mtindo na maudhui unajidhihirisha kama usimilisho wa kiwango cha chini uliokuwa ukifanywa na wasanii kwa nia ya kuzifanya tungo fulani za kigeni kueleweka katika mazingira mapya ya utunzi na utamaduni. Kwa baadhi ya waandishi, iliafiki kuzisimilisha tungo za kigeni kimtindo na kimaudhui kama njia bora ya kupata msingi wa kutunga kazi za fasihi andishi. Baadhi ya wahakiki akiwemo Ntarangwi (2004) wametambua kuwa, riwaya za Shabaan Robert zilifanana sana na kazi za kigeni. Mathalan, riwaya ya *Adili na Nduguze*, *Kufikirika* na *Kusadikika* zinasheheni muundo na maudhui ya kigeni yanayopatikana katika baadhi ya tafsiri, hasa hadithi za *Alfu- Lela- Ulela*. Wahusika wengi wa Shabaan Robert walionyesha hali ya unyenyekevu huku wafalme wakisawiriwa kama wenye nguvu sana na wahusika wakuu wakiwa waadilifu. Kwa maoni ya Ntarangwi (2004), hizo ni athari zilizotokana na falsafa za Wakoloni kwa wenyeji. Aidha, Waafrika walilazimika kufuata mkondo wa

tafsiri za tungo za kigeni ili kufuta kasumba ya wakoloni kwamba viwango vyao vya usanifu vilikuwa chini mno vikilinganishwa na vile vya wageni.

Hata hivyo, kazi hizo zilizoiga sifa za kigeni haziwezi kutazamwa kwa jicho la kigeni pekee. Hii ni kwa sababu tungo hizo zilijumuisha vipengele vingi vya fasihi simulizi ya Kiafrika katika muundo na maudhui yake. Huu ulikuwa usimilisho mahuluti, uliojumuisha malighafi ya kigeni na yale ya kiasilia.

Usimilisho katika fasihi ya Kiswahili uliendelea kusakini katika utunzi huku ukijidhihirisha kwa sura mbalimbali. Kama inavyobainika, usimilisho huo ulikuwa ukichukua sura ya tafsiri na mwingiliano matini. Tungo andishi za Kiswahili kama vile riwaya, tamthilia, hadithi fupi na ushairi, ziliathirika sana kutokana na utunzi wa kigeni na ule wa fasihi simulizi ya Kiafrika. Kwa sababu hiyo, kazi za awali katika tanzu hizo zinasheheni umahuluti mwingi.

Hata hivyo, miaka ya sitini na sabini ya karne ya ishirini ilishuhudia mabadiliko makubwa katika utunzi wa riwaya, tamthilia, ushairi na hadithi fupi. Katika ushairi, miaka ya sitini ilikuwa muhimu katika kuvyaza ushairi huru ambao ulipindua mitindo iliyoenziwa katika utunzi wa mashairi. Kulingana na Ruo (2003), wafuasi wa mkondo huo mpya wa utunzi wa mashairi walisisitiza kuwa kuna sifa nyingine zinazoutambulisha na kuufanikisha ushairi zaidi ya vina na mizani. Ushairi huru huchukuliwa kuwa matokeo ya athari za ushairi wa kigeni kwa ushairi wa Kiswahili. Wanamapinduzi wa ushairi wa Kiswahili walikuwa wasomi ambao walifaidi sana kutoka fasihi za ulimwengu, hasa ile ya Kiingereza. Azma yao ilikuwa kujumuisha sifa za kigeni katika ushairi wa Kiswahili. Kulingana na Kezilahabi (2003), mapinduzi yalilenga pia ujumuishaji wa sifa

nyingine kutoka ushairi wa jamii nyingine za Kiafrika. Kezilahabi (2003: 147-148) anaeleza jambo hili hivi:

Ushairi wa Kiswahili ulikuwa umefikia hali hii ya uozo. Hali ya kupanga ma-vina kama mapambo bila kujali maana. Ili kuokoka, ushairi wa Kiswahili unahitaji damu mpya. Damu hii mpya inapatikana katika ushairi wa makabila mbalimbali... Mawazo yao (wanamapokeo) yote yanaishia kwenye ukingo wa 'Waswahili wenyewe', wameshindwa kutoka nje ya hapo... Hivi sasa Kiswahili kimevuka mipaka yao na kimefikia kifasihi 'Waswahili wenyewe' (ambao) wana madaraka makubwa juu ya mwelekeo wake.

Hali hii ya kuhulutisha sifa za ushairi wa Kiswahili, ule wa kigeni pamoja na ule wa makabila mengine ya Kiafrika inajidhihirisha kama usimilisho. Ama kweli, huu ni mwingiliano matini ambao umejadiliwa kama sura nyingine ya usimilisho.

Katika miaka hiyo ya sitini na sabini, watunzi wa Kiafrika walianza kutunga tamthilia zao zilizokuwa na uzito wa maudhui yaliyokuwa yakimlenga Mwafrika. Hata hivyo, baadhi ya tamthilia zilitafsiriwa kutoka tamthilia za kigeni. Mifano yake ni kama vile *Mfalme Edipode*, *Juliasi Kaizari* na *Mabepari wa Venisi*. Tafsiri ya baadhi ya tamthilia hizo ilifanywa kama usimilisho. Mwandishi Julius Nyerere aliitafsiri tamthilia ya Sheakespeare *Mercharnts of Venice* kama *Mabepari wa Venisi* badala ya *Wafanyabiashara wa Venisi*. Yamkinika kwamba, Nyerere aliathiriwa sana na itikadi aliyoihusudu ya ujamaa na akadhamiria kuusuta ubepari katika tafsiri hiyo.

Miaka ya sitini na sabini ilishuhudia uchapishaji wa diwani za mwanzo za hadithi fupi katika fasihi ya Kiswahili. Diwani za kwanza kuchapishwa zilikuwa hadithi fupi za kimapokeo kama vile *Hekaya za Abunuwas* na *Hadithi za Bibi*. Kama inavyobainika, diwani za mwanzo za hadithi fupi katika fasihi ya Kiswahili zilikuwa similisho za ngano na hadithi za fasihi simulizi. Madai haya yanaungwa mkono na wahakiki mbalimbali wa hadithi fupi kama vile Mohochi (1997),

King'ei na Kisovi (2005), Wamitila (2004), Musokile (1992) na Senkoro (1982). Kulingana na wahakiki hawa, usuli wa hadithi fupi iliyoandikwa katika fasihi ya Kiswahili upo kwenye fasihi simulizi. Kabla ya kuasisiwa kwa maandishi, hadithi hizo zilikuwa zikisimuliwa lakini fani ya kuandika ilipoletwa na wakoloni Waafrika wakaanza kuzitia katika maandishi. Kutegemea mizizi yake, hadithi fupi ilinawiri kwa kuhulutisha sifa za hadithi simulizi na zile za hadithi fupi za kigeni. Ni uvyazaji huo wa utanzu wa hadithi fupi ambao unachukuliwa na tasnifu hii kama zao la usimilisho.

Maendeleo ya tanzu za fasihi ya Kiswahili yalishuhudiwa pia katika utanzu wa riwaya. Kwa mujibu wa Njogu na Chimera (1999), miaka ya sabini ndiyo inayochukuliwa kama kipindi cha kuzaliwa kwa riwaya ya kisasa ya Kiswahili. Waandishi walianza kuangazia uongozi wa Waafrika na usaliti wa kisiasa. Huu ukawa wakati wa S.M. Mohamed kuandika riwaya zake mbili: *Kiu* (1972) na *Nyota ya Rehema* (1978). Riwaya hizi zilikuwa na msukumo mkubwa kwa utunzi wa riwaya katika visiwa vya Jamhuri ya Tanzania. Baadhi ya riwaya zilizotungwa huko visiwani baadaye zilionekana kuathiriwa kimaudhui na kimtindo na hizi za S.M. Mohamed. Mathalan, riwaya za S.A. Mohamed; *Asali Chungu* (1978), *Utengano* (1980), *Dunia Mti Mkavu* (1980), *Kiza katika Nuru* (1988) na *Tata za Asumini* (1990). Katika kushadidia jambo hili, Njogu (1997) anamrejelea Kitsao, J. (1982) aliyesema hivi katika tasnifu yake:

... Ingawa *Utengano*, *Asali Chungu*, na *Dunia Mti Mkavu* zependeza hasa kuhusiana na matumizi ya lugha, zimechukua mfano wake katika *Nyota ya Rehema* hivi kwamba hatimaye kazi hizi zaonekana kana kwamba ni...miigo, hasa kimaudhui na kifani.

(Tafsiri ya Njogu, 1997)

Umelea huu wa kisanaa unajitokeza kama usimilisho, pale maudhui na mtindo katika kazi moja hufinyangwa ili kuiunda kazi nyingine mpya. Fauka ya haya, riwaya hizi za S.A. Mohamed zinaonekana kusimilishana kimaudhui na kifani. Katika riwaya hizi, mwandishi S.A. Mohamed amejaribu kuonyesha jinsi nyenzo za uzalishaji mali zilivyotwaliwa na mamwinyi na mabepari wa nchi za kigeni na kuwaacha Waafrika kama wachochole katika ardhi yao. Maudhui ya utabaka ambayo pia yanasawiriwa kama utengano yamezagaa katika riwaya hizi tatu. Wahusika nguli Fauz katika *Dunia Mti Mkavu*, Zuberi katika *Asali Chungu*, na Maksuudi katika *Utengano*, ni matajiri waliomiliki mali mengi na wanafyoza masikini wasiokuwa na mbele wala nyuma. Wasifu wa wahusika hawa na nafasi zao katika riwaya hizi umefanana sana kiasi cha kufanya utofautishaji wao mgumu. Mathalan, Zuberi na Maksuudi wamesawiriwa kama riale kwa ya pili. Zuberi ni mkuu wa wilaya na amewakodisha masikini shamba lake kubwa. Naye Maksuudi tunaarifiwa kuwa aliwahi kuwa mkuu wa wilaya, na alikuwa amerithi shamba kubwa kutoka kwa bwenyenye mmoja aliyegura nchini humo. Huu ni mfanano ambao hauelekei kuwa wa kinasibu. Kwa kiwango kikubwa, maudhui na fani katika riwaya hizi za Mohamed yanaweza kulinganishwa na kuonyesha mfanano mkubwa. Kutokana na mfanano huu, ni maoni ya mtafiti kwamba kazi hizi zinasimilishana kwa njia ya mwingiliano matini na kusemezana. Labda S.A. Mohamed anatumia usimilisho kama mkakati wa kuendeleza falsafa yake na kuisitiza baadhi ya maudhui na mtazamo wake.

Maendeleo katika historia ya usimilisho wa fasihi ya Kiswahili yamepiga hatua kubwa katika robo ya kwanza ya karne ya ishirini na moja. Usimilisho huu umetamalaki katika vipera mbalimbali vya fasihi simulizi na andishi. Wa aidha, madhumuni ya kusimilisha tungo za fasihi yamekuwa yakipanuka na kubadilika

kila uchao. Mathalan, kutokana na haja ya kuwa na vitabu vya fasihi ya watoto, baadhi ya waandishi wamekuwa wakivisimilisha vitabu vya kusomwa na watu wazima ili kuviwezesha kusomwa na hadhira ya watoto. Methali za fasihi simulizi zimeanza kusimilishwa kwa malengo mbalimbali kama kuzua ucheshi, kukosoa mantiki yake, na kuziwianisha na muktadha.

Katika kipera cha nyimbo, nyimbo za kidini (sifo) zimesimilishwa kuwa nyimbo za kisiasa. Nyimbo maarufu hapa ni '*Yote Yawezekana*' na '*Mapambano*'. Hizi nyimbo mbili zilisimilishwa mwaka wa 2002 na kutumika na mrengo wa upinzani (NARC) katika kampeni za kutafuta mrithi wa rais wa pili wa Kenya Daniel Arap Moi. Maudhui katika nyimbo hizi yalibadilishwa na badala yake maudhui ya kisiasa na mapinduzi yakachopekwa.

Usimilisho wa aina hiyo umekithiri sana miongoni mwa makundi ya kisiasa, vyama vya wafanyakazi, na makundi ya kijamii. Katika kuendeleza azma yao, makundi haya huzisimilisha nyimbo maarufu na kuzigeuza ili ziwiane na malengo wanayoendeleza kama vile mgomo, kampeni ama kupinga maamuzi ya kiseru na kisheria. Kwa mujibu wa Nkichabe na Mwamzandi (2008), mirengo ya wanasiasa iliendelea kuzibadilisha (kuzisimilisha) nyimbo za kidini na nyimbo pendwa ili kuweza kutimiza azma zao za kisiasa. Wakati muungano wa NARC ulipoanza kuyumbayumba, vyama tanzu katika muungano huo vilianza kurushiana semi za kusutana na kuumbuana. Wimbo pendwa wa Prince Adio *Nikiwa Ndani*, ulisimilishwa na baadhi ya wanasiasa kuashiria manung'uniko yaliyotawala serikali ya muungano ya NARC. Katika mwaka wa 2005, wimbo wa kidini *Kuna Dawa* ulisimilishwa na mrengo uliokuwa ukipinga katiba pendekezi katika kura ya maoni ya mwaka huo. Maneno '*Yesu ndiye dawa*' katika wimbo huo yalisimilishwa kuwa '*dawa ni chungwa*'.

Katika kampeni za urais za mwaka wa 2013 na miaka iliyotangulia, viongozi wa kisiasa walionekana wakisimilisha tanzu za fasihi simulizi kama mkakati wa kusuta, kukejeli, kujisifu, ama kujipigia debe. Mfano mzuri ni aliyekuwa Waziri Mkuu Raila Odinga aliyejitokeza kama msimilishaji hodari wa vitendawili. Katika ugwiji wake, Raila angevisimilisha vitendawili maarufu ili viweze kuafiki muktadha wake wa kampeni. Matumizi ya vitendawili jinsi hiyo yalikuwa sehemu ya kampeni ya Raila, akilenga kushirikisha hadhira yake katika kujipigia debe ama kuwasuta wapinzani wake. Uhodari huo wa kusimilisha vitendawili ulimpa Raila jina la lakabu, ‘Bwana Vitendawili’.

Mwongo wa mwisho wa karne ya ishirini umepanua mawanda ya usimilisho kwa kuvyaza aina nyingine ya usimilisho katika fasihi ya Kiswahili. Huu ni usimilisho ambao unaonekana kuvuma nchini na ambao unahusu maigizo ya tungo za kinathari. Wasimilishaji wamekuwa wakizigeuza riwaya na hadithi fupi, hasa zinazotahiniwa katika kidato cha nne, na kuziigiza kama drama jukwaani.

Usimilisho huu unakisiwa kupenyeza katika majumba ya kuigizia mwanzoni mwa mwongo wa mwisho wa karne ya ishirini. Miongoni mwa vikundi vya mwanzo kuigiza vitabu teule vya shule ni CHAKINA ambacho kiliyafanya maigizo yake katika shule jijini Nairobi na janibu zake. Katika mwaka wa 1993 kikundi cha *Visions* kilikuwa kikiigiza vitabu teule vya shule jijini Nairobi. Ugizaji wa vitabu teule ulikita mizizi na vikundi mbalimbali vya uigizaji vikachipuka. Hata hivyo, vitabu vya Kiswahili vilivyoigizwa wakati huo vilikuwa ni tamthilia teule zilizokuwa zikitahiniwa katika mtihani wa KCSE. Baadhi ya tamthilia zilizoigizwa katika vipindi mbalimbali ni kama vile *Kinjeketile*, *Buriani*, *Visiki*, *Amezidi*, *Kilio cha Haki*, na *Kifo Kisimani*.

Usimilisho kamili wa kazi za kimasimulizi ulijitokeza katika mwaka wa 2000. Huu ulikuwa wakati wa kuigiza riwaya ya Ken Walibora, *Siku Njema*. Vikundi mbalimbali vilikuwa vimechipuka na kusajiliwa na wizara ya michezo, utamaduni na sanaa. Miongoni mwa vikundi hivyo ni kama vile *Jicho Four* katika mwaka wa 2000, *Planets Theatre (1999)* na *Nairobi Theatre Group (1998)*. Mbali na *Siku Njema*, vikundi hivi viliendelea kusimilisha riwaya kila zilipoteuliwa na Taasisi ya Ukuzaji wa Mitaala nchini K.I.C.D. Riwaya zilizofuata kusimilishwa ni *Kiu, Walenisi, Utengano* na *Kidagaa Kimemwozea*.

Hadithi fupi za kwanza kusimilishwa zilikuwa katika diwani ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine*. Usimilisho na uigizaji wa hadithi hizo ulianza mwakani 2008 na kuhitimishwa mwakani 2012, pale diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* ilipoteuliwa kutahiniwa katika mtihamu wa KCSE kuanzia 2013.

Mbali na vikundi vilivyotajwa, kuna vikundi vingine kama vile *Fanaka, Jawabu, Theatrics, Four Sight, Pace Setters*, miongoni mwa vingine vingi. Kawaida na ilivyo katika sanaa, vikundi hivi vimekuwa na vipindi vya ufanisi na mpomoko. Vingine vimeweza kuvunjwa na vingine vikanawiri kiasi cha kuwa na vipera zaidi. Zaidi ya kuigiza na kusimilisha, baadhi ya vikundi vimeanza pia kuandaa semina za walimu wa sekondari zinazolenga kujadili masuala mbalimbali kuhusu masomo ya shule za upili. Aidha, vikundi hivi huigiza kazi nyingine za fasihi ya Kiswahili, Kiingereza na lugha za Kiafrika.

Usimilisho wa mwanzo wa vikundi hivi ulikuwa chapwa na wa kijuujuu ukidhamiriwa kuwasaidia wanafunzi waelewe baadhi ya matukio ya hadithi fupi na riwaya. Wasimilishaji hawakuwa na ujuzi wa kuwawezesha kubuni masimilisho yaliyoafikia viwango bora. Kwa sasa vikundi hivyo huhitajika

kusajiliwa katika idara ya utamaduni na huduma za kijamii. Aidha, maigizo ya vikundi hivyo hukadiriwa ubora na afisi ya ukadiriaji ubora ya wizara ya elimu. Vikundi vinavyohitimu vigezo vinavyotarajiwa hupewa cheti cha kuigizia wanafunzi. Hata hivyo, wizara ya elimu haina vigezo wazi vilivyoratibiwa vya kuyatathmini maigizo ya tungo za kinathari zinazotahiniwa. Aidha, ilibainika kwamba baadhi ya vikundi, hasa vinavyoigizia katika majukwaa ya shule, huwa havijaidhinishwa kufanya hivyo. Mbali na kubainisha mbinu za usimilisho, utafiti huu umeratibu vigezo vya kuzingatiwa ili kuyatathmini masimilisho ya vikundi hivyo.

4.4 Kiishilio

Sura hii imeshughulikia dhana ya usimilisho, sababu za kusimilisha, na historia ya usimilisho. Imebainika katika sura hii kwamba, dhana ya usimilisho ina fasiri nyingi kutegemea mchakato na matokeo yake. Sura hii imebaini kwamba zipo sababu nyingi za kuzisimilisha kazi za kifasihi, na usimilisho wa riwaya na hadithi fupi kwa dhamira ya kuinua viwango vya uelewa wa wanafunzi, ni mojawapo ya sababu hizo. Historia ya usimilisho imeonyesha maendeleo ya sasa ya usomi katika taaluma hiyo na jinsi yameathiriwa na mabadiliko ya kinadharia. Ingawa wahakiki wa mwingiliano matini wameonekana kupinga uwezekano wa kuwepo na usimilisho aminifu, tasnifu katika utafiti huu ni kuhusu jinsi usimilisho aminifu hauwezi kuepukika katika usimilisho wa tungo zinazotahiniwa katika mtihani wa KCSE.

Sura inayofuata imeendeleza mjadala huu na inahusu ubainishaji wa mbinu katika usimilisho wa riwaya. Katika sura hiyo, matatizo ya usimilisho wa riwaya yamebainishwa na kuelezewa.

SURA YA TANO

MBINU NA MATATIZO YA USIMILISHO WA RIWAYA

5.0 Utangulizi

Sura iliyotangulia imejadili dhana ya usimilisho, sababu za kusimilisha, na historia yake ulimwenguni. Dhamira katika sura hiyo ilikuwa kueleza dhana, historia ya usimilisho wa fasihi na sababu za kusimilisha. Utafiti umebaini kuwa dhana ya usimilisho ina fasiri nyingi kutegemea mchakato na matokeo yake. Aidha, imebainika kwamba kuna sababu mbalimbali za kusimilisha kazi za fasihi na sababu hizo hutegemea msimilishaji. Historia ya usimilisho imeonyesha kwamba chimbuko la usimilisho lipo katika fasihi simulizi ya jamii za ulimwengu. Fauka ya hayo, historia ya usimilisho imedhihirisha kwamba usimilisho wa riwaya na hadithi fupi zinazotahiniwa ni maendeleo ya sasa ya usimilisho. Sura ya tano imeendeleza mjadala huo kwa kuangazia moja ya sababu za kusimilisha, na aina moja ya usimilisho iliyojadiliwa katika historia ya usimilisho. Katika sura hii, utafiti umedhamiria kuchunguza na kueleza mbinu zinazotumika kuisimilisha na kuiigiza riwaya. Matatizo yaliyobainika katika usimilisho wa riwaya yameelezwa, pamoja na mwelekeo kuhusu jinsi yanavyoweza kutatuliwa. Data iliyochanganuliwa na kuwasilishwa katika sura

hii, ilikusanywa kutoka kwa riwaya za *Utengano* na *Siku Njema*, masimilisho na maigizo yake nyanjani. Uchanganuzi wa data umefanywa kwa misingi ya nadharia changamano.

5.1 Mbinu za Usimilisho katika Matini

Hizi ndizo mbinu ambazo huongoza ubunaji na usanifu wa simlilisho la riwaya. Msimilishaji huzitumia mbinu hizo kwa dhamira ya kuuwasilisha ujumbe na usanifu wa riwaya husika. Katika mchakato wa kuzisimilisha matini za riwaya ya *Utengano* na *Siku Njema*, utafiti huu ulibaini mbinu zifuatazo:

Usimulizi: Mbinu ambayo kwayo mhusika mtambaji aliumbwa na kukabidhiwa nafasi ya mwandishi katika usimuliaji wa hadithi katika simlilisho. Utambaji ulifanywa na mhusika mmoja au wawili kutegemea dhamira ya msimilishaji. Mbinu hii ilitumika na vikundi vingi.

Maelezo ya jukwaani: Hii ni mbinu iliyohusisha uandalizi wa maelezo yaliyoelekeza uigizaji na kutoa sifa za mandhari na wahusika. Matumizi ya maelezo ya jukwaani yalithibitika katika masimilisho ya makundi yote. Hata hivyo, ufundi wa kuyasanifu ulitofautiana kutoka kikundi kimoja hadi kingine.

Ufaraguzi wa msuko: Hii ni mbinu ya kusimilisha matini ya riwaya kwa njia ya kuyapanga upya matukio ya riwaya hiyo ili kuyawasilisha kulingana na utokeaji wake kiwakati. Aghalabu, msuko wa riwaya huwasilisha matukio kwa njia ya kwenda mbele na kurudi nyuma. Huu ni msuko tukizi katika muundo wa tamthilia nyingi. Wasimilishaji wa vikundi vingi waliyapangua matukio ya

riwaya, mengine ya mbele yakayapisha ya nyuma, kwa lengo la kuhakikisha kuwa tukio lililotangulia kiwakati lilitangulia pia kuonyeshwa jukwaani.

Matumizi ya mbinu za kiutendaji: Mbinu za kiutendaji ni mbinu ambazo utendakazi wake hufasirika katika muktadha wa kidrama tu. Mfano wa mbinu hizo ni kama usemaji kando, usemaji wa mawazo ya wahusika, na uzungumzi nafsi. Kaida hizo za kidrama zilitumika na baadhi ya masimilisho, ingawa uhalisi wake ulidhihirika tu jukwaani.

Matumizi ya mazungumzo: Hii ni mbinu ya kuwapa wahusika wa riwaya maneno ya kujibizana ambayo hokusudiwa kuiendeleza hadithi na kuwasilisha dhamira na maudhui ya mwandishi. Riwaya zilizotafitiwa ziliwasilishwa kisimulizi lakini masimilisho yake yakawasilishwa kimazungumzo. Huu ni ufundi uliobainishwa na vikundi vyote vilivyotafitiwa.

Usimilisho wa fani: Mbinu hii ilihusu ugeuzaji wa fani zilizotumika kuiwasilisha riwaya ili kuziwasilisha kwa njia iliyoruhusu uigizaji wake. Baadhi ya mbinu za fani zilibadilishwa kimakusudi na zikawasilishwa kimaigizo. Mfano ni kuigizwa kwa ndoto jukwaani.

Ubunaji wa tendo: Katika mbinu hii ya usimilisho wa riwaya, maelezo ya mwandishi yalifanywa kuwa tendo la kuigizwa jukwaani. Baadhi ya masimilisho yaliashiria tendo lenyewe katika maelezo ya jukwaani, lakini masimilisho mengine yaliwabunia wahusika maneno ya kuongoza tendo hilo.

Uhusika ziada na kapa: Uhusika ziada ni mbinu ya kuumba mhusika ambaye hakisawiriwa katika riwaya na mwandishi. Aghalabu, mhusika huyo alichukua maneno yaliyokuwa yametumika katika usimulizi wa riwaya. Katika uhusika kapa, maneno ya mhusika asiyekuwapo yaliashiriwa kama sauti. Mbinu ya

uhusika kapa ilidhihirika vizuri jukwaani ambapo maneno hayo yalisemwa ama na mwigizaji nyuma ya jukwaa au sauti ya mwigizaji iliyorekodiwa.

Mshindilio: Hii ni mbinu ambayo kwayo matukio mengi ya hadithi hupakiwa pamoja na kuwasilishwa kwa kipindi kifupi cha wakati. Huu ni uwasilishaji wa matukio mengi ya riwaya kwa njia ya muhtasari na kwa pamoja.

Udondoshaji: Udondoshaji ni mbinu ambayo kwayo msimilishaji aliacha kimakusudi habari fulani katika riwaya alipoandika similisho lake. Mbinu ya udondoshaji ilibainika kutegemea fasiri ya msimilishaji kuhusu kile kilichofaa kujumuishwa katika similisho na kile kilichopaswa kuachwa nje.

Katika usimilisho wa matini ya riwaya kuwa matini ya similisho, mbinu zilizotajwa na kuelezewa zilitumika na vikundi vilivyokuwa vikitafitiwa. Matumizi ya mbinu hizo yalifanywa kwa namna iliyodhihirisha tofauti. Baadhi ya vikundi vilitumia mbinu chache miongoni mwa zile zilizotajwa na kuelezewa, huku vingine vikijumuisha mbinu nyingi. Masimilisho ya riwaya ya *Utengano* yalidhihirisha matumizi ya mbinu nyingi yakilinganishwa na lile la riwaya ya *Siku Njema*. Hali hiyo ilitokana na mtindo wa mtunzi wa riwaya, ambapo mtindo changamano, ulihitajia mbinu tofauti tofauti.

Katika sehemu inayofuata, tasnifu hii imezitalii baadhi ya mbinu za usimilisho katika matini kwa undani na kuzielezea katika muktadha wa nadharia changamano. Aidha, mbinu hizo zimejadiliwa kama zilivyobainika kutegemea kikundi na riwaya husika.

5.1.1 Usimulizi

Nafasi ya mwandishi ya kuisimulia hadithi katika riwaya ilichukuliwa na mhusika mtambaji katika masimilisho. Mtambaji alibainishwa kama mmoja wa wahusika katika mazungumzo ya masimilisho.

Masimulizi yalidondolewa kutoka maneno ya riwaya na ubunifu wake ulitegemea msimilishaji. Sura hii ilibaini kwamba, ubunaji wa usimulizi ulisheheni uhuru mwingi wa msimilishaji. Katika uhuru wake, msimilishaji alidondoa, akachopeka na kubatilisha yaliyomo katika usimulizi wa riwaya. Uhuru huo wa kibinafsi ulisababisha tofauti za usimulizi miongoni mwa vikundi teule.

Masimulizi ya kutambwa jukwaani yalibainisha sifa mbalimbali. Zifuatazo ni miongoni mwa sifa zilizobainika sana:

5.1.1.1 Uziada

Hali ya kuyasimilisha maneno yaliyotumika katika riwaya haikufanywa kwa usahihi wa mtazamo wa mwandishi kuhusu maudhui na dhamira ya riwaya. Mara kadha, wasimilishaji walivuka mipaka ya usimulizi wa riwaya na kusimulia nje ya mtazamo wa mwandishi. Mfano kutoka kikundi cha *Jicho Four*:

Waswahili walisema ‘mchimba kaburi huingia mwenyewe’. Ama kweli Bw. Zanga na Bw. Makuudi kwa muda mrefu wamekuwa wakichimba makaburi yao na kama alivyosema Kazija hivi leo ilibidi wazikwe humo...

(Similisho la *Utengano*)

Msimilishaji wa nukuu hili ametumia methali “mchimba kaburi huingia mwenyewe” kuonyesha jinsi wanawake walivyolipiza kisasi kwa Makuudi. Riwaya inaeleza namna Makuudi alivyowadhulumu na kuwadunisha wanawake, na Makuudi alipowaomba kura awe mbunge wao walimnyima. Hata hivyo, fasiri ya methali hii inavuka mipaka ya mtazamo wa mwandishi wa riwaya.

Methali ambayo ingefaa katika muktadha huo ingekuwa “mhini na mhiniwa njia yao moja” kwani Makuudi aliwahini wanawake haki zao nao wakamhini haki ya kuwaongoza. Hali ya kuubadilisha mtazamo wa mwandishi ni ukiushi wa mhimili wa nadharia ya usimilisho unaohimiza vipengele vya maana vihamishwe kwa usahihi iwezekanavyo. Usimilisho unaonuiwa kuinua viwango vya uelewa wa wanafunzi na walimu unapaswa kukitwa kwa maneno ya riwaya.

5.1.1.2 Udondoshaji

Uandalizi wa masimulizi ya kutambwa jukwaani ulidhihirisha sifa ya udondoshaji. Mambo yaliyofikiriwa kuwa na umuhimu mdogo yaliwachwa nje katika usimulizi. Hii ni sifa iliyodhihirika katika masimilisho ya vikundi vyote na riwaya zote teule. Udondoshaji ulinuiwa kuyafupisha masimulio ili kuyafanya yaafikiane na kanuni ya mshindilio inayodhibiti uwasilishaji wa matukio ya hadithi katika drama. Kwa mujibu wa kanuni hii, matukio mengi ya hadithi hupakiwa pamoja na kuwasilishwa kimuhtasari. Packard (1997) anaeleza kuwa, maandishi ya kisimulizi huwa marefu na yenye maelezo, ilhali tungo za kidrama huwa fupi na za kuona. Kwa mfano, udondoshaji ulidhihirika katika simulio la kikundi cha *Jicho Four*, similisho la *Utengano*:

... utengano ulikithiri nyumba ile kweli. Bi Tamima hakuwa na pa kuuweka uso wake. Hapo basi Biti Kocho akamnasihia aende kwao shamba naye Biti Kocho akenda Madongoporomoka kwa Bi. Farashuu. Maimuna naye kwa sasa alikuwa rembeo jingine la jamii. Alikuwa katika utoro wa hiyari na kutendwa. Hakujali kwani alikuwa na kiu ya utengamano, yaani kutoka katika jela ya babaake. Baada ya kuagana na Bi Tamima, Biti Kocho alimwendea Bi Farashuu, kwa hamu na ghamu alimongea mlango.

Nukuu hili limekusudiwa kuelezea utengano uliotokea kwa Bw Makuudi na hatima ya waathiriwa. Hata hivyo, limesondosha habari muhimu kuhusu matamano ya Maimuna na kinaya kilichogubika matamano hayo kama anavyosimulia mwandishi. Udondoshaji ulikuwa muhimu katika maandalizi ya masimulio, ingawa mara nyingi ulifanywa kwa kutozingatia uzito wa vipengele vya maudhui na fani vilivyodondoshwa. Utafiti huu unahimiza udondoshaji ufanywe kwa msingi wa kuondoa uziada katika simulio linalobuniwa.

5.1.1.3 Maelezo na Ubunifu katika Usimulizi

Uhakiki wa masimulio ulibaini kwamba, ubunaji wa usimulizi ulifanywa kutokana na maelezo ya riwaya na ubunifu wa msimulishaji. Ingawa vikundi vingi viliyatumia maelezo ya riwaya neno kwa neno katika ubunaji wa usimulizi, baadhi ya vikundi viliubuni usimulizi kwa kufuata mitindo mbalimbali ya kiufundi. Ubunifu huu uliupa uwasilishaji wa simulio jukwaani uhai, kinyume na pale maneno ya mwandishi yalipokaririwa pasipo na ubunifu wowote wa msimulishaji. Baadhi ya mitindo iliyotumika kuyasanifu masimulio ni kuwepo na kauli za ufunguzi na za uhitimishaji wa simulio. Mfano wa kauli ya ufunguzi:

MTAMBAJI (II): Ukidhani wewe mkali, subiri siku yako.
Wakali wapo wengi. Biti Kocho alikuwa mwanamke kidete
kweli kweli...

(Kutoka kikundi cha *Jicho Four, Utengano*)

Mfano wa kauli ya uhitimishaji kutoka kikundi hicho:

MTAMBAJI (I): ... Mussa angalitamani kukutana
na Kazija kila siku lakini wapi, ilimbidi afuate ratiba
au mkipenda 'programme', kwani yeye na babake walikuwa

wakila chungu kimoja, na kila mtu alikuwa na siku zake.

Lakini leo mambo yalikuwa kinyume. Hebu na tuone.

Katika madondoo haya mawili, msimilishaji amebuni masimulio kwa ubunifu wake lakini akizingatia maelezo ya mwandishi wa riwaya. Mtindo huo wa kusimulia ulitekeleza dhima ya kuwanda watazamaji kujua mwanzo na mwisho wa simulio. Aidha, ubunifu huo ulikata kiu ya watazamaji kuhusu walichotarajia kuona katika maonyesho yaliyofuata. Vilevile, mtindo huo ulitumika kuyaunganisha matukio yaliyofuata na yale yaliyokuwa yamekwishaigizwa. Maandalizi ya namna hiyo yalifanywa kwa kutilia maanani kuwa masimulio hayo yalikuwa yawasilishwe jukwaani.

Mitindo mingine iliyonogesha masimulizi hayo ilihusu matumizi ya methali, nahau, misemo, takriri na tanakali za sauti. Vilevile, lugha ya kuyaandika masimulio hayo ilikuwa ya kiutendaji. Tuzingatie mfano huu kutoka simulio la *Jicho Four*, similisho la *Utengano*:

MTAMBAJI (II): Haya ‘tuyaache hayo’ ya Maimuna
na nyama yenye jichwa kubwa kama sinia la pilau na
‘tumrejeele’ babake Bw. Maksuudi...

Maneno yaliyotumika katika dondoo hili yanaashiria lugha ya kiutendaji ama ya uwasilishaji. Hii ndiyo lugha inayoleta uhai katika usimulizi kinyume na ile iliyotumika kwenye riwaya. Diyanni (2004) anasema kwamba, mazungumzo ya kidrama ni vitendo na yana uwezo wa kuathiri waigizaji na hadhira. Maneno katika mazungumzo na masimulizi ya kidrama yanapaswa kuashiria vitendo vinavyotekelezwa katika uigizaji. Hata hivyo, ubunifu wa namna hiyo ulikuwa adimu miongoni mwa vikundi vilivyokuwa vikitafitiwa.

5.1.1.4 Dhima ya Usimulizi katika Usimilisho wa Riwaya

Utafiti huu ulibaini kwamba usimulizi katika usimilisho hunuiwa kutekeleza majukumu mbalimbali. Kwanza, usimulizi hunuiwa kuwasilisha matukio ya kinathari ambayo hutatiza kuyasimilisha. Matukio hayo hutatiza kutokana na urefu wake, lugha ngumu, udhahanifu, na mandhari yasiyosawirika jukwaani.

Matukio yaliyofasirika marefu kuigizwa jukwaani, yaliigizwa sehemu moja na sehemu nyingine ikasimuliwa. Aidha, sehemu za riwaya zilizotumia lugha ngumu zilisimuliwa bila mabadiliko yoyote. Matukio ya riwaya yaliyosawiriwa kidhahanifu nayo pia yalisimuliwa badala ya kuigizwa.

Ilibainika kwamba matukio kuhusu safari hayakuwa rahisi kuigizwa kikamilifu jukwaani ikizingatiwa uchangamano wake. Kwa sababu hiyo yalisimilishwa katika usimulizi. Katika riwaya ya *Utengano*, safari ya Maimuna kugura Pumziko kuelekea Bobea ilisimilishwa sehemu moja kusimuliwa na sehemu nyingine kuigizwa jukwaani. Hali kama hiyo ilishuhudiwa katika usimilisho wa safari ya Kongowea kutoka Tanga kuelekea Mombasa katika riwaya ya *Siku Njema*.

Pili, usimulizi ulitekeleza dhima ya kuwa dira ama kiunzi kiunganishi katika msuko wa similisho. Kama ilivyobainika, usimilisho uliegemezwa sana kwa matukio yaliyosawiriwa kimazungumzo na kiutendaji. Kwa sababu hiyo, usimulizi ulikuwa muhimu katika kuunganisha sehemu hizo na sehemu nyingine zilizobeba habari zaidi ya hadithi. Baadhi ya masimulio yalianza kwa kuarifu kuhusu mambo yaliyokwisha kushuhudiwa jukwaani, mengine ambayo yalikuwa yamepitikia wahusika wa riwaya na labda hayakuigizwa, na halafu yakahitimisha kwa yale yaliyokuwa yafuate jukwaani.

Tatu, usimulizi ulijitokeza kama mkakati wa kuhakikisha kuwa baadhi ya mbinu za utunzi zimewasilishwa katika uigizaji. Matumizi ya lugha kama vile tamathali za usemi na semi hayakutoa changamoto kubwa kwa ambavyo mbinu hizo ziliwasilishwa kupitia mazungumzo na usimulizi. Wahusika walizifaragua katika mazungumzo yao ama zikatumika na watambaji katika usimulizi. Mbinu zilizoonekana kuwatatiza wasimilishaji ni kama vile ndoto, jazanda, na mbinu rejeshi. Uigizaji wa mbinu hizo ulihitaji ufundi wa hali ya juu. Haya yanajadiliwa baadaye katika sura hii.

Matumizi ya ndoto na jazanda tata kuigiza jukwaani yalipatikana katika riwaya ya *Utengano*. Kuna ndoto mbili alizoota Maimuna akiwa kwa Biti Sururu zilizokuwa za kijazanda. Ndoto ya kwanza ilihusu nyama kubwa ambalo halikuwa na miguu wala mikono na ambalo lilikuwa na majichwa mawili; moja la panya, kubwa kama jabali na jingine la mende, kubwa kama sufuria la pilau na yote yalitisha kummeza Maimuna (uk.96). Ndoto ya pili ya Maimuna ilihusu chatu—mtu aliyekuwa akimfukuza Maimuna na taratibu kubadili sura na kuwa Maksuudi.

Katika usimilisho, ilikuwa vigumu sana kuziwasilisha mbinu hizo jukwaani kwa ufasaha kama zilivyowasilishwa na riwaya yenyewe. Aidha, mbinu hizo zilisanifiwa kwa udhahanifu mwingi ambao haungeweza kupata uhalisi jukwaani. Kwa hivyo, ilihalisi kuzisimulia mbinu hizo na kuweka utendaji mdogo ili kuiwasilisha maana yake kwa usahihi kama alivyodhamiria mtunzi wa riwaya. Usimulizi ulihakikisha kwamba vipengele vilivyozi buni mbinu hizo viliwasilishwa pasipo na mabadiliko yoyote.

Kwa upande mwingine, mbinu rejeshi ilisimuliwa ili kuwiana na msuko wa hadithi. Baadhi ya wasimilishaji waliufaragua msuko wa riwaya ili kuwawezesha kuiigiza mbinu rejeshi. Hata hivyo, ufaraguzi huo haukuwezekana kwa kila tukio lililotumia mbinu hiyo. Kwa mfano, katika riwaya ya *Utengano*, tukio la Mussa kukutana na Kazija katika Klabu Tafrija liliigizwa na baadhi ya vikundi na vikundi vingine vikalisimulia tukio hilo. Ugizaji ulihusisha ufaraguzi wa msuko kuhakikisha kuwa tukio hilo lililetwa mbele ili kuifuta mbinu rejeshi.

Usimulizi wa mbinu rejeshi katika riwaya ya *Siku Njema* ulifanywa na wahusika katika mazungumzo yao. Huo ni usimulizi uliochanganywa na mazungumzo ya wahusika. Bi. Rahma, katika mazungumzo yake na Kongowea, alisimulia wasifu wa Zainabu na wosia aliomwachia kumhusu mwanawe Msanifu Kombo. Vilevile, Amina akizungumza na Kongowea alikisimulia kisa cha kibaradhuli kilichomfika baada ya babake kutalakiana na mamake. Babake wa kambo alimbaka na kumwacha na majeraha ya moyo yaliyompelekea kuwa kahaba. Ingawa similisho liliyaumba maneno yao kama mazungumzo ya kawaida, mazungumzo hayo yalibeba hadithi iliyodhamiriwa kusimuliwa.

Nne, usimulizi ulitekeleza dhima kuu ya kuwasilisha wasifu wa wahusika na mandhari. Vipengele vya wahusika na mandhari kwa pakubwa vilisimilishwa ili vibainike katika ugizaji jukwaani. Hata hivyo, kuna sifa fulani zilizohitaji kusimuliwa ili ziweze kudhihirika ifaavyo na hadhira. Aidha, uteuzi wa wahusika na maandalizi ya mandhari kwingineko ulipungukiwa na ikawa jambo la busara kuambatisha usimulizi ili kuziba udhaifu huo. Kwa mfano, kikundi cha *Jicho Four* kilitumia usimulizi kuelezea sifa za mji wa Pumziko ambapo Maimuna alitoroshewa na Bi. Farashuu. Msimilishaji aliunda simulio hilo hivi:

MTAMBAJI: ... Pumziko, Pumziko kweli. Licha ya ukubwa wake

ambao ungalikadiriwa na jiji lolote la kisasa ... lilikuwa na uzuri wa sifa na mastakimu ya kustarehe. Vilabu vya siku, na nyumba za siri au ukipenda (ma)danguro yalijaa tele. Usiseme sinema na ‘drive-ins’ mbali na mahoteli makubwa, majumba ya kukodi ya kulala na kula na kuoga tena vizuuuuri ...

(Similisho la riwaya ya *Utengano*)

Simulio hili linashadidia umaarufu wa jiji la Pumziko kutokana na ukubwa na uzuri wake. Wasifu huu haungeweza kusawiriwa jukwaani kwa usahihi kama ilivyokuwa katika riwaya. Kwa hivyo, usimulizi ulitumika kuziwasilisha sifa za mandhari na wahusika zilizokosa kubainishwa na mbinu nyingine za usimilisho.

Tano, usimulizi ulitumika na baadhi ya vikundi kama mkakati wa kuichambua riwaya kwa wanafunzi. Baadhi ya matukio yaliyokuwa yakisimuliwa yalifasiriwa na maswala tata yakawekwa kwa lugha wazi iliyokusudiwa wanafunzi. Kwa mfano, tukio la utengano wa familia ya Makuudi, katika riwaya ya *Utengano*, lilifasiriwa hivi na msimilishaji wa *Fanaka*:

MTAMBAJI: ... Utengano. Tayari Makuudi alikwisha jitenganisha na Kazija, mtoto wake Mussa, kisha Maimuna alikuwa ametoroka nyumbani na sasa Bi. Tamima na mtumishi wake Biti Kocho. Ama kweli utengano ulikuwa umekithiri nyumba ile ya Bw. Makuudi...

Simulio hili lilibuniwa kimakusudi ili kuwafafanulia wanafunzi mifano ya utengano wa kifamilia uliokuwa umeshuhudiwa nyumbani kwa Bw. Makuudi. Mwanzoni mwa similisho, msimulizi alikuwa ameyateka makini ya hadhira na kuwataka wawe makini kushuhudia utengano ambao ungedhihirishwa na riwaya hiyo.

Baadhi ya vikundi vilitumia usimulizi katika utangulizi wa masimilisho kwa dhima ya kuichambua riwaya husika kwa kifupi. Dhima ya usimulizi huo ilikuwa kuifafanua anwani ya riwaya, kugusia maudhui yaliyomo, na kuufafanua mgogoro mkuu na wahusika wake.

Mbinu ya usimulizi ni muhimu katika usimilisho wa riwaya. Booth na wengine (2006) wanasema kwamba, tamthilia inaweza kumtumia mtambaji kando ya jukwaa ili kuifafanulia hadhira yanayojiri jukwaani. Usimulizi uliobuniwa katika masimilisho ulidhamiriwa kusemwa na mtambaji jukwaani. Nadharia changamano hutambua umuhimu wa usimulizi katika uwasilishaji wa hadithi kama alivyodhamiria mwandishi. Lhermitte (2005) ansema kuwa, katika kusimilisha vipengele vya maana kama usimuliaji hutakiwa kuhamishwa kama vinavyobainishwa na mwandishi. Kwa kuzingatia mhimili huu, hali ya ubunaji wa masimulio ilidhihirisha udhaifu unaopaswa kusahihishwa. Uhuru usio na mipaka wa kuyabuni masimulio; ulioongeza, ukadondoa, na kubatilisha usimulizi halisi wa riwaya, haupaswi kushirikishwa kama sifa ya mbinu ya usimulizi. Hii ni kwa sababu hali ya kuongeza, kudondosha, na kubatilisha maelezo ya riwaya inapotosha yale yanayotahiniwa wanafunzi katika mitihani.

Usimulizi hutarajiwa kuwasilisha vipengele mbalimbali katika hadithi ambavyo hutatiza hali ya kuviigiza jukwaani. Nadharia ya uigizaji hutambua usimulizi kama nyenzo moja ya kuiwasilisha hadithi katika drama. Usimulizi unapobuniwa kwa uzingatifu wa mihimili hii, usimilisho aminifu utafikiwa kikamilifu. Udhaifu uliobainika miongoni mwa masimilisho ulitokana na matumizi machache na yasiyofaa ya usimulizi.

5.1.2 Mazungumzo

Usimilisho wa riwaya hufuata muundo wa kitamthilia wa mazungumzo na matendo. Utanzu wa riwaya hutumia mtindo wa mazungumzo katika usimulizi wa hadithi. Hii ni sifa ya mwingiliano tanzu inayobainishwa na utanzu wa riwaya. Hata hivyo, mtindo wa mazungumzo ulibainika kutegemea mtindo uliotumika kuibuni riwaya. Riwaya ya *Utengano* ilitumia mbinu ya mazungumzo kwa wingi kuiliko riwaya ya *Siku Njema*. Hali hiyo ilionekana kurahisisha usimilisho wa riwaya ya *Utengano*.

Kuna mitindo mitatu iliyotumika kuyabuni mazungumzo. Kwanza, mazungumzo ya riwaya yalifanywa mazungumzo ya similisho. Katika sehemu fulani, mazungumzo hayo yalidondolewa bila mabadiliko yoyote. Lakini kuna sehemu ambapo mazungumzo hayo yalifanyiwa mabadiliko. Mathalan, kikundi cha *Jicho Four* kilifanyia mazungumzo yafuatayo mabadiliko katika similisho lao la riwaya ya *Utengano*:

MAIMUNA: (Akidondokwa na machozi) Mama usifanye ‘vyo.
 Ikiwa kuogopa kuvunja miko ya nyumba hii, tusiogope.
 Naivunjwe leo hiyo miko. Hujui utazaa vipi mama.
 Tutangojea idhini ya mtu asiyekuwepo mpaka lini? Basi yeye
 baba hatofahamu ilibidi tukuchukue hospitali au tumwite mkunga.

BI KOCHO: Kweli bibi, mimba ya kwanza ulizalia hapa
 nyumbani, ya pili pia hivyo na hii ya tatu ndiyo haina
 mkunga wala daktari.

BI. TAMIMA: (Kwa maumivu) Maim-u, mmu... na
 babaako hataki tutoke nje ila kwa ruhusa yake, na humu
 asiingilie mtu ila kwa ruhusa yake.

Huu ni mfano wa mazungumzo yaliyofanyiwa mabadiliko. Usemi wa Biti Kocho ulitoholewa kutoka usimulizi wa riwaya, na katika muktadha wa mazungumzo haya. Kwa namna hiyo, mazungumzo ya riwaya yamehamishwa pamoja na sehemu ya usimulizi ili kuiwasilisha hadithi kama ilivyoendelezwa katika muktadha wake.

Pili, mazungumzo yalibuniwa kulingana na ujumbe na mtazamo wa riwaya. Ubunaji wa mazungumzo namna hiyo ulitegemea ubunifu wa msimilishaji na fasiri yake kwa dhamira na maudhui ya riwaya. Zingatia mfano ufuatao kutoka similisho la *Siku Njema*:

BIBIYE KONGOWEA: Yamenitosha ukewenza.

Boma hii hainiweki tena. Nataka janga la kwanza

lisinipate hapa. Umasikini na uhasama kila uchao ...

sistahimili tena ...

MKE MWENZA 1: (Akimsihi) Vumilia ... vumilia ...

vumilia jamani!

(Similisho la *K.I.C.D, Siku Njema*)

Mazungumzo haya yamebuniwa kutokana na usimulizi wa riwaya. Kuchipuka kwa ugomvi wa wakewenza wa Makame Mwinyi kunakorejelewa kulielezwa na usimulizi wa riwaya hiyo. Msimilishaji wa similisho hili aliyabuni mazungumzo haya kwa uzingatifu wa maudhui na mtazamo wa mwandishi kuyahusu.

Tatu, mawazo ya wahusika yalifanywa mazungumzo yao. Huu sio uzungumzi nafsi, bali ni fikira za mhusika zilizonakiliwa na msimilishaji kama maneno ya kuashiria mawazo yake. Aghalabu, jukwaani, mawazo hayo ya wahusika yalirekodiwa na kusomwa kwa sauti zao. Zingatia mfano kutoka kikundi cha

Fanaka kilichoyabadilisha mawazo ya Rashid, katika riwaya ya *Utengano*, kuwa maneno yake:

RASHID: (Akiwaza) Leo nimekwenda marikiti kununua nyama ya bwana. Niliporudi nilitumwa kwa dobi kuchukua nguo za bwana. Tena nikenda kununua sanduku la chupa za bia, nikazipeleka. Rudi kwa yule bibi ... nani vile ... Bibi ... Kazi ... Kazija, ndiyo Kazija ...

Mbinu ya kuyageuza mawazo ya wahusika kuwa mazungumzo yao ilikuwa muhimu katika usimilisho. Kulingana na Diyanni (2004), ingawa mazungumzo katika tamthilia hutekeleza dhima tatu kuu: kuendeleza ploti, kukuza mandhari, na kuwabainisha wahusika, dhima yake muhimu huwa ni kuwabainisha wahusika. Mazungumzo ya wahusika yaliyobuniwa yaliweza kuwasilisha mawazo yao, yaliyokuwa muhimu katika kuelewa wasifu wao na maudhui waliokuwa wakiwasilisha.

Matumizi ya mazungumzo katika usimilisho wa riwaya yalinuiwa kuabadilisha muundo wake ili uafikiane na ule wa tamthilia. Kwa mujibu wa Wamitila (2008), mazungumzo ya wahusika ni mojawapo wa njia tatu muhimu za usimulizi katika matukio ya drama. Mazungumzo ndiyo huchukua nafasi kubwa ya usimuliaji wa hadithi katika matini ya tamthilia. Hali hiyo ni tofauti katika riwaya ambapo sehemu kubwa ya usimuliaji huchukuliwa na usimulizi. Utafiti huu uliweza kubaini kwamba, sifa za usimulizi na mazungumzo hudhihirika katika tanzu za riwaya na hadithi fupi.

Katika matumizi ya nadharia changamano ili kuhakiki usimilisho wa riwaya, utafiti uliweza kugundua udhaifu wa nadharia hii katika kuelekeza namna mazungumzo yanavyopaswa kusimilishwa. Nadharia ya usimilisho inahimiza

vipengele vya maana vihamishwe kwa usahihi kama vilivyo katika matini chasili (Lhermitte 2005). Namna ya kuyafanya mazungumzo yaafikie usahihi huo haionyeshwi. Licha ya kwamba nadharia ya uigizaji inatoa kaida za kuyabuni mazungumzo ya kidrama, ukweli ni kwamba, haina msingi unaoweza kutumika ili kuyageuza ‘maneno’ ambayo hayakudhamiriwa kuigizwa kuwa ya kidrama. Udhaifu huo wa kinadharia unaifanya nadharia changamano kushindwa kuelekeza jinsi mazungumzo ya riwaya yanavyoweza kusimilishwa yawe ya kidrama.

Kuna haja ya kuwepo na msingi wa kufuatwa katika usimilisho na uhakiki wa mazungumzo. Msingi huo unapaswa kuelekeza jinsi mazungumzo ya riwaya yanavyoweza kusimilishwa kwa usahihi ili kubuni matini ya kitamthilia. Uchanganuzi wa masimilisho ulibaini ufanisi na upungufu wa wasimilishaji katika ubunaji wa mazungumzo sahihi. Masimilisho yaliyodhihirisha uaminifu katika usimilisho wa mazungumzo ya riwaya ni yale yaliyoyadondoa mazungumzo hayo na kuyawasilisha pasipo kuyafanyia mabadiliko yoyote. Mazungumzo yaliyobuniwa kutokana na usimulizi na mawazo ya wahusika yalifanywa kwa uzingatifu wa maudhui na fani. Usimulizi ulitumika kuwasilisha sehemu za riwaya ambazo hazingeweza kusimilishwa kuwa mazungumzo. Huu ni mwelekeo unaoweza kufuatwa kama msingi wa kuyasimilisha mazungumzo ya riwaya kuwa ya kitamthilia. Usahihi katika usimilisho wa mazungumzo ni kwa kigezo cha maudhui na fani ya riwaya, lakini si kwa utiifu wa kanuni na sheria za utunzi wa mazungumzo ya kitamthilia. Mazungumzo ya riwaya yanaweza yakakosa sifa za mazungumzo ya kidrama, kwani riwaya nyingi hazitungwi kuigizwa.

5.1.3 Udondoshaji

Udondoshaji ni mbinu ambayo kwayo msimilishaji huacha kimakusudi habari fulani katika riwaya anapoandika similisho lake. Utanzu wa riwaya hubeba masuala mengi kutokana na urefu wake. Utafiti ulibaini kwamba baadhi ya masuala yalikuwa yakiachwa nje katika mchakato wa kuisimilisha riwaya. Ingawa lilikuwa chaguo la msimilishaji kudondosha masuala fulani, kigezo cha kufanya hivyo kilikuwa uzito wa maudhui na fani zilizodondoshwa.

Udondoshaji ulifanywa kwa sababu kadha wa kadha. Kwanza, ni uchangamano wa tukio la kuigizwa. Matukio yaliyotatiza uigizaji na usimuliaji yalidondoshwa. Mazishi ya Zainabu katika riwaya ya *Siku Njema* hayakusimuliwa wala kuigizwa na msimilishaji. Mazishi hayo yanasimuliwa:

Nikumbukapo siku ya mazishi ya mama, machozi hunilengalenga machoni.

Maziara ya umma mjini Tanga yalijaa watu sisisi. Hapakuwa na nafasi ya hata kutema mate wala nzi kupita. Wapo waliopiga usiahi na waliolia kwa shake. Huzuni ilitawala katika nyoyo na nyuso za watu.

(*Siku Njema* 1996, uk. 15)

Tukio hili halikusimilishwa kuigizwa wala kusimuliwa kutokana na matakwa mengi ya kuliigiza. Kuweka tukio hilo jukwaani kulihitaji ubunifu mkubwa na huenda hata kwa kufanya hivyo athari yake haingehisika kama ilivyotarajiwa. Hali hiyo ilipelekea kudondoshwa kwake, ingawa hamkuwa na sababu thabiti ya kutolisimulia tukio hilo. Kutoliigiza ama kulisimulia tukio hilo hakukuzingatia kigezo cha uzito wa maudhui na fani. Kwa sababu hiyo, habari muhimu na jinsi ilivyowasilishwa na riwaya iliwachwa nje na similisho lake. Udondoshaji wa namna hiyo ulikosa kuwazingatia wanafunzi ambao azma yao ilikuwa kuitazama riwaya katika vipengele vyake vyote kama wanavyotahiniwa.

Pili, udondoshaji ulifanywa kwa madhumuni ya kuyawacha nje matukio yaliyofikiriwa kutokuwa na athari kubwa katika riwaya. Kwa mfano, katika riwaya ya *Utengano*, wasimilishaji wengi waliyadondosha matukio yaliyohusu maisha mapya ya Maimuna Futoni kabla akutane na Kabi. Usimilisho wa matukio katika mandhari ya Futoni uliangazia harakati za uchumba wa Maimuna na Kabi. Kwa kufanya hivyo walibainisha jinsi hawakuona uzito wa sehemu hiyo katika athari nzima ya kuelezea maisha mapya ya Maimuna. Hatima ya mabadiliko ya Maimuna ilikuwa kukubali ndoa, ambayo awali alikuwa ameghairi, jambo ambalo lilipewa uzito zaidi na wasimilishaji hao. Hali hiyo ilidhoofisha usawiri wa Maimuna kwa kuondoa sehemu muhimu zake. Kwa namna hiyo, udondoshaji uliathiri kwa njia hasi namna wanafunzi walivyoupokea wasifu wa Maimuna.

Tatu, udondoshaji ulifanywa kwa misingi ya kiusanifu. Huu ni udondoshaji uliofanywa ili kutimiza malengo fulani ya usanifu wa similisho. Ili kuafikia muundo wa kitamthilia katika usanifu wa masimilisho, baadhi ya wasimilishaji waliyahamisha mazungumzo ya riwaya na kudondosha sehemu ya usimulizi. Huu ulijitokeza kama udhaifu katika usimilisho. Udondoshaji wa aina hiyo ulifanywa kwa madhumuni ya kuyabuni masimilisho mafupi. Ingawa kulikuwako na malengo mahsusi ya udondoshaji wa aina hii, hali ya kutozingatia kigezo cha uzito wa maudhui na fani iliudhoofisha usimilisho.

Hali ya kuyadondosha matukio fulani ya riwaya iliongozwa na madai ya misingi ya nadharia ya usimilisho. Kwa mujibu wa Hutcheon (2013), majadiliano ya hadithi hupotea katika usimilisho, lakini vipengele vya hadithi hutafutiwa visawe katika mfumo wa similisho. Msingi huu unahimiza udondoshaji wa ‘majadiliano’ ama sehemu za riwaya zinazoendeleza mawazo yaliyo sawa. Udondoshaji

uliobainishwa na masimilisho ya riwaya haukuzingatia msingi huo kikamilifu. Baadhi ya sehemu zilizodondoshwa ni zile zilizobeba maudhui muhimu ya riwaya. Ili kuitumia mbinu ya udondoshaji kwa ufanisi na kudumisha usahihi wa matini chasili, utafiti huu umependekeza kigezo cha uzito wa maudhui na fani, ambacho kinaweza kuimarisha msingi huu. Iwapo kigezo hicho kitazingatiwa kikamilifu, visehemu muhimu badala ya kudondoshwa vinaweza vikawa usimulizi, mazungumzo ya wahusika, na hata utendaji.

5.1.4 Mshindilio

Mshindilio ni mbinu ya usimilisho ambapo matukio ya riwaya hupakiwa katika kipindi kifupi cha wakati wa similisho. Hali hii hutokana na suala la ufupi wa drama, ufupi wa wakati wa kuigiza, na uwezo wa hadhira kumakinikia igizo refu. Booth na wengine (2006) wanahoji kuwa, drama hufupisha na kurahisisha wasifu wa wahusika kwa vile ina muda wa takriban masaa mawili kudhihirisha visa na hulka zao pasipo kutumia maelezo ya kimsingi mbali na maelezo ya utangulizi. Matukio yanaposhindiliwa pamoja huwa na maana kwamba muda wake wa kuwasilishwa huwa tofauti na ule wa kutendeka kwake katika riwaya.

Usimilisho wa riwaya ya *Utengano* una mifano kemkem ya mbinu ya mshindilio. Mbinu ya mshindilio ilitumika katika riwaya hiyo kwa madhumuni ya kufuta muda mrefu wa matukio na kuyafanya yafanyike kwa muda mfupi katika similisho na jukwaani. Aidha, matumizi ya mbinu ya mshindilio yaliafiki katika maandalizi ya masimulio yaliyolengwa kusimuliwa hadhira na wasimulizi. Matukio yaliyochukua muda mrefu kufanyika yalipakiwa pamoja kana kwamba yalifanyika katika kipindi kimoja na kifupi cha wakati. Mfano mwafaka

umerejelewa kutoka similisho la riwaya ya *Utengano* kuhusu wasifu wa Maksiudi:

...Uhuru ulipatikana na mkoloni akatoweka na hapo Maksiudi aliweka wazi nia yake. Kwa sababu aliaminiwa kutokana na juhudi zake za kumtimua mkoloni, Maksiudi alipewa madaraka akawa mkuu wa wilaya, hapo hakukaa alivuliwa mbeleko lakini kwa bahati nzuri akafanywa kuwa mkurugenzi wa shirika la Bima la Taifa. Akamuoa Mwanasururu. Akamtenga na kuoia Bi. Tamima, wakawazaa, Mussa na Maimuna na wa tatu sasa angali tumboni...

(Kutoka similisho la *Fanaka*)

Habari inayowasilishwa na kifungu hiki cha simulio ilikuwa imechukua muda mrefu katika riwaya. Hata hivyo, simulio hili limeipakia pamoja na kufuta dhana ya wakati husika. Msimilishaji ameitumia mbinu hii ili kuufupisha wakati wa matukio katika jaribio la kutimiza matakwa ya sifa ya ufupi katika drama. Usimilisho wa riwaya ya *Siku Njema* vilevile ulidhihirisha matumizi ya mbinu hii.

Kulingana na Hutcheon (2013), msimilishaji anaweza kuvifupisha vihadithi katika hadithi na kuufinya muda wake. Habari kuu ya vihadithi hivyo huchukuliwa na kuwekwa pamoja kwa madhumuni ya kusimuliwa kwa njia ya muhtasari. Kama ilivyotanguliwa kusemwa, drama haipaswi kuchukua muda mrefu kuigizwa jukwaani. Wamitila (2008) ameeleza mshindilio kama mojawapo ya kanuni tatu zinazotumika kudhibiti uwasilishaji wa matukio ya hadithi katika drama. Kwa ambavyo riwaya haikuandikwa kuigizwa, kanuni ya mshindilio iliwawezesha wasimilishaji kuiwasilisha hadithi ya riwaya kwa muda wa drama.

5.1.5 Ubunaji wa Maelezo ya Jukwaani

Mohamed (1995:62) anaeleza umuhimu wa maelezo ya jukwaani hivi:

Ili maana na taathira ya kisanaa iwe kamili, sehemu ya maelezo ya jukwaa ni muhimu sana katika tamthilia yoyote ile. Umuhimu huu unatokana na kwamba, katika tamthilia hakuna maelezo ya mandhari, mavazi na nyakati mbalimbali za uhai wa kadhia yote ya tamthilia ... hakuna maelezo na simulizi tunazozikuta kwenye riwaya na hadithi fupi, bali kuna utendaji unaosimamia maelezo na simulizi. Hali hii kwa hivyo, inalazimisha kuwepo maelezo mafupi mafupi ya jukwaa yanayoshughulikia vifaa, samani, mavazi, mapambo, mazingira na hata matendo ya wahusika.

Riwaya huwasilishwa kisimulizi jambo linaloiwezesha kubeba maelezo mengi ya wahusika, mandhari, na utendaji. Packard (1997) anasema kwamba, utungo wa kisimulizi hutumia msimulizi kutufafanulia msingi wa matukio, mandhari, na hadithi, ilhali utungo wa kidrama haumhitaji msimulizi kwani hadhira inatarajiwa kuyaona matukio kadri yanavyofunguka jukwaani. Ili kuiwasilisha hadithi ya riwaya kitamthilia, msimilishaji hana budi ila kuyabuni maelezo ya jukwaani ambayo yanatarajiwa kuongoza uigizaji wa similisho. Maelezo ya jukwaani yalibuniwa kutimiza dhima fulani katika similisho. Kwanza, maelezo ya jukwaani yalielekeza utendaji katika similisho. Mara nyingi yalikuwa yakifafanua kitendo kilichokuwa kikitarajiwa kutoka kwa wahusika. Kikundi cha *Nairobi Theatre Group* kilibuni maelezo haya ya jukwaani kuongoza utendaji katika riwaya ya *Utengano*:

Punde dereva anasikia hatua za viatu zikiteremka ngazi toka mle ndani ya jumba. Hima, anafungua mlango wa gari. Bwana mkubwa anaingia. Kavaa kanzu ya melmel, koti na suruali. Kichwani ana kofia ya viua, miguuni viatu vya buti vyekundu vinang'aa.

Maelekezo haya yalinuiwa kuongoza vitendo vya waigizaji Maksuudi na Rashid jukwaani. Ubunaji wa maelekezo hayo ulizingatia masimulizi ya riwaya kuhusu

kitendo kinachorejelewa. Kwa namna hiyo, nafasi ya usimulizi katika riwaya ilitekelezwa na maelezo ya jukwaani katika matini ya similisho.

Pili, maelezo ya jukwaani yalichukua nafasi ya usimulizi katika uelezaji wa sifa za wahusika na mandhari. Katika riwaya, usimulizi ulitumika kuwasilisha wasifu wa vipengele hivyo vya fani, lakini similisho likaendeleza hayo kupitia maelezo ya jukwaani. Zingatia mfano ufuatao:

Ukumbini kwa Kazija. Madirisha matatu na yote ni vioo vilivyoziwa kwa ndani na vitambaa. Upande wa kushoto meza tayari imetandikwa kwa vyakula. Kazija mwanamke mrembo mwenye rangi ya kunde amesimama mbele ya kioo anamaliza hatua yake ya mwisho ya kujikwatua. Saa ilioko ukutani inaonyesha ni saa tatu za usiku. Mlango unabishwa taratibu.

(Kikundi cha *Jicho Four, Utengano*)

Maelezo haya ya jukwaani yamefumbata wasifu wa mhusika na mandhari yake. Ubunaji wa maelezo ya jukwaani ulifanywa kwa jinsi tofauti na wasimilishaji.

Tatu, maelezo ya jukwaani yalitumika kuongoza mazungumzo ya wahusika na hali zao jukwaani. Kwa vile similisho lililengwa kuigizwa, wasimilishaji walibuni maelezo ambayo yangewaongoza waigizaji katika kufuata mkondo wa mazungumzo na hali iliozingatia dhamira ya riwaya. Zingatia mfano ufuatao kutoka similisho la *Nairobi Theatre Group, Utengano*:

{Bwana Maulidi, mkuu wa anasa na tafrija wa Rumbalola, anapita nyuma ya nyumba ya Biti Sururu. Anevutiwa na sauti ya Maimuna na kujitoma chumbani kwa Maimuna bila hodi. }

MAIMUNA: (Akishtuka na kufurukuta kanga ili kujisitiri) Ala! mbona waingia bila hodi.

MAULIDI: Samahani, usitie shaka. Nimevutiwa na sauti yako ya

kupendeza. Kwa kweli, umekirimiwa kipawa kikubwa.

MAIMUNA: (Akibabaika) Asante sana.

Maneno yaliyofungiwa kwenye mabano yanastahili kuzingatiwa katika utendaji jukwaani. Msimilishaji amezingatia hali za wahusika na tendo kama zilivyowasilishwa na mtunzi katika riwaya.

Maelezo ya jukwaani yanaorodheshwa na nadharia ya uigizaji kama jinsi moja ya usimulizi katika matini ya drama. Diyanni (2004) anaeleza kwamba, utanzu wa tamthilia una uhusiano na tanzu za riwaya na ushairi. Hii ni kwa sababu tamthilia husheheni sifa za usimulizi. Tamthilia husimulia hadithi kupitia kwa msuko. Tamthilia kama riwaya hutegemea mazungumzo na maelezo kusimulia hadithi, na usimulizi huo huchukua umbo la maelezo ya jukwaani, kauli zinazoeleza wahusika, maonyesho, na utendaji. Hali ya kuingiliana katika tanzu za tamthilia na riwaya ilionekana kurahisisha ubunaji wa maelezo ya jukwaani.

Katika usimilisho, maelezo ya jukwaani hutekeleza dhima kuu ya kuwasilisha vipengele vya maana ambavyo haviwezi kuwasilishwa na usimuliaji, mazungumzo na matendo. Mandhari, wahusika na uhusika wao, ni vipengele vilivyotegemea sana maelezo ya jukwaani kuvikamilisha namna vilivyokuwa katika riwaya. Msimilishaji hutakiwa kuwasilisha vipengele vya maana ya riwaya kwa similisho lake kama vinavyobainishwa na mwandishi wake. Maelezo ya jukwaani yaliyobuniwa katika masimilisho yalionekana kuzingatia msingi huu. Ingawa riwaya nyingi hazitungwi kuigizwa, ilibainika kwamba, usimulizi wake hudhihirisha sifa za maelezo ya jukwaani. Maelezo ya mandhari, wahusika, na utendaji ni sifa ya kimwingiliano matini inayobainika katika tanzu za tamthilia na riwaya.

5.1.6 Ufaraguzi wa Msuko

Dhana ya ufaraguzi wa msuko inatumika kufafanua mbinu ya usimilisho ambayo kwayo msuko wa riwaya hufaraguliwa na kupangwa kihadithi katika similisho, ili uigizaji wake jukwaani uingiliane na utendekaji wa matukio kiwakati. Ili kuifafanua dhana ya ufaraguzi wa msuko kwa ufasaha, inatubidi kupata fasiri ya dhana mbili muhimu za muundo: hadithi na msuko. Wamitila (2008:283) anaeleza kuwa:

Hadithi ni ule mfuatano wa matukio kutegemea kutokea kwake kiwakati.

Msuko ni ule mfuatano wa matukio kutegemea kutokea na kusababishana kwake pamoja na jinsi matukio hayo yanavyohusiana kimantiki.

Kutokana na fasiri hii, inabainika kwamba, tofauti kati ya dhana hizi ni jinsi matukio yanavyopangwa katika kazi ya fasihi. Msuko wa moja kwa moja huenda sambamba na hadithi ya kazi husika. Kwa upande mwingine, msuko changamano huashiria mpangilio tofauti wa hadithi na msuko.

Riwaya zilizohakikiwa usimilisho wake zilisukwa kichangamano. Wasimilishaji wengi waliamua kuufaragua msuko wake ili uumane na hadithi ya riwaya hizo. Kwa kufanya hivyo, matukio yaliyowasilishwa kupitia mbinu rejeshi yalipanguliwa na kufanywa kutendeka kabla ya matukio yaliyokuwa yameyatangulia. Msuko wa moja kwa moja huwa ni mwepesi kueleweka na kuigizika. Ikizingatiwa kuwa dhamira kuu ya maonyesho hayo ilikuwa

kuwasaidia wanafunzi na walimu kuelewa riwaya husika, mbinu hiyo iliwarahisishia mtiririko wa hadithi.

Riwaya ya *Utengano* ilisimilishwa na vikundi vingi kwa kuufaragua msuko wake na kuwezesha tukio la kwanza la hadithi kutangulia. Tamthilia-riwaya ya *Utengano* ilitanguliza na tukio katika Klabu Tafrija ambapo wasomaji na watazamaji walikutanishwa na wahusika Mussa na Kazija wakiendelea kuburudika na mwishowe wakajuana na kuwa wapenzi. Wasimilishaji waliunda mazungumzo baina ya wahusika hao wawili kwa kufuata maneno yaliyotumiwa na mwandishi katika riwaya. Tukio lililokuwa limetangulia katika riwaya ilibidi lifuate baada ya hilo kufanyika.

Katika riwaya ya *Siku Njema* mbinu ya ufaraguzi wa msuko ilitumika. Matukio yaliyotokea shuleni Tanga, ambamo Kongowea alikuwa akisomea, yalipangwa kutokea namna yalivyofuatana kiwakati. Tukio lililotangulia lilikuwa la Kongowea kupelekwa shule mnamo Januari 1962.

Matukio hayo yalipanguliwa na kupangwa upya ili yafuatane na wakati wa kutokea kwake. Hamon (1977), akielezea kuhusu nadharia ya usimilisho alihoji kuwa, msuko wa riwaya unaweza ukafaraguliwa na mwendo wa hadithi ukaumbwa upya katika harakati za kuisimilisha. Msingi huu wa nadharia ya usimilisho uliumana na kanuni ya mpishano katika nadharia ya uigizaji ambayo hutumika ili kudhibiti uwasilishaji wa hadithi katika drama. Kanuni ya mpishano, kama anavyoeleza Wamitila (2008), hutumika katika usukaji wa drama ili kuepuka matumizi ya mbinu rejeshi katika msuko wake. Usimilisho wa riwaya ulilenga kuwasilisha muundo wa similisho ambao ulikuwa rahisi kuigiza jukwaani, na kufuatiliwa na wanafunzi. Hali ya kupanga upya msuko

haikubainika kuathiri kwa namna hasi uelewa wa wanafunzi wa matukio ya riwaya. Hata hivyo, kwa mwanafunzi ambaye hakuwa ameisoma riwaya ifaavyo angeweza kutatizika kung'amua matumizi ya mbinu rejeshi iwapo angekabiliwa na swali hilo katika mtihani.

5.2 Mbinu za Usimilisho Jukwaani

Sehemu hii ilizichunguza mbinu za usimilisho katika uigizaji wa similisho. Hatua ya kulisimilisha similisho jukwaani husawiana na ile ya uigizaji wa matini ya tamthilia yoyote ile. Hatua hii ndiyo inayoikamilisha shughuli ya usimilisho wa utungo wa kinathari.

Usimilisho wa riwaya jukwaani ulidhihirisha matumizi ya mbinu tofauti tofauti kutegemea eneo la uigizaji, kikundi husika, na riwaya iliyokuwa ikiigizwa. Eneo la uigizaji liliathiri mbinu zilizotumika kuigiza similisho la riwaya fulani. Similisho la kuigizwa nalo lilitegemea msimilishaji na kikundi chake. Fasiri za wasimilishaji ziliathiri mbinu walizoteua. Utafiti ulibaini kwamba, mtindo wa riwaya uliathiri mbinu ambazo zingetumika kuisimilisha.

Kwa kuwa mbinu za usimilisho jukwaani zilidhihirika katika maeneo ya uigizaji, tasnifu hii iliweza kuziainisha mbinu hizo kwa kuzingatia maeneo matatu ya uigizaji zilikobainika:

I. Majukwaa ya shule

II. Majukwaa ya thieta, na

III. Majukwaa ya mseto

Majukwaa ya thieta yalitumika na vikundi vilivyofanyia maigizo yake katika gatuji la Nairobi. Yale ya shule yalitumika na vikundi vilivyoigizia katika shule

za upili za Kisasi na Ikanga katika gatuji la Kitui. Majukwaa ya mseto yalitumika na kikundi kilichokuwa kimeyanasa maigizo yake katika filamu. Kikundi hicho kilitumia majukwaa ya shule, thieta na yale wazi.

Majukwaa ya thieta yalibainisha mbinu zifuatazo za usimilisho katika uigizaji wa riwaya ya *Utengano*: matumizi ya mtambaji, utendaji, uzungumzi nafsi, usemaji wa mawazo ya mhusika, sauti, muziki, mandhari, pazia, uangazaji, uigizaji wa mbinu, uhusika kapa, uhusika ziada, mazungumzo, na uteuzi wa wahusika.

Katika uigizaji wa riwaya ya *Utengano* shuleni, mbinu zifuatazo za usimilisho jukwaani zilibainika: matumizi ya mtambaji, utendaji, sauti, muziki, mandhari, udondoshaji na uigizaji wa mbinu, mazungumzo, usemaji kando, uzungumzi nafsi, na uteuzi wa wahusika.

Majukwaa ya mseto katika uigizaji wa riwaya ya *Siku Njema* yalidhihirisha mbinu zifuatazo za usimilisho jukwaani: matumizi ya maandishi, mtambaji, utambaji wa wahusika, uigizaji wa mbinu, utendaji, pazia, sauti, muziki, mazungumzo, usawiri wa mandhari na wahusika.

Mbinu ambazo zimejadiliwa na utafiti huu ni kama vile: matumizi ya msimulizi, ubunaji wa mbinu za kiutendaji, uteuzi wa wahusika, matumizi ya jukwaa, matumizi ya mazungumzo, na uigizaji wa mbinu za utunzi. Hizi ndizo zilizotumika kwa wingi katika uigizaji.

5.2.1 Matumizi ya Msimulizi

Masimulio yaliyoandaliwa katika similisho yaliyakinishwa jukwaani. Mtambaji alikuwa mhusika katika similisho na mwigizaji jukwaani. Baadhi ya vikundi havikuitumia mbinu hiyo ya msimulizi kwa ukamilifu wake, na mtambaji

alijitokeza tu katika baadhi ya matukio ya kusimuliwa. Packard (1997) anasema kuwa kuna tamthilia ambazo hutumia watambaji, lakini kwa minajili ya kutimiza athari fulani. Mojawapo ya sababu za kuwatumia watambaji huwa ni kuunganisha matendo kiwakati na kimahali. Uhakiki wa mbinu ya kumtumia mtambaji ulidhihirisha matumizi ya mitindo mbalimbali kutegemea ufundi wa msimilishaji wa kikundi.

Kwanza, kuna utambaji uliofanywa na watambaji wawili kwa kupokezana nafasi. Usimulizi huo ulionekana kufanywa kwa matukio marefu yaliyokuwa yakisimuliwa. Kila mtambaji alikuwa na sehemu aliyotengewa ya kusimulia. Utambaji wa aina hiyo ulionekana kupata ufanisi kwa vile watambaji walikuwa na fursa ya kufafanulia hadhira baadhi ya mambo ambayo hayakujitokeza wazi jukwaani ama katika riwaya.

Mbinu ya kuwatumia watambaji wawili ilitumika na kikundi cha *Jicho Four*. Huu ni mkakati ambao ulionekana kuhamishwa kutoka utambaji wa simulizi (narratives) katika mashindano ya kitaifa ya drama. Mbinu hiyo inahulutisha mitindo ya kiutambaji kutoka watambaji wawili tofauti. Fauka ya haya, masimulio yalikuwa mafupi na watambaji waliyafanya kwa kuelekezana na kukumbushana.

Pili, waelekezi walimtumia mtambaji aliyekuwa mhusika katika matukio yaliyokuwa yakisimuliwa. Kwa namna hiyo, matukio mengi yaliyosimuliwa ni yale yaliyoruhusu kuhusika kwa mtambaji huyo. Ingawa usimulizi ulifanywa kama unaoripotiwa na shahidi, simulio la similisho lilikuwa limeandaliwa kwa kuifuata riwaya. Jambo hilo liliashiria kuwepo na usimilisho mwingine jukwaani, pale mtambaji alitia ubunifu wake katika kusimulia visa na kufaragua maneno

yaliyokuwa yametumika na msimilishaji. Aidha, mtambaji mhusika alisawiriwa kuakisi sifa mbalimbali za matukio aliyoyasimulia. Baadhi yao walijitokeza jukwaani kama walevi, wadaku, jamaa za wahusika, na wandani.

Hali ya kumtumia mhusika mtambaji ilikuza uhai katika usimulizi kwa kuifanya hadhira kuamini kwamba yaliyosimuliwa yalikuwa yameshuhudiwa kutokea kwake. Hata hivyo, matumizi ya mbinu hiyo yalipata ufanisi katika matukio ambayo ilihalisi kuitumia. Usimulizi wa namna hiyo ni sharti ufanywe kwa kuzingatia ukweli na mantiki ya riwaya inayosimilishwa. Iwapo usimilisho utakiuka ukweli na mantiki ya riwaya, basi huo utakuwa upungufu unaopotosha usawiri wa wahusika na maudhui ya riwaya. Hali ya kumfanya mtambaji kuaminika kwa kumpa sifa za kihulka, kijinsia, lafudhi, kimavazi na nyinginezo, ilipaswa kuafikiana na mtazamo wa mwandishi kuhusu wahusika na usimulizi wake.

Tatu, kulikuwa na msimulizi aliyetekeleza wajibu wa mwandishi katika riwaya. Msimulizi huyo alisimulia matukio kwa kuyaunganisha akilenga kuyawasilisha jinsi mwandishi alivyokuwa ameyasuka katika riwaya yake. Kwa ambavyo haikuwezekana kuigiza kila tukio la riwaya, msimulizi wa aina hiyo alitumika kama kiunzi cha kuyaunganisha yaliyoigizwa, yaliyodondoshwa na yaliyokuwa yamesimuliwa. Utambaji huu ulikuwa muhimu katika kuviwasilisha vipengele vya hadithi ambavyo vingepotea katika uigizaji wa matendo na mazungumzo.

Nne, kulikuwa na usimulizi uliojidhihirisha katika mazungumzo ya waigizaji. Ingawa masimilisho yalikuwa yameandaa mazungumzo ya jukwaani baina ya wahusika, uwasilishaji wake ulijitokeza kama usimulizi. Waigizaji walitumia mbinu za kiutambaji katika mazungumzo yao. Aghalabu mazungumzo hayo ni

yale ambayo mwandishi wa riwaya alidhamiria yawasilishe ujumbe wake kiusimulizi. Utambaji wa namna hiyo ulijitokeza mara nyingi katika riwaya ya *Siku Njema*. Mazungumzo katika riwaya ya *Siku Njema* yalibuniwa sehemu kubwa kama usimulizi. Mazungumzo ya wahusika katika riwaya hiyo yalikuwa marefu na yalipakiwa ujumbe mpana. Maneno haya ya Bi Rahma yaliigizwa kama utambaji:

BI RAHMA: ... Zainabu alikuwa mwanamke mmoja katika elfu.

Alikuwa hapendi rafu wala ushabiki wa namna yoyote ile.

Hakupenda kugombezana wala kujibizana na mtu. Alikuwa na ukarimu uliopita mipaka. Tena hakuwa na majisifu na ndarire nyingi zisizo na maana. Alikuwa na moyo mweupe. Zainabu alikuwa mwanamke adibu na muungwana kweli. Haikuwa laiki yake kumuudhi nzi, sembuse mwanaadamu. Watu kama hao ni tunu sana hapa duniani. Utawapata kwa nadra sana ...

(Kutoka similisho la K.I.C.D, *Siku Njema*)

Kifungu hiki hakikubuniwa na mwandishi kwa sifa za mazungumzo ya kidrama, lakini kama simulio katika mazungumzo. Aghalabu, mazungumzo ya riwaya hubuniwa kama masimulizi yanayotolewa na wahusika kwa njia ya kupokezana. Mazungumzo ya kidrama huwa mafupi na yenye kauli zinazolenga utendaji. Diyanni (2004) anahoji kuwa mazungumzo ya drama yenyewe ni kitendo kwa vile yana uwezo wa kufanya mambo, kubadilisha hali, na kuibua visa. Iliafiki mazungumzo hayo kusimuliwa ili yaibue matokeo yaliyodhamiriwa na kazi chasili.

Nadharia ya uigizaji, kama ilivyoelezewa, huchukulia hadithi kama msingi wa matini ya kidrama. Ingawa kuna njia nyingine za kuisimulia hadithi ya tamthilia, mazungumzo na utambaji ndizo zilizotumika sana katika usimilisho wa riwaya.

Hizi ni sifa mbili zilizobainika kuwepo katika riwaya na tamthilia, ijapo kwa viwango vinavyotofautiana. Aidha, imebainika kwamba baadhi ya mitindo ya riwaya hushirikisha usimulizi katika mazungumzo ya wahusika.

Usimulizi unaohusisha watambaji jukwaani una mizizi yake katika masimulizi ya fasihi simulizi ya jamii za Kiafrika. Huu ni usimulizi ambao pia umetumika katika baadhi ya tamthilia za Kiswahili kwa mfano, tamthilia za Peninah Muhando kama *Lina Ubani* na *Nguzo Mama*. Booth na wengine (2006) wanasema kuwa mara nyingine tamthilia huwatumia watambaji ambao hutazama na kueleza tendo wakiwa kando ya jukwaa. Katika baadhi ya tamthilia watambaji huzungumzia hadhira moja kwa moja. Hata hivyo, Booth na wengine (2006) wanaongeza kuwa, hata ikiwa mtambaji atasema akiwa kando ya jukwaa yeye ni sehemu ya waigizaji. Kama mwigizaji, sharti mtambaji asimulie simulio lake kama msimulizi wa kazi asilia. Hali ya watambaji kutia madoido na ucheshi katika usimulizi inapingana na msingi huu wa kinadharia. Aidha, madoido na ucheshi yalipotumika pale haikufaa katika riwaya, huo ulikuwa upotoshi ambao ungeathiri kwa namna hasi uelewa wa wanafunzi wa riwaya husika.

5.2.2 Utendaji

Packard (1997) anaifafanua tamthilia kama tendo. Maelezo yake yanalingana na ya wahakiki wengi wanaoifasiri tamthilia kama utanzu unaoundwa na mazungumzo na matendo. Mazungumzo ya tamthilia hudhihirika hata kupitia usomaji, lakini matendo yake huwa yanaashiriwa tu. Matendo hayo hudhihirika wazi yanapowekwa jukwaani. Riwaya kwa upande wake, huwa na mazungumzo na matendo. Ingawa mtindo mkuu wa uwasilishaji katika riwaya ni usimulizi, baadhi ya riwaya husheheni mazungumzo na matendo kwa kiasi kikubwa sana.

Kupitia mazungumzo na masimulizi, mwandishi wa riwaya anaweza kuwasilisha matendo yanayopatikana yakitendwa na wahusika wa riwaya yake.

Mbinu ya utendaji inahusu hali ya kuyaweka matendo yanayorejelewa katika riwaya jukwaani. Usimilisho jukwaani ulihusisha utendaji wa baadhi ya visa vilivyosimuliwa katika riwaya. Katika riwaya ya *Siku Njema*, kisa cha Selemani Mapunda kulazimishwa kukoga na mwalimu mkuu shuleni kiliigizwa mbele ya hadhara ya wanafunzi. Katika utendaji tofauti, Selemani na wenzake waliigizwa wakila njama na kumshambulia mwalimu mkuu na kumjeruhi vibaya. Utendaji katika riwaya ya *Utengano* uliigiza visa mbalimbali kikiwemo kile cha kufumanizwa kwa Mussa na Maksuudi kwake Kazija. Makabiliano makali yaliyokuwa yameelezwa katika riwaya yalitendwa jukwaani.

Utendaji katika usimilisho ni hali moja ya kuibua vipengele vya riwaya vinavyosakini katika usimulizi na mazungumzo yake. Mbinu hii huwasilisha maudhui na wasifu wa wahusika jukwaani. Vikundi mbalimbali viliyaweka matendo hayo jukwaani kwa namna tofauti tofauti. Mohamed (1995), anaeleza kwamba, tamthilia hutofautiana na tungo za kinathari kwa vile imeundwa kwa maneno yanayolenga utendaji jukwaani, lakini maneno ya tungo hizo hulenga kuarifu tu. Kinyume na anavyodai Mohamed (1995), utafiti huu ulibaini kwamba, riwaya kadha hushirikisha maneno ya kiutendaji kwa kiwango kikubwa. Aidha, riwaya nyingine huwa na visa vingi vya kiutendaji, hata kuliko baadhi ya tamthilia. Hizi ni sifa za kimwingiliano matini zilizouwezesha usimilisho wa riwaya kuwa drama.

5.2.3 Mazungumzo

Mazungumzo yaliyobuniwa kwenye similisho yalisemwa na waigizaji jukwaani. Sehemu ya usimilisho katika matini, imejadili jinsi mazungumzo hayo yalivyobuniwa. Katika sehemu hii, utafiti umeyajadili jinsi yalivyodhihirika jukwaani. Mbinu ya mazungumzo jukwaani ilijumuisha sifa za kiutendaji katika mazungumzo kama vile usemaji kando, uzungumzi nafsi, na usemaji wa mawazo ya wahusika. Hizi ni kaida za mazungumzo ya kidrama.

Diyanni (2004) anafafanua uzungumzi nafsi kama mazungumzo yanayotolewa na mwigizaji kana kwamba anajisemea peke yake hata ikiwa waigizaji wengine wapo jukwaani. Uzungumzi nafsi huwasilisha mawazo ya mhusika na kuifanya hadhira kuelewa anayofikiria kwa wakati huo. Packard (1997) anahoji kwamba uzungumzi nafsi ni mazungumzo mradi yanaweza kutumika na kualika vitendo kutoka kwa waigizaji wanaofikiriwa kulengwa. Kama mbinu ya utunzi, uzungumzi nafsi hutumika katika tamthilia na riwaya. Uzungumzi nafsi ni kaida ya mazungumzo ya drama kwa vile mwigizaji anayesema pekee jukwaani huchukuliwa kuwa na walengwa wake japo huwa hawaonekani. Haya ni mazungumzo baina ya mwigizaji na hadhira tuli, ambayo haitarajiwi kumjibu ama kuitikia ayasemayo bali kuupokea ujumbe wake.

Utafiti ulibaini kwamba uzungumzi nafsi ulioshuhudiwa jukwaani ulikuwa umebuniwa kutokana na usimulizi wa mwandishi ama ukadondolewa kutokana na matumizi yake katika riwaya. Uzungumzi nafsi uliobuniwa kutokana na usimulizi wa mwandishi ulidhihirika katika masimilisho machache. Masimilisho mengi yalitegemea matumizi ya mbinu hiyo katika riwaya na kuiwasilisha. Uzungumzi nafsi ufuatao ulisemwa na Inspekta Fadhili katika riwaya ya *Utengano*:

FADHILI: Sofa seti aina tatu zote kutoka ulaya, rediogramu,

televisheni inchi ishirini na sita, mapambo, zulia jipya, picha za mkono zilizotoka Ulaya, tepurekoda yenye mabomba mawili. (akicheka moyoni mwake) Watu wanatajirika upesi upesi, sisi tumekaa tu (akicheka kimoyomoyo).

(Kikundi cha *Fanaka*, similisho la *Utengano*)

Uzungumzi nafsi huu ulisimilishwa na kuigizwa jukwaani kama ulivyotumika katika riwaya. Jukwaani mwigizaji Fadhili aliyasema kwa sauti sebuleni kwa Maksuudi, lakini ilichukuliwa kwamba Maksuudi wala mtumishi wake hawakuyasikia. Utafiti huu uligundua kwamba mbinu hii ilipata ufanisi katika majukwaa ambayo yalikuwa na mgawanyo wa vyumba vilivyomtenga msemaji na wahusika wengine. Majukwaa wazi yaliibua matumizi haya kama usemaji kando. Hali hiyo ilivunja kanuni ya uzungumzi nafsi kwa vile maneno hayo yalisemwa mbele ya wahusika wengine.

Katika uzungumzi nafsi ambao ulibuniwa na wasimilishaji, maneno ya mwandishi katika riwaya yaliumbwa kimazungumzo na kupewa wahusika. Katika riwaya ya *Utengano*, mwandishi aliitanguliza riwaya kwa kutoa wasifu wa mhusika Kazija. Usimulizi huo ulitumika na wasimilishaji kubunia Kazija maneno aliyoyatoa kama uzungumzi nafsi:

KAZIJA: (*Akijizungumzia*) Mwanamume! Nani aliyemweka mbele?
Daima nitamchukia... Naichukia hali yangu, naichukia jamii yangu,
nachukia kila kitu...

(Kikundi cha *Nairobi Theatre Group*, similisho la *Utengano*)

Maneno haya yalikuwa yamemlenga mhusika Kazija na ndiyo maana yalichukuliwa na kufanywa usemi wake. Nadharia ya uigizaji huchukulia uzungumzi nafsi kama sehemu ya mazungumzo ya tamthilia. Packard (1997)

anasema kwamba, mazungumzo bora ya kidrama ni yale yanayoibua matendo makuu ya tamthilia. Hiki ni kigezo muhimu cha kupima ufaafu wa uzungumzi nafsi uliobuniwa katika masimilisho. Uzungumzi nafsi uliorejelewa una maneno yanayoibua matendo na kwa hivyo unafuzu katika kigezo hicho.

Kama mazungumzo, uzungumzi nafsi huwa na dhima ya kuisimulia hadithi ya tamthilia. Dhima hiyo hutekelezwa kupitia ukuzaji na uendelezaji wa wahusika ambao ni kiungo cha msingi katika hadithi ya drama. Kwa hivyo, uzungumzi nafsi unasaidiana na usimulizi na maelezo ya jukwaani katika kuisimulia hadithi ya tamthilia. Utafiti ulibaini kwamba ni rahisi kugeza usimulizi wa riwaya unaomlenga mhusika fulani kuwa uzungumzi nafsi wake ama maelezo ya jukwaani. Huu ni utelezi wa kimtindo uliothibitishwa katika tanzu za riwaya na tamthilia.

Utafiti uligundua sifa nyingine ya uzungumzi nafsi katika usimilisho huo, ambayo inatosha kujisimamia. Hii ni mbinu ya usemaji wa mawazo ya wahusika. Katika mbinu hii, mawazo ya mhusika katika riwaya, yalisemwa na kurekodiwa kisha yakachezwa kama sauti jukwaani. Vikundi vilivyokosa vifaa vya kuicheza sauti hiyo, vilimtumia mhusika mwingine kuyasema nyuma ya jukwaa. Mwigizaji alionekana akiyafikiria na kujihusisha na miondoko jukwaani.

Usemaji wa mawazo ya mhusika uliorekodiwa na kusemwa kama sauti ulidhihirishwa na mawazo yaliyomserereka Mussa, alipomtembelea mpenzi wake Kazija katika riwaya ya *Utengano*. Ingawa baadhi ya vikundi vilidondosha sehemu hiyo, vikundi vilivyoiigiza viliirekodi sauti ya Mussa ama vikatumia mwigizaji mwingine kuyasema mawazo yake. Zingatia mfano wenyewe:

SAUTI YA MUSSA: Miezi sita sasa. Nimekuwa duwaza kwa

mwanamke huyu. Toka kupatana naye, nimeoza. Sisikii
wala sioni. Ijapokuwa nilisema najipumbaza na kupoteza wakati,
Jumamosi hata Jumamosi, najiona taratibu natekwa na mizungu yake.
Nikaingia kiganjani. Lau kama ingalikuwa si kwa kupangiwa
na mwenyewe Kazija, ningalipenda nikutane naye kila siku.

(Kikundi cha *Planets*, similisho la *Utengano*)

Mbinu hii haikutumika katika riwaya ya *Siku Njema* kwa sababu mtindo wa kuonyesha mawazo ya wahusika haukutumika na mtunzi. Riwaya ya *Siku Njema* ilitumia mtindo wa usimulizi wa nafsi ya kwanza huku riwaya ya *Utengano* ikitumia nafsi ya tatu. Usimulizi wa nafsi ya kwanza humnyima mwandishi nafasi ya kuingia akilini mwa wahusika wake na kuwasilisha mawazo yao. Utafiti huu ulibaini kwamba mbinu ya usemaji wa mawazo ya wahusika iliwezekana kwa riwaya zilizosimuliwa katika nafsi ya tatu.

Mbinu ya usemaji wa mawazo ya wahusika hutekeleza dhima sawa na uzungumzi nafsi. Hali ya kukosekana kwake katika usimilisho wa riwaya ya *Siku Njema*, haikuathiri usimilisho wake kwani mbinu ya uzungumzi nafsi ilikuwa mbadala wake. Aidha, matumizi yake hayangewezekana katika riwaya hiyo. Hata hivyo, matumizi ya usemaji wa mawazo ya wahusika yalidhoofisha usimilisho kwa kutumia sauti ya mwigizaji tofauti na yule aliyekuwa akisemewa mawazo yake. Utafiti huu unapendekeza usemaji wa mawazo ya mhusika ufanywe kwa sauti ya anayemwigiza jukwaani. Kwa namna hiyo, matumizi ya mbinu hii yatapata uhalisi jukwaani na kukubaliwa na hadhira.

Usemaji kando ni sifa nyingine iliyodhihirishwa na mazungumzo ya masimilisho jukwaani. Diyanni (2004) anaeleza usemaji kando kama maneno yanayosemwa moja kwa moja na mwigizaji kwa hadhira mbele ya waigizaji wengine ambao

inafikiriwa kwamba hawayasikii maneno hayo. Kinyume na uzungumzi nafsi, usemaji kando huwa ni mfupi. Usemaji kando ni mbinu ya kiutendaji ambayo huweza tu kuyakinikishwa jukwaani. Ingawa riwaya haukudhihirisha matumizi ya usemaji kando moja kwa moja, utafiti ulibaini kuwepo na miktadha mahsusi iliyoalika matumizi ya mbinu hiyo.

Mbinu ya usemaji kando ilibuniwa na baadhi ya wasimilishaji ili kuwasilisha habari fulani ambazo ziliafiki matumizi yake. Vikundi vingi viliweza kuitumia mbinu hiyo ya usemaji kando katika sehemu mbalimbali za riwaya. Katika riwaya ya *Utengano*, mawazo ya Kazija yaligeuzwa usemaji kando ufuatao:

KAZIJA: (Alimchuja Mussa, akashangaa naye akisema kando)

He, si mtoto huyu, ana maneno ya kumtoa nyoka pangoni.

Na sijui kayapata wapi!

(Kikundi cha *Jicho Four*, similisho la *Utengano*)

Usemaji kando ulitumika tena katika riwaya hiyo, pale Maimuna na Biti Kocho walipokuwa wakishauriana kuhusu wazo la kwenda kumwita mkunga amzalisha Tamima. Maneno yao yaliwatenga Tamima na wahudumu wengine pale jukwaani, japo walikuwa wakiyasikia, lakini hadhira ilifanywa kuamini kuwa hawakuyasikia yasemwayo. Mbinu ya usemaji kando haikudhihirika katika usimilisho wa riwaya ya *Siku Njema*. Hata hivyo, utafiti ulibainisha kuwapo kwa miktadha ambayo ingeruhusu matumizi yake katika riwaya hiyo.

Usemaji kando ni mbinu ya kiutendaji ambayo hudhamiriwa kuendeleza msuko wa tamthilia. Kama ilivyotanguliwa kusemwa, usemaji kando ni sifa mojawapo ya mazungumzo ya drama. Kanuni kuu inayoongoza matumizi ya usemaji kando hushikilia kwamba, maneno katika usemaji kando hayapaswi kusikika wala

kuendelezwa na mhusika asiyekusudiwa. Uigizaji wa riwaya jukwaani ulioitumia mbinu hii ulionekana kuiheshimu na kuifuata kikamilifu. Ingawa matumizi ya mbinu hii hayadhihiriki wazi wazi katika riwaya, mtafiti alibaini kwamba, kuna miktadha mahsusi katika riwaya inayoalika matumizi ya mbinu hiyo pale riwaya inapoigizwa. Katika riwaya, kuna miktadha ambapo wahusika waliomo katika mazungumzo hujitenga na wenzao ama kwenye chumba au kwa kusonga mbali nao. Huko kujitenga katika mawasiliano ndiko huzalisha matumizi ya usemaji kando jukwaani.

Kwa muhtasari, mazungumzo ya similisho jukwaani husheheni sifa mbalimbali kama ilivyodhihirishwa. Utafiti umeangazia sifa zilizojitokeza sana miongoni mwa maigizo. Upungufu uliodhihirika katika mbinu hii unajadiliwa katika sehemu ya matatizo ya usimilisho wa riwaya.

5.2.4 Matumizi ya Jukwaa

Ufundi wa matumizi ya jukwaa hujumuisha mbinu mbalimbali ambazo huisimilisha matini ya similisho la riwaya na kuiigiza jukwaani. Miongoni mwa mbinu hizi ni matumizi ya pazia, sauti, muziki, mandhari na uangazaji. Mbinu hizi za jukwaani zilitumika na vikundi teule kwa jinsi tofauti tofauti.

5.2.4.1 Matumizi ya pazia

Booth na wengine (2006) wanahoji ya kwamba, katika tamthilia ya kisasa kuna uwezekano wa kuwa na mabadiliko mbalimbali ya onyesho. Waandishi hawa wanataja kufungua na kufunga pazia kama njia moja ya kuashiria mabadiliko ya onyesho. Maelezo yao yanashadidia umuhimu wa pazia katika maigizo. Mbinu ya pazia ilitumika na vikundi vilivyoigizia katika kumbi za thieta. Mapazia makubwa yaliyoangikwa jukwaani yalitumika na vikundi hivyo kufanikisha

usimilisho. Kwanza, pazia ilitumika kufungua na kufunga maonyesho. Pili, pazia ilitumika kuweka mpaka baina ya muktadha halisi jukwaani na ule usio halisi. Matukio yaliyotokea katika muktadha usio dhahiri yaliwekwa mbele ya pazia. Tatu, pazia ilitumika kumtenga mtambaji na muktadha wa onyesho. Msimulizi alijitokeza mbele ya pazia katika maigizo mengi.

Matumizi ya pazia ni kipengele muhimu cha mandhari. Pazia hubainisha mabadiliko ya mandhari katika uigizaji. Vikundi vilivyokosa pazia vilipungukiwa katika ubainishaji wa mandhari kwani waigizaji walifanya hivyo kwa kuingia na kutoka baada ya kila igizo. Hali hii iliwabidi waelekezi kuwa na vifaa vichache ambavyo viliruhusu kupanguliwa kwa urahisi pale mandhari yalipobadilika. Pazia huwa ni kifaa muhimu katika kukuza mazaji ya igizo kupitia uteuzi wa rangi yake. Utafiti ulibaini kwamba usimilisho wa riwaya haukuzingatia kigezo cha rangi ya pazia katika uigizaji wa masimilisho. Mapazia yaliyotumika yalikuwa ya rangi moja katika mandhari yote ya maigizo. Hali hii haikudhoofisha usawiri wa mandhari, kwani mazaji ya maigizo yaliweza kukuzwa kwa muziki na sauti.

5.2.4.2 Matumizi ya Sauti

Wilson na Goldfarb (1991) wanafafanua athari ya sauti kama sauti yoyote inayotolewa kwa njia za kimitambo ama kibinadamu ili kukuza kwa hadhira kelele ama sauti inayohusishwa na tamthilia inayoigizwa. Wanaongeza kwamba, kuna njia mbalimbali za kielektroniki zinazotumika kutayarisha sauti. Sauti inaweza kutayarishwa kitaalamu na kisha ikarekodiwa katika tepurekoda na kanda za kunasa sauti. Katika usimilisho wa riwaya, sauti ilitumika katika maigizo yaliyofanywa katika majumba ya thieta na shuleni. Mbinu ya sauti

ilitumika kuwasilisha maneno ya wahusika na kujenga mazaji katika igizo jukwaani. Vikundi vyote vilitumia mbinu hiyo kwa ufundi tofauti. Sauti iliyotumika katika kumbi za thieta ilikuwa imerekodiwa, ilhali katika majukwaa ya shule waigizaji walitumika kuyasema yaliyotakiwa kusemwa wakiwa nyuma ya jukwaa.

Sauti ilirekodiwa na kucheza jukwaani ili kuwasilisha maneno ya waigizaji ambao hawakutarajiwa kuonekana ama kuyasema jukwaani. Matumizi haya yamezungumziwa katika mbinu ya mazungumzo. Aidha, mbinu ya sauti ilitumika kujenga mazaji ya tukio lililokuwa likiigizwa jukwaani. Katika riwaya ya *Siku Njema*, sauti ya ndege wa mwituni ilichezwa na kikundi cha *K.I.C.D* ili kuyakinisha maisha ya mashambani nyumbani kwa Mzee Makame.

Matumizi ya sauti yalisaidia kuleta uhalisi katika tukio lililokuwa likiigizwa. Katika riwaya ya *Utengano*, sauti ya kilio cha kitoto kichanga ilikuwa imerekodiwa na ilichezwa wakati Tamima alipojifungua. Aidha, mbinu hiyo iliweza kuwasilisha baadhi ya mbinu za utunzi jukwaani. Barua katika riwaya ya *Siku Njema* iliwasilishwa kwa sauti iliyokuwa imerekodiwa huku mwigizaji akionyeshwa akiisoma, lakini kimya kimya.

5.2.4.3 Matumizi ya Muziki

Mbinu ya matumizi ya muziki ilidhihirika sana katika kumbi za thieta zaidi kuliko ilivyodhihirika katika majukwaa ya shule. Katika kumbi za thieta, muziki ilikuwa imerekodiwa na ilichezwa kwa madhumuni tofauti. Kwingineko katika majukwaa ya shule, vikundi husika viliwatumia wahusika kuimba nyimbo nyuma ya jukwaa ama vikatumia redio ili kucheza muziki hiyo.

Matumizi ya muziki yalitekeleza dhima mbalimbali. Kwanza, muziki ulitumika kujenga mazaji ya igizo jukwaani. Katika klabu Tafrija, muziki ulioalika hisia za furaha na hali ya sherehe ulichezwa pale Kazija alipolikubali ombi la Mussa la kumtaka awe mpenzi wake. Muziki wenye mazaji ya huzuni ulichezwa chini kwa chini baada ya tangazo la kifo cha Maksuudi. Pili, muziki wa sauti nzito na kubwa ulichezwa mwanzoni na mwishoni mwa kila onyesho kuashiria mwanzo na mwisho wake. Tatu, muziki ulishadidia maudhui ya igizo fulani. Wimbo wa bendi la Les Wanyika, *Amigo*, ulichezwa pale Maksuudi alipomkabidhi Tamima talaka na kutengana na familia yake yote. Wimbo huo ulibeba ujumbe uliomsuta Maksuudi kwa kuifukuza familia yake akijidai bingwa wa maisha na kupuuza ushauri wa wenzake. Maksuudi alishauriwa aheshimu mke na watoto wake. Nne, katika riwaya ya *Utengano*, muziki wenye mahadhi ya kihindi ulichezwa katika tukio dukani mwa mhindi Ganj ili kuleta uhalisi.

Dhima ya kidrama ya sauti ni sawa na ya muziki. Mbinu hizi hujenga hali na hisia katika uigizaji jukwaani. Diyanni (2004) anasema kuwa muziki na sauti hutumika ili kuimarisha hali ya taharuki katika maigizo. Muziki na sauti inayochezwa ni lazima ioane na mazaji ya tukio linalolengwa. Mazaji ni vizuri yachukuane na maudhui lengwa na mandhari ya tukio hilo. Kwa kigezo cha mandhari, nyimbo na sauti nyingine zilizochezwa zilishindwa kuzingatia wakati uliokuwa unalengwa na riwaya husika. Ingawa nadharia ya usimilisho inaelekeza namna ya kuandaa similisho, haionyeshi jinsi similisho hilo linavyoweza kusimilishwa jukwaani. Nadharia ya uigizaji ina udhaifu kwa vile misingi yake inahusu tungo zilizotungwa kwa dhamira ya kuigizwa. Ili usimilisho wa riwaya inayotahiniwa utathminiwe kwamba umefaulu, ni muhimu mbinu za jukwaani ziteuliwe kulingana na maudhui, mandhari, na mtazamo wa riwaya.

5.2.4.4 Mandhari

Mandhari katika matumizi ya jukwaa hurejelea jinsi mazingira ya tukio yanavyosawiriwa jukwaani. Usawiri wa mandhari jukwaani ni mbinu ya usimilisho kwani mwelekezi hujaribu kufasiri mazingira ya tukio hilo katika riwaya na kufikiria namna ya kuliwasilisha jukwaani. Kwa mujibu wa Booth na wengine (2006), usawiri wa mandhari huhusisha namna jukwaa lilivyopangwa, lilivyopambwa, na lilivyoandaliwa ili kuashiria mazingira halisi ya tukio.

Ubona wa majukwaa katika kumbi za *National Theatre* na *Liberty Theatre* ulifanikisha usawiri wa mandhari kwenye maigizo yaliyofanyiwa katika kumbi hizo. Usanifu wa jukwaa la *National Theatre* uliashiria kuwepo kwa sebule, chumba cha malazi, jikoni na vyumba vinginevyo. Jukwaa la *Liberty Theatre*, japo usanifu wake haungeufikia wa *National Theatre*, lilidhihirisha ubora huo pia. Ubona kama huo ulikosekana katika majukwaa ya shule. Katika majukwaa ya shule, ilikuwa vigumu kujenga uhalisi wa mandhari kama yalivyosawiriwa katika riwaya.

Mfano wa kulinganisha ubona huu ulionekana katika uigizaji wa tukio la kujifungua kwa Bi.Tamima katika riwaya ya *Utengano*. Katika majukwaa ya thieta, igizo hilo lilionyesha Bi.Tamima akiwa amelazwa kwenye chumba cha malazi na matukio mengine yakifanyikia sebuleni. Katika chumba cha kulala kitanda kilionekana, na sebuleni kulikuwa na samani kama vile viti vya sofa seti, meza, kabati na nyinginezo ambazo zilishadidia tabaka la juu la Bw. Makuudi. Mgawanyo na samani kama hizo zilikosa katika majukwaa ya shule. Mbinu za kiufaraguzi zilizotumika hazikutosha kuviwasilisha visa vya riwaya kama vilivyokuwa katika riwaya.

Kikundi cha *K.I.C.D* kilichokuwa kimeyanasa maigizo yake kilipata ufanisi mkubwa katika usawiri wa mandhari kwa vile kila tukio liliigiziwa katika mandhari yake mwafaka. Matukio ya shuleni yaliigiziwa shuleni, yale ya nyumbani na mjini, yaliigiziwa maeneo ambayo yangetuaminisha hayo. Katika tukio ambalo mhusika Kongowea alielezewa kwamba alipanda basi la *Kenya Bus*, igizo lake lilinaswa katika kituo cha mabasi ya *Kenya Bus* na mwigizaji alionekana akilipanda basi hilo.

Uchaguzi wa jukwaa hufanywa kwa kuzingatia aina ya utungo na dhamira yake (Diyanni, 2004). Majukwaa ya shule yalidhihirisha upungufu kwa uigizaji wa riwaya ya *Utengano*. Matukio kadha katika usimilisho wa riwaya hiyo yalihitajia majukwaa changamano ili kuyadhihirisha. Ingawa tamthilia nyingi huandikwa zikilengwa kuigizwa, riwaya huandikwa kwa dhamira ya kusomwa tu. Matukio kadha ya riwaya huwa na changamoto ya kuyasimilisha na kuyaigiza. Uigizaji aminifu zaidi wa riwaya zenye sifa hizo hufanikishwa katika majukwaa yenye sifa mbalimbali. Unasaji wa matukio katika filamu kwenye mandhari mbalimbali ni njia moja ya kufanikisha usimilisho wake.

5.2.4.5 Uangazaji

Hii ni mbinu ya usimilisho jukwaani inayohusisha umulikaji wa kimakusudi ama matumizi ya mwangaza. Mbinu ya uangazaji ilipata ufanisi wake tu katika majukwaa ya thieta. Vifaa vya umulikaji havikupatikana katika mazingira ya shule.

Wilson na Goldfarb (1991) wanaorodhesha dhima mbalimbali za umulikaji katika uigizaji. Dhima wanazoorodhesha ni:

- I. Kumulika ukumbi wenye kiza ili kutambulisha waigizaji na vitendo vyao jukwaani.
- II. Kuashiria majira ya siku na mahali. Mwangaza hafifu kuashiria mapambazuko, ule angavu kuashiria aduhuri, na ule wenye rangi ng'avu kuonyesha machweo.
- III. Kukuza mazaji katika igizo. Hili hutekelezwa na umulikaji hukishiriki pamoja na maleba ya waigizaji na pambo la jukwaa.
- IV. Kuimarisha mtindo kwa kuonyesha iwapo tamthilia ni ya kihalisia ama isiyo ya kihalisia.
- V. Kuonyesha msisitizo jukwaani. Eneo linalomulikwa ndilo huwa na msisitizo katika igizo fulani.
- VI. Kujenga ridhimu. Mwangaza wa aina tofauti tofauti humulika na kuzima nyakati tofauti tofauti na kwa malengo tofauti tofauti.

Katiko usimilisho wa riwaya jukwaani, baadhi ya dhima wanazotaja Wilson na Goldfarb (1991) zilitambuliwa. Mwangaza ulitumika kuonyesha mwanzo na mwisho wa onyesho jukwaani. Onyesho lilitangulizwa na mwangaza angavu jukwaani na mwisho wake uliashiriwa na kuzimwa kwa mwangaza huo. Aidha, uangazaji ulitambulisha majira ya siku katika tukio. Zaidi yake, mwangaza wa spotilaiti ulimulika jukwaani penye giza totoro na mbele ya pazia kumwonyesha msimulizi aliyekuwa akisimulia matukio ya hadithi.

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), umulikaji hufanywa kutimiza dhima mahsus katika uigizaji. Aidha, uangazaji huwa wa aina mbalimbali na wenye athari mbalimbali. Uigizaji katika majukwaa ya thieta ulidhihirisha matumizi mwafaka

ya uangazaji na athari yake jukwaani ilijitokeza. Hadhira ilifanywa kusadiki kwamba kila aina ya umulikaji ulitekeleza dhima fulani mahsusi jukwaani. Katika usimilisho wa riwaya, umulikaji uliafiki zaidi katika kutambulisha majira ya siku, kumbainisha mtambaji, na kuweka mipaka ya maonyesho. Hayo ni mambo yaliyolenga kuisimilisha riwaya jukwaani. Kama ilivyosemwa awali, vipengele vya uigizaji jukwaani vinapaswa kuchaguliwa kulingana na umuhimu wake katika kuendeleza usimilisho wa riwaya kama ilivyodhamiriwa.

5.2.5 Uteuzi wa Wahusika

Wahusika wa riwaya waliwakilishwa jukwaani na waigizaji. Waigizaji hutarajiwa kuwa viwakilishi vikamilifu vya wahusika wanaowakilishwa jukwaani. Booth na wengine (2006) wanahoji kwamba, dhana mhusika hurejelea zaidi ya mtu anayewakilishwa katika ploti inayofikiriwa kwani matumizi yake hujumuisha sifa za kipekee zinazomkamilisha mtu huyo. Hii ina maana kwamba wahusika wanaotumika katika tamthilia sharti wafumbate sifa halisi za wahusika wanaowakilishwa. Kwa namna hiyo, waigizaji wanapaswa kusawiriwa kwa njia itakayotuaminisha kwamba hao ndio binadamu wanaoigwa. Vigezo muhimu vilivyozingatiwa katika uteuzi huo ni kama vile maleba, lugha, na maumbile.

5.2.5.1 Maleba

Maleba hurejelea mavazi maalum ya waigizaji. Wilson na Goldfarb (1991) wanasema kwamba, watu hawavaliu nguo kwa nia ya kuwasetiri tu, lakini huvalia nguo kwa dhamira ya kupitisha ujumbe fulani. Kwa kawaida nguo huwasilisha ujumbe fulani kwa yule aliyezivalia kama vile: cheo na hadhi, jinsia, kazi, mwana-mitindo, vazi la kazi ama starehe au hafla maalumu. Wilson na Goldfarb wanaendelea kusema kwamba, katika uigizaji maleba hutumika ili kuwasilisha

habari fulani kama ilivyo katika mavazi ya kawaida. Hata hivyo, habari inayopitishwa jukwaani hupigiwa chuku kwa sababu kila kitu jukwaani hupewa uzito. Aidha, maleba ni sharti yatimize mahitaji mengine ambayo si ya kawaida katika maisha ya kila siku. Wilson na Goldfarb (1991) wanaorodhesha mahitaji yanayopaswa kutimizwa na maleba ya waigizaji. Maleba yanahitajika:

- I. Kuweka toni na mtindo: Maleba yakishiriki pamoja na pambo la jukwaa na uangazaji yanapaswa kuarifu hadhira kuhusu mtindo wa tamthilia.
- II. Kuashiria wakati na mahali: Maleba huonyesha kipindi cha wakati na mahali yanayorejelewa na tamthilia, iwapo ni kipindi cha sasa ama cha kihistoria, na tendo linahusu nchi gani. Maleba ni sharti yatuarifu ni wapi na lini tendo linafanyika.
- III. Kuonyesha wasifu wa mhusika: Maleba ni sharti yaonyeshe kazi ya mhusika, tabia yake, na uhusika usio na uhalisi.
- IV. Kuonyesha uhusiano miongoni mwa wahusika: Wahusika wanaweza kulinganuliwa kupitia maleba yao. Kwa mfano, wahusika nguli watepewa mavazi tofauti na wahusika wasaidizi. Aidha, maleba yataonyesha migawanyo ya kimakundi kwa misingi ya kijinsia, kiumri, kitabaka, na kitamaduni.

Mahitaji haya yanayotolewa na Wilson na Goldfarb (1991) yalionekana kuzingatiwa katika usimilisho wa riwaya jukwaani. Maleba ya wahusika yaliteuliwa kwa misingi ya tabaka la kiuchumi, umri, dini, utamaduni, na usasa.

Uteuzi wa maleba ya waigizaji Makuu, Inspekta Fadhili, Mussa, Rashidi, Kabi, Bi. Farashuu, Maimuna, Biti Kocho, na Selume katika riwaya ya *Utengano*

ulifanywa kwa kigezo cha dini. Hali ilikuwa hiyo kwa waigizaji Zainabu, Kitwana, Bi. Rahma na Rashid katika riwaya ya *Siku Njema*. Waigizaji wa kiume walivalia kanzu na kofia maalum zinazovaliwa na waumini wa dini ya Kiislamu. Mavazi ya waigizaji wa kike yalikuwa ni buibui na mtandio. Katika riwaya mwandishi alikuwa amewadhihirisha baadhi ya wahusika hao kama waumini wa dini ya kiislamu. Mandhari yaliyosawiriwa katika riwaya hizo yaliwafanya waelekezi kuteua mavazi mahsusi ya kidini ya waigizaji.

Katika msingi wa matabaka ya kiuchumi, waigizaji walivalishwa mavazi yaliyobainisha hadhi zao za kiuchumi. Wachochole walivalia mavazi machafu, matambara, nguo zenye rangi zisizopendeza na baadhi hawakuvaa viatu. Katika riwaya ya *Utengano* kulikuwa na Shoka, Kabi, Bamkubwa, Kijakazi, Mabruk na Bwana Haji. Wachochole katika riwaya ya *Siku Njema* walikuwa Zainabu, Kongowea, wakewenza wa Mwinyi Makame na Amina. Kwingineko, ufahari wa wahusika katika ngazi za kiuchumi ulidhihirishwa jukwaani kupitia mavazi kama vile suti na tai, kanzu zenye thamani kubwa, viatu na kofia za kifahari. Wahusika matajiri walikuwa wachache wakilinganishwa na wachochole katika riwaya zote mbili.

Utamaduni ulidhihirishwa na mavazi kama vile mitandio, kanga na lesa, hasa kwa wahusika wa kike waliopatikana katika riwaya hizo mbili. Katika maigizo ya *Siku Njema*, wachuuzi sokoni Mombasa walivalia buibui na wengine wakajifunga kanga. Hali ilikuwa kinyume katika mazingira ya Kitale ambapo mavazi hayakujibainisha kitamaduni. John Amon, kutoka Umaasaini, ndiye aliyebainishwa Kimaasai kwa kuvishwa kanga nyekundu yenye mistari nyeupe.

Usasa na umri ni misingi miwili iliyodhihirishwa kwa jinsi zinazokaribiana. Vijana walivaa mavazi ya kisasa na watu wazima wakavaa mavazi yaliyoambatana na heshima zao. Maeneo ya starehe kama vilabu na miji yalidhihirishwa kwa mavazi ya aina yake. Katika riwaya ya *Utengano*, matukio katika Klabu Tafrija na Rumbalola, waigizaji wa kike walivalia mini-sketi, suruali ndefu, na mapambo ya kila aina.

5.2.5.2 Lugha

Lugha ya wahusika inaweza kufafanuliwa ili kujumuisha sauti, lafudhi na matumizi ya lugha. Kigezo cha lugha kiliongoza kuteuliwa kwa waigizaji waliofumbata sifa na kanuni za lugha zilizokuwa muhimu kuwasilishwa jukwaani.

Lafudhi ni matumizi ya lugha yanayobainisha lugha asili ya mzungumzaji hasa kulingana na jinsi mzungumzaji anavyoyatamka maneno na muundo wa sarufi yake. Waigizaji kadha walibainishwa kwa sifa ya lafudhi kutegemea asili yao katika riwaya. Wahusika waliokuwa na asili ya kipwani kama Amina, Rashid, Zawadi na wachuuzi katika soko la Kisauni, katika *Siku Njema*, walipewa lafudhi ya Kimvita. John Amon, alipewa lafudhi ya Kimaasai, waigizaji kadha mjini Kitale wakipewa lafudhi ya Kiluhya. Katika riwaya ya *Utengano*, matumizi ya lafudhi yalitofautiana miongoni mwa vikundi. Kuna matumizi ya lafudhi yaliyoelekezwa na riwaya kama ya Ganj na Ashuru, lafudhi ya Kihindi na Kiarabu kwa usajali huo. Matumizi mengine ya lafudhi yalitawaliwa na sifa za Kimvita. Haikuwa rahisi kubaini jinsi uamuzi wa matumizi hayo ulivyokuwa ukifanywa.

Sauti ilitumika katika uteuzi wa waigizaji ili kubainisha sifa za wahusika wa riwaya. Mwigizaji aliyeigiza nafasi ya Kazikwisha, katika *Siku Njema*, alipewa sauti yenye kitembe katika uzungumzi wake. Katika riwaya ya *Utengano*, wahusika Zanga na Bi Mtumwa walidhihirishwa jukwaani kwa sauti ya kigugumizi kama inavyoashiriwa na riwaya.

Matumizi ya sauti yaliongoza kuteuliwa kwa wahusika waliodhihirisha namna mbalimbali za kuitumia sauti yao ili kuuwasilisha ujumbe uliokuwa ukidhamiriwa. Kulingana na Odeo na Maina (2008), aina ya sauti huwasilisha maana mahsusi ya ujumbe katika mazungumzo. Aghalabu, sauti ya Makuudi ilikuwa nzito na ya juu kuashiria ukali, mamlaka, ujasiri na ghadhabu. Katika riwaya ya *Siku Njema*, waigizaji Rashidi, Bi Rahma, Kitwana, Zawadi na Mercy MacDonald walipewa sauti nyororo na zenye upole zilizokwenda sambamba na maudhui yaliyokuwa yakipitishwa. Kuna wahusika walioigizwa jukwaani kwa sauti nzito na ya juu katika miktadha mbalimbali. Hao ni kama Mwana Saumu, wakewenza wa Mwinyi Makame, hedimasta, na polisi.

5.2.5.3 Maumbile

Maumbile katika muktadha huu hurejelea umri na tambo la mwigizaji. Hizi ni sifa za nje za kimaumbile ambazo hadhira iliweza kuzihusisha na zile za mhusika mwenyewe katika riwaya. Uteuzi wa waigizaji unapaswa kulenga kuwasilisha maumbile ya wahusika kama vile yanavyofasiriwa katika riwaya.

Kwa vile waigizaji wengi walikuwa vijana, sifa mbadala zilijumuishwa ili kuwasawiri waigizaji wazee. Sifa hizo zilijumuisha sauti ya kujikokota, hali ya kupindika mgongo, na nywele nyeupe. Wahusika walioigizwa hivyo ni kama vile Mzee Haji, Mabruk, na Makuudi, wote katika riwaya ya *Utengano*. Waigizaji

wenye tambo kubwa waliteuliwa kuwakilisha wahusika Mama Jeni, Biti Sururu, Farashuu, Biti Kocho, na Shoka, katika masimilisho ya *Utengano*. Sifa ya ulemavu bandia ilitumika kumwigiza mhusika Kabi katika maigizo ya riwaya ya *Utengano*. Katika tamthilia-riwaya ya *Siku Njema*, waigizaji wazee halisi waliteuliwa kuigiza nafasi za Kazikwisha na Kitwana.

Wahusika ni kipengele muhimu cha msuko wa drama (Diyanni, 2004). Msuko huweza kufasiriwa, pia, kama utendaji wa wahusika. Nadharia ya uigizaji huwataka wahusika wa tamthilia wabainishwe kiumri, kihulka, kiitikadi, kisura, misingi yao ya kiuchumi na kijamii pamoja na lugha wanayoitumia. Diyanni (2004), anahimiza kuwa, vigezo hivyo vinapaswa kushirikiana kumsawiri mhusika kwa ukamilifu. Uigizaji wa riwaya ulizingatia vigezo vya kinadharia vya uteuzi wa waigizaji. Vigezo vya maumbile na maleba viliambatana na usawiri wa wahusika katika riwaya teule. Hata hivyo, kigezo cha lugha ya wahusika, hakikufanywa kwa matakwa ya riwaya zinazotahiniwa shuleni. Ingawa kilifanywa kinadharia, usimilisho unaowalenga wanafunzi unapaswa kuzingatia lugha sanifu iliyotumika katika riwaya inayosimilishwa. Kabla Taasisi ya Ukuzaji Mitaala ya Kenya kuiidhinisha riwaya kusomwa na kutahiniwa, lugha ya riwaya hiyo hupitiwa na kuhaririwa ili kuafikia viwango vinavyotarajiwa kwa wanafunzi wa sekondari. Hali ya kuiboronga lugha ya riwaya, ni udenguzi unaopotosha usimilisho wake.

5.2.6 Uigizaji wa Mbinu za Utunzi

Uigizaji wa mbinu za utunzi ni jambo gumu sana kutekeleza jukwaani. Hata hivyo, mbinu kadha za utunzi ziliigizwa. Kama ilivyoelezwa katika sehemu ya

usimilisho wa matini, mbinu za matumizi ya lugha zilifaraguliwa na kutumika katika usimulizi na mazungumzo ya waigizaji.

Kuna njia mbili zilizotumika kuigiza mbinu za kisanaa. Kwanza, mbinu fulani ziliwasilishwa kupitia sauti iliyorekodiwa ama ya mwigizaji nyuma ya jukwaa, kutegemea mtindo uliozisanifu. Hizo ni kama matumizi ya ndoto, gazeti, simu, na shairi. Aghalabu, mwigizaji alionyeshwa jukwaani katika miondoko iliyokwenda sambamba na sauti hiyo.

Njia ya pili iliyotumika kuigiza mbinu za kisanaa ilihusisha utendaji na ufaraguzi. Nyimbo zilizotumika katika riwaya ziliimbwa jukwaani na waigizaji. Mbinu hii ilitumika katika maigizo ya riwaya zote. Mbinu rejeshi iliyotumika katika riwaya hizo ilifaraguliwa kimsuko ili kuruhusu uigizaji wake kama ilivyokwisha kuelezewa. Aidha, baadhi ya vikundi viliitia mbinu rejeshi katika utendaji jukwaani na kuiigiza. Hata hivyo, uigizaji huo ulikosa namna ya kuashiria hadhira kwamba matukio hayo yalikuwa yamekwisha kufanyika.

Nadharia ya usimilisho huelekeza kwamba vipengele vya maana ni sharti vihamishwe katika mchakato wa usimilisho (Lhermitte, 2005). Mbinu za uwasilishaji wa maudhui ni mojawapo wa vipengele hivyo. Kwa ambavyo mbinu hizo hubeba maana ya riwaya, namna zinavyowasilishwa huathiri namna maana hupokelewa. Usimilisho wa mbinu za kisanaa, ndoto na jazanda, haukuakisi matumizi yake katika riwaya teule. Kwa kuzingatia mtindo, riwaya ya *Utengano* na *Siku Njema*, hazikuandikwa kuigizwa. Kwa hivyo, kuna vipengele ambavyo uigizaji ulitoa matokeo ambayo hayakudhamiriwa na mwandishi. Njia iliyostahili ilikuwa kuvisimulia vipengele hivyo kama alivyokuwa amefanya mwandishi wa riwaya.

5.3 MATATIZO YA USIMILISHO WA RIWAYA

Sehemu hii inalitekeleza lengo la tatu la utafiti kwa kuchunguza matatizo ya usimilisho wa riwaya. Matatizo yanayoangaziwa yalibainika katika masimilisho na maigizo yake. Aidha, hojaji na mahojiano zilitumika kukusanya data hasa kuhusu matatizo yaliyobainika katika uigizaji wa masimilisho.

5.3.0 Uwasilishaji wa Data Kuhusu Matatizo ya Usimilisho wa Riwaya

Uchanganuzi wa hojaji za walimu ulifanywa kwa programu ya tarakilishi ya SPSS na umewasilishwa kwa njia za kijarabati. Data iliyokusanywa katika hojaji hizo na mahojiano, pia, ilichanganuliwa kwa mbinu ya kimaelezo. Kwa kuwa wasimilishaji walikuwa wachache, mtafiti alipata fursa ya kuwahoji kila mmoja na kukusanya mambo mengi. Walimu waliohojiwa kuhusu usimilisho wa riwaya walikuwa kumi.

5.3.1 Data Kutokana na Hojaji za walimu

Hojaji za walimu ziliwataka wajibu maswali mbalimbali kuhusu usimilisho wa riwaya. Maswali walioulizwa yalizua data ifuatayo:

5.3.1.1 Tathmini ya Usomaji wa Riwaya

Walimu walitakiwa katika hojaji kusema iwapo walikuwa wameisoma riwaya iliyokuwa ikiigizwa. Asilimia mia moja (100%) ya walimu walikuwa wameisoma. Hii ilikuwa na maana kwamba walimu walifahamu yaliyokuwa yakisimilishwa katika riwaya. Kwa namna hii, walimu walikuwa katika nafasi nzuri ya kutathmini usimilisho kwa kuonyesha mafanikio na upungufu wake.

5.3.1.2 Kutathmini Kiwango cha Usahihi wa Usimilisho

Katika kutathmini usahihi wa maigizo, asilimia 40 ya walimu ilikiri kwamba uigizaji wa riwaya ulikuwa na dosari. Zingatia jedwali 1.1:

JEDWALI 5.1 KUTATHMINI USAHIHI WA MAIGIZO

VIWANGO	IDADI RADIDI	ASILIMIA	ASILIMIA JUMLIFU
VIBAYA SANA	0	0.0	0.0
VIBAYA	0	0.0	0.0
WASTANI	4	40.0	40.0
VIZURI	4	40.0	80.0
VIZURI SANA	2	20.0	100.0
JUMLA	10	100.0	100.0

Asilimia 60 ya wahojiwa ilijibu kwamba usimilisho wa riwaya ulifanywa vizuri. Hata hivyo, ingawa asilimia kubwa (60%) ilikiri kwamba usimilisho ulipata ufanisi, kuwepo na asilimia 40 ya wahojiwa waliokosa kuridhika na namna usimilisho ulivyofanywa ni dalili ya kuwepo na matatizo katika usimilisho huo. Aidha, usahihi wa masimilisho ulikadiriwa katika viwango vitatu tofauti ikionyesha kutotimizwa kwa matarajio fulani.

5.3.1.3 Kutathmini Umuhimu wa Usimilisho wa Riwaya kwa Wanafunzi

Wahojiwa walitakiwa katika hojaji kutathmini umuhimu wa maigizo ya riwaya kwa maandalizi ya mtihani wa KCSE. Uchanganuzi wa majibu yao ulizalisha matokeo yafuatayo:

Asilimia 10 walisema si ya lazima.

Asilimia 60 wakasema ni muhimu.

Asilimia 30 walisema ni muhimu sana.

Hali ya kuwepo na tathmini tofauti ilibainisha upungufu wa maigizo katika kutimiza dhamira yake. Hii inaashiria kuwepo na matatizo ya usimilisho

5.3.1.4 Kutambua Matatizo ya Usimilisho wa Riwaya

Katika hojaji walimu walitakiwa watambue matatizo yaliyoufanya usimilisho kutoiwasilisha riwaya kwa usahihi. Majibu yao yalikuwa ifuatavyo:

JEDWALI 5.2 MATATIZO YA USIMILISHO WA RIWAYA

AINA YA MAKOSA	IDADI RADIDI	ASILIMIA
KUTIA CHUMVI	4	40.0
USAWIRI WA WAHUSIKA	6	60.0
UBAINISHAJI WA MAUDHUI	7	70.0
MTIRIRIKO WA MSUKO	6	60.0
USAWIRI WA MANDHARI	5	50.0
UDONDOSHAJI WA MATUKIO	4	40.0
USIMILISHO WA MBINU	7	70.0
MATUMIZI YA LUGHA	3	30.0
MUDA MFUPI WA KUIGIZA	3	30.0

Data iliyotokana na hojaji za walimu ilidhihirisha kuwepo na makosa mengi ya usimilisho wa riwaya yaliyodhihirika katika viwango mbalimbali. Makosa yaliyodhihirika sana yalihusu ubainishaji wa maudhui, usawiri wa wahusika, usimilisho wa mbinu, na usawiri wa mandhari. Aidha, makosa hayo yalibainika kutegemea kikundi cha uigizaji.

5.3.1.5 Njia za Kuboresha Usimilisho wa Riwaya

Wahojiwa walitakiwa kupendekeza jinsi ya kuyaboresha maigizo ya riwaya kwa manufaa ya wanafunzi wanaotahiniwa katika mtihani wa KCSE. Yafuatayo ni mapendekezo yao:

Yanapaswa kukaguliwa kabla yaidhinishwe – 60%

Wasimilishaji wasomeshe jinsi ya kusimilisha – 40%

Walimu washirikishwe katika usimilisho – 40%

Maigizo potovu yaharamishwe – 20%

Wasimilishaji wapate ushauri wa mtunzi wa riwaya – 20%

Kuhimiza ushindani miongoni mwa vikundi – 30%

Asilimia kubwa (60%) ya wahojiwa ilipendekeza usimilisho wa vikundi vya uigizaji ukadiriwe ubora wake kabla uidhinishwe kufanyiwa wanafunzi. Kukaguliwa kwa usimilisho huo kutafanywa kwa kuzingatia yale yanayopaswa kusimilishwa katika riwaya husika. Aidha, wahojiwa walipendekeza wasimilishaji washirikishe walimu na watunzi ili kupata ushauri na mwongozo katika mchakato wa kusimilisha riwaya. Kulikuwa na maoni kwamba ushindani miongoni mwa vikundi unaweza kuinua viwango vya usimilisho. Hata hivyo, asimilia 20 ya walimu iliunga mkono kupigwa marufuku kwa usimilisho ambao hautimizi viwango vinavyotarajiwa.

5.3.2 Data Kutokana na Hojaji na Mahojiano na Wasimilishaji

Hojaji za wasimilishaji ziliwataka wajibu maswali mbalimbali kuhusu usimilisho wa riwaya. Maswali walioulizwa yalizua data ifuatayo:

5.3.2.1 Mwaka wa Kuanza Kusimilisha

Hojaji ya wasimilishaji iliwauliza kutaja mwaka walioanza kusimilisha riwaya na hadithi fupi. Kipindi cha kuanza kusimilisha riwaya kilikuwa kati ya mwaka 2000 na 2002 miongoni mwao. Hii ina maana kwamba wasimilishaji waliohojiwa walikuwa na tajriba pana katika usimilisho. Kwa hivyo, ilitarajiwa kwamba walikumbana na matatizo mbalimbali katika kusimilisha na walikuwa na mikakati ya kuyatatua.

5.3.2.2 Kiwango cha Elimu

Wasimilishaji walitakiwa kutaja kiwango cha juu katika somo la fasihi. Data iliyokusanywa ilionyesha kwamba kiwango cha juu cha usomi wa fasihi kwa wasimilishaji hao kilikuwa kidato cha nne. Hali hii ilionyesha kwamba wasimilishaji walikuwa na ufahamu wa kimsingi tu katika tanzu za riwaya, hadithi fupi, na tamthilia. Aidha, hawakuwa na msingi wa kinadharia kuwaongoza katika kusimilisha na kuchambua kazi za fasihi. Baadhi ya makosa ya usimilisho yaliyobainishwa katika tasnifu yalitokana na ukosefu wa elimu ya juu katika taaluma ya fasihi.

5.3.2.3 Ujuzi wa Kusimilisha

Kuhusu namna walivyopata ujuzi wa kusimilisha na kuigiza riwaya, majibu yao yalikuwa hivi:

- a. Kusoma chuoni – 0%.
- b. Kuwa kwenye kikundi cha uigizaji – 100%
- c. Kutazama yakifanywa na wengine – 75%
- d. Maarifa na ubunifu wako – 50%
- e. Njia nyingine – 0%

Majibu ya wasimilishaji yalionyesha pengo katika utoaji wa mafunzo ya kusimilisha kazi za kinathari. Njia za kupata maarifa ya kusimilisha zilikuwa kushiriki katika kikundi cha uigizaji, kutazama jinsi maigizo ya masimilisho hufanywa, na ubunifu wa mtu. Ikizingatiwa kwamba kiwango cha elimu cha wasimilishaji katika taaluma ya fasihi kilikuwa cha chini, ukosefu wa mafunzo ya usimilisho uliathiri kwa namna hasi jinsi walivyoitekeleza shughuli ya kusimilisha.

5.3.2.4 Malalamishi ya Hadhira

Wahojiwa walipoulizwa iwapo walikuwa wamepokea malalamishi kutoka kwa wanafunzi na walimu, asilimia 100 ilikiri kupokea malalamishi kuhusu usimilisho wao. Walitaja malalamishi yafuatayo:

- a. Kutoigiza sehemu fulani za riwaya – 75%
- b. Miondoko inayoudhi ama kuaibisha hadhira – 50%
- c. Waigizaji kuigiza nafasi nyingi – 25%
- d. Kutumia waigizaji vijana kuigiza watu wazima na wazee – 50%
- e. Kutoiwasilisha riwaya kama mwandishi – 25%

Malalamishi kutoka kwa hadhira yalihusu udondoshaji wa matukio, usawiri wa wahusika, na usimilisho wa maudhui. Idadi kubwa ya wahojiwa ililalamika kuhusu jinsi matukio fulani yalivyodondoshwa. Udondoshaji kama ulivyoelezwa na hoja ya awali, ulikuwa tatizo kubwa katika usimilisho wa kazi za kinathari na uliathiri uwasilishaji wa fani na maudhui ya matini chasili. Uteuzi wa waigizaji ulikuwa tatizo lililowafanya walimu na wanafunzi kutoa malalamiko. Mavazi ya kuaibisha, miondoko iliyoudhi jukwaani, lugha isiyo na

adabu, na matumizi ya waigizaji vijana kuchukua nafasi za watu wazima, ni baadhi ya mambo yaliyoudhi hadhira.

5.3.2.5 Matatizo ya Usimilisho

Wahojiwa walitakiwa kutaja matatizo ya usimilisho na yafuatayo ndiyo majibu yao:

- a. Matukio magumu kusimilika – 100%
- b. Lugha ngumu ya mwandishi – 75%
- c. Kuwepo na wahusika wengi katika riwaya ambao lazima waigizwe – 75%
- d. Mandhari ya kitamaduni yasiyo na visawe kwa muktadha lengwa – 50%

Asilimia 100 ya wasimilishaji ilitaja matukio magumu kama tatizo kuu la usimilisho. Matukio yalifasirika magumu kutokana na jinsi yalivyosimuliwa na lugha iliyotumika na mwandishi. Lugha ya Kiswahili katika riwaya za Kitanzania ilifasirika kuwa ngumu ikilinganishwa na ile ya riwaya za Kikenya. Aidha, utanzu wa riwaya kutokana na urefu wake una changamoto za kusimilishwa hasa ikizingatiwa idadi ya visa na wahusika.

5.3.2.6 Utatuzi wa Matatizo ya Usimilisho

Wahojiwa walipotakiwa kutaja namna wanavyoyatatua matatizo hayo, majibu yao yalikuwa ifuatavyo:

- a. Matukio magumu husimuliwa badala ya kuigizwa – 100%
- b. Walimu wa fasihi hushirikishwa kuifasiri lugha ya mtunzi – 50%

- c. Usimulizi hutumika kupunguza athari za udondoshaji matukio –
50%

Majibu ya wahojiwa yalibainisha usimulizi kama mbinu bora zaidi ya kusimilisha matukio magumu na kupunguza udondoshaji wa matukio. Usimulizi una uwezo wa kuwasilisha vipengele vya matini chasili kama vilivyowasilishwa na mwandishi. Asilimia 50 ya wasimilishaji ilikiri kwamba imekuwa ikiwashirikisha walimu wa fasihi katika usimilisho wa tanzu za riwaya na hadithi fupi. Walimu waliokuwa wakishirikishwa ni wale waliokuwa wameandikia vitabu hivyo tahakiki.

Utafiti umeyawasilisha matatizo ya usimilisho wa riwaya kama yalivyobainishwa na wasimilishaji na walimu. Sehemu inayofuata ni mijadala na maelezo kuhusu matatizo hayo ikihusisha mifano mahsusi kutoka kwa masimilisho na data iliyowasilishwa kijarabati. Misingi ya nadharia changamano iliyoongoza utafiti huu, imetumika katika mijadala na maelezo hayo.

5.3.3 Matatizo Yaliyotokana na Mbinu za Usimilisho

Cahir (2006) anasema kwamba matatizo ya usimilisho yanaweza kutokana na matini inayosimilishwa na mbinu zinazotumika kusimilisha. Utafiti ulibaini kuwepo na matatizo ya usimilisho yaliyotokana na uteuzi wa mbinu fulani ya usimilisho. Sehemu hii imejadili matatizo yaliyodhihirika sana. Matatizo hayo yalibainishwa na wahojiwa na mtafiti ameyajadili kupitia mifano aliyogundua katika masimilisho na maigizo yake.

5.3.3.1 Udondoshaji wa Maudhui Muhimu

Udondoshaji umeelezewa kama mbinu ya usimilisho katika matini. Hata hivyo, pale udondoshaji huo ulipofanywa pasipo kufikiria maudhui yaliyowachwa, ulizua tatizo la usimilisho. Sehemu zilizodondoshwa mara nyingi ni kama vile usimulizi dhahania, matukio tata kuigizika, utendaji unaopingana na maadili, na matukio yanayotokea kwa mandhari yenye ugumu kuwekwa jukwaani.

Wasimilishaji walishindwa kusimilisha matukio yaliyokuwa yakisimuliwa katika udhahanifu. Katika riwaya ya *Utengano*, ndoto mbili zilizotumia jazanda yenye usimulizi wa kidhahania zilidondoshwa. Baadhi ya matukio yalitatiza namna ya kuyaigiza. Matukio hayo ni kama yale yaliyohitajia jukwaa kubwa ama huria ili kuyaigiza. Katika riwaya ya *Siku Njema*, matukio kama vile mazishi ya Zainabu na kushambuliwa kwa Bi. Rahma na fahali wakubwa hayakusimilishwa. Fauka ya haya, kuna matukio yaliyowachwa nje kutokana na misingi ya maadili ya kijamii. Haya ni yale yangeitudhi hadhira ama kuikosea heshima. Katika riwaya ya *Siku Njema*, matukio mawili yaliyofanyika katika mochari ya Makadara yalidondoshwa. Hiyo ni kutokana na miiko ya kitamaduni ambayo hupinga hali za kusawiri wafu kwa namna wazi.

Kwa kuwa riwaya nyingi haziandikwi kuigizwa jukwaani, baadhi ya matukio yake huwa sio rahisi kufikiria jinsi unavyoweza kuyaigiza. Kudondoshwa kwa sehemu zozote za riwaya kulifanya maudhui muhimu kutobainishwa katika similisho. Mtihani wa fasihi hutahini wanafunzi maswali ya muktadha kubaini usomaji na uelewa wao wa riwaya. Kama mbinu ya usimilisho, udondoshaji ulibainika kuwa na upungufu mwingi kwa kigezo cha uwasilishaji wa riwaya kwa usahihi wake. Nadharia ya usimilisho huhimiza vipengele vya maana viwasilishwe kwa usahihi kama vilivyowasilishwa na matini chasili (Lhermitte,

2005). Hali ya kudondoa matukio na usimulizi wa riwaya ilikuwa ikipangana na msingi huu wa nadharia ya usimilisho.

Udondoshaji unaafiki usimilisho iwapo utatumika ili kuondoa uziada katika usimulizi unaohusu wasifu wa wahusika na mandhari. Hii ni kwa sababu vipengele hivyo vya fani katika riwaya vinaweza kudhihirishwa jukwaani na hadhira ikavifasiri kwa ukamilifu wake. Kulingana na Booth na wengine (2006), kazi za kimasimulizi hulenga kumsawiri mhusika kwa ukamilifu wa sifa zake, ilhali tamthilia huzirahisisha na kuzifupisha sifa za mhusika ili zionyeshwe jukwaani pasipo kuzieleza. Kwa mujibu wa kauli hii, maelezo ya vitu ambavyo hadhira inaweza kuviona jukwaani hayahitajiki katika tamthilia. Jambo la muhimu ni kuhakikisha kuwa mandhari na wahusika wanasawiriwa namna walivyo katika matini chasili.

Kama ilivyobainika, udondoshaji wa mazungumzo ya wahusika na matendo yao huathiri uwasilishaji wa maudhui na fani moja kwa moja. Kwa mujibu wa hoja ya awali, kigezo muhimu cha kuongoza udondoshaji ni ukadiriaji wa uzito wa maudhui na fani kwa uelewa wa kazi nzima na dhamira ya mwandishi.

5.3.3.2 Usawiri wa Wahusika

Matatizo katika mbinu hii yalibainika sana katika uigizaji. Namna vipengele fulani vya usawiri wa wahusika vilivyosimilishwa, ilizua hitilafu zilizoathiri uwasilishaji wao kwa usahihi wa riwaya. Udhaifu uliobainika ulihusu lugha yao, mavazi, umbile, idadi, na jinsia.

Wasimilishaji waliniuia kuwasilisha lugha ya wahusika kwa misingi ya lugha ya mazingira ya mtunzi. Tatizo moja ni kwamba hawakufaulu kuiwasilisha lugha ya mazingira ya mtunzi. Kwa vile riwaya za *Utengano* na *Siku Njema* zilikuwa na

uelemeo katika mazingira ya Uswahilini, waigizaji walichagua kutumia lafudhi za Uswahilini katika matumizi yao ya lugha, hasa lahaja ya Kimvita. Ingawa nadharia ya uigizaji huhimiza wahusika wabainishwe kijamii na lugha, utahini wa riwaya unafanywa kwa misingi ya lugha sanifu. Matumizi ya lahaja na lafudhi hupotosha lengo la kuwafundisha wanafunzi lugha sanifu.

Mbali na lahaja, sifa za matumizi ya lugha zilitiwa chuku. Kwa mfano, waigizaji Zanga na Bi. Shomari katika similisho la *Utengano*, walitia chuku ugugumu wao. Ilikuwa vigumu kusema hata neno moja liweze kueleweka. Matumizi ya lugha sanifu yaliwapiku waigizaji kadha na badala yake wakaitumia lugha isiyo sanifu ama msimbo wa sheng'. Mathalan, katika kikundi kimoja, mwigizaji Maksuudi alinukuliwa akimuuliza Bi. Tamima hivi:

MAKSUUDI: Unataka katoto aka ukakaue kama wale wengine?

Kauli hii siyo sahihi kisarufi, na zaidi inapotosha, kwani hamna mtoto wa Maksuudi alikuwa amefariki wakati ilipotolewa. Lhermitte (2005) anasema kwamba, katika mchakato wa kusimilisha uhamishaji wa vipengele vya kiisimu ni sharti ulenge kuwasilisha maana ya matini chasili kwa ulinganifu na usahihi wake. Kwa mujibu wa hoja ya awali, hali ya kukiuka matumizi ya lugha sanifu katika usimilisho ilikuwa ikipotosha malengo ya kufundisha lugha hiyo shuleni na hata kule kuteuliwa kwa riwaya husika. Mbali na kufundisha maadili, vitabu teule vya fasihi huwa kama vielelezo vya matumizi bora ya lugha.

Usawiri wa wahusika ulikosewa katika vipengele vya mavazi, jinsia na umbile. Maleba ya waigizaji mara nyingi hayakuzingatia maelekezo ya riwaya. Katika riwaya ya *Utengano*, inaarifiwa kwamba mhusika Dora alikuwa amevalia skati na blauzi ya manjano iliyoandikwa TOYOTA. Maleba hayo hayakudhihirishwa.

Diyanni (2004) anaeleza kwamba, maleba yanaweza kubainisha sifa za ndani za mhusika pamoja na mabadiliko ya hisia ya mhusika huyo. Vazi la Dora lilifumbata sifa zake muhimu na kule kutumia vazi tofauti kulimsawiri kinyume na sifa hizo.

Upungufu ulihusu, pia, kipindi cha wakati na maleba mwafaka ya kipindi hicho. Haya yanaihusu zaidi riwaya ya *Utengano*. Hamkuwa na mavazi mahsusi yaliyodhihirisha kipindi cha miaka ya themanini ya karne ya ishirini wakati riwaya hiyo iliandikwa. Mavazi ya waigizaji yalisawiri usasa. Kulingana Wilson na Goldfarb (1991), maleba ya waigizaji yanapaswa kuarifu hadhira kuhusu kipindi cha wakati kinachorejelewa na mahali ama nchi ambapo tendo la tamthilia limekitwa. Hali ya kutosawiri wakati ipasavyo iliathiri uelewa wa wanafunzi kwa baadhi ya masuala ya kihistoria katika riwaya.

Maelekezo ya riwaya kuhusu umbile la wahusika fulani hayakuzingatiwa. Wahusika walioelezwa kuwa wanene na wenye misuli kama vile Biti Sururu, Mama Jeni na Shoka waliigizwa na vijana wembamba. Aidha, kuna wahusika ambao hawakuwa na ngozi nyeusi kama vile Ganj na Ashuru, lakini wakaigizwa na waigizaji weusi.

Jinsia na idadi ya wahusika ilikosewa katika usimilisho. Katika uigizaji wa *Siku Njema*, sehemu fulani iliyorejelea banati mmoja iliigizwa na wavulana wawili. Hii ni fasiri kinyume ya jinsia na idadi ya wahusika.

Wahusika ni kipengele muhimu katika ufundishaji wa fasihi shuleni. Wanafunzi hutarajiwa kujifunza maadili kutoka kwa wahusika. Aidha, fasihi hutahini uelewa wa wanafunzi kuhusu wasifu na nafasi za wahusika katika riwaya. Hali ya kutowasilisha usawiri wa wahusika ipasavyo katika usimilisho ni kinyume na

nadharia ya uigizaji, na matarajio ya wanafunzi na walimu kwa usimilisho wa riwaya. Usimilisho wa aina hiyo unapotosha usawiri wa wahusika. Kuna haja uteuzi wa waigizaji ufanywe kwa vigezo vya umri, jinsia, rangi, lugha, umbile, idadi, na mavazi, kama inavyoelekezwa na nadharia ya uigizaji. Uzingatiaji wa vigezo hivyo utahakikisha kuwa usimilisho wa riwaya umefanywa kwa usahihi wake.

5.3.3.3 Ubunaji wa Muundo wa Tamthilia

Utafiti ulibaini tatizo la jinsi muundo wa riwaya ulivyosimilishwa. Kulingana na Wilson na Goldfarb (1991), muundo wa kidrama una vipengele vinne vikuu:

- I. Ploti: Mpangilio wa matukio ama uteuzi na mpangilio wa maonyesho katika tamthilia.
- II. Mgogoro: Mgongano ama upinzani baina ya wahusika ama kani katika tamthilia ambazo husababisha tendo la kidrama.
- III. Kani kinzani: Wahusika wanaovutana huwa na malengo mahsusi ambayo sharti wayatimize; hata hivyo, huwa ni wapinzani wa dhati ambao wako tayari kufanya kila jambo ili waafikie malengo yao.
- IV. Usawazishaji wa kani: Wahusika wanaokinzana ama kani ni lazima zisawazishwe. Ingawa upande mmoja ni lazima ushinde, lakini kabla ya ushindi huo ni lazima pande zote zionyeshwe zikiwa sawa katika uwezo na matamano. Ushindani baina ya pande zote mbili haufai kujitokeza kama unaegemea upande mmoja.

Katika tamthilia, onyesho la ufunguzi huanzisha tendo na huweka toni na mtindo kwa matukio yanayofuata. Mwandishi hubunia wahusika tatizo ama hukuza kutolingana kwa kani ambazo hulazimu wahusika kuitikia. Wilson na Goldfarb

wanasema kwamba, kwa kawaida kutolingana kwa kani kunapaswa kudhihirishwa kabla ya kuanza kwa tamthilia ama kujitokeze mara tu baada ya tamthilia kuanza.

Mtazamo wa Wilson na Goldfarb (1991) kuhusu muundo wa tamthilia unakaribiana na ule unaofafanuliwa na Diyanni (2004), na Booth na wengine (2006). Diyanni, Booth na wengine wamekubaliana kimaoni kwamba muundo wa tamthilia unakuzwa na hatua tano katika uendelezaji wa mgogoro: maelezo ya ufunguzi, kupanda kwa tendo, kilele, mpomoko, na hitimisho au utatuzi wa migogoro. Kwa maoni yao mgogoro ndio injini inayoendesha ploti, na uwasilishaji wa mgogoro ndio unaoupa sura muundo wa tamthilia.

Usimilisho wa riwaya haukuonekana kuzingatia matakwa ya muundo wa kidrama kama yanavyojadiliwa na waandishi hawa. Riwaya za *Utengano* na *Siku Njema* zilibuniwa kwa muundo ambao ungesimilishwa kuwa wa kidrama. Katika riwaya ya *Utengano*, mhusika Maimuna amesawiriwa akiwa na malengo wazi ya kujitafutia uhuru kwa vyovyote vile. Mhusika Farashuu alikuwa mkinzani wake katika juhudi za kujitafutia uhuru. Aidha, Makuudi amesawiriwa akiwa na lengo la kutaka kuipatanisha familia yake baada ya kutengana. Katika riwaya ya *Siku Njema*, Kongowea amechorwa akiwa na lengo dhahiri la kumsaka na kumpata baba yake. Katika azimio lake anakabiliwa na ukinzani kutoka kwa Saumu na Suleimani Mapunda. Hatua ya ufunguzi katika *Utengano* ni utengano uliotokea katika familia ya Makuudi. Katika *Siku Njema* ufunguzi ni mafarakano yaliyotokea katika familia ya Makame Mwinyi yanayosababisha nyanya yake Kongowea kugura na kwenda kuishi kwa wazazi wake. Hiki ndicho kiini cha umaskini unaoathiri majaaliwa ya Kongowea. Riwaya zote mbili zina sehemu ya kilele, mpomoko, na hitimisho. Kilele katika *Utengano* ni pale Farashuu

anapopinga ndoa ya Kabi na Maimuna. Katika hatua hii haibainiki kama baba yake Makuudi atakubali ndoa hiyo ikizingatiwa Kabi ni mtoto wa bibi yake waliotalakiana. Sehemu ya mpomoko inajitokeza pale radhi za ndoa zinapotolewa na riwaya inahitimishwa kwa habari ya tanzia ya kifo cha Makuudi. Kilele katika riwaya ya *Siku Njema* ni pale Kazikwisha anaposababisha kutibuka kwa mhadhara uliokuwa ukiendeshwa na Kongwea shuleni. Hitimisho linatokea pale Kongwea anapofika kwa Kazikwisha na kupata maiti yake pamoja na waraka aliomwachia. Kutokana na waraka huo anapata kubaini kwamba Kazikwisha ndiye aliyekuwa baba yake mzazi.

Wasimilishaji walijifunga katika muundo wa riwaya ambao ulisimilishwa na kuigizwa jukwaani. Hii ilikuwa sababu moja ya udondoshaji kwani sehemu ambazo hazingeweza kuigizwa kwa muundo wa riwaya zilidondoshwa. Aidha, kuufuata muundo wa riwaya katika usimilisho kulifanya kuwa vigumu kubuni maonyesho ambayo yangeigizika na kueleweka kwa urahisi. Matokeo yake yalikuwa ubunaji wa maonyesho mengi ambayo yalishindwa kuonyesha msababishano. Kwa mujibu wa Diyanni (2004), ploti ni mfuatano wa visa vinavyohusiana na kusababishana. Visa kadha vilivyoigizwa havikuonyesha kusababishana na uhusiano uliopo ulijengwa mara nyingine na msimulizi. Ingawa matarajio ya usimilisho aminifu ni kuwa muundo wa riwaya utahamishwa kwa matini ya similisho kwa usahihi, uigizaji wa muundo huo ulionyesha upungufu mwingi jukwaani, na kuleta ugumu wa kuyafuatilia matukio ya riwaya.

Mbali na muundo wa ndani wa tamthilia, kuna muundo wa nje ambao hufafanuliwa kutokana na jinsi tamthilia inavyoonekana kwa macho. Tamthilia hubuniwa na mazungumzo ambapo kila mhusika huonyeshwa pamoja na maneno

yake. Aidha, muundo huu huhusisha migawanyo ya sehemu za matendo na maonyesho.

Muundo wa mazungumzo hubuniwa ukiwa na sehemu mbili. Kuna sehemu ya wahusika ambayo mara nyingi huendelezwa kwa herufi kubwa. Sehemu ya pili ya muundo wa mazungumzo huwa ni maneno ya wahusika (mazungumzo) ambapo kila mhusika huambatanishwa na maneno yake. Sehemu hizo mbili hutenganishwa na alama ya uakifishaji ya nukta mbili (koloni). Maneno ambayo hayatoki katika vinywa vya wahusika hufungiwa katika mabano. Muundo huo haukuzingatiwa na wasimilishaji wote. Zingatia mfano ufuatao:

MAKSUUDI: Okay, toka humu (akibweka) (Fadhili anatoka huku akiwaza
kufukuzwa kwake halafu anajisemea) Damu ni nzito kuliko
maji! Damu ni nzito kuliko pesa!

Katika upangaji huu wa mazungumzo, maneno ya wahusika wawili yamewekwa kwa usemi wa mhusika mmoja kana kwamba ndiye aliyezisema kauli hizo zote. Ingawa masimilisho hayakulengwa kusomwa na wanafunzi, udhaifu kama huo ulikuwa chanzo cha makosa mengine katika uigizaji wa riwaya. Mbali na kusoma riwaya, wanafunzi hujifunza tamthilia na sifa zake kupitia usimilisho.

Tasnifu hii ilithibitisha tatizo la muundo wa maonyesho na matendo. Ingawa muundo huo ulitumika katika masimilisho, mantiki ya kisanaa ya kuyaweka maonyesho katika tendo moja hayakubainika. Aidha, kuna masimilisho yaliyounda maonyesho kutokana na sura za riwaya. Sura moja iliunda onyesho ambalo liligawika tena katika matukio mbalimbali. Idadi ya matukio ilitegemea idadi ya visa vya kuigizwa katika sura ya riwaya. Kulingana na nadharia ya uigizaji, onyesho hurejelea tukio mahsus ambalo huonyeshwa jukwaani kwa

wakati maalumu na katika mandhari sawa. Ubunaji wa matukio ndani ya maonyesho uliunda vijionyesho vingine vilivyotatiza mtiririko wa hadithi na msuko.

Usimilisho wa riwaya unastahili kufanywa kwa uzingatifu wa vipengele vya muundo wa kitamthilia. Kuzitii kanuni za kimuundo kutazuia kuhamishwa kwa matatizo ya kimuundo katika uigizaji.

5.3.3.4 Usawiri wa Mandhari

Mandhari ni mahali ama wakati unaorejelewa wa kutokea kwa tukio fulani katika kazi ya fasihi. Riwaya zilizosimilishwa zilikuwa zimeyaelezea mandhari ya matukio yaliyomo. Masimilisho hayakuwasilisha usawiri huo kikamilifu katika usimulizi na maelezo ya jukwaani. Kama ilivyobainika awali, masimilisho mengine yalikosa ama yakapungukiwa katika matumizi ya mbinu ya usimulizi.

Upungufu katika usawiri wa mandhari katika masimilisho uliathiri namna maandalizi yake yangefanywa jukwaani. Katika riwaya ya *Utengano*, vikundi vyote vilikosa kusawiri dhana ya mabadiliko katika nyumba ya Makuudi. Samani na vifaa vilivyotumika kusawiri utajiri wa Makuudi nyumbani mwake havikubadilishwa, licha ya riwaya kuelezea kwamba alipoteza baadhi ya mali yake. Aidha, mandhari ya shambani kwa Makuudi na mjini Liwazoni yaliwasilishwa kwa jinsi sawa. Makosa hayo yalititiza kuelewa maudhui ya mabadiliko na mtazamo wa mwandishi kuyahusu.

Usawiri wa mandhari kiwakati ulidhihirisha kasoro kubwa. Maigizo yalishindwa kuakisi vipindi vya wakati vilivyokuwa vikiangaziwa na riwaya hizo. Kama ilivyotanguliwa kusemwa, riwaya ya *Utengano* ilikuwa ikisawiri kipindi cha miaka ya themanini na nyuma, ya karne ya ishirini. Hicho ni kipindi ambacho

elimu ya Kimagharibi ilikuwa inatumika kuondoa mila na itikadi za Waafrika zilizokuwa zimepitwa na wakati. Riwaya hiyo inakashifu taasubi za kiume na kutawishwa kwa wanawake. Masuala yanayojadiliwa na riwaya hiyo yalidhihirishwa katika wakati wa sasa. Nyimbo zilizoimbwa katika matukio mbalimbali zilikuwa za kisasa, hata na miondoko. Usasa katika maleba ya wahusika ulidhihirishwa na minisketi za kisasa, wasichana kuvalia suruali ndefu, na wavulana kuvalia vipuli masikioni na kusukwa nywele.

Usawiri wa mandhari wenye upungufu ulikosa kuiwasilisha riwaya jinsi ilivyokuwa imeandikwa na mwandishi. Dhana ya wakati wa utunzi ni muhimu katika uelewa wa masuala ibuka ya wakati huo, na jinsi yameendelea kusakini katika jamii zetu. Hili ni lengo moja linaloongoza uteuzi wa riwaya za zamani ili zitahiniwe wanafunzi. Hali ya kutouwakilisha wakati ipasavyo inakwenda kinyume na matarajio katika riwaya teule. Kwa mujibu wa Mohamed (1995), suala la wakati unaomulikwa na tamthilia ni muhimu na linapaswa kuzingatiwa katika uigizaji.

5.3.3.5 Uigizaji wa Mbinu

Uigizaji wa mbinu za utunzi ni mbinu ya usimilisho jukwaani. Namna uigizaji wa mbinu hizo ulivyotekelezwa uliweza kuibua matatizo fulani. Upungufu huo ulibainika kupitia hojaji za wahojiwa na utazamaji wa maigizo ya riwaya. Wahojiwa walionyesha kutoridhika na jinsi usimilisho wa mbinu ulivyofanywa. Mbinu za utunzi zilijumuisha:

I.Mbinu za lugha

II. Mbinu za kisanaa

Mbinu za lugha, ambazo zilijumuisha tamathali za usemi, uteuzi wa msamiati, methali, nahau, misemo, miongoni mwa nyingine, hazikuleta changamoto zaidi kwa vile zilifaraguliwa katika mazungumzo ya wahusika. Mbinu za lugha ambazo zilitumika katika usimulizi wa riwaya, ziliwasilishwa na watambaji jukwaani. Tatizo lilidhihirika kwa makundi ambayo hayakutumia wasimulizi na yale yaliyowatumia wasimulizi kwa kiwango kidogo katika maigizo yao. Makundi hayo yalishindwa kuwasilisha mbinu zote za lugha ambazo zilikuwa zimetumika katika usimulizi na mwandishi. Aidha, udondoshaji wa sehemu fulani za riwaya ulichangia kutowasilishwa kwa mbinu fulani za lugha.

Mbinu za kisanaa zilijumuisha ndoto, jazanda, sadifa, majazi, simu, gazeti, shairi, nyimbo, barua, miongoni mwa nyingine nyingi. Vikundi teule vilionyesha ufanisi katika matumizi ya simu, gazeti, nyimbo, barua na mashairi. Kama ilivyoelezewa katika mbinu za usimilisho, mbinu hizi ziliwasilishwa jukwaani kupitia sauti ama utendaji. Hata hivyo, sauti iliyorekodiwa ama kusema, mara nyingi haikuwa ya mwigizaji aliyerejelewa jukwaani. Hali hiyo iliyafanya matumizi hayo kupoteza uhalisi na kupotosha usawiri wa wahusika wa riwaya.

Uigizaji wa jazanda, ndoto, mbinu rejeshi, na sadifa, ulihitaji ufundi kutoka kwa msimilishaji. Namna mbinu hizo zilivyosimilishwa imeelezwa katika sehemu iliyotangulia. Utazamaji wa maigizo ya riwaya na uhakiki wa masimilisho ulibaini kwamba vikundi kadha vilishindwa kuwasilisha mbinu rejeshi kama ilivyokuwa imetumika na mwandishi. Matukio ilimotumika yaliigizwa yakifuatana bila kiashiria kuonyesha tofauti ya kiwakati. Hali hiyo ilipotosha mtiririko wa msuko, na kuifanya vigumu kwa hadhira lengwa kuipokea riwaya kama ilivyokuwa imewasilishwa na mwandishi. Kulingana na Booth na wengine (2006), tofauti za kiwakati baina ya maonyesho aghalabu huonyeshwa kupitia

pambo la jukwaa, sauti, na maelezo ya jukwaani. Mbinu ya sauti ama upangaji wa jukwaa ungetumika kuashiria mbinu rejeshi jukwaani. Aghalabu, mwangaza hufanywa hafifu ama sauti nzito kucheza, ili kuashiria kuwa matukio yanayoendelea jukwaani yamechukua mkondo mwingine kiwakati.

Ingawa mbinu ya sadifa ilitumika sana katika riwaya ya *Utengano*, masimilisho na maigizo yake hayakuitokeza kikamilifu. Msisitizo na nafasi iliyopewa katika hadithi ulikosa kudhihirika. Mbinu ya jazanda ilitegemea utambaji, na masimilisho yaliyopungikiwa katika utambaji yalikosa vilevile kuiwasilisha mbinu hiyo. Jazanda ilitumika kuwasilisha maudhui fulani ya riwaya na hali ya kuidondoa ilidhoofisha viwango vya usahihi wa masimilisho.

Maigizo ya riwaya ya *Siku Njema* yalidhihirisha udondoshaji wa mbinu za kisanaa kuliko ilivyokuwa katika riwaya ya *Utengano*. Katika riwaya ya *Siku Njema*, baadhi ya mbinu za kisanaa kama vile ushairi (uk.4, 7 na 95), gazeti (uk.15), ilani (uk.100), na barua (uk. 119, 92 na 94), hazikuigizwa. Mbinu hizo za kisanaa zilikuwa zimebeba maudhui muhimu katika riwaya na kudondoshwa kwake kulidhoofisha uwasilishaji wa dhamira ya mwandishi.

Kama ilivyotajwa awali, mbinu za utunzi huchukuliwa kama vipengele muhimu vya hadithi na maana. Kipengele cha utamaduni huweza kuwasilishwa kupitia matumizi ya mbinu mbalimbali za utunzi. Usimilisho unapokosa kuzitilia maanani, malighafi za kitamaduni na maana, zitakosa kudhihirika katika masimilisho ya riwaya. Nadharia ya usimilisho husisitiza vipengele hivyo kuwasilishwa kwa uaminifu iwezekanavyo.

Kwa kifupi, hayo ni baadhi ya matatizo makuu yaliyodhihirishwa na mbinu za usimilisho. Matatizo hayo yamejadiliwa kama yalivyojitokeza katika masimilisho na maigizo yake.

5.3.4 Matatizo Yaliyotokana na Wasimilishaji

Haya ni matatizo yaliyobainika kuwa na chanzo chake kwa wasimilishaji wa riwaya. Kupitia hojaji na mahojiano, wasimilishaji waliweza kutaja baadhi ya matatizo yanayowakabili katika mchakato wa kusimilisha kazi za kimasimulizi. Aidha, uhakiki wa masimilisho na maigizo yake uliweza kubainisha matatizo ambayo yamehusishwa na wasimilishaji. Matatizo ya usimilisho yaliyotokana na wasimilishaji ni kama vile matini zilizotumia lugha ngumu na tata, utegemezi uliokithiri wa mazungumzo, kutia chumvi katika matukio ya riwaya, na tatizo la kifedha. Matatizo haya yameelezwa kwa kina na kutolewa mifano kutoka kwa masimilisho na maigizo yake.

5.3.4.1 Matini Zilizotumia Lugha Ngumu na Tata

Wasimilishaji walioisimilisha riwaya ya *Utengano* walilalama kuwa, lugha ya Said Ahmed Mohamed ilikuwa ngumu kufasirika. Kwa kuwa kiini cha usimilisho kilikuwa kuisoma riwaya husika, ilibidi katika sehemu fulani za riwaya wasimilishaji wategeme miongozo ya uhakiki, walimu wa fasihi ama masimilisho yaliyokuwa yakiuzwa katika soko la uigizaji.

Utafiti ulibaini kuwa wasimilishaji walikuwa na elimu ya kiwango cha chini katika masuala ya lugha na fasihi yake. Wasimilishaji waliohojiwa na mtafiti walikuwa na elimu ya kidato cha nne, lakini tajriba pana katika masuala ya uigizaji na utunzi. Lugha katika riwaya ya *Utengano* ilisheheni jazanda tata,

taswira nzito, methali zenye asili ya kipwani, lugha ya kimkato, ndoto na ishara, ufundi wa kuyasuka mazungumzo na uteuzi wa msamiati sanifu na usio sanifu.

Usimilisho hudhamiriwa kuinua viwango vya uelewa wa wanafunzi kwa riwaya inayotahiniwa ili kuwawezesha kuupita mtihani wa fasihi. Hii ndiyo maana asilimia 90 ya walimu iliutaja kuwa muhimu kwa maandalizi ya mtihani wa KCSE. Ili usimilisho uweze kuwafaidi wanafunzi kama unavyodhamiriwa, ni muhimu wasimilishaji wasomeshe wapate maarifa na ujuzi wa kuitekeleza fani hii.

5.3.4.2 Utegemezi Uliokithiri wa Mazungumzo

Mazungumzo ndiyo mbinu kuu iliyotumika kusimilisha riwaya kuwa tamthilia ya kuigiza jukwaani. Hata hivyo, wasimilishaji wengi waliyategemea mazungumzo ya riwaya na kupuuza usimulizi wake. Hali hiyo iliathiri uwasilishaji ufaao wa mandhari na wasifu wa wahusika. Hata katika maelezo ya jukwaani, usawiri wa mandhari na wahusika haukujitokeza kama ulivyosawiriwa katika riwaya.

Hali ya kuyategemea mazungumzo ya riwaya ilitokana na ujuzi waliohodhi wa tanzu za fasihi. Tamthilia huigizika kwa sababu ya muundo wake wa mazungumzo na matendo. Ukweli huu uliyafanya mazungumzo ya riwaya kuwa kivutio kwa wasimilishaji. Mazungumzo hayo yalidondolewa pasipo na fikira ya jinsi sehemu nyingine za riwaya zingewasilishwa. Kwa jicho pevu, usimilisho ulifanywa kama udhihirishaji wa jinsi umatini wa tamthilia katika riwaya ungeigizwa. Kutokana na hali hiyo, vipengele vya maudhui na fani vilivyowasilishwa ni vile vilivyopatikana katika umatini wa kitamthilia katika riwaya. Kila msimilishaji alidhihirisha kiwango fulani cha tatizo hili, ambalo ndilo chanzo cha udondoshaji.

Kuna haja ya kuukagua usimilisho unaohusu vitabu vinavyotahiniwa. Jambo hilo halifai kufanywa kwa madhumuni ya kuharamisha usimilisho huo, bali ni kutambua masimilisho yenye udhaifu na kuelekeza jinsi ya kuyaboreshwa kabla yaidhinishwe kuigiziwa wanafunzi.

5.3.4.3 Kutia Chumvi katika Matukio ya Riwaya

Uchanganuzi wa masimilisho, maigizo yake, na hojaji za walimu zilibainisha kwamba wasimilishaji walikuwa wakiongeza mambo ambayo hayakuwepo katika riwaya. Hivyo ni vimatini vya vichekesho na utendaji kinyume. Walimu kupitia hojaji walilalamikia kuwepo na vimatini ziada na madoido mengi katika maigizo hayo. Baadhi ya wahusika wa riwaya walipotoshwa na kusawiriwa kama wacheshi na walevi katika miktadha mbalimbali. Hata mavazi yao yalitoa taswira ya kuchekesha.

Utendaji kinyume ulihusu tendo la riwaya kupinduliwa na kuigizwa kinyume na hali ilivyokuwa. Baadhi ya vitendo vilifanywa hivyo kutokana ujuzi mdogo wa msimilishaji, huku vingine vikifanywa kwa madhumuni ya kuwafurahisha wanafunzi. Katika riwaya ya *Utengano*, Mama Jeni alionekana akiwaachia wahudumu hotelini na madukani masalio ya bili, huku Zanga na Maksuudi wakionyeshwa wakitoa hongo hadharani katika mkutano wa siasa. Hayo yote yanapingana na usawiri wa riwaya.

Hali ya kutia chumvi katika usimilisho ilikuwa ikiipotosha riwaya. Matarajio ya kuiwasilisha riwaya kwa usahihi yalikiukwa moja kwa moja. Upotoshaji huo huenda uliathiri matokeo ya wanafunzi katika mtihani wao wa kidato cha nne. Walimu wana jukumu la kuhakiki maigizo hayo yanapokamilika na kuelekeza wanafunzi kwa sehemu ambazo zimepotoshwa. Utafiti ulibaini kwamba walimu

hawakuwa wamefikiria kuhusu athari hasi za usimilisho huo kwa ufundishaji wa riwaya.

5.3.4.4 Tatizo la Fedha

Usimilisho ulibainika kuwa shughuli ghali na inayohitaji mtaji kuifanikisha. Fedha zilihitalijika ili kuwalipa walimu walioshauriwa kuhusu mchakato wa kuisimilisha riwaya. Majumba ya kuigizia hulipisha hela nyingi kwa siku kufanyia maigizo humo. Vikundi vinavyotembelea shule, huhitaji kugharamia usafiri wa waigizaji na malazi yao.

Kutokana na mahojiano na wasimilishaji, tatizo la kifedha lilibainika kuathiri matokeo ya usimilisho kwa njia tatu. Kwanza, liliwafanya baadhi ya wasimilishaji kuwatumia waigizaji chipukizi kwa vile waigizaji wenye ujuzi mpana walihitaji kulipwa hela nyingi. Pili, ili kuepuka gharama kubwa ya kuwasafirisha na kuwalipia malazi waigizaji wengi, wasimilishaji waliwatumia waigizaji wachache ili waigize nafasi nyingi. Tatu, vikundi vilivyotembelea shule viliigiza vitabu vitatu kwa siku moja ili kupunguza gharama.

Utazamaji wa maigizo uliweza kubainisha kwamba waigizaji chipukizi na wale walioigiza zaidi ya nafasi moja ya mhusika walitatizika kuimudu matini ya similisho. Hali ya kusitasita na kusahau ilithibitika. Kuigiza nafasi nyingi kulipotosha namna hadhira ilivyotakiwa kuhusisha sifa za mwigizaji na mhusika wa riwaya. Ubadilishaji wa nafasi ulifanywa hata pasipo na mabadiliko yoyote kwa mwigizaji. Kwa hivyo, haikuhalisi mwigizaji mmoja kubeba wasifu wa wahusika wengi. Ni jambo linaloweza kujadiliwa kuhusu uwezekano wa kikundi kuigiza tamthilia, riwaya, na diwani ya hadithi fupi katika siku moja, na kwa kutumia waigizaji wale wale. Utafiti ulibaini hicho kama chanzo kimoja cha

matatizo ya usimilisho. Maigizo ya aina hiyo yaliwezekana kupitia udondoshaji wa maudhui muhimu katika tungo zilizokuwa zikisimilishwa. Wasimilishaji waliigiza tamthilia jinsi ilivyotungwa, lakini maigizo ya riwaya na hadithi fupi yakafanywa kwa mujibu wa muda uliokuwa umesalia.

Ingawa ni jambo la busara kufanyiwa maigizo hayo shuleni, hali ya kuyafanya yagharamike ilionekana kushusha viwango vyake. Maigizo hayo yalianza mwendo wa saa nne na kukamilika mwendo wa saa kumi. Hicho kilikuwa kipindi kirefu kwa wanafunzi kumakinikia maigizo ya vitabu vitatu tofauti. Ili usimilisho wa riwaya upokelewe kama usomaji wake, ni muhimu maigizo yake yatengewe muda unaotosha. Kwa vile ni vigumu kuisoma riwaya na hadithi fupi nyingi siku moja, maigizo ya kila kitanzu yanapaswa kutengewa siku yake.

5.4 Kiishilio

Sura hii imejadili aina moja ya usimilisho iliyoelezewa katika sura ya nne. Huu ni usimilisho wa tanzu za fasihi zinazotahiniwa katika mtihani wa KCSE. Sura imebainisha na kutathmini mbinu za usimilisho wa riwaya. Mbinu hizo zimedhihirika katika hatua mbili; usimilisho katika matini na usimilisho jukwaani.

Sura imezjadili hatua hizo pamoja na kuzibainisha mbinu zinazopatikana katika kila hatua. Mifano na maelezo yaliyotumiwa yalitokana na riwaya teule: *Utengano* na *Siku Njema*. Mtafiti amezihakiki mbinu hizo kwa misingi ya nadharia changamano iliyoongoza utafiti huu. Utafiti umebaini kwamba, mbinu za usimilisho hutegemea mtindo uliotumika kuiandika riwaya husika. Aidha, utafiti umegundua kuwa, riwaya husanifiwa kwa sifa fulani za kitamthilia ambazo huwa ni msingi wa mbinu za kuisimilisha.

Mbali na kujadili mbinu za usimilisho wa riwaya, sura imeyabainisha matatizo yaliyodhihirishwa na usimilisho. Utafiti umebaini chanzo cha matatizo hayo kuwa ni msimilishaji mwenyewe na mbinu anazotumia kuisimilisha riwaya. Aidha, sura imeweza kupendekeza namna matatizo hayo yanavyoweza kusuluhishwa. Sura hii imebaini kwamba usimilisho wa riwaya kwa minajili ya kuwaandaa wanafunzi kwa mtihani wa KCSE unachukuliwa kwa umuhimu mkubwa. Hivyo basi, kuna haja ya kuyakagua maigizo hayo mara kwa mara ili kukadiria ubora wake na kuharamisha mitindo isiyofaa.

Sura ya sita ni mwendelezo wa sura ya tano. Sura hiyo imezibainisha baadhi ya mbinu za usimilisho zilizodhihirisha tofauti katika usimilisho wa hadithi fupi.

SURA YA SITA

MBINU NA MATATIZO YA USIMILISHO WA HADITHI FUPI

6.0 Utangulizi

Sura iliyotangulia imeshughulia mbinu za usimilisho wa riwaya. Aidha, sura hiyo imeyabainisha na kuyaeleza matatizo ya usimilisho huo, pamoja na jinsi yanavyoweza kutatuliwa. Sura hii inauendeleza mjadala huo kwa kuchunguza na kueleza mbinu za usimilisho wa hadithi fupi. Mjadala huo utajikita katika mbinu za usimilisho wa hadithi fupi zilizobainisha tofauti ikizingatiwa jinsi zilivyotumika katika usimilisho wa riwaya. Aidha, matatizo ya usimilisho wa hadithi fupi yamejadiliwa. Diwani za hadithi fupi zinazohusika ni *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* na *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*.

Tasnifu imezjadili mbinu za usimilisho wa hadithi fupi katika hatua mbili:

a) Mbinu za usimilisho wa matini za hadithi fupi

b) Mbinu za usimilisho wa hadithi fupi jukwaani

6.1 Mbinu za usimilisho wa matini za hadithi fupi

Masimilisho ya hadithi fupi hayakubainisha mbinu tofauti za usimilisho yakilinganishwa na riwaya. Hata hivyo, namna usimilisho wa mbinu fulani ulivyojitokeza katika hadithi fupi ilikuwa tofauti na hali ilivyokuwa katika riwaya. Sehemu hii ya tasnifu imeshughulikia mbinu za usimilisho zilizodhihirisha tofauti katika usimilisho wa hadithi fupi.

6.1.1 Mazungumzo

Katika sura iliyotangulia, tasnifu hii imeeleza kwamba utungo wa riwaya hudhihirisha baadhi ya sifa za kitamthilia. Baadhi ya sifa zilizobainishwa ni mazungumzo, uzungumzi nafsi, utendaji na miktadha ya usemaji kando. Hadithi fupi, sawa na riwaya, hushirikisha sifa za kitamthilia katika muundo wake. Kama ilivyobainika, wasimilishaji huzitegemea sana sifa hizo za kimfanano ili kuisimilisha hadithi fupi kuwa tamthilia.

Matumizi ya mazungumzo yanahusu uvunjaji wa masimulizi na kuyafanya kuwa mazungumzo ya wahusika. Mazungumzo ni majadiliano na majibizano miongoni mwa wahusika wa tamthilia, na katika muktadha huu, similisho la hadithi fupi. Ubunaji wa mazungumzo ulifanywa kwa kuzingatia mbinu mahsusi za kisanaa. Baadhi ya mbinu hizo zimejadiliwa katika sura iliyotangulia.

Mbinu moja kati ya zile ambazo zimekwisha kujadiliwa ni uhamishaji wa mazungumzo ya matini chasili. Katika mbinu hii, mazungumzo yaliyotumika katika hadithi fupi yalidondolewa moja kwa moja ili kubuni similisho lake. Baadhi ya masimilisho yalikuwa matokeo ya sehemu hizo peke yake. Mbinu hii ilifanywa sambamba na udondoshaji, kwani sehemu ambazo hazikusimuliwa wala kuchukuliwa kama mazungumzo zilidondoshwa. Tofauti iliyobainika katika mazungumzo hayo ni namna yalivyopangwa upya. Zingatia mfano ufuatao kutoka similisho la *Nairobi Theatre Group*:

(Nyumbani kwa msimulizi. Msimulizi anachana nywele. Aziza anamtazama kwa unyarafu.)

MUME: Nini wewe, Aziza? Mara nyingi nakuona unanichuja namna hiyo. Nini hasa?

AZIZA: *(Kwa utaratibu)* Sikuchuji, lakini nakusikitikia mwenzangu. Mimi nilikuwa nikitazamia nitaolewa na nani katika dunia hii? Mungu hakukasiri kakuleta wewe kuja kunioa, nifanyeje? Sina hila. Kaa ukijua, mimi huniwafiki wewe hata vibaya vibaya. Basi kule kukutazama ninakokutazama, huwa najisikitikia nafsi yangu ...

MUME: *(Akimrudishia maneno hayo)* Basi mimi hunioni kuwa mume, gumegume tu ... na unajisikitia nafsi yako?

AZIZA: Najisikitia, au najililia hasa – niche!

(Similisho la hadithi fupi ya Mke Wangu, diwani ya Damu Nyeusi na hadithi Nyingine)

Kifungu hiki cha mazungumzo kilidondolewa kutoka matini chasili na kikapangwa upya katika muundo wa mazungumzo. Kama ilivyobainika, baadhi ya hadithi fupi zilibuniwa kwa mazungumzo ya matini chasili pekee. Hali hiyo ilionekana kudhoofisha usimilisho wake.

Mbinu nyingine iliyokuwa imejadiliwa ya ubunaji wa mazungumzo, ni ubunaji unaotokana na usimulizi wa hadithi. Kwa kuongozwa na maudhui yaliyomo, wasimilishaji walifanikiwa kubuni mazungumzo yaliyowasilisha maudhui hayo kupitia wahusika waliokuwemo. Zingatia usimilisho ufuatao wa hadithi fupi, *Uteuzi wa Moyoni*:

A: Kifungu asilia,

Siku iliyofuatia (Zena) aliitisha mkutano huko katika uwanja wa Bajuri.

Uwanja huo ulijaa tele na kufurika. Siku ile Zena alikuwa amevalia kama kawaida yake, kanzu na buibui lake ...

Kwa utaratibu na kwa nadhari alianza kueleza yale mambo ambayo aliyaona muhimu. Hakuahidi mifereji wala barabara za lami wala kupatia watu makazi.

La! Muhimu kwake lilikuwa ni elimu na kumaliza umasikini. Alitambua angewapa elimu mengine yote yangekuja. Hasa zaidi alisisitiza elimu ya wanawake, wote wadogo na watu wazima.

(Kutoka hadithi fupi, *Uteuzi wa Moyoni*, katika *Mayai*

Waziri wa Maradhi na Nyingine, uk.17)

B: Kifungu cha mazungumzo ya similisho,

(*Katika kiwanja cha mkutano watu tayari wamefika uwanjani. Zena ananyanyuka kuwahutubia*)

ZENA: Wazee wangu, ndugu zangu, dada zangu hamjambo?

UMATI: Hatujambo.

ZENA: Mimi Zena wa Saidi ni mtoto wenu hapa katika eneo hili la Mtondo Kaskazini. Ni mzaliwa wa hapa na kama mjuavyo fimbo ya mbali haiuwi nyoka.

Na mimi sitaenda kutafuta kura pahali pengine mbali na papa hapa. Zena hoyee.

UMATI: Hoyee.

ZENA: Mimi sitawahidieni mambo ya maji au mifereji, sitawahidi

barabara za lami wala kuwapatia kazi. La! Kitu muhimu ni
 elimu kwa wote. Wasichana na waume, wadogo kwa wakubwa.
 Na ni hiyo tu ndiyo sera nitafuatilia kikamilifu.
 Kwa hivyo, nawaomba nyote mnipigie kura.
 Zena hoyee.

UMATI: Hoyee...

ZENA: Asanteni sana ...

(Kutoka similisho la *Jicho Four*, hadithi fupi, *Uteuzi wa Moyoni*,
 diwani ya *Mayai na Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine*)

Kama inavyobainika, msimilishaji wa kikundi hicho alikuwa ameisoma hadithi fupi hiyo kwa makini na akang'amua maudhui yaliyokuwemo pamoja na mtazamo wa mwandishi kuyahusu. Katika mazungumzo hayo, maneno fulani yalitokana na usimulizi wa mwandishi na mengine yakabuniwa na msimilishaji.

Ubunaji wa mazungumzo ya namna hiyo ulipunguza matumizi ya usimulizi katika masimilisho ya hadithi fupi. Kwa sababu ya ufupi, masimulizi ya hadithi fupi yalikuwa mafupi na pale yalipogeuzwa mazungumzo hamkuwa na mengi yaliyohitaji kusimuliwa. Hii ni kinyume na hali ilivyokuwa katika usimilisho wa riwaya ambapo mbinu za usimulizi na mazungumzo hazikuonekana kuathiriana kinafasi.

Mtindo wa tatu wa kuyabuni mazungumzo ulidhihirishwa na usimilisho wa hadithi fupi na haukujitokeza katika usimilisho wa riwaya. Huu ni mtindo wa ubunaji wa mazungumzo huru. Mazungumzo huru ni yale ambayo hayakutokana na mazungumzo wala usimulizi wa mwandishi wa hadithi fupi. Haya ni mazungumzo yaliyobuniwa na msimilishaji kwa dhamira ya kuendeleza maudhui fulani na hulka za wahusika katika hadithi fupi. Zingatia mfano huu wa mazungumzo huru kutoka similisho la hadithi fupi, *Msamaria Mwema*:

(Barabarani mchana. Waumini wanatembea kando ya barabara.

Likono ni mmoja wao.)

MTU I: *(Kwa Likono akiwa upande mwingine)*

Hujambo Bw. Likono?

LIKONO: Sijambo! Wewe leo ulisusia kuja kanisani.

MTU I: Shughuli mwenzangu, shida za dunia tena haziishi.

LIKONO: Hata mimi ninazo chungu mzima, lakini kwangu
Mungu kwanza.

MTU I: Na mbona unatembea kando namna hivyo ni kana
kwamba barabara itakuambukiza maradhi?

LIKONO: Barabara za jiji bwana, zina wenyewe.

MTU I: Inshallah mwenzangu.

LIKONO: Kila la heri *(Likono anapita na kupotea kidogo,
punde inasikika honi ya gari. Likono anagongwa na gari
na kurushwa jukwaani tena) ...*

*(Similisho la Fanaka, Msamaria Mwema, diwani ya Mayai Waziri wa
Maradhi na Hadithi Nyingine.)*

Msimilishaji wa mazungumzo haya aliyabuni kwa jinsi huru, lakini akizingatia dhamira ya mwandishi wa hadithi fupi. Maneno yaliyopewa wahusika katika mazungumzo yamebuniwa kwa ustadi na msimilishaji. Msimilishaji katika kuyabuni mazungumzo hayo, alibuni pia mhusika aliyeshiriki mazungumzo na Likono. Utafiti ulibaini kwamba hadithi fupi kwa sababu ya ufupi wake ilihusisha wahusika wachache katika matukio yake. Hii ndiyo maana msimilishaji alilazimika kuwabuni wahusika wapya ili watumike katika mazungumzo yakubuniwa.

Kama ilivyobainika, ubunaji wa mazungumzo kutokana na usimulizi na utendaji, ulifanyika katika hadithi fupi chache, na aghalabu, haukuyafuata maneno ya

hadithi fupi moja kwa moja. Mtindo huu wa kuyabuni mazungumzo ulibainika kwa wingi katika usimilisho wa riwaya. Hali ya kuyageuza mawazo ya wahusika kuwa mazungumzo yao haikudhihirishwa na usimilisho wa hadithi fupi. Mitindo hiyo ya kuyabuni mazungumzo ilibainika kutegemea mtindo uliotumika kuibuni kazi ya kinathari. Mtindo wa usimulizi, utendaji, na udhihirishaji wa mawazo ya wahusika, ulidhihirika kwa uchache sana miongoni mwa hadithi fupi, ikilinganishwa na hali ilivyokuwa katika riwaya. Hali ya kuyabuni mazungumzo huru ilikuwa na upekee wake katika usimilisho wa hadithi fupi. Ubanifu wa kimtindo katika usanifu wa hadithi fupi uliathiri moja kwa moja jinsi tungo hizo zilivyosimilishwa.

Kwa mujibu wa Packard (1997), mazungumzo ni mabadilishano ya kasi (ya kauli) yanayotokea baina ya wahusika jukwaani, na mazungumzo bora ya kidrama huwa yanaendeleza matendo makuu ya tamthilia. Packard anaongeza kwamba, mazungumzo hayalengi tu kupitisha ujumbe lakini hulenga kuonyesha matendo makuu yaliyofichama katika lugha. Katika usimilisho wa hadithi fupi, usimilisho wa mazungumzo ulionekana kuhusisha kwa wingi ubunifu wa mtunzi. Maneno yaliyopewa wahusika fulani hayakutumika katika matini chasili. Aidha, wahusika fulani walibuniwa na kupewa maneno katika mazungumzo. Ubunaji wa mazungumzo jinsi hii unaonekana kufanywa kwa dhamira ya kuibua matendo makuu ya hadithi fupi ili yadhihirishwe jukwaani.

Kulingana na Wamitila (2008), mazungumzo ya wahusika ni njia moja ya kuiendeleza hadithi katika drama. Mazungumzo hutumika kuwasilisha maudhui na dhamira ya kazi ya fasihi. Katika muktadha huu, mazungumzo yaliyobuniwa katika masimilisho yalionekana kutekeleza wajibu wake wa kuisimulia hadithi. Hali ya kuyabuni mazungumzo huru ilionekana kukinzana na nadharia ya

usimilisho ambayo huhimiza vipengele vya maana viwasilishwe kwa usahihi iwezekanavyo (Lhermitte, 2005). Kuyabuni mazungumzo tofauti na yale yaliyotumika katika hadithi fupi kuliongezea kimatini ziada ambacho hakikudhamiriwa na mwandishi wa kazi hiyo. Utahini wa fasihi hulenga matini ya mwandishi wala siyo maneno ya wasimilishaji. Kwa hivyo, misingi ya nadharia ya uigizaji inayoelekeza kuhusu ubunaji wa mazungumzo ya kidrama ni muhimu ihulutishwe na ile ya nadharia ya usimilisho, pamoja na malengo ya kusimilisha.

6.1.2 Usimulizi

Usimulizi ni mbinu ya kuiwasilisha hadithi kwa matumizi ya mhusika mtambaji katika matini ya similisho. Wahakiki wa fasihi huifafanua hadithi fupi kama utungo wa kimasimulizi. Hili hutokana na muundo wake unaotawaliwa na masimulizi katika uwasilishaji wa hadithi. Sehemu kubwa ya hadithi fupi huwa ni masimulizi.

Uhakiki wa masimilisho ulibaini kiwango kikubwa cha matumizi ya usimulizi. Kinyume na ilivyodhihirika katika usimilisho wa riwaya, mbinu ya usimulizi ilitumika katika takriban masimilisho yote ya hadithi fupi. Hali hiyo, labda, ilitokana na mtindo wa kiutambaji uliokuwa umetumika katika hadithi fupi nyingi. Mtindo huo wa kiutambaji ulifanana na ule unaotumika katika usimuliaji wa ngano za fasihi simulizi. Utafiti haukubaini usimulizi unaopitishwa na mhusika katika mazungumzo kama ilivyogunduliwa katika riwaya ya *Siku Njema*.

Usimulizi katika hadithi fupi ulibuniwa ili kutekeleza madhumuni mahsusi ya usanifu wa similisho. Kwanza, usimulizi ulikuwa na dhima ya kuitanguliza na

kuihitimisha matini ya kidrama ya hadithi fupi. Kwa vile usimilisho ulikuwa umeibuni upya hadithi fupi na kudondosha sehemu muhimu za utangulizi wake, usimulizi ulionekana muhimu katika kuitanguliza hadithi. Usimulizi ulioitanguliza hadithi uliarifu kuhusu mtunzi wa hadithi fupi hiyo na maudhui muhimu yaliyomo. Zingatia mfano ufuatao kutoka similisho la hadithi fupi, *Uteuzi wa Moyoni*:

MTAMBAJI: *Uteuzi wa moyoni* ni hadithi yake Rayya Timammy na inahusu binti ya mzee Saidi aliyejulikana kama Zena. Zena alitoka wilaya ya Mtondo Kaskazini. Mbali na Zena, Saidi alikuwa na watoto wengine pia. Watoto wa mzee Saidi waliona milango ya shule ijapokuwa kwa taabu mno. Ilikuwa ni aibu kwa msichana kuonekana barabarani akienda au kutoka shuleni. Hata hivyo, Zena alijikakamua na kufika darasa la saba. Hakupita vizuri, na hivyo baada ya hapo ilibidi aozwe. Baada ya harusi yake na Ali, walianza maisha yao ya bwana na bibi.

(Similisho la *Uteuzi wa Moyoni* kutoka *Jicho Four*)

Hadithi fupi ya *Uteuzi wa Moyoni*, inahusu changamoto zinazomkabili mwanamke katika jamii inayojengeka katika mfumo wa kuumeni. Kwa hivyo, utangulizi wa matini ya similisho ulifanikisha uwasilishaji wa mambo muhimu yaliyopaswa kufahamika kabla ya hadithi yenyewe kuigizwa. Ikumbukwe kwamba, maandalizi ya masimilisho hayo yalinuiwa kuigizwa jukwaani.

Hitimisho la similisho lilisimuliwa kwa kusudi la kuonyesha mwisho wa igizo na vilevile kuashiria mwanzo wa hadithi nyingine. Mathalan, simulio la kuhitimisha katika similisho la hadithi fupi, *Msamaria Mwema*, liliandaliwa namna ifuatayo na kikundi cha *Fanaka*:

MTAMBAJI: ... Baada ya miezi mitatu Likono aliweza kutembea tena lakini

mshahara wake ulikwisha simamishwa na wanawe waliokuwa shule walikwisha fukuzwa... Basi tumuache Likono aendelee na msako nasi tuchukue hatua nyingine, tuone mwandishi Sinjiri Mukuba ametuandalia nini katika hadithi yake, *Fumbo la Mwana*.

Simulio hili limehitimisha hadithi kwa kuonyesha mwisho wake. Na kwa vile hayo yaliandaliwa kwa minajili ya kuigizwa jukwaani, msimulizi alikuwa na wajibu wa kuifahamisha hadhira hadithi iliyokuwa ikitarajiwa kufuata jukwaani. Usimulizi wenye dhima hii katika riwaya ulikosa, kwani hakukuwa na riwaya nyingine iliyohitajika kutangulizwa jukwaani.

Pili, usimulizi ulinuiwa kutoa muhtasari wa hadithi baada ya matukio fulani kuigizwa jukwaani. Kama ilivyotajwa mwanzoni mwa sura hii, maigizo ya hadithi fupi yalidhamiriwa kuwa mafupi kama utanzu wenyewe unavyoashiria. Kwa hivyo, mbinu ya kusimulia ilitumika ili kufupisha uigizaji wa matukio jukwaani. Zingatia mfano ufuatao:

MTAMBAJI : Kwa hakika ugonjwa huo ulikuwa mmoja wa ajabu ambao Mwaibale alikuwa hajaushuhudia kabla. Mteja wake alikuwa amekonda kama sindano na kubaki mifupa mitupu huku akiwa amenyonyoka nywele karibu zote. Hata hivyo, Mwaibale hakuthubutu kumweleza mteja wake chochote. Aliamua kuonyesha ubingwa wake katika uganga. Miezi mitatu baadaye mke wa mteja alifariki na baada ya miaka miwili mteja naye aliletwa akiwa na ugonjwa kama ule ule wa marehemu mkewe.

(Similisho la *Siku ya Mganga* kutoka *Jicho Four*)

Simulio hili ni muhtasari wa matukio kadha katika hadithi fupi ya *Siku ya Mganga*. Msimilishaji aliamua kusimulia yaliyofuata baada ya mteja wa kwanza wa mganga Mwaibale kuondoka. Ingechukua muda mrefu kuweka jukwaani

matukio hayo, hata kuonyesha kifo cha mteja yule na mahangaiko yaliyomfika mganga akijaribu kubaini chanzo na tiba ya ugonjwa huo. Hali hiyo ya kuyasimulia matukio ya hadithi fupi, ili kupunguza uigizaji wake, ilitumiwa katika hadithi fupi nyingi, na haikubainika katika usimilisho wa riwaya.

Tatu, usimulizi ulifanywa kwa dhamira ya kuyawasilisha matukio tata na changamano katika hadithi fupi. Hadithi fupi kwa kawaida huwasilishwa kwa mitindo sahili. Hata hivyo, baadhi ya hadithi fupi teule zilikuwa zimetumia mitindo migumu kusawiri matukio yake. Matukio yaliyotoa changamoto ya kufasiri namna yangewekwa jukwaani yaliwasilishwa kwa mbinu ya usimulizi. Sehemu kubwa ya similisho la hadithi fupi ya *Kikaza* ilitawaliwa na masimulio ya watambaji. Hii ni kwa sababu hadithi fupi hiyo ilikuwa imesukwa kwa lugha ya kimafumbo na mambo fulani yaliyorejelewa yalionekana magumu kuwekwa jukwaani.

Usimulizi ulitokea kuwa moja kati ya mbinu kuu za kuisimilisha hadithi fupi kuwa matini ya drama. Kinyume na riwaya iliyoonyesha sehemu nyingi za kuigizwa, hadithi fupi ilikuwa na sehemu chache za kuigizwa kutokana na ubanifu wa utanzu wenyewe. Ili kuiwasilisha hadithi iliyomo kisawasawa, ilibidi usimulizi ufanywe kwa upana.

Hutcheon (2013) anaeleza hadithi kuwa kiungo muhimu katika usimilisho. Aghalabu, usimulizi huiwasilisha hadithi kama ilivyowasilishwa na mwandishi wa matini chasili. Hata hivyo, matumizi mapana ya mbinu hii yalionekana kudhoofisha utendaji wa hadithi fupi. Kwa vile wahusika wa tamthilia huendelezwa kupitia utendaji na mazungumzo, usimilisho wa namna hiyo ulionekana kupungukiwa katika ubainishaji wa wahusika wa hadithi fupi.

6.1.3 Matumizi ya Muundo wa Kitamthilia

Muundo hurejelea jinsi matukio ya kidrama yalivyofumwa pamoja. Katika kushughulikia muundo, ni vyema kueleza kwamba kuna aina mbili za kimsingi za muundo. Hizi ni muundo wa ndani na muundo wa nje. Muundo wa ndani unarejelea vipengele vya kimuundo vinavyodhihirika pale kazi husika ya kifasihi inaposomwa. Muundo wa namna hii unahusisha vipengele kama vile migogoro, kani kinzani, msuko, na hadithi. Jinsi hii ya muundo imeelezewa katika mbinu ya ufaraguzi wa msuko katika sura hii ya tasnifu. Aidha, matumizi yake hayakubainisha tofauti katika usimilisho wa riwaya na hadithi fupi.

Mbinu ya matumizi ya muundo wa kitamthilia inalenga kuelezea muundo wa nje wa tamthilia. Muundo huo unahusu namna tamthilia inavyoonekana machoni mwa msomaji. Haimhitaji mtu kuisoma kazi ya kitamthilia ili aweze kuubaini muundo wa nje wa kazi hiyo. Masimilisho yaliyokuwa yakitafitiwa yalibuniwa kwa muundo wa kitamthilia.

Matumizi ya muundo wa kitamthilia yalibainika katika viwango viwili tofauti:

- a) Muundo wa mazungumzo
- b) Muundo wa sehemu

6.1.3.1 Muundo wa Mazungumzo

Tamthilia huhadithiwa kimazungumzo. Wahusika huonyeshwa wakiambatanishwa na maneno yao na katika hali ya kujibizana na wahusika wengine. Muundo wa mazungumzo huhitaji majina ya wahusika yaandikwe pambizoni upande wa kushoto katika matini, na maneno yao baada ya alama ya kiakifishi ya nukta mbili.

Usimilisho wa hadithi fupi ulizingatia muundo wa mazungumzo ya kitamthilia. Kulingana na hoja ya awali, mazungumzo mengine ya hadithi fupi yalibuniwa kwa namna huru na msimilishaji. Katika mazungumzo ya namna hiyo, msimilishaji alibuni pia, vipengele kama wahusika na maelekezo ya jukwaani ambavyo havikutokana na matini ya hadithi fupi. Ufupi wa hadithi fupi uliifanya kukosa masimulizi mengi ambayo yangerejelewa katika ubunaji wa mazungumzo yake. Mazungumzo ya hadithi fupi yalionekana mafupi mafupi na yenye kauli fupi za wahusika. Zingatia mfano ufuatao kutoka *Jicho Four*:

(Katika afisi. Mwalimu mkuu yuko afisini. Mzee Atanasi anabisha.)

MWALIMU MKUU: Naam karibu ukae mzee.

ATANASI: Mwalimu nimepata wito ...

MWALIMU MKUU: Naam, naam, wewe ndiwe mzee Atanasi Mukosa, babake Nanda?

ATANASI: Ndimi ...

(Similisho la hadithi fupi, Fumbo la Mwana)

Nukuu hili ni kielelezo cha muundo wa mazungumzo ya tamthilia uliotumika katika masimilisho mengi. Muundo wa mazungumzo ya kitamthilia katika usimilisho wa hadithi fupi ulionekana kuathiriwa na sifa za kimuundo za hadithi fupi. Kama ambavyo imedhihirishwa, ufupi wa hadithi fupi uliufanya muundo wa mazungumzo yake kuwa tofauti na wa riwaya. Usimilisho ulionekana kuakisi sifa za utanzu ambazo zilikuwa muhimu katika ufundishaji wa hadithi fupi kwa wanafunzi.

Kuna vipengele vingine ambavyo hushirikishwa katika ufumaji wa muundo wa mazungumzo. Vipengele hivyo ni uzungumzi nafsi, usemajji kando, na usemajji wa mawazo ya mhusika. Tunavirejelea vipengele hivyo kama vya muundo wa

mazungumzo kwa sababu uundaji wake unaibua sifa zaidi zinazoubainisha muundo huo. Hata hivyo, vipengele hivyo havikubainisha tofauti katika usimilisho wa muundo wa mazungumzo ya hadithi fupi na riwaya.

6.1.3.2 Muundo wa Sehemu

Kulingana na Syambo na Mazrui (1992), tamthilia huundwa na sehemu mbili kuu: sehemu (matendo) na maonyesho. Sehemu ndefu katika mgawanyo huo huitwa matendo. Matendo huweza kugawanywa katika sehemu nyingine fupi ambazo huitwa maonyesho. Idadi ya matendo na maonyesho hutegemea aina ya tamthilia na mtunzi anayeitunga.

Istilahi ya onyesho imekuwa ikifasiriwa kwa njia tofauti. Baadhi ya waandishi wameifasiri istilahi hii kwa maana ya sehemu fupi ya tamthilia inayoashiriwa na kuingia na kuondoka kwa waigizaji jukwaani katika kipindi mahsusi cha wakati. Pazia inapofunguliwa huashiria mwanzo wa onyesho fulani, na inapofungwa huwa ni mwisho wa onyesho hilo. Pia, onyesho hufasiriwa kama sehemu ya muundo wa tamthilia inayobainishwa jukwaani na mabadiliko ya mandhari. Mandhari ya tukio yanapobadilika katika igizo fulani jukwaani, huashiria onyesho jingine. Kutokana na fafanuzi hizi, inajitokeza kwamba istilahi ya onyesho haiwezi kufasirika nje ya muktadha wa uigizaji jukwaani. Hii ni kwa sababu dhana yenyewe ina uamilifu katika uigizaji. Onyesho ni sehemu inayojumuisha kitendo kinachoendelezwa na wahusika wa tamthilia katika wakati na mahali mahsusi.

Mgawanyo na idadi ya maonyesho katika masimilisho hayo ilitofautiana hadithi hadi hadithi, na ilitegemea msimilishaji. Tofauti na maonyesho ya riwaya, hadithi fupi ilidhihirisha maonyesho machache. Hadithi fupi nyingine zilisimilishwa kwa

onyesho moja. Hii ni kutokana na ufupi wake. Uhakiki wa masimilisho ya hadithi fupi ulibaini usimilisho ufuatao wa maonyesho katika hadithi fupi zilizotajwa:

JEDWALI 6.1 : IDADI YA MAONYESHO KATIKA HADITHI FUPI TEULE

NA.	HADITHI FUPI	MAONYESHO
1.	<i>UTEUZI WA MOYONI</i>	3 - 6
2.	<i>SIKU YA MGANGA</i>	1 - 3
3.	<i>KACHUKUA HATUA NYINGINE</i>	2 - 3
4.	<i>MKE WANGU</i>	1
5.	<i>SAMAKI WA NCHI ZA JOTO</i>	3 - 6
6.	<i>GILASI YA MWISHO MAKABURINI</i>	3 - 7

Jedwali hili linatoa taswira ya jinsi ubunaji wa maonyesho ulivyotofautiana miongoni mwa wasimilishaji katika usimilisho wa hadithi fupi. Hadithi fupi zilizokuwa na hadithi yenye matukio mengi kama vile *Uteuzi wa Moyoni*, *Samaki wa Nchi za Joto*, na *Gilasi ya Mwisho Makaburini* zilisimilishwa zikiwa na maonyesho mengi. Baadhi ya hadithi fupi kama vile *Mke Wangu* zilisimilishwa kwa onyesho moja kwa sababu zilijikita katika tukio moja kuu katika mandhari sawa.

Kama ilivyobainika, usukaji wa muundo wa similisho la hadithi fupi ulitegemea mtindo wa msimilishaji, sawa na ilivyokuwa katika usimilisho wa riwaya. Muundo wa hadithi fupi ulipelekea kuwepo na maonyesho machache na mafupi katika masimilisho yake.

Tendo ni sehemu ya tamthilia inayobainishwa na ukuzaji wa tendo la kidrama, upeo na suluhisho. Tamthilia huweza kugawika katika matendo mbalimbali ili kudhihirisha namna tendo linavyochipuka na kuendelezwa hadi upeoni pamoja na

suluhisho linalotolewa na mtunzi. Inatarajiwa kwamba drama inapoanza mwandishi atatanguliza kiini cha tendo, mhusika nguli na migogoro. Hili linaweza kujumuisha tendo moja. Namna migogoro inapopevuka na kutiwa makali linaweza kuwa tendo jingine. Tendo la mwisho linaweza kuonyesha namna migogoro hiyo inavyosuluhishwa. Kila tendo hujumuisha maonyesho kadha.

Uhakiki wa masimilisho ya hadithi fupi ulibaini kwamba muundo wa sehemu za tamthilia ulikuwa umetumika katika mchakato wa usimilisho wake. Hata hivyo, kinyume na ilivyobainika katika riwaya, masimilisho ya hadithi fupi yalikosa sehemu ya matendo. Muundo wa riwaya uliruhusu kuwa na hadithi ndefu yenye matukio mengi, na hivyo ilibainika kuruhusu migawanyo ya sehemu na maonyesho katika usimilisho wake. Sifa ya kuwepo na sura mbalimbali ilionyesha uwezo wa riwaya kugawika katika maonyesho na sehemu kutegemea urefu na uchangamano wa sura hizo.

Kama ilivyobainika, usukaji wa muundo wa kitamthilia ulifanywa kwa misingi ya nadharia ya uigizaji. Nadharia hiyo huonyesha kuwa muundo wa kitamthilia una sehemu mbili muhimu zinazokamilisha: matendo na maonyesho. Iliyodhihirika ni kuwa, sio lazima sehemu ya matendo ikawepo katika muundo wa kitamthilia, ingawa huwa na uamilifu wake. Riwaya ilibainika kusheheni sifa za muundo wa kitamthilia kupitia mgawanyo wake wa sura. Hali hii iliwezesha masimilisho yake kudhihirisha mgawo wa matendo na maonyesho. Usimilisho wa hadithi fupi ulizingatia muundo wa maonyesho kama ilivyo kwa baadhi ya tamthilia.

6.2 Mbinu za Usimilisho wa Hadithi Fupi Jukwaani

Sehemu iliyotangulia imezjadili mbinu zilizotumika kuigeuza hadithi fupi kuwa matini ya kuigizwa. Katika sehemu hii, utafiti umezibainisha na kuzieleza mbinu zilizotumika kuigiza matini ya similisho iliyoandaliwa katika sehemu iliyopita. Uchunguzi wa maigizo ya hadithi fupi jukwaani ulibaini matumizi ya mbinu mbalimbali za usimilisho huo. Mbinu hizo ni kama vile uteuzi wa wahusika, mazungumzo, matumizi ya mtambaji, uigizaji wa mbinu, utendaji, uzungumzaji nafsi, matumizi ya mbinu kama vile pazia, muziki, mandhari, na uangazaji. Ingawa masimilisho ya hadithi fupi na riwaya yalionekana kutumia mbinu zilizofanana, maigizo ya hadithi fupi yalidhihirisha tofauti za ndani katika jinsi mbinu hizo zilivyotumika. Sehemu hii imeangazia kwa undani tofauti hizo katika mbinu hizi.

6.2.1 Matumizi ya Mtambaji

Nafasi ya mtambaji katika masimilisho ilichukuliwa na mwigizaji mtambaji katika uigizaji wa masimilisho hayo. Mbinu ya kumtumia mtambaji ilidhihirika karibu katika hadithi fupi zote zilizoigizwa jukwaani. Katika baadhi ya hadithi fupi mtambaji alikuwa mhusika mojawapo. Mathalan, hadithi fupi *Mke Wangu*, *Samaki wa Nchi za Joto*, *Tuzo*, *Kikaza*, na *Maskini, Babu yangu!* Aghalabu, mhusika mtambaji alikuwa mhusika mkuu katika hadithi hizo na usimulizi wake ulimlenga moja kwa moja kama ilivyoendelezwa na matini ya hadithi fupi. Kinyume na katika uigizaji wa riwaya ambapo mhusika mtambaji alionekana kulazimishiwa uhusika katika matini chasili, mtambaji huyo alikuwa mhusika halisi katika matini ya hadithi fupi.

Sehemu iliyotangulia iliyafafanua majukumu yaliyotekelezwa na mbinu ya kumtumia mtambaji katika usimilisho wa hadithi fupi. Majukumu hayo ni kama vile kuwa dira katika msuko wa hadithi, kufupisha matukio, kutanguliza na kuhitimisha uigizaji. Uigizaji wa hadithi fupi ulibaini kuwa, jukumu la kuifupisha hadithi lilikuwa muhimu. Dhima hii iliwezesha hadithi fupi kuchukua muundo wake wenye sifa ya ufupi jukwaani. Zingatia mfano ufuatao:

MTAMBAJI : Kama mlivyoona, Waziri alivaa vazi lake la kitaifa wakaondoka. Msafara wa rais ulichelewa kidogo kwanza. Ulianza saa tatu. Mawaziri, wazee wa ukoloni mkongwe, ma PC na ma DC wote walikuwepo kushuhudia maendeleo ya miaka kumi. Mambo yalianza. Ngonjera zilichezwa, mashairi yaliimbwa, mzee Moris alicheza ngoma zake kumi na baadaye watoto kumi waliozaliwa siku ya uhuru walionyeshwa. Watu wakashangilia. Rais alitoa hotuba na akapiga ngoma kubwa kufungua sherehe. Mayai Waziri wa Maradhi akili yake ikiwa imekwamilia kwa wale watoto. Akashangazwa na Mzee Moris kupiga ngoma kumi na tena akiwa kipofu. Sherehe ikakwisha saa nane. Waziri Mayai alikwenda moja kwa moja kwa daktari Pondamali.

(Kutoka similisho la hadithi fupi, *Mayai Waziri wa Maradhi*, kikundi cha *Jicho Four*)

Kifungu hiki cha similisho kilisimuliwa na mwigizaji mtambaji wa *Jicho Four* na kujitokeza kama muhtasari wa matukio ya sherehe ya kuadhimisha miaka kumi ya uhuru wa nchi hiyo. Matukio ya sherehe hiyo hayakuigizwa jukwaani. Mbali na kuzingatia sifa ya ufupi wa utanzu, mbinu hiyo hali kadhalika, ilihifadhi muundo wa tamthilia. Packard (1997) anasema kwamba tamthilia huwa fupi na ya kuona. Tamthilia hutokea kama matokeo ya uteuzi kuhusu matukio yanayoigizwa. Sifa ya ufupi ni mojawapo ya sifa za kitamthilia zilizoivezesha hadithi fupi kuigizika.

Jukumu jingine lililojitokeza kuwa muhimu katika uigizaji ni lile la kumtumia mtambaji kuitanguliza na kuihitimisha hadithi. Ingawa si hadithi zote zilizotangulizwa na kuhitimishwa na mtambaji, wajibu huo ulidhihirika kuwa muhimu katika maigizo ya hadithi fupi. Hii ni kwa sababu hadithi fupi nyingi zilikuwa zikiigizwa kwa mkupuo mmoja na kwa kufuatana. Kwa hivyo, dhima ya mtambaji ilikuwa kuifahamisha hadhira kwamba hadithi fupi fulani inaanza ama imekwisha. Mtambaji wa hadithi fupi, *Uteuzi wa Moyoni*, aliyahitimisha maigizo ya hadithi fupi hiyo namna hii:

MTAMBAJI : Kwa hayo mambo yaliendelea na Zena hakubadilisha msimamo wake. Siku ya kura ilipofika watu walijitokeza na wakapiga kura. Kura zilipohesabiwa, mpinzani wa Zena alitangazwa mshindi. Baada ya miezi mitatu mbunge alihamia Nairobi akawacha wananchi na majuto. Haya basi tuyaache hayo ya Zena na wenzake na tuelekee kwa mwandishi Chesi Mpilipili na hadithi yake fupi ‘Siku ya nani?’ – Mganga.

(Similisho la *Fanaka*, *Uteuzi wa Moyoni*)

Mtambaji alilisimulia nukuu hili kama hitimisho la maigizo ya hadithi fupi ya *Uteuzi wa Moyoni*. Mfano wa utambaji wa kitangulizi ulitumika katika hadithi fupi ya *Kachukua Hatua Nyingine*:

Haya basi tuyaache hayo ya Mwaibale na tuelekee kwa shemeji au bwanake Mavitu au mkipenda ‘*Kachukua Hatua Nyingine*’. Mavitu alikutana na Sakina miaka mingi iliyopita yapata miaka ya 1960 akiwa akifanya kazi katika kampuni ya kuuza cherahani ya Singer jijini Nairobi ...

(Similisho la hadithi fupi, *Kachukua Hatua Nyingine*, Kikundi cha *Jicho Four*)

Uhakiki wa utambaji ulibaini kwamba masimilisho mengi yalibuni utambaji wa kuhitimisha hadithi ukijumuisha pia utangulizi wa hadithi nyingine. Mtindo huo

ulitumika na vikundi vingi vilivyokuwa vikifanyiwa uchunguzi. Utambaji huo ulikuwa na umuhimu kwa wanafunzi kwani uliwabainishia hadithi iliyokuwa ikifuata kuigizwa jukwaani. Kwa mujibu wa hoja ya awali, masimilisho ya hadithi fupi yaliigizwa kwa wakati mmoja na kwa kufuatana. Hii ndiyo iliyokuwa njia ya kipekee ya kuitambulisha hadithi kabla ianze kuigizwa.

Sehemu iliyotangulia ilibainisha umuhimu wa hadithi katika usimilisho na uigizaji. Njia moja ya kuiwasilisha hadithi katika usimilisho na uigizaji ni kwa kutumia mhusika mtambaji. Kwa ambavyo usimilisho na uigizaji hupoteza baadhi ya vipengele fulani vya matini ya fasihi, inakuwa muhimu mtambaji akiwemo ili kuziba mapengo katika hadithi. Nadharia ya uigizaji hutambua jinsi tatu za kuiwasilisha hadithi katika uigizaji: kupitia mazungumzo, maelezo ya jukwaani na matumizi ya mtambaji (Wamitila, 2008). Hata hivyo, matumizi ya mtambaji yalichukua nafasi kubwa ya kuisimulia hadithi katika usimilisho wa hadithi fupi kuliko njia hizo nyingine. Aidha, utafiti uliweza kubaini kwamba, usimulizi ni sifa ya kiutanzu inayodhihirika katika tungo za kinathari na kidrama, ingawa kwa miundo tofauti. Hii ni sifa moja iliyotegemewa katika usimilisho wa hadithi fupi.

6.2.2 Mazungumzo

Mazungumzo yaliyoandaliwa katika matini ya similisho yalikaliririwa na waigizaji jukwaani. Kulikuweco na mabadiliko machache katika matumizi ya mazungumzo hayo. Mbinu ya mazungumzo ilitumika na vikundi vyote vilivyokuwa vikitafitiwa. Mazungumzo ya jukwaani yalidhihirisha sifa mbili kuu.

Katika uwasilishaji wa mazungumzo jukwaani, waigizaji walitumia lafudhi kudhihirisha asili ya wahusika wa hadithi fupi. Kinyume na matumizi ya lafudhi

katika usimilisho wa riwaya, ambayo yalijikita zaidi katika lahaja za Kiswahili, lafudhi katika usimilisho wa hadithi fupi zilitoka lugha mbalimbali. Hadithi fupi zilizosimilishwa zilikuwa zimewasawiri wahusika wenye asili tofauti. Lafudhi za lugha zifuatazo zilitumika katika hadithi fupi zilizoonyeshwa:

JEDWALI 6.2: LAFUDHI ZILIZOTUMIKA KATIKA MAIGIZO YA HADITHI FUPI

NA.	LAFUDHI	HADITHI FUPI
1	KIINGEREZA	<i>DAMU NYEUSI, SAMAKI WA NCHI ZA JOTO, NA TAZAMANA NA MAUTI</i>
2	LAHAJA YA KIMVITA	<i>UTEUZI WA MOYONI, NDOA YA SAMANI, MKE WANGU, MAEKO, NA PWAGUZI</i>
3	KILUHYA	<i>KIKAZA NA FUMBO LA MWANA</i>
4	KIKAMBA	<i>MWANA WA DARUBINI NA NDIMI ZA MAUTI</i>

Kama ilivyobainika, lafudhi iliyochaguliwa ilitegemea asili ya wahusika walioigizwa. Lafudhi ya Kiingereza ilitumika na wazungu waliokuwa wakisoma pamoja na Fikirini, katika hadithi fupi ya *Damu Nyeusi*. Kiingereza kilitumika kuwatambulisha waigizaji katika nafasi za Wazungu na Wamarekani weusi. Katika kuigiza wahusika wenye asili ya lugha za Kikamba na Kiluhya, baadhi ya fonimu za Kiswahili zilibadilishana nafasi katika maneno na fonimu za Kiluhya ama Kikamba. Zingatia mifano miwili ifuatayo:

Mfano 1: Lafudhi ya Kiluhya

JEDWALI 6.3: LAFUDHI YA KILUHYA

NA.	LAFUDHI YA KILUHYA	KISWAHILI SANIFU
1.	Bwana	Pwana
2.	Nauliseko hifi	Nauliza hivi
3.	Tulifanyieko Mungu nini?	Tulifanyia Mungu nini?
4.	Kitoko	Kidogo
5.	Pawa	Mbawa

Mfano 2: Lafudhi ya Kikamba

JEDWALI 6.4: LAFUDHI YA KIKAMBA

NA.	LAFUDHI YA KIKAMBA	KISWAHILI SANIFU
1.	Kumbambaika	Kubabaika
2.	Sili	Siri
3.	Niyuafyo	Nijuavyo
4.	Ndalumbini	Darubini
5.	Kanzi ngani	Kazi gani

Kulingana na Pfiester (1991), mazungumzo ndiyo mbinu ya kimsingi katika uwasilishaji wa drama. Mazungumzo ndiyo kiini cha hadithi katika uigizaji. Mbali na kuiwasilisha hadithi mazungumzo hutakiwa kuwabainisha wahusika wa tamthilia. Diyanni (2004) anasema kwamba mazungumzo ya kidrama kimsingi hutekeleza dhima tatu kuu: kuendeleza ploti, kuthibitisha mandhari, na kuwabainisha wahusika. Hata hivyo, Diyanni anadai kwamba dhima muhimu zaidi ya mazungumzo ni ubainishaji wa wahusika. Matumizi ya lafudhi ni namna moja inayotumika kuwakuza na kuwabainisha wahusika wa tamthilia. Kupitia matumizi ya lafudhi wahusika wenye asili mbalimbali hutambulishwa kwa hadhira jukwaani. Hata hivyo, matumizi ya lafudhi yalifanywa kwa makosa mengi katika uigizaji wa hadithi fupi. Kwanza, lafudhi nyingine zilizoteuliwa kutumika hazikuafiki wahusika waliodhamiriwa katika hadithi fupi husika. Kwa mfano, lafudhi ya Kimvita haikustabili kutumika katika hadithi fupi ya *Mke Wangu*, kazi iliyosawiri wahusika wake katika mazingira ya kisiwa cha Unguja.

Pili, matumizi ya lafudhi yalifanywa kwa makisio kwamba wahusika waliosawiriwa na mwandishi walikuwa na athari hizo katika mazungumzo yao.

Utafiti ulibaini kwamba matumizi ya lafudhi hayakuafiki katika usimilisho wa hadithi fupi zilizodhamiriwa kuigizwa shuleni. Usimilisho wa aina hiyo ulipungukiwa katika kiwango cha uaminifu kwa matini chasili. Kama ilivyotajwa na hoja ya awali, wanafunzi hufundishwa na kutahiniwa katika Kiswahili sanifu. Kwa hivyo, matumizi hayo yalipotosha malengo ya ufundishaji wa Kiswahili katika shule za upili.

Mazungumzo ya jukwaani yalidhihirisha matumizi ya uzungumzi nafsi. Mafungu ya mazungumzo yaliyolenga uzungumzi nafsi yalikuwa yameandaliwa katika masimilisho. Waigizaji waliyasema maneno hayo kwa namna iliyoonyesha kwamba walikuwa wakijisemea wao wenyewe. Katika similisho la *Mayai Waziri wa Maradhi*, mwigizaji Mayai alijisemea maneno jukwaani aliporejea nyumbani mwake kulala na kuhisi hofu ya kutembelewa tena na mizuka. Mayai alinakiliwa katika igizo la *Planets* akisema:

MAYAI: (*Akijisemea*) Hivi naogopa nini, naogopa Ukombozi?

Hapana Ukombozi ni mtoto wangu, ninamhitaji... Nafikiri nimefanya vibaya kuja kulala katika nyumba hii usiku wa leo.

(Nukuu kutoka maigizo ya *Mayai Waziri wa Maradhi*, kikundi cha *Planets*)

Uzungumzi nafsi ulibainika tena katika maigizo ya hadithi fupi, *Samaki wa Nchi za Joto*, kupitia mwigizaji Christine. Kifungu kifuatacho kilinakiliwa kutoka kikundi cha *Nairobi Theatre Group* kikilenga maneno ya Christine.

CHRISTINE: (*Akijisemea*) Haya ndiyo matokeo ya uovu na utundu wangu. Nifanyaje sasa. Niavye mimba? Nikiwa tasa ama niitwe muuaji?

Mungu wangu we! ...

(Similisho la *Samaki wa Nchi za Joto, Nairobi Theatre Group*)

Kulingana na hoja ya awali, uzungumzi nafsi ni mbinu ya kimazungumzo inayotumika kubainisha mawazo, mitazamo na hisia za wahusika. Hii ni mbinu inayodhihirika katika tungo za kinathari na kidrama. Katika usimilisho wa hadithi fupi, matumizi ya uzungumzi nafsi yalikuwa machache, kinyume na ilivyodhihirika katika usimilisho wa riwaya. Ubanifu wa utungo wa hadithi fupi ulipunguza miktadha ya matumizi ya mbinu hii katika utanzu huo.

6.2.3 Uteuzi wa Waigizaji

Uteuzi wa waigizaji ulifanywa kwa misingi mitatu iliyobainika katika uchunguzi huu: mavazi, umbo, na lugha. Utafiti huu umejadili misingi hiyo kama ilivyobainika katika maigizo ya vikundi teule.

6.2.3.1 Mavazi

Wasimilishaji waliyateua mavazi ya waigizaji ili yawalande wahusika wa hadithi fupi. Ingawa hadithi nyingi hazikuelekeza mavazi mahsusi ya wahusika wake, wasimilishaji na waelekezi walitumia vidokezo mbalimbali vilivyotajwa na mwandishi ili kufikiria na kuteua mavazi ya waigizaji wa wahusika hao. Baadhi ya vidokezo vilihusu dini, tabaka la kiuchumi, na jamii alikosawiriwa mhusika fulani. Michoro na picha zilizopatikana mwanzoni mwa hadithi zilitumika kutoa fununu kuhusu mavazi ya waigizaji.

Mazrui na Syambo (1992) wanasema kwamba maleba ya waigizaji ni muhimu yakubaliane na mazaji ya mchezo, maumbile ya wahusika, na wakati unaorejelewa na tamthilia. Uchunguzi ulibaini tofauti na mifanano iliyojitokeza miongoni mwa vikundi katika uteuzi wa mavazi ya waigizaji. Mganga Mwaibale

katika similisho la hadithi fupi, *Siku ya Mganga*, aliigizwa kwa namna sawa na vikundi vingi. Mwigizaji huyo alivishwa mavazi makuukuu yaliyochanikachanika na katika baadhi ya vikundi mararururu. Aidha, alionyeshwa akiwa amevalia suruali fupi na viatu aina ya *akala*. Mikononi mganga Mwaibale alivalishwa bangili na mabegani alifungiwa kitambaa kilichokuwa kimefuma pamoja manyoya ya rangi mbalimbali. Kisha kichwani alikuwa amevishwa kofia ya manyoya na uso ukapakwa wanja wa chokaa kuyazingira macho na kipaji chake. Kwa hakika, Mwaibale akiwa jukwaani alishawishi hadhira kwamba alikuwa mganga na hiyo ilikuwa siku yake. Uteuzi wa maleba namna hiyo ulijitokeza kama uigaji wa filamu maarufu zinazosawiri waganga za Kinaijeria na Kitanzania.

Mavazi ya waigizaji yalitumika na waelekezi kuwabainisha wahusika kwa namna mbalimbali. Kwanza, mavazi ya waigizaji yalitambulisha imani zao za dini. Kwa mfano, waigizaji katika hadithi fupi *Pwaguzi* na *Ndoa ya Samani*, wote walisawiriwa kama Waislamu. Waigizaji wa kike walivalishwa buibui na wale wa kiume wakavalishwa kanzu.

Pili, mavazi yalitambulisha tabaka la wahusika. Katika hadithi fupi *Mayai Waziri wa Maradhi*, *Msamaria Mwema*, *Tuzo* na *Fumbo la Mwana*, baadhi ya waigizaji walibainishwa na vikundi vingi kitabaka. Waigizaji katika nafasi za Kizito Kibambo, Mayai, Rais na mawaziri wake, wote walivalishwa mavazi ya kifahari. Hata hivyo, vitoto kumi, Likono, Ananda na Atanasi walivishwa mavazi ya kimasikini. Kwa namna hiyo, maudhui ya utabaka yaliwasilishwa kupitia uteuzi wa mavazi ya waigizaji.

Tatu, mavazi ya waigizaji yaliweza kubainisha utamaduni wao. Mathalan, katika hadithi fupi za *Kikaza* na *Fumbo la Mwana*, dhamira kuu ya baadhi ya waelekezi ilikuwa kuwatambulisha waigizaji katika utamaduni wa jamii za Kiluhya. Hilo ni jambo lililojitokeza katika hadithi fupi ya *Uteuzi wa Moyoni* pale kina mama wengi walionekana kujirushia kanga kichwani na kujifunga lesu kiunoni. Uteuzi huo ulitambulisha utamaduni wa Waswahili.

Uteuzi wa maleba ya waigizaji ulibainika kuwa njia moja ya kuwasaidia wanafunzi kuwaelewa zaidi wahusika wa hadithi fupi. Aghalabu, tamthilia huelekeza jinsi wahusika wake watakavyovalia jukwaani. Maelezo kama hayo yalibainika katika hadithi fupi nyingi zilizokuwa zikihakikiwa. Hadithi fupi hizo ziliambatana na picha ama michoro ya wahusika, huku nyingine zikiwa na usimulizi ulioelekeza namna mhusika fulani alivyokuwa amevalia. Maelezo na picha kuhusu mavazi ya wahusika zilithibitisha kuwepo na sifa za kitamthilia katika hadithi fupi.

6.2.3.2 Umbo

Umbo hurejelea sifa za nje katika maumbile ya mwigizaji. Nadharia ya uigizaji huelekeza uteuzi wa waigizaji uzingatie umbo la wahusika wanaoigwa (Ntarangwi, 2004). Wahusika wanene huwakilishwa jukwaani na waigizaji wanene, na vivyo hivyo wale wadogo huwakilishwa na waigizaji wenye umbo ndogo. Uteuzi wa waigizaji wa masimilisho ya hadithi fupi, kwa kiwango fulani, ulionekana kuzingazitia kigezo cha umbo.

Kigezo cha umbo kiliongoza kuteuliwa kwa waigizaji wanene na wadogo. Katika hadithi fupi ya *Damu Nyeusi*, mwanamke Mmarekani mweusi aliyemsaliti Fikirini anaelezwa na mwandishi hivi:

... Alikuwa pandikizi la jimama limekula likashiba.

(Diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, uk.25)

Waelekezi wa vikundi vingi waliteua waigizaji wa kike wenye tambo kubwa kumwigiza mwanamke huyo. Kwa njia ya ulinganuzi, Fikirini aliigizwa na mwigizaji mwenye mwili mdogo. Syambo na Mazrui (1992) wanahoji kuwa, waigizaji hutofautiana kimaumbile, na maumbile ya mwigizaji huleta athari fulani jukwaani. Tambo la mwanamke Mmarekani liliashiria sifa yake ya unyang'anyi, na umbo ndogo la Fikirini likaashiria sifa ya unyonge ndiposa akawa windo la mwanamke huyo.

Vilevile, kigezo cha umbo kilielekeza kuteuliwa kwa waigizaji ili kuashiria umri wa wahusika. Waigizaji waliteuliwa kuwakilisha watoto, vijana, watu wazima na wazee. Katika masimilisho ya hadithi fupi ya *Ngome ya Nafsi*, wahusika Naseko, Samba na Neema, waliigizwa na waigizaji wenye umbo ndogo kama watoto. Mabarobaro wanne waliomteka nyara Naseko waliigizwa na waigizaji wenye tambo wastani ili kuwakilisha vijana. Nafasi za mzee Sakaja na mzee Mengo ziliigizwa na waigizaji wenye tambo kubwa na ambao walipewa mafunzo ya kuiga wazee. Wanawake na wanaume waliokuwa wamealikwa kumlaki Naseko kwa Mzee Sakaja waliigizwa na waigizaji wenye umbo linaloashiria watu wazima.

Umbo la waigizaji lilihusisha pia rangi ya ngozi na jinsia. Waigizaji wa jinsia ya kike na kiume waliwakilisha jinsia zao katika masimilisho. Hata hivyo, haikuwezekana kuwakilisha wahusika wenye rangi nyeupe ya ngozi katika masimilisho ya hadithi fupi, *Damu Nyeusi na Tazamana na Mauti*. Upungufu wa namna hiyo umejadiliwa katika sehemu inayofuata ya sura hii.

6.2.3.3 Lugha

Nadharia ya uigizaji huelekeza uteuzi wa waigizaji uzingatie uwezo wao wa kuitumia lugha kama inavyotumiwa na wahusika wanaoigwa. Ntarangwi (2004) anasema kwamba ni lazima usawiri wa waigizaji kimaneno, kimatendo, na kiumbo uchukuane na hali halisi wanayowakilisha. Waigizaji wanapaswa kuwasilisha sifa teule za lugha katika maigizo yao jukwaani. Sifa teule za lugha katika uigizaji huhusisha matumizi ya lafudhi, ugugumizi, msimbo, na ulumbi.

Sifa ya lugha iliyoonekana kuzingatiwa sana na vikundi vingi ni matumizi ya lafudhi. Lafudhi ni matumizi ya lugha fulani kwa namna inayotambulisha athari za lugha nyingine kwayo. Athari kuu zinazotambulishwa ni kama vile matamshi, matumizi ya shadda na kwa kiasi fulani muundo wa sarufi. Matumizi ya lafudhi yameshughulikiwa katika mbinu ya mazungumzo na usimilisho wa riwaya.

Nadharia ya uigizaji imeelekeza namna waigizaji wanavyopaswa kuteuliwa katika kazi ya drama. Kwa mujibu wa Ntarangwi (2004), waigizaji ndio uti wa mgongo katika kitendo kizima cha drama kwa vile wao ndio wanaokitoa na kukiwasilisha kwa hadhira. Uteuzi wao kimaneno, kimatendo, na kiumbo, ni muhimu uchukuane na hali halisi wanayowasilisha. Hii ina maana kuwa, waigizaji ni muhimu kuwaiga wahusika wa hadithi fupi kwa ukamilifu wao. Hali ya kuwawakilisha wahusika wa hadithi fupi kwa ukamilifu huo haikuwezekana. Ingawa wahusika wa tamthilia nyingi hudhamiriwa kuigizwa, wahusika wa hadithi fupi hawakudhamiriwa hivyo. Hali ya kuwafanya wafanane na wahusika wa tamthilia katika uigizaji, kwa kiwango fulani ilipotosha dhamira asilia ya mwandishi. Wahusika wa masimilisho yanayolenga usahihi wanapaswa

kuwasilishwa ili wawe na uaminifu kwa wahusika wa matini chasili, lakini siyo kwa misingi ya nadharia ya uigizaji.

6.2.4 Matumizi ya Jukwaa

Matumizi ya jukwaa ni mbinu ya usimilisho jukwaani ambayo inaleta pamoja mbinu mbalimbali. Matumizi ya jukwaa yalikusisha mbinu za sauti, muziki, mandhari, pazia, na uangazaji.

6.2.4.1 Matumizi ya Sauti

Matumizi ya sauti yalibainika miongoni mwa vikundi vilivyofanyia maigizo yake katika kumbi za thieta. Kama ilivyotanguliwa kutajwa katika tasnifu hii, kumbi za thieta zilitoa mazingira mwafaka yaliyoruhusu matumizi ya mbinu mbalimbali za jukwaa.

Katika kumbi za thieta vikundi vya *Jicho Four* na *Fanaka* vilitumia mbinu ya sauti kujenga uhalisi na mazaji ya visa vilivyokuwa vikiigizwa. Sauti za vifaa mbalimbali zilikuwa zimerekodiwa na kucheza kama vile simu, kengele, gari, upepo, maji, moto, mlio wa risasi na ndege. Sauti hizo zilichezwa katika muktadha ulioalika kuwepo kwake. Katika hadithi fupi, *Damu Nyeusi*, sauti iliyoashiria mngurumo wa gari ilichezwa huku mwigizaji Fikirini akionekana kutia bidii kulisimamisha. Gari hilo lilipodinda kusimama, mlio wa kulikanyagia mafuta ulibainika na kutoweka kwake kukaashiriwa na kufifia kwa sauti hiyo. Katika hadithi fupi, *Samaki wa Nchi za Joto*, sauti ya filamu ilichezwa katika tukio nyumbani kwa Peter alipowawekea Zac na Christine filamu ya *Karate Kids*. Waigizaji walionekana kuitizama ukutani ijapokuwa haikuwapo, lakini hadhira ilifanywa kuamini ilikuwapo.

Katika kumbi za shule za upili, sauti ya mngurumo wa gari ilichezwa kuashiria kuingia kwake lakini haikuendelezwa. Sauti ya filamu iliyochezwa katika hadithi fupi ya *Samaki wa Nchi za Joto*, ilikuwa na tangazo la mtangazaji wa filamu iliyeitangaza kwa sauti yenye madoido na mvuto. Kiswahili kilichotumika na mtangazaji kilikuwa kimesanifiwa barabara. Matumizi haya yalidhihirishwa kwa jinsi sawa na vikundi vya *Planets* na *Nairobi Theatre Group*.

Mbinu za kiufaraguzi zilitumika kuwakilisha sauti zilizotarajiwa kucheza, hasa katika majukwaa ya shule. Kikundi cha *Planets* kilitumia kengele ya shule kuashiria kengele ya mlango, mngurumo wa gari ulitolewa na mwigizaji, na filamu ilitangazwa na mwigizaji nyuma ya jukwaa. Matumizi haya yaliwawezesha wanafunzi kuzipokea sauti hizo, ijapo kwa kiwango duni.

Mbinu ya sauti ilitumika kujenga uhalisi na mazaji katika matukio jukwaani. Wamitila (2002) anahoji kuwa, mbinu za sauti, nyimbo, muziki, vicheko, vigoma, na sauti nyinginezo hutumika ili kuunda mpatano wa kimaonyesho ambao unachangizana na vipengele vingine kama msuko na wahusika kuifanya kazi iwe kamilifu. Aidha, anaongeza kuwa, mbinu hizi huchangia kwenye wizani na hali nzima ya mchezo. Usimilisho wa hadithi fupi ulidhihirisha kiwango cha chini katika matumizi ya sauti. Ingawa kwa ujumla maigizo ya riwaya yalitumia sauti za aina nyingi, similisho la utungo wa hadithi fupi lilidhihirisha matumizi machache mno. Hali hii ilichangiwa na ubanifu wa utungo huo.

6.2.4.2 Matumizi ya Muziki

Matumizi ya muziki yalidhihirika katika vikundi vyote vilivyokuwa vikitafitiwa. Katika kumbi za thieta muziki ulichezwa katika vifaa vilivyokuwa vimeandaliwa kwa ajili hiyo. Majukwaa ya shule yalikota vifaa muhimu vya kuchezea muziki.

Kikundi kimoja kilitumia redio ndogo iliyotumia kani za batari, huku kikundi kingine kikiwatumia waigizaji kuimba nyimbo zilizobeba maudhui muhimu kuhusu tukio husika.

Muziki ulitumika ili kujenga mazaji ya matukio yaliyokuwa yakiigizwa. Katika hadithi fupi, *Gilasi ya Mwisho Makaburini*, mandhari ya baa ya Makaburini yalipambwa na muziki wa kila aina uliochezwa chini kwa chini. Muziki wa *kilingala, regae, hip hop, bongo flava*, miongoni mwa mingine ilisikika. Hali hiyo iliyapa mandhari hayo mazaji ya burudani na uchangamfu. Vikundi vitatu vilivyokuwa vikitafitiwa viliucheza muziki wa Michael Jackson, *Thriller*, uliodokezwa na mwandishi wa hadithi fupi.

Mbinu ya muziki ilitumika kuwasilisha maudhui yaliyowiana na tukio lililokuwa likiigizwa. Kwa mfano, kikundi cha *Jicho Four* kiliucheza muziki wake Eric Wainaina, *Daima Mkenya*, kushadidia maudhui katika maigizo ya hadithi fupi, *Maskini, Babu yangu!* Muziki huo ulibeba maudhui ya kukemea ukabila, maudhui yaliyozagaa katika hadithi fupi hiyo ya Ken Walibora. Katika uigizaji wa hadithi fupi, *Uteuzi wa Moyoni*, muziki wa kuwahimiza wanawake, *Hongera Kinamama*, ulichezwa wakati Zena alipokuwa akiendesha kampeni zake za kutafuta kuchaguliwa mbunge.

Nadharia changamano huchukulia ngoma na muziki kama sifa muhimu katika drama za Kiafrika. Kulingana na Wamitila 2008, ngoma hutumiwa kama ishara ya kutanguliza mambo fulani yanayotokea katika tendo la kidrama au pamoja na muziki kama njia ya kuongeza kiwango cha hisia katika tendo fulani. Aidha, sifa hizi hushadidia maudhui na ni sehemu ya vijenzi vya wizani katika tamthilia husika. Uigizaji wa hadithi fupi ulikitwa zaidi katika msingi huu wa kinadharia.

Utafiti ulibaini kwamba hadithi fupi nyingi zilikuwa na miktadha mbalimbali iliyoalika matumizi ya ngoma ama nyimbo fulani. Fauka ya haya, kuna hadithi fupi zilizosheheni matumizi ya nyimbo fulani mahsusni. Kwa jicho pevu, hizi ni sifa za kitamthilia ambazo hudhihirika katika matini za kinathari.

6.2.4.3 Usawiri wa Mandhari

Usawiri wa mandhari ya jukwaani ni mbinu ya usimilisho ambayo ikizingatiwa hufanikisha shughuli nzima ya kusimilisha. Mwelekezi wa similisho hujaribu awezavyo kuyasawiri jukwaani mandhari ya hadithi fupi kama yalivyosimilishwa katika similisho. Mandhari yanapaswa kuwabainisha wahusika na kushadidia maudhui ya mwandishi.

Matini za hadithi fupi zilidhihirisha upungufu katika kuelekeza mandhari ya matukio. Kinyume na riwaya iliyotumia usimulizi kuelezea mandhari yake, hadithi fupi zililenga sana kuendeleza wazo kuu na mhusika mkuu. Hali hiyo iliathiri jinsi mandhari yake yangesawiriwa jukwaani. Hata hivyo, kuna hadithi fupi zilizoелеkeza kwa namna kamilifu jinsi mandhari ya tukio fulani yalivyokuwa. Katika maigizo ya *Samaki wa Nchi za Joto*, mandhari ya chumba cha Zac yalidokezwa kwa njia dhahiri. Kulikuwa na kitanda kimoja walipoketi Peter na mwenyeji Zac, na kiti kimoja alichokalia Christine. Kimeza kilichokuwa mbele ya kiti hicho kilikuwa na vitabu kadha juu yake. Ukutani kuliangikwa picha kubwa ya Bob Marley.

Nadharia ya uigizaji huelekeza kwamba usawiri wa mandhari jukwaani ni sharti uoane na mazaji na maleba ya waigizaji (Syambo na Mazrui, 1992). Mandhari ni lazima yabainishe uhalisi katika jamii. Waigizaji wenye hadhi kijamii ni sharti wapatikane katika mandhari yenye ufahari. Mandhari ya maombolezo yataigizwa

na waigizaji wanaoomboteza. Usawiri wa mandhari katika usimilisho wa hadithi fupi jukwaani ulionekana kupata ufanisi katika mandhari ya thieta na kupungukiwa katika majukwaa ya shule. Upungufu katika usawiri wa mandhari uliashiria upungufu katika uwasilishaji wa maudhui na ubainishaji wa wahusika.

6.2.4.4 Matumizi ya Pazia

Mbinu ya matumizi ya pazia ilitumika katika majukwaa ya kumbi za thieta na ikakosekana katika kumbi za shule. Katika maigizo ilipotumika, mbinu ya matumizi ya pazia ilitokeleza dhima mbalimbali.

Kwanza, pazia ilitumika kuashiria mwanzo na mwisho wa onyesho fulani la hadithi fupi. Baadhi ya hadithi zilikuwa na maonyesho kadha, huku hadithi fupi nyingine zikiwa na onyesho moja tu. Katika hadithi fupi zilizokuwa na onyesho moja, pazia ilitumika kuonyesha mwanzo na mwisho wa maigizo ya hadithi fupi.

Pili, pazia ilitumika kumtenga msimulizi na waigizaji wengine. Msimulizi alionyeshwa mbele ya pazia ikiwa imefungwa, huku waigizaji wakiigizia nyuma ya pazia ilipofunguliwa. Jambo hilo lilisaidia hadhira kumtambua mtambaji kwa urahisi.

Tatu, pazia ilitumika kuonyesha mandhari yasiyo dhahiri kuwekwa jukwaani. Matukio ambayo hayakuwa rahisi kuwekwa jukwaani, mengine yalionyeshwa mbele ya pazia. Kwa mfano, wezi waliowaibia kina Msoi na wenzake katika hadithi fupi, *Gilasi ya Mwisho Makaburini*, walionyeshwa mbele ya pazia wakiwa wamebeba mali waliyoiba.

Katika maigizo yote ambayo yalitumia mbinu ya pazia, matumizi yake yalionekana kuwiana sana. Iliyobainika ni kwamba, matumizi ya pazia ni

mojawapo wa mbinu muhimu zinazotumika kufanikisha uigizaji jukwaani. Pazia iliandaa mazingira muruwa ya kutayarisha maonyesho na kuyaelekeza kupitia kwa mtambaji.

6.2.4.5 Uangazaji

Mbinu ya uangazaji ilihusisha umulikaji wa aina mbalimbali uliofanywa jukwaani. Matumizi ya mbinu hii yalidhihirika tu katika majumba ya thieta ambayo usanifu wake ulifanywa kwa uzingatifu wa kuruhusu matumizi ya mbinu za jukwaani. Majukwaa ya shule yalikosa vifaa vya mwangaza na zaidi yake hamkuwa na njia mwafaka ambayo ingetumika ili kujaza chumba giza ndiposa umulikaji uwezekane.

Syambo na Mazrui (1992) wanadai kwamba, umulikaji wa aina mbalimbali huwa na athari mbalimbali jukwaani katika kudhihirisha mazaji mbalimbali ya tamthilia fulani. Waandishi hawa wametaja dhima moja ya umulikaji ambayo ni udhihirishaji wa mazaji. Wilson na Goldfarb (1991) wameorodhesha dhima mbalimbali za umulikaji: kutambulisha waigizaji, kuashiria majira ya siku, kukuza mazaji, kuimarisha mtindo, na kuonyesha msisitizo jukwaani. Uangazaji katika usimilisho wa hadithi fupi jukwaani ulifanywa kwa madhumuni mbalimbali. Kwanza, uangazaji ulitumika ili kumtambulisha mtambaji alipokuwa akisimulia jukwaani. Katika hali hii, jumba lote lilikuwa limegubikwa kiza totoro isipokuwa taa ya spotilaiti iliyokuwa imemumulika mtambaji mbele ya pazia. Pili, uangazaji jukwaani ulifanywa kwa dhamira ya kubainisha mwanzo na mwisho wa onyesho. Mwanzoni mwa onyesho baada ya pazia kufunguliwa, mwangaza angavu ulimulika eneo la kuigiziwa na kuonyesha mandhari yake pamoja na waigizaji. Onyesho lilipokwisha mwangaza huo ulizimwa na

kukaribisha kiza totoro. Tatu, uangazaji ulitumika kuashiria majira ya siku; usiku na mchana. Mwangaza angavu uliashiria mchana na mwangaza usio na uangavu thabiti ukaashiria usiku.

Fauka ya hayo, uangazaji ulitumika kujenga mazaji ya igizo jukwaani. Mambo yakiwa shwari mwangaza mwangavu ulitumika, ilhali mambo yakiwa ya shaka na masikitiko mwangaza hafifu ama kiza ulitumika. Katika maigizo ya hadithi fupi *Gilasi ya Mwisho Makaburini*, wezi walipovamia hotelini hali ya wasiwasi iliashiriwa na mwangaza hafifu kisha kiza totoro. Matumizi kama hayo yalionekana katika tukio sawa na hilo katika similisho la *Mayai Waziri wa Maradhi*. Majilio ya mizuka kumi nyumbani kwa Mayai yaliashiriwa na mwangaza angavu. Hali ilipomzidia Mayai, kiza totoro kilihanikiza chumbani mwote.

Nadharia ya uigizaji huelekeza umulikaji ufanywe kwa jinsi mbalimbali ili kuleta athari mbalimbali za mazaji ya tamthilia inayoigizwa. Uigizaji katika majukwaa ya thieta ulidhihirisha matumizi mwafaka ya uangazaji na athari yake jukwaani ilijitokeza. Hadhira ilifanywa kusadiki kwamba kila aina ya umulikaji ulitekeleza dhima fulani mahsusi jukwaani. Kwa sababu ya ubanifu wake, hadithi fupi ilidhihirisha matumizi machache ya mbinu hii.

6.2.5 Utendaji

Utendaji ni mbinu ya usimilisho jukwaani ambapo matendo yanayoashiriwa na maneno katika similisho huigizwa. Aidha, mbinu ya utendaji inaweza kuhusisha ubunaji wa vitendo vinavyochangiana na maudhui ya similisho linaloigizwa.

Utafiti wa maigizo ya hadithi fupi ulibainisha kwamba vitendo mbalimbali vilivyokuwa vimeashiriwa na matini za hadithi fupi vilionyeshwa jukwaani. Hata

hivyo, mbinu ya utendaji ilibainika sana katika maigizo ya riwaya kuliko ilivyojitokeza katika maigizo ya hadithi fupi. Aidha, uigizaji wa hadithi fupi uliofanywa katika majukwaa ya shule haukuonyesha utendaji mwingi. Hii ni kwa sababu vikundi vilivyoigiza katika majukwaa hayo vilikuwa na muda mfupi wa kuigiza hadithi fupi za diwani husika.

Uigizaji wa hadithi fupi uliruhusu utendaji wa vitendo vifupi tu jukwaani. Katika similisho la *Maskini, Babu Yangu!*, kisa cha kupigwa na kuchomwa moto kwa babu ya msimulizi kiliigizwa kwa kifupi na baadhi ya vikundi. Aidha, katika hadithi fupi ya *Mke Wangu*, kitendo cha mume wa Aziza kuchukua kichana na kuanza kuchana nywele zake kabla mgogoro baina yake na Aziza kuzuka, kiliigizwa na vikundi vingi.

Uchunguzi huu ulibaini kwamba utendaji katika uigizaji wa hadithi fupi ulitegemea aina ya jukwaa, muda uliotengewa uigizaji, na usanifu wa similisho. Kuna vitendo vilivyohitaji majukwaa makubwa na yenye muundo changamano kama vile kutekwa nyara kwa Naseko, kupelekwa kwa Mzee Sakaja, kutoroka kwake kwa Mzee Sakaja na kukimbilia Mkomani kwa Bi. Tesi. Vitendo hivyo vilisimilishwa katika hadithi fupi ya *Ngome ya Nafsi*. Vikundi ambavyo havikuwa na muda mrefu wa kuigiza vilipuuzilia mbali maigizo ya vitendo vilivyokuwa vikichukua muda mwingi jukwaani. Usanifu wa similisho ndio ulioelekeza vitendo vya kuigizwa jukwaani. Uigizaji wa hadithi fupi ulibainisha kuwepo na utendaji uliopigwa chuku na mwingine kufanywa kinyume. Kulingana na hoja ya awali, utendaji ni njia moja ya kuwabainisha wahusika katika uigizaji. Vitendo vinavyoigizwa vinapaswa kulenga kuibua sifa za wahusika jinsi zilivyosawiriwa na mwandishi pasipo mapendeleo wala kuzipotosha.

Utendaji uliojumuisha ubunaji wa vitendo ulidhihirishwa na maigizo machache ya hadithi fupi. Utendaji wa jinsi hiyo ulifumwa kwa usanii wa msimilishaji na sio wasimilishaji wote walihitimu kufanya hivyo. Kwa mfano, katika hadithi fupi ya *Gilasi ya Mwisho Makaburini*, wezi waliowavamia Msoi na marafiki zake walionyeshwa mbele ya pazia katika mwangaza hafifu wakiwa wamebeba mali waliyoiba. Kisa hicho cha wizi kilikuwa kimeelezwa kama uvamizi uliotekelezwa na kundi la vizuu vilivyofufuka kutoka eneo la makaburi. Kwa watazamaji waliofikiria kwamba hiyo ilikuwa ni mizuka, utendaji wa aina hiyo uliwakosoa.

Kama ilivyotanguliwa kusemwa, nadharia ya uigizaji huutambua utendaji kama kipengele muhimu katika muundo wa tamthilia. Tamthilia huwasilisha maudhui na fani kupitia mazungumzo na utendaji. Packard (1997) anadai kuwa tendo ndilo nguzo kuu ya tamthilia. Kulingana na Packard, matendo ya kidrama ndiyo muhimu zaidi kuliko lugha hata kama lugha hiyo imesanifiwa kwa ufundi wa juu. Hii ina maana kwamba lugha ya drama inatarajiwa kuzua na kuendeleza tendo. Kwa maoni ya Packard (1997), tendo la kidrama ndilo huongoza usawiri wa wahusika wa kidrama na tendo nzuri hutakiwa kuwa wazi, thabiti, na linalojibainisha katika matini ya kidrama.

Hadithi fupi zilithibitisha kusheheni visa vya utendaji ambavyo vilikuwa muhimu kuongoza ubunaji wa matendo ya kuigizwa. Hii ni sifa ya mwingiliano tanzu baina ya hadithi fupi na tamthilia. Kinyume na riwaya, utendaji wa hadithi fupi ulikuwa mchache na mfupi. Ingawa nadharia ya uigizaji huhimiza utendaji katika drama, ni muhimu usimilisho ushirikishe msingi wa nadharia ya usimilisho unaohimiza usahihi katika kusimilisha. Utendaji unapaswa kufanywa namna unavyoelekezwa katika matini chasili pasipo kuopotosha kwa hali yoyote.

6.2.6 Uigizaji wa Mbinu

Uigizaji wa mbinu umejadiliwa kikamilifu katika usimilisho wa riwaya. Hata hivyo, kuna mbinu za usanifu wa hadithi fupi zilizowasilishwa kwa namna tofauti. Sehemu hii ilidhamiria kuzibainisha na kuzielezea mbinu hizo. Kutokana na ubanifu wa utungo, hadithi fupi zilifumwa kwa matumizi ya mbinu chache. Kwa hivyo, mbinu zilizoigizwa na masimilisho yake zilikuwa chache.

Baadhi ya mbinu zilizoigizwa ni kama vile kisengere nyuma, matumizi ya barua, picha, redio na uzungumzi nafsi. Kulikuwa na jinsi mbili za kuigiza mbinu ya matumizi ya barua. Barua zilizokuwa zimeandikwa katika hadithi fupi, zilisimilishwa hivyo na kuigizwa kupitia usomaji wa sauti jukwaani. Jinsi ya pili ilihusu kuzibunia maneno barua zilizodokezwa na kuyasoma kupitia sauti. Mfano ni barua za Masazu na Sela katika similisho la *Kanda la Usufi*. Hayo yalifanywa na takriban vikundi vyote vilivyokuwa vikitafitiwa. Maneno yaliyotumika yalitokana na maudhui ya hadithi fupi. Hali ya kuzibunia barua maneno haikujitokeza katika usimilisho wa riwaya. Kutokana na urefu wake, riwaya iliweza kujumuisha maneno ya barua zilizotumika. Kubuni ujumbe wa barua kulifanywa kama njia moja ya kuendeleza muundo wa mazungumzo ya kitamthilia. Maneno katika barua hizo yaliwekwa katika mazungumzo ya kujibizana baina ya wahusika. Hata hivyo, umatini wa ziada ambao haukulengwa kuwasilishwa na mwandishi, kama ilivyotajwa awali, ulipotosha wanafunzi kwa vile haukuwa sehemu ya yale yaliyopaswa kutahiniwa.

Mbinu ya kisengere nyuma iliwasilishwa kwa kuigizwa. Hadithi fupi zilizokuwa zimeitumia mbinu hiyo ni kama vile: *Kachukua Hatua Nyingine*, *Masikini*, *Babu Yangu!* na *Samaki wa Nchi za Joto*. Kutokana na ubanifu wa hadithi fupi,

haikuwa rahisi kuufaragua msuko wake na kuiwasilisha hadithi fupi hiyo kwa msuko tofauti. Wasimilishaji walionekana kupendelea msuko wa mtunzi ambao uliwawezesha kuziwasilisha hadithi hizo kwa namna ambayo hadhira ingeikumbuka vyema.

Matumizi ya picha yalibainika katika hadithi fupi ya *Mayai Waziri wa Maradhi*. Maigizo ya hadithi fupi hiyo yalikusisha picha halisi ambazo mwigizaji Mayai alionekana akizikagua katika buku la picha. Matumizi ya mbinu hiyo yalileta uhalisi katika maigizo ya hadithi fupi hiyo. Matumizi kama hayo yalidhihirika katika takriban vikundi vyote vilivyotafitiwa.

Mbinu nyingine iliyosimilishwa na kuigizwa ni matumizi ya redio. Matumizi ya redio yalipatikana katika maigizo ya hadithi fupi *Kachukua Hatua Nyingine*. Katika matini chasili ni ujumbe wa redio hiyo uliokuwa umetajwa na mwandishi, lakini maigizo yalijumuisha kifaa na sauti yenye ujumbe huo. Kifungu kifuatacho kilinakiliwa kutoka mojawapo wa vikundi:

REDIO: Hii ni sauti ya redio ya taifa na ifuatayo ni taarifa ya habari.

Serikali imetangaza kusitishwa mara moja kwa mpango wa elimu ya bure. Wazazi watahitajika kuwanunulia watoto wao vitabu na vifaa vingine muhimu. Akiyatangaza hayo, Rais alisema kuwa, ni lazima anayebewa ajikaze.

(Similisho la *Kachukua Hatua Nyingine*, Jicho Four)

Kama ilivyobainika, uigizaji wa hadithi fupi uliwasilisha mbinu chache za utunzi kutokana na ubanifu wake. Mbinu za uwasilishaji wa maudhui huwa ni muhimu katika kuibua masuala yaliyomo katika utungo wa hadithi fupi. Hata hivyo, ilibainika kwamba, wasimilishaji walizidondosha baadhi ya mbinu zilizotakikana kuigizwa jukwaani ili wafupishe muda wa kuigiza. Hali hiyo ilipunguza maudhui

ya hadithi fupi yaliyobainishwa na usimilisho. Matatizo ya usimilisho wa hadithi fupi yamejadiliwa katika sehemu inayofuata.

6.3 MATATIZO KATIKA USIMILISHO WA HADITHI FUPI

Sehemu hii imeshughulikia matatizo yaliyobainishwa na usimilisho wa hadithi fupi. Data kuhusu matatizo hayo ilitokana na hojaji, uchanganuzi wa masimilisho na maigizo yake, na mahojiano kwa wasimilishaji. Matatizo hayo yamechanganuliwa na kuwasilishwa kijarabati na kimaelezo.

6.3.0 Uwasilishaji wa Data kuhusu Matatizo ya Usimilisho wa Hadithi Fupi

Uchanganuzi wa hojaji za walimu ulifanywa kwa programu ya tarakilishi ya SPSS na unawasilishwa kwa njia za kijarabati. Hojaji na mahojiano kwa wasimilishaji yamechanganuliwa kijarabati na kimaelezo. Wasimilishaji walikuwa wanne na mtafiti alipata fursa ya kuwahoji kila mmoja na kukusanya mambo mengi. Walimu waliohojiwa walikuwa tisa.

6.3.1 Data Kutokana na Hojaji za Walimu

Hojaji za walimu ziliwataka wajibu maswali mbalimbali kuhusu usimilisho wa riwaya. Maswali walioulizwa yalizua data ifuatayo:

6.3.1.1 Kutathmini Usomaji wa Hadithi Fupi

Kuhusu iwapo wahojiwa walikuwa wamezisoma hadithi fupi zilizokuwa zikiigizwa, asilimia mia moja (100%) ilikiri ilizisoma. Jambo hili lilikuwa na maana kuwa walimu walifahamu kilichokuwa kikisimilishwa. Kwa hivyo, iliwezekana walimu kutambua matatizo yaliyobainika katika mchakato huo.

6.3.1.2 Kutathmini Usahihi wa Maigizo

Asilimia 66.7 ya wahojiwa ilionyesha kutoridhika na jinsi hadithi fupi zilivyokuwa zimesimilishwa. Idadi hiyo ilikuwa kubwa ikilinganishwa na asilimia 40 ambayo haikuridhishwa na jinsi usimilisho wa riwaya ulivyofanywa. Hii ina maana kwamba usimilisho wa hadithi fupi ulidhihirisha matatizo mengi kuliko ule wa riwaya. Hali za kuwepo na hadithi fupi nyingi za kusimilishwa na ufupi wa utanzu wenyewe zilisababisha baadhi ya matatizo hayo. Usimilisho wa hadithi fupi ulionekana kuigiza tukio kuu katika hadithi fupi husika na kupuuza vitukio vingine. Zingatia jedwali 6.5:

JEDWALI 6.5 KUTATHMINI USAHIHI WA MAIGIZO

VIWANGO	IDADI RADIDI	ASILIMIA	ASILIMIA JUMLIFU
VIBAYA SANA	1	11.1	11.1
VIBAYA	0	0.0	0.0
WASTANI	5	55.6	66.7
VIZURI	3	33.3	100.0
VIZURI SANA	0	0.0	
JUMLA	9	100.0	100.0

6.3.1.3 Umuhimu wa Usimilisho wa Hadithi Fupi kwa Maandalizi ya KCSE

Wahojiwa walipotakiwa kutathmini umuhimu wa maigizo ya hadithi fupi kwa maandalizi ya mtihani wa KCSE, majibu yao yalikuwa hivi:

Asilimia 66.7 walisema si ya lazima.

Asilimia 22.2 wakasema ni muhimu.

Asilimia 11.1 walisema ni muhimu sana.

Asilimia 66.7 ya wahojiwa ambao hawakuona umuhimu wa usimilisho wa hadithi fupi kwa maandalizi ya KCSE ilikuwa kubwa ikilinganishwa na asilimia 10 ambao hawakuona umuhimu wa usimilisho wa riwaya kwa maandalizi ya KCSE. Ingawa hadithi fupi zilisheheni sifa zilizokaribiana sana na zile za tamthilia kama vile ufupi wa utungo na usawiri wa tukio moja kuu, maigizo yake yalionekana kusesitiza zaidi matukio ambayo yangeigizika na kudondosha sehemu nyinginezo.

6.3.1.4 Utambuzi wa Matatizo ya Usimilisho wa Hadithi Fupi

Wahojiwa walitambua matatizo yafuatayo katika usimilisho wa hadithi fupi:

JEDWALI 6.6 MATATIZO YA USIMILISHO WA HADITHI FUPI

AINA YA MAKOSA	IDADI RADIDI	ASILIMIA
KUTIA CHUMVI	5	55.6
USAWIRI WA WAHUSIKA	7	77.8
UBAINISHAJI WA MAUDHUI	9	100.0
MTIRIRIKO WA MSUKO	7	77.8
USAWIRI WA MANDHARI	4	44.4
UDONDOSHAJI WA MATUKIO	6	66.7
USIMILISHO WA MBINU	5	55.6
MATUMIZI YA LUGHA	4	44.4
MUDA MFUPI WA KUIGIZA	3	33.3

Asilimia 100 ya walimu ilitaja kwamba usimilisho wa hadithi fupi haukubainisha maudhui kama yalivyoelezwa na matini chasili. Aidha, asilimia 77.8 haikupendezwa na namna msuko ulivyotiririshwa na wahusika kusawiriwa. Zaidi ya nusu ya wahojiwa ilibaini matatizo katika usimilisho wa mbinu, udondoshaji wa matukio, na hali ya kutia chumvi. Matatizo ya ubainishaji wa maudhui, mbinu, na wahusika yalisababishwa na udondoshaji wa sehemu fulani ambazo

hazikushirikisha utendaji. Hali ya kutia chumvi ilitokea katika usawiri wa sifa fulani za wahusika na utendaji wao jukwaani.

6.3.1.5 Utatuzi wa Matatizo ya Usimilisho wa Hadithi Fupi

Wahojiwa walipotakiwa kupendekeza jinsi ya kuyaboresha maigizo ya hadithi fupi, walitaja njia zifuatazo:

Yanapaswa kukaguliwa kabla yaidhinishwe- 77.8%

Wasimilishaji wasomeshe jinsi ya kusimilisha – 55.6%

Walimu washirikishwe katika usimilisho – 33.3%

Maigizo potovu yaharamishwe – 44.4%

Kuhimiza ushindani miongoni mwa vikundi – 11.1%

Zaidi ya asilimia 50 ya wahojiwa ilipendekeza maigizo ya hadithi fupi yakaguliwe kabla ya kuidhinishwa na wasimilishaji wapewe mafunzo ya kusimilisha. Karibu nusu ya wahojiwa (44.4%) ilipendekeza maigizo yanayoshuka kiviwango yaharamishwe. Asilimia 33.3 ilitaja kwamba ni muhimu walimu kuhusishwa katika usimilisho wa hadithi fupi. Idadi kubwa ya wahojiwa, kama ilivyoonyeshwa, ilipendekeza kuhusishwa kwa wataalamu katika usimilisho, na kuwekwa vigezo vya kufuatwa pamoja na adhabu kwa wale watakaokaidi. Ni asilimia ndogo (11.1%) iliyofikiria kwamba vikundi vinaweza kuweka viwango na kuvizingatia.

Mtafiti hakubaini tofauti zozote katika data iliyochanganuliwa kutoka hojaji na mahojiano na wasimilishaji kuhusu usimilisho wa hadithi fupi na riwaya. Mbali na maswali ya kutaka kubaini tajriba yao, mtafiti alikuwa amewauliza maswali

yaliyolenga kubaini matatizo ya usimilisho wa hadithi fupi. Aidha, mtafiti aliwataka waeleze njia wanazotumia kuyatatua matatizo waliyoyataja. Fauka ya haya, hojaji za walimu zilibaini matatizo sawa ya usimilisho wa hadithi fupi na riwaya. Utafiti ulihitimisha kuwa, matatizo makuu ya usimilisho wa tungo za kinathari ni ya aina sawa. Tofauti katika matatizo hayo zinasababishwa na miundo na mitindo ya tungo mahsusi katika tanzu hizo.

Matatizo ya usimilisho wa tungo za kinathari yalibainika kuwa: udondoshaji wa maudhui muhimu, upungufu wa kuwasawiri wahusika, miundo potovu ya kitamthilia, upungufu wa kuyasawiri mandhari, na ugumu wa kuigiza mbinu za sanaa na lugha. Haya ni matatizo yaliyokuwa na chanzo chake katika matini ya kusimilishwa. Utafiti ulibaini kuwapo na matatizo mengine ya usimilisho huo ambayo chanzo chake kilikuwa wasimilishaji wenyewe. Haya ni kama vile: matini ngumu kusimilika, utegemezi uliokithiri wa mazungumzo, matumizi ya chuku, na tatizo la kifedha.

Sura hii imejadili matatizo mawili yaliyokuwa na chanzo katika matini, na tatizo moja lililokuwa na chanzo kwa wasimilishaji. Matatizo haya yalibainika kusababisha makosa mengine katika usimilisho wa hadithi fupi yalipofanywa.

6.3.2 Matatizo Yalitokana na Mbinu za Usimilisho

Matumizi ya mbinu fulani za usimilisho yaliweza kusababisha matatizo yaliyoathiri kwa njia hasi namna vipengele vya hadithi fupi vilivyowasilishwa. Matatizo ambayo yamejadiliwa ni udondoshaji na miundo potovu ya kitamthilia.

6.3.2.1 Udondoshaji

Udondoshaji ni hali ya kuwacha nje sehemu muhimu za hadithi. Hali ya kuwacha nje sehemu muhimu za hadithi ilidhihirika sana katika hadithi fupi kinyume na ilivyokuwa katika riwaya. Mahojiano na hadhira yalibainisha kwamba udondoshaji ulikuwa tatizo kubwa katika usimilisho wa hadithi fupi. Hadhira ililalama kwamba baadhi ya sehemu muhimu za hadithi fupi zilikosa kuigizwa na hivyo kuathiri mtiririko na maudhui ya hadithi fupi hiyo.

Mpangilio wa maigizo ulichangia kwa kiwango kikubwa udondoshaji uliodhihirika katika uigizaji wa hadithi fupi. Hitaji la kuigiza hadithi zote katika diwani moja ilifanya baadhi ya sehemu za hadithi fulani kudondoshwa ili zifupike. Hali hiyo ilizidishwa na mpangilio wa kutaka kuigiza vitabu teule vitatu kwa siku moja. Kwa hivyo, mbinu ya udondoshaji ilitumika kuleta sifa ya ufupi katika maigizo ya hadithi fupi.

Udondoshaji ulikuwa tatizo kwa usimilisho wa hadithi fupi iwapo ulifanywa pasipo kuzingatia madhara yake kwa maudhui na fani. Hivyo ni vipengele muhimu vya maana katika hadithi fupi. Udondoshaji uliathiri ubainishaji na ukuzaji wa wahusika wa hadithi fupi. Similisho la *Uteuzi wa Moyoni* liliwacha nje sehemu muhimu zilizonuiwa kumkuza mhusika Zena. Habari kuhusu kusoma kwa Zena na dada zake na jinsi walivyokejeliwa na wanakijiji iliwachwa nje na masimilisho mengi. Maelezo hayo yaliimarisha sifa ya ustahimilivu iliyothibitishwa na Zena, hata kustahimili vituko vya Ali na dhihaka wakati wa kampeni. Kuwachwa nje kwa sehemu hizo na nyingine kulidhoofisha wasifu wa mhusika huyo na maudhui yaliyomzingira.

Tatizo la udondoshaji halikuathiri kipengele cha wahusika peke yake bali pia vipengele vinginevyo vya fani. Masimilisho mengi ya *Samaki wa Nchi za Joto*,

yaliwacha nje sehemu ya utangulizi iliyokuwa ikibainisha kwamba hadithi fupi hiyo ilichukua mtindo wa mbinu ya kioo. Matukio ya hadithi yaliwasilishwa kwa mbinu rejeshi, lakini masimilisho hayakudokeza hivyo.

Nadharia changamano haipingi kwa vyovyote hali ya kudondosha matukio ya hadithi. Katika harakati za kuisimilisha kazi ya fasihi huenda majadiliano ya hadithi yakapotea na kubakisha vile vipengele vyake muhimu (Hutcheon, 2013). Hata hivyo, usimilisho wenye dhamira ya kusimilisha hadithi fupi zinazotahiniwa unapaswa kuwasilisha vipengele vyote vilivyobuniwa na mwandishi. Kuna mbinu nyingine za usimilisho ambazo zinaweza kutumika ili kuifupisha hadithi na kudumisha vipengele vyake kama vile mshindilio na usimulizi. Hali ya kudondosha sehemu za hadithi fupi hakuonekana kuwanufaisha wanafunzi waliokuwa wakijiandaa kwa mtihani wa KCSE kwa sababu iliwaondolea baadhi ya vipengele vya fani na maudhui vilivyokuwa muhimu katika kuifuatilia na kuelewa hadithi.

6.3.2.2 Miundo Potovu ya Kitamthilia

Muundo wa kitamthilia umejadiliwa kwa mapana katika sura iliyotangulia. Kama ilivyobainika, usimilisho wa hadithi fupi hulenga kuwasilisha hadithi katika muundo wa kitamthilia. Muundo wa kitamthilia hushirikisha mazungumzo, matendo, maelekezo ya jukwaani, na sehemu. Miundo potovu ilihusu hali ya kukosa kufuata msuko wa hadithi fupi kama ulivyoelekezwa na mwandishi ama kuufuata vibaya. Hali hiyo ilidhihirika sana katika usimilisho wa hadithi fupi ikilinganishwa na usimilisho wa riwaya. Aidha, tatizo la namna hiyo lilidhihirika sana katika uigizaji kuliko lilivyokuwa katika similisho la hadithi fupi.

Muundo wa sehemu za drama haukuzingatiwa katika uigizaji. Baadhi ya masimilisho ya hadithi fupi yalikuwa yamebuniwa kwa onyesho moja (Tazama jedwali 1.3). Hizi ni hadithi ambazo zilikosa kuwa na sehemu nyingi zenye utendaji na mazungumzo. Kwa vile wasimilishaji walitegemea kuchukua sehemu zenye mazungumzo na matendo, hadithi fupi zilizobuniwa kwa unathari mwingi zilisimilishwa kwa kifupi na kama onyesho moja jukwaani. Hili lilikuwa tatizo kubwa kwa vile usimilisho haukuonekana kuzingatia kipengele cha maudhui na fani. Kilichoongoza usimilisho wa aina hiyo kilibainika kuwa udhihirishaji wa umatini wa kitamthilia katika hadithi fupi.

Tatizo jingine la kimuundo lilibainika katika uigizaji wa hadithi fupi ulioichukulia diwani ya hadithi fupi kama matini moja ya tamthilia yenye dhamira zilizowiana. Katika muundo huu, hadithi fupi zilizokuwa katika diwani hiyo ziliigizwa kama maonyesho ya kazi hiyo moja. Uigizaji ulifanywa kufuatana jukwaani, hadithi baada ya nyingine. Usimilisho huu ulikitwa kwa matukio muhimu ya hadithi, hasa upeo wake. Mkusanyiko wa hadithi fupi hauwezi kuigizwa kama kazi moja yenye dhamira sawa. Ingawa inawezekana kukusanya pamoja tungo zenye dhamira sawa, diwani zilizokuwa zikitafitiwa zilikuwa na mchanganyiko wa dhamira. Hali ya kudhihirisha makosa mengi ya uigizaji, iliwapanya walimu kupitia hojaji zao kuonyesha kutoridhishwa na usimilisho wa hadithi fupi. Kama ilivyotanguliwa kusemwa, maigizo ya hadithi fupi yalikosa msisimko ulioshuhudiwa katika maigizo ya riwaya. Hiki ni kinyume na hali halisi kwa vile tungo za hadithi fupi hudhihirisha msisimko mwingi kwa wasomaji.

Hali ya kuzilazimisha hadithi fupi kuigizika kama kazi moja ilifanya hadithi fupi zilizosheheni miundo changamano kukosa kusimilishwa ama kuigizwa ipasavyo. Hadithi fupi zilizokuwa zimetumia mbinu za kioo kama vile *Kachukua Hatua*

Nyingine, Mayai Waziri wa Maradhi, Samaki wa Nchi za Joto, Maskini, Babu Yangu!, na *Mke Wangu*, zilisimilishwa kwa kukiuka misuko yake. Wasimilishaji kwa kudhamiria waliruka sehemu za usimulizi na kuigiza sehemu zenye mazungumzo. Kwa vile mbinu rejeshi iliwasilishwa katika usimulizi, haikuwezekana kuidhihirisha jukwaani. Mbali na kuigizwa visivyo kwa mbinu rejeshi, habari muhimu iliyowasilishwa kupitia mbinu hiyo ilipotea katika uigizaji.

Msuko ni kipengele muhimu cha hadithi. Hadithi hupatikana katika msuko wa kazi fulani ya fasihi. Kwa hivyo, msuko ni namna mbalimbali za kuiwasilisha hadithi ya kazi fulani ya fasihi. Kulingana na Hutcheon (2013), nadharia ya usimilisho huitambua hadithi kama kiungo muhimu cha usimilisho. Kutokana na utambuzi huo, msuko unachukuliwa kuwa kipengele muhimu cha kuzingatiwa katika usimilisho. Hali ya kutowasilisha msuko wa hadithi ipasavyo iliathiri kwa jinsi hasi uwasilishaji wa hadithi.

Nadharia ya uigizaji huelekeza namna msuko wa kidrama unavyopaswa kubuniwa. Kulingana na Diyanni (2004), msuko wa kidrama ni mpangilio wa matukio yanayohusiana na kusababishana. Tukio husababisha kutokea kwa tukio jingine ama hutokana na tukio jingine moja kwa moja. Kwa kutathmini usimilisho wa muundo wa hadithi fupi, kipengele cha msuko hakikusimilishwa kama anavyoelekeza Diyanni (2004). Hali ya usimilisho kutegemea sana mazungumzo na utendaji katika hadithi ilisababisha mapengo katika mtiririko wa msuko katika baadhi ya masimilisho ya vikundi. Aidha, usimilisho wa hadithi fupi za diwani moja kama matini moja yenye dhamira moja, haungeweza kubainisha hatua tano za muundo wa kidrama: maelezo ya ufunguzi, mkweo wa tendo, upeo, mshuko wa tendo, na ufumbuzi/ mwisho. Diyanni (2004) anasema

kwamba muundo wa kimsingi wa drama unapaswa kudhihirisha hatua hizo tano. Hadithi fupi katika diwani moja hazikuendeleza mgogoro mmoja na hivyo misuko yake ilikuwa mbalimbali. Usimilisho wa aina hii ulikuwa ukiwapotosha wanafunzi katika kuelewa ubainifu wa kila hadithi fupi kimaudhui na kifani.

6.3.3 Tatizo Lililotokana na Wasimilishaji

Mbali na matatizo hayo mawili yenye chanzo katika matini, kuna tatizo la matini kuwa ngumu kusimilika, ambalo lina chanzo kwa wasimilishaji. Usimilisho wa hadithi fupi ulidhihirisha tatizo hili kitofauti na jinsi lilivyodhihirika katika usimilisho wa riwaya.

6.3.3.1 Matini Ngumu Kusimilika

Kupitia mahojiano na hojaji, wasimilishaji walitaja kwamba mitindo ya baadhi ya waandishi iliwatatiza na kwa hivyo ikaathiri usimilisho kwa njia hasi. Kwa mfano, matini ya hadithi fupi ya *Kikaza* iliwatatiza wasimilishaji wengi kuifasiri namna ya kuiigiza. Kikundi cha *Nairobi Theatre Group* kilikosa kuisimilisha hadithi fupi hiyo, na hata kuiigiza. Masimilisho ya hadithi fupi hiyo hayakuonekana kuiendeleza hadithi namna ilivyokuwa imewasilishwa na mwandishi wake.

Kulingana na Mohammed na Walibora (2007), hadithi fupi ya *Kikaza* imesukwa ikisisitiza ‘dhana’ badala ya ‘tendo’, ‘tukio’ au ‘mhusika’. Masimilisho yaliyofanywa ya hadithi hiyo yalionekana kutoka nje ya hadithi na kuanza kusisitiza kipengele cha utamaduni. Ingawa maudhui ya utamaduni yalikuswa na mwandishi, msisitizo wake katika masimilisho uligubika dhana ya ‘kikaza’ kama alivyodhamiria mtunzi wake.

Mbali na hadithi fupi ya *Kikaza*, kulikuwapo na hadithi fupi nyingine kama vile *Mayai Waziri wa Maradhi* na *Gilasi ya Mwisho Makaburini*. Hadithi fupi hizo zilisawiri matukio mahsusi ambayo hayakuwa rahisi kusimilika ipasavyo. Hadithi fupi hizo zilionekana kuzungumzia matukio hayo kwa mtazamo wa kinjozi ama kidhahania. Katika hadithi fupi ya *Mayai Waziri wa Maradhi*, Mayai anaelezewa kutembelewa na mizuka usiku akiwa amelala. Tukio hilo lilisawiriwa kinjozi namna ambavyo haingewezekana kuliwasilisha kwa usahihi jukwaani. Mfano kama huo ulishuhudiwa katika hadithi fupi ya *Gilasi ya Mwisho Makaburini* ambapo burudani ya Msoi na marafiki zake ilikatizwa na wahusika wanaorejelewa kama vizuu. Tukio hilo linasimuliwa hivi na mwandishi:

... Kule mavani kundi la vizuu limejifufua kwa mtindo wa *Thriller* wa Michael Jackson. Linakuja kule baa kwa kujikongoja na kujitetemesha na kutoa sauti za kiufu. Nyuso nyeupe kama chokaa – mabufuru ya vichwa yanayoning'inia hewani nyuso, kama tungeliweza kuziita nyuso zilikuwa nyeupeeee! Kwa hakika yalikuwa mabango ya nyuso yenye matundu yaliyopoteza macho na pua. Baadhi yamezongwa sanda, vingine mwili mtupu. Harufu kali ya vundo la maiti ilivamia baa na kuzifurusha zile harufu nzuri za maua na manukato na vyakula...

(Diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, uk. 37)

Mifano ya matukio ambayo imetolewa inashadidia ugumu uliokuwapo wa kuyasimilisha matukio yaliyosawiriwa kidhahanifu. Kwa vile masimilisho yalikuwa yakilenga kuigizwa, matukio yaliyotatiza fikira za namna ya kuyaigiza yalidondoshwa. Udondoshaji umekwisha kujadiliwa madhara yake katika usimilisho wa hadithi fupi (Taz. uk. 209).

Matukio mengine ambayo yalitatiza usimilisho ni yale yaliyohusu safari na mengine yaliyosawiriwa katika mandhari ambayo hayawezi kuruhusu uigizaji.

Katika hadithi fupi ya *Ngome ya Nafsi*, mwandishi alijenga taswira za mandhari ambayo hayakuruhusu uigizaji. Msitu alimotembelea mhusika Naseko akikimbilia mafichoni kwa Bi. Tesi haungeonyeshwa jukwaani. Katika msitu huo kulikuwa na nyasi ndefu, miti mikubwa yenye majani yaliyoyumbayumba, na giza totoro. Kwa ajili hiyo wasimilishaji walidondosha sehemu hiyo ya hadithi. Kama ilivyoelezewa mapema katika sehemu hii (Taz. uk. 209), kuwachwa nje kwa matukio ama sehemu za hadithi kuliathiri ukuzaji wa wahusika, uwasilishaji wa maudhui na mtindo wa mwandishi.

Tatizo la ugumu wa matini lilionekana kuwa na chanzo kwa wasimilishaji wa hadithi fupi. Mahojiano yalikuwa yameonyesha kwamba idadi kubwa ya wasimilishaji haina elimu ya viwango vya juu katika somo la fasihi na lugha ya Kiswahili. Wasimilishaji hao walidhihirisha kukosa mikakati bora ya kuzisoma na kuzifasiri kazi za fasihi. Kuna haja ya kuwafundisha wasimilishaji stadi na ujuzi wa kufanya usimilisho iwapo usimilisho wa hadithi fupi utaendelea kutumiwa kwa maandalizi ya mtihani wa KCSE. Mihimili ya kinadharia ambayo imejadiliwa na utafiti huu inaweza kutumika kama vigezo vya kuyakagua masimilisho na maigizo yake, kwa lengo la kuweka viwango na ubora.

6.4 Kiishilio

Sura hii imejadili mbinu mbalimbali za usimilisho wa hadithi fupi. Kama ilivyobainishwa na sura hii, mbinu za usimilisho wa hadithi fupi zinaweza kuwekwa katika aina mbili kuu:

I. Mbinu za usimilisho katika matini

II. Mbinu za usimilisho jukwaani

Sura hii imezjadili aina hizo pamoja na kuzibainisha mbinu zilizopatikana katika kila aina. Imebainika kwamba hadithi fupi husheheni sifa za kitamthilia ambazo huwa msingi wa kusimilishwa kwake. Aidha, riwaya na hadithi fupi husimilishwa kwa mbinu zinazofanana. Hata hivyo, mitindo inayobainisha tanzu hizo huibua tofauti katika matumizi ya mbinu hizo. Mifano na maelezo yaliyotumiwa yalitokana na hadithi fupi kutoka diwani za: *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* na *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*. Mtafiti amezihakiki mbinu hizo kwa misingi ya nadharia ya usimilisho na ya uigizaji.

Aidha, sura hii imeyabainisha matatizo mbalimbali yaliyodhihirishwa na mchakato mzima wa usimilisho wa hadithi fupi. Hata hivyo, matatizo ambayo yamejadiliwa ni yale yaliyodhihirika kwa jinsi tofauti katika usimilisho wa hadithi fupi. Matatizo ya usimilisho wa riwaya na hadithi fupi yamebainika kuwa na vyanzo sawa, ingawa mitindo ya tanzu hizo huyadhihirisha kwa njia tofauti.

Sura inayofuata imehitimisha tasnifu hii kwa kushughulikia muhtasari wa sura za tasnifu, matokeo ya utafiti na mapendekezo.

SURA YA SABA

HITIMISHO

7.0 Utangulizi

Sura iliyotangulia imeshughulikia mbinu na matatizo ya usimilisho wa hadithi fupi. Sura hii imehitimisha tasnifu kwa kutoa muhtasari wa sura zake. Katika sura

hii, matokeo yaliyotokana na uchanganuzi wa data iliyokusanywa yamewasilishwa kwa mujibu wa malengo ya utafiti. Sura hii imeyaeleza kwa kifupi matatizo mbalimbali yaliyomkumba mtafiti katika kuitafitia mada yake. Aidha, mapendekezo ya utafiti wa baadaye katika eneo lililotafitiwa yametolewa.

7.1 Muhtasari

Utafiti huu ilihusu tathmini ya usimilisho wa riwaya na hadithi fupi kwa wanafunzi wa sekondari nchini Kenya. Mada hii imetafitiwa kwa mujibu wa malengo manne ya utafiti. Kwanza, mtafiti alilenga kueleza dhana ya usimilisho, historia ya usimilisho wa fasihi na sababu za kusimilisha. Pili, mtafiti alidhamiria kuainisha na kutathmini mbinu zinazotumika katika usimilisho wa riwaya na hadithi fupi. Tatu, utafiti huu ulidhamiria kuyabainisha matatizo yanayokumba mchakato wa kuzisimilisha riwaya na hadithi fupi. Lengo la nne lilihusu kuonyesha njia bora zinazoweza kuzingatiwa ili kuyatatua matatizo ya usimilisho. Nadharia changamano iliyohulutisha misingi ya nadharia ya uigizaji na ya usimilisho ilitumika katika ubainishaji na uelezaji wa mbinu na matatizo ya usimilisho. Utafiti huu umeyatekeleza malengo yake kupitia sura saba za tasnifu.

Sura ya kwanza imejadili msingi wa utafiti. Vipengele vilivyojadiliwa ni usuli wa utafiti, suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada, na upeo na mipaka ya utafiti. Sura imebainisha kwamba kuna haja ya kuchunguza na kutathmini mbinu za usimilisho wa riwaya na hadithi fupi kwa wanafunzi wa sekondari nchini Kenya. Tathmini hiyo ililenga kubaini ufaafu wa mbinu hizo na matatizo yanayokabili usimilisho wa kazi zinazotahiniwa, pamoja na kupendekeza namna ya kuyatatua.

Sura ya pili ilifafanua misingi ya nadharia na yaliyoandikwa kuhusu mada. Sura imebainisha kwamba utafiti uliongozwa na nadharia changamano iliyoleta pamoja misingi ya nadharia za usimilisho na uigizaji. Aidha, kazi mbalimbali zinazohusiana na utafiti huu zimeelezwa na ulinganifu na tofauti zilizopo zikabainishwa. Sura hiyo imebainisha kwamba suala kuhusu tathmini ya usimilisho wa riwaya na hadithi fupi kwa wanafunzi wa Sekondari nchini Kenya halijatafitiwa.

Sura ya tatu imeshughulikia mbinu za utafiti. Vipengele vilivyofafanuliwa ni mbinu changamano za utafiti, mahali pa utafiti, uteuzi wa sambuli, ukusanyaji, uchanganuzi na uwasilishaji wa data. Sura imeonyesha namna mbinu mbalimbali zilivyotumika kuteua sampuli, kukusanya, kuchanganua, na kuwasilisha data.

Sura ya nne imechunguza na kueleza dhana ya usimilisho, historia ya usimilisho wa fasihi, na sababu za kusimilisha kazi za fasihi. Imebainika kwamba usimilisho ni dhana tata, na mikabala minne inayosaidia fasiri ya dhana hiyo ikaelezewa. Mikabala hiyo ni usimilisho kama tafsiri, mwingiliano matini, mwingiliano wa njia za kimawasiliano, na usimilisho halisi. Utafiti umebaini kwamba zipo sababu nyingi za kusimilisha kazi za fasihi, na usimilisho wa riwaya na hadithi fupi kwa dhamira ya kuinua viwango vya uelewa wa wanafunzi ni mojawapo ya sababu hizo. Katika kuijadili historia ya usimilisho ulimwenguni, sura hiyo imebaini kwamba, usimilisho una historia ndefu na chanzo chake kipo katika fasihi simulizi ya jamii.

Sura ya tano imeziainisha na kuzitathmini mbinu mbalimbali za usimilisho wa riwaya. Utafiti umegundua kwamba riwaya hudhihirisha sifa za kitamthilia ambazo hutoa mazingira mufti ya usimilisho. Sura hiyo imeyabainisha matatizo

ya usimilisho wa riwaya. Matatizo ya usimilisho yamebainika kuwa na vyanzo viwili: udhaifu wa mbinu za usimilisho na udhaifu wa msimilishaji.

Sura ya sita imeendeleza sura ya tano kwa kuchunguza baadhi ya mbinu za usimilisho na matatizo ya kusimilisha, ambayo yalijibainisha kwa namna tofauti katika hadithi fupi. Utafiti umebaini kwamba mbinu za kusimilisha riwaya na hadithi fupi zinafanana. Aidha, matatizo ya usimilisho yamebainika kuwa na vyanzo sawa katika usimilisho wa riwaya na hadithi fupi.

Utafiti huu umehitimishwa katika sura ya saba. Sura hii imetoa muhtasari wa kila sura ya tasnifu. Matokeo na mchango wa utafiti huu yametolewa. Aidha, mtafiti ameitumia sura hii kueleza matatizo yaliyomkabili nyanjani na mapendekezo kwa utafiti wa baadaye katika eneo lililoshughulikiwa.

7.2 Matokeo na Mchango wa Utafiti

Utafiti huu ulidhamiria kutathmini usimilisho wa riwaya na hadithi fupi kwa wanafunzi wa sekondari nchini Kenya. Usimilisho wa riwaya ulihusu riwaya ya *Utengano* na *Siku Njema*. Hadithi fupi zilizohakikiwa usimilisho wake ni diwani ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* na *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*. Uchunguzi huu umeziainisha na kuzitathmini mbinu za usimilisho wa riwaya na hadithi fupi. Utafiti umepiga hatua mbele na kuyachunguza na kuyabainisha matatizo ya usimilisho huo. Uchunguzi huu umeongozwa na nadharia changamano iliyoshirikisha misingi ya nadharia ya uigizaji na ya usimilisho.

Tasnifu imebaini kwamba, fani ya usimilisho ni mwendelezo wa mwingiliano matini na tanzu. Mwingiliano matini ni hali ya matini kudhihirisha urejeleaji na ugeuzaji wa matini nyingine. Matini inapovuka mipaka ya tanzu na kudhihirisha

sifa za utanzu mwingine, hali hiyo inaweza kurejelewa kama mwingiliano wa tanzu. Uchunguzi umegundua kwamba mbinu za usimilisho ni za kimwingiliano matini. Tanzu za riwaya na hadithi fupi zilizochunguzwa zilibainisha sifa za kitamthilia. Sifa za kitamthilia zilizobainishwa katika matini hizo ni kama vile: muundo wa kimazungumzo, utendaji, uzungumzi nafsi, na miktadha ya usemajji kando. Aidha, ilibainika kuwa, kuna sifa za kimfanano katika tanzu za kinathari na tamthilia. Hizi ni kama vile: usimulizi, muundo wa sehemu, mbinu za kimtindo, usawiri wa wahusika, na maelezo ya mandhari. Hali ya kuwepo na sifa za kitamthilia na kimfanano katika tanzu za riwaya na hadithi fupi, ilikuza mazingira mufti yaliyotumiwa na wasimilishaji kubuni mbinu za kuzisimilisha tanzu hizo.

Uchunguzi unahitimisha kuwa, mwingiliano wa matini na tanzu ndicho kiini cha usimilisho wa tanzu za riwaya na hadithi fupi. Kinyume na inavyodaiwa na baadhi ya wahakiki wa mwingiliano matini, matini zinaweza kuingiliana na zikadumisha uaminifu wa matini chasili. Tasnifu imebaini kwamba uaminifu wa masimilisho kwa matini chasili ulitegemea ustadi wa msimilishaji katika kuzitumia mbinu za mwingiliano matini. Wasimilishaji waliokuwa na ustadi mwingi wa kuzitumia mbinu hizo walibuni masimilisho yaliyokuwa na uaminifu mwingi, huku waliokosa ustadi mwingi wakibuni masimilisho yaliyokengeuka sana. Usimilisho unaodhamiriwa kuibua sifa ya uaminifu kwa matini chasili, unapaswa kulenga uhamishaji wa sifa za kitamthilia na kimfanano kwa usahihi wake. Huenda pawepo na sifa za ki-riwaya ama ki-hadithi fupi ambazo hazitaweza kuhamishwa kupitia sifa hizo, na katika hali hiyo, msimilishaji anapaswa kutumia ubunifu wake lakini adumishe usahihi wa vipengele hivyo.

Tasnifu imegundua kwamba mchakato wa kusimilisha hukumbwa na matatizo mbalimbali. Matatizo hayo yamebainika kutokana na matini zinazosimilishwa, mbinu za usimilisho, na wasimilishaji wenyewe. Ugunduzi uliofanywa na utafiti huu ni kuwa, isipokuwa tatizo la kifedha, matatizo hayo mengine yalisababishwa na viwango vya chini vya ujuzi wa fasihi na lugha ya Kiswahili miongoni mwa wasimilishaji. Ingawa wasimilishaji wengi walidhihirisha tajriba pana katika uigizaji, viwango vyao katika somo la fasihi na lugha ya Kiswahili vilikuwa sawa na vile vya wanafunzi waliolengwa. Kama ilivyobainika kupitia mahojiano, kiwango cha juu kimasomo walichohitimu wasimilishaji wengi kilikuwa ni kidato cha nne. Uchunguzi huu umebaini kwamba, fani ya usimilisho inahitaji masomo ya fasihi na lugha, juu ya kidato cha nne, na mbali na tajriba ya uigizaji. Kuna haja ya kuasisiwa kwa fani hiyo katika taaluma ya fasihi vyuoni ili kuwanufaisha wasimilishaji wanaoiendeleza. Uchunguzi ulibaini kutokuwepo kwa chuo chochote nchini Kenya kinachotoa mafunzo katika fani ya kusimilisha tungo za fasihi.

Ingawa sifa za kitamthilia na kimfanano hubainika katika riwaya na hadithi fupi, utafiti huu umebaini kwamba, mwingiliano huo hutegemea mtindo wa mwandishi na sifa za utanzu. Baadhi ya riwaya na hadithi fupi husheheni sifa nyingi za kimwingiliano kuliko nyingine. Aidha, uchunguzi umegundua kuwa, riwaya hudhihirisha sifa nyingi za kimwingiliano na tamthilia kuliko utanzu wa hadithi fupi. Ubanifu wa hadithi fupi humfunga mwandishi katika mipaka fulani ya mitindo ya kuisanifu. Tasnifu imebaini kwamba mbinu za usimilisho wa riwaya na hadithi fupi zinafanana, na tofauti ndani yake hutokana na sifa za kiutanzu.

Mbali na kubainisha kuwepo na sifa za kitamthilia na kimfanano katika tanzu za kinathari, utafiti umetoa mchango katika eneo hili la kinadharia kwa kuonyesha

dhima ya mwingiliano matini katika uelewaji na ufundishaji wa tanzu za fasihi. Hamna utafiti ambao umeonyesha jinsi sifa ya mwingiliano wa matini na tanzu inavyoweza kutumika kuinua viwango vya uelewa na kuufundisha utanzu fulani. Utafiti umegundua kuwa, usimilisho unaweka dhahiri sifa za kimwingiliano katika tanzu, na kudhihirisha sifa za kiutanzu zisizoonyesha mwingiliano wowote. Aidha, uchunguzi umebaini kwamba, tanzu pendwa na zenye njia mbalimbali za mawasiliano zinaweza kutumika ili kufundishia tanzu zinazotegemea njia moja ya mawasiliano. Drama imebainika kutumia njia mbalimbali za mawasiliano, hali iliyoifanya kupendelewa ili itumike kufundishia riwaya na hadithi fupi. Ufundishaji wa tanzu za fasihi haupaswi kusisitiza ubainifu wa sifa za utanzu, bali kusisitiza namna sifa za utanzu mmoja zinavyoweza kudhihirika katika utanzu mwingine. Msisitizo wa awali umeonekana kuwabana wasomi katika mipaka ya tanzu za fasihi ambayo kihalisi haipo.

Usimilisho wa riwaya na hadithi fupi kwa wanafunzi wa sekondari ulibainika kuwa na umuhimu mkubwa katika maandalizi ya mtihani wa KCSE. Licha ya kuwa usimilisho huo ulidhihirisha matatizo mbalimbali, walimu waliohojiwa walibainisha umuhimu wake. Usimilisho huo ulidhamiriwa kuinua viwango vya uelewa kwa wanafunzi waliokuwa wakitahiniwa katika mtihani huo. Mbali na dhamira hiyo, usimilisho ulibainika kujumuisha dhamira nyingine ambazo hazikwenda sambamba na dhamira hiyo kuu. Usimilisho ulifanywa kama nyenzo ya kuchumia riziki, na ili kuwavuta wanafunzi kuyapenda maigizo ya kikundi fulani, dhamira ya burudani ilijumuishwa. Dhamira mbadala zilifanywa kwa kupotosha na kutia chuku katika vipengele vya matini chasili ili kuwafanya

wanafunzi wacheke. Usimilisho wenye dhamira potovu haupaswi kuhalalishwa kufanyiwa wanafunzi wanaojiandaa kwa mitihani yao.

Utafiti umebaini kwamba hamna vigezo vilivyoratibiwa kufuatwa na kuutathmini usimilisho wa riwaya na hadithi fupi zinazotahiniwa shuleni. Usimilisho huo umebainika kukumbwa na matatizo mbalimbali yaliyojadiliwa katika tasnifu. Kuna haja ya kuwepo na vigezo vinavyotumiwa kuvisajili vikundi hivyo, pamoja na vigezo vya kuyaidhinisha maigizo yake. Ni muhimu vikundi vinavyoigiza vitabu vinavyotahiniwa visajiliwe na wizara ya elimu, kinyume na hali ilivyo sasa, ambapo vinasajiliwa na wizara ya michezo, utamaduni na sanaa. Hali hii itawezesha wizara ya elimu kuvisajili vikundi hivyo baada ya kuthibitisha kwamba vina mtaalamu wa masuala ya fasihi atakayeelekeza usimilisho na uigizaji. Utafiti huu umetoa mwelekeo unaoshirikisha vigezo vinavyoweza kutumika kuyatathmini masimilisho kabla yaigiziwe wanafunzi.

7.3 Matatizo ya Utafiti

Utafiti kuhusu usimilisho wa riwaya na hadithi fupi kwa wanafunzi wanaotahiniwa haukufanywa pasipo kubainika matatizo ya utafiti. Kama ilivyotajwa katika sura ya kwanza, usimilisho wa matini kwa matini katika taaluma ya fasihi una tafiti chache zilizofanywa. Utafiti mwingi ambao umefanywa unahusu ugeuzaji wa matini za fasihi kuwa filamu. Aidha, usimilisho katika fasihi ya Kiswahili ni eneo changa ambalo halina kazi nyingi za kurejelewa. Ukosefu wa vyanzo muhimu vya kurejelewa uliathiri ugunduzi wa masuala muhimu katika fani ya usimilisho.

Tatizo la haki miliki na wizi wa kisanaa liliathiri ukusanyaji wa data nyanjani. Juhudi za mtafiti kutaka kuwahi masimilisho ya riwaya na hadithi fupi kabla ya

maigizo yake hazikufaulu kwa vikundi vyote. Baadhi ya wasimilishaji walidinda kuyatoa masimilisho hayo kabla ya uigizaji wake wakihofia kwamba yangetumika kuutathmini uigizaji wao. Kwa sababu hiyo, haikuwezekana kukadiria kikamilifu namna uigizaji ulivyozingatia masimilisho yaliyokuwa yameandaliwa. Tatizo hilo lilipunguzwa kwa kuzitumia video zilizorekodiwa na kuzilinganisha na masimilisho hayo baadaye ili kubaini matatizo katika uigizaji.

Aidha, wasimilishaji waliidhinisha kurekodiwa kwa visehemu muhimu tu vya maigizo kwa hofu ya wizi wa kisanaa. Kwa sababu hiyo, ilimlazimu mtafiti kutumia mbinu ya kuandika mambo muhimu ambayo hayakurekodiwa. Mbinu ya kuandika haikuweza kuwasilisha mambo fulani muhimu katika uigizaji. Hali hiyo iliufanya utafiti ukose kubaini matatizo madogo madogo yaliyotokana na uigizaji wa masimilisho. Hata hivyo, utafiti umefanikiwa kuyawasilisha matatizo yaliyojitokeza sana na kubainika kuathiri usimilisho kwa kiwango kikubwa.

7.4 Mapendekezo

Utafiti huu ulilenga kutathmini usimilisho wa riwaya na hadithi fupi kwa wanafunzi wa sekondari nchini Kenya. Hii ni mada moja katika eneo pana la usimilisho. Kuna mambo mbalimbali kuhusiana na mada hii ambayo utafiti haukuweza kuyatafitia. Mtafiti mwingine anaweza kutafiti kuhusu upokezi wa usimilisho wa riwaya na hadithi fupi kwa wanafunzi wa sekondari nchini Kenya. Ni muhimu kuchunguza namna masimilisho hupokelewa yakilinganishwa na matini chasili. Utafiti wa aina hiyo unaweza kuarifu masuala mengi katika usomi wa usimilisho, na fasihi kwa kijumla.

Usimilisho uliochunguzwa katika tasnifu hii ulihusu fasihi andishi ya Kiswahili. Tasnifu imebaini kuwa, chanzo cha usimilisho kipo katika fasihi simulizi ya

jamii. Mtafiti mwingine anaweza kuchunguza usimilisho katika fasihi simulizi ya Kiswahili, na nafasi yake katika uvyazaji wa tungo mpya za fasihi hiyo. Mbali na kuwa na dhima katika ufundishaji, usimilisho una dhima ya kisanaa ambayo inaweza kutafitiwa. Namna utanzu mmoja unavyovyaza utanzu mwingine ni mada ambayo haijashughulikiwa katika fasihi ya Kiswahili. Kuna uwezekano ikawa tanzu fulani katika fasihi andishi na simulizi ni matokeo ya usimilisho.

MAREJELEO

Adair-Lynch, T. (2006). *The Basic Elements of Theatre*. homepage.smc.

edu/adair.../elements.html

Andrew, D. (1984). *Concepts in Film Theory*. New York: Oxford University

Press.

Aragay, M. (Mhr.) (2005) *Books in Motion: Adaptation, Intertextuality,*

Authorship. New York: Editions Rodopi B.V.

Baldick, C. (2004). *The Concise Oxford Dictionary of Literary Terms.* U.K:

Oxford University Press.

Bakari, M. (2008). “Usemezano kama Mkakati wa Kufahamu Riwaya za

Babu Alipofufuka (2001), Bina - Adamu (2002) na

mkusanyiko wa hadithi fupi wa *Sadiki Ukipenda (2002).*”

Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta

(Haijachapishwa).

Beja, M. (1979). *Film and Literature.* New York: Routledge.

Booth, A. et al. (2006). *The Norton Introduction to Literature.* New York:

W.W. Norton and Company, Inc.

Cahir, L. C. (2006). *Literature into Film: Theory and Practical Approaches.*

www.books.google.co.ke/books?isbn=0786425970.

Cartmell, D. & Whelehan, L. (Whr.) (2007). *The Cambridge Companion to*

Literature on Screen. Cambridge: Cambridge University

Press.

Cattrysse, P. (1992b). “Film (Adaptation) as Translation: Some Methodological

Proposal”, Katika *Target: International Journal of*

Translation Studies 4 (1), 53-70.

- Carroll, R. (Mhr.) (2009). *Adaptation in Contemporary Culture: Textual Infidelities*. London: Continuum International Publishing Group.
- D'Angelo, F. (2010). "The Rhetoric of Intertextuality", In *Rhetoric Review*. Vol. 29, No. 1, 31-47. London: Taylor & Francis Group.
- Dean, J. (2009). "Adapting History and Literature into Movies", In *American Studies Journal*.
- Diyanni, R. (2004). *Literature: Approaches to Fiction, Poetry, and Drama*. New York: McGraw- Hill.
- Dorsch, S. T. (1965) (Mhr). *Aristotle/ Horace/ Longinus: Classical Literary Criticism*. Harmondsworth: Penguin.
- Edmunds, L. (2006). *Oedipus*. New York: Routledge.
- Elliot, K. (2003) *Rethinking the Novel/Film Debate*. New York: Cambridge University Press.
- Engelstad, Arne (2012). "Literary Film Adaptations as Educational Text"
[www. Fillingstation.can/in...cinematic- exercises- film- inspired- writers.](http://www.Fillingstation.can/in...cinematic-exercises-film-inspired-writers)
- Finnegan R. (1987). "The Perception of African Oral Literature" In *Oral Literature in Africa*. Nairobi: O.U.P.

Frye, N. (1957). *Anatomy of Criticism*. New Jersey: Princeton University Press.

Gituku, A. N. (1990). “Maigizo ya Kienyeji ya Watoto Nchini Kenya: Nafasi ya

Kuyatumia katika Ufundishaji.” Tasnifu ya Uzamili,

Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Goodman, N. (1976). *Languages of Art*. Indianapolis: Hackett.

Holquist, M. (Mhr.) (1981) *The Dialogic Imagination*. Texas: University of Texas

Press.

Hussein, E. (1983). “Hatua Mbalimbali za Kubuni na Kutunga Tamthiliya

Kufuatana na Misingi ya Ki-Aristotle”. Katika *TUKI*.

Dar es salam: TUKI.

Hutcheon, L. (2013). *A Theory of Adaptation*. New York: Routledge.

Kairu, W.M. (2005). “Uhalisi na Mtindo wa Ken Walibora katika Fasihi ya

Watoto.”Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta

(Haijachapishwa).

Kandoro, S.A (2003). “Hatua mbalimbali za Kubuni na Kutunga Shairi la

Kiswahili.” Katika *Fasihi: Makala za Semina ya Kimataifa*

ya Waandishi wa Kiswahili III. Dar es Salaam: TUKI.

Kamau, M. (1992). “Ufundi katika Riwaya za Mohammed Said Abdulla.”

Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta

(Haijachapishwa).

Kavuria, P. (2008). "Dhuluma Dhidi ya Watoto katika Riwaya ya Kiswahili."

Tasnifu ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Kenyatta

(Haijachapishwa).

Kerr (1995). *African Popular Theatre*. London: Villiers publications Ltd.

Kezilahabi, E. (2003). "Utunzi wa Riwaya na Hadithi Fupi." Katika *Fasihi:*

Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili

III. Dar es Salaam: TUKI.

Khamis, S.A.M. (2008). "Nadharia, Ubunifu, Uchambuzi na Taaluma ya

Kiswahili." Katika Ogechi N., Shitemi N., na Simala

K. *Nadharia katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za*

Kiafrika. M.U.P., Eldoret.

Kiai, A.W. (1996). A Discourse Analysis of Educational Radio Programmes to

Farmers: Adaptation in Register. University of Nairobi,

M.A Thesis. (Haijachapishwa).

Kimani, C. W. (2003). "Swala la Dhuluma Dhidi ya Wanawake katika Fasihi ya

Kiswahili." Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta

(Haijachapishwa).

Kinge'i, K. na C. N. Kisovi (2005). *Msingi wa Fasihi Simulizi*. Nairobi: Kenya

Literature Bureau.

Klein, M. na G. Parker (Whr) (1981). *The English Novel and the Movie*.

New York: Frederick Ungar Publishing.

Leitch, V. (Mhr.) (2001). *The Norton Anthology of Theory and Criticism*.

New York: W.W. Norton and Company.

Lhermitte, C. (2005). "A Jakobsonian Approach to Film Adaptations of Hugos

Les Miserables" In *NEBULA: A Journal of Multidisciplinary*

Scholarship pp. 97-107.

<http://www.nobleworld.biz/nebulaarchive/nebula21.html>

Magaju, J. (2004). "Uhalisiajabu katika Riwaya za *Babu Alipofufuka (2001)* ya

Said A. Mohamed *Binadamu (2002)* ya K.W. Wamitila."

Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Massamba D.P.M (2003). "Utunzi wa Ushairi wa Kiswahili" Katika Fasihi:

Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili

III. Dar es Salaam: TUKI.

Mayaka, G. (1991). "Ukengeushi wa Wahusika Wasomi katika Riwaya Nne `za

Euphrase Kezilahabi: *Rosa Mistika, Kichwamaji, Dunia*

Uwanja wa Fujo, na Gamba la Nyoka." Tasnifu ya Uzamili,

Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Mavisi, R. (2007). "Usawiri wa Wahusika wa Kike katika Kazi za Zainabu

Burhani." Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta

(Haijachapishwa).

Mbaabu, I. (1991). *Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili*. Nairobi: Longman.

Mbatiah, A. M. (1999). "The Origin and Development of the Swahili Thesis Novel in Tanzania." *Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa)*.

_____ (Mhr) (2000). *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Mbuthia, E. M. (2005). "A Stylistic and Thematic analysis of Kiswahili Short Stories." *Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa)*.

McFarlane, B. (1996). *Novel to Film: An Introduction to the Theory of Adaptation*. Oxford: Clarendon Press.

Michael, P. (1997) (Mhr). *Dictionary of Cultural Theory and Critical Theory*.
<http://www.blackwellreference.com>

Mohochi, S. E. (1995). "Fani katika Hadithi Fupi za Kiswahili." *Tasnifu za Uzamili, Chuo Kikuu cha Egerton (Haijachapishwa)*.

Mohamed, S. A. (1980). *Utengano*. Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.

_____ (1983) "Hatua Mbalimbali za Kubuni na Kutunga Riwaya."
Katika Fasihi: Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III. Dar es Salaam: TUKI.

_____ (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mpesha, N. (1995). "Children's Literature in Tanzania: A Literature Appreciation of Its Growth and Development." Ph.d Thesis, Kenyatta University.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uihakiki wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mugenda, A. (2008). *Social Science Research: Theory and Principles*. Nairobi: Applied Research and Training Services Press.

Muindi, A. (1990). "Usawiri wa Wahusika Makahaba katika Vitabu vya S. A. Mohamed." Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Mulewa, A. (2008). "Wahusika katika Hadithi Fupi za Kiswahili." Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Musee, A. M. (2007). "Matumizi ya Majazi kama Mkakati wa Kuepuka Upigaji Marufuku katika Riwaya za *Mafuta (1984)* na *Walenisi (1995)*." Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Musembi, N. (2008). "Matumizi ya Taswira na Ukinzani kama Kichocheo cha

Zinduko katika Riwaya za *Mafuta (1984)* na *Walenisi* (1985).” Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Mutegi, L. (2010). “Maigizo katika Fasihi Simulizi: Mfano wa Kirarire katika Nyimbo za Tohara za Wameru.” Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Muthubi, F. (2005). “Usimilishaji katika Fasihi ya Watoto.” Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Ndung’u, N. (1996). “Uhakiki wa Fani katika Riwaya za Katama Mkangi.” Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Njogu, K. na R. Chimerah (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Njogu, K. (1997). *Uhakiki wa Riwaya za Visiwani Zanzibar*. Nairobi: Nairobi University Press.

Nkichabe G.S. na Mwamzandi I.Y. (2008). “Udenguzi wa Maana katika Diskosi ya Kisiasa Nchini Kenya: Mifano ya Nyimbo Pendwa.” Katika Ogechi, O. na wengine (Whr.), *Nadharia katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika*. Eldoret: Moi University Press.

Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Augustana College, Rock Island.

Lang, C. (2012). "A Brief History of Literary Theory." Xenos Christian Fellowship. <http://www.xenos.org/essays/litthry4.htm>

Ley, G. (2006). *A Short Introduction to Ancient Greek Theater*. Chicago: The University of Chicago.

Ochenja, R. (2008). "Maigizo kama Mbinu ya Maudhui katika Riwaya na Mbili za Ken Walibora." Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Odeo, I. na Maina, G. (2008). *Isimujamii*. Nairobi: Oxford University Press.

Osore, M. K. (1994). "Uhakiki wa Kiisimu wa Riwaya za Suleiman Mohamed." Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

_____ (2008). "Defamiliarization in the Novels of Euphrase Kezilahabi and Said Ahmed Mohamed." Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Oloruntoba-Oju (2009). "Translation, Adaptation, Intertextuality in African Drama: Wole Soyinka, Zulu Sofola, Ola Rotima" In Petra R. na Konrad G. (Whr.), *Translation of Cultures: An*

Introduction. New York: Editions Rodopi B.V.

Packard, W. (1997). *The Art of the Playwright: Creating the Magic of Theatre*.

New York: Thunder's Mouth Press.

Pfister, M. (1991). *The Theory and Analysis of Drama*. New York: Cambridge

University Press.

Punzi, M.P. (Mhr.) (2007). *Literature Intermediality: The Transit of Literature*

through the Media Circuit. Germany: International

Academic Publishers.

Ruo, K.R. (2003). "Suala la Ushairi wa Kiswahili" *Fasihi: Makala za Semina ya*

Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III. Dar es Salaam:

TUKI.

Schechner, R. (2003). *Performance Theory*. New York: Routledge Classics.

Selden, R. (1989). *Practicing Theory and Reading Literature: An Introduction*.

Lexington: The University Press of Kentucky.

Shepherd, B.J. (2009) "Adaptation from Novels into Films: A Study of Six

Examples, with Accompanying Screenplay and Self-

Analysis." M.A. Thesis, University of Waikato.

Sianghio, C. S. L. (Hakuna tarehe). *Elements of Drama*. [http:// literal no4. tripod](http://literal.no4.tripod.com/elements.html)

[.com/ elements. html](http://literal.no4.tripod.com/elements.html).

Stam, R. (2000) "Beyond Fidelity: The Dialogics of Adaptation", In Naremore

(Mhr.) *Film Adaptation*. London: Athlone, 54 – 76.

Starrs, D. B. (2006). “A Queer New World: Adaptation Theory and the Zeugma of Fidelity in Derek Jarman’s *The Tempest*.” The University of Melbourne, Vol. Iv. Issue 1. <http://docs.google.com>

Syambo, B. na A. Mazrui (1992). *Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Tompkins, J. (1980) (Mhr). *Reader Response Criticism: From Formalism to Post-Structuralism*. Baltimore & London: John Hopkins.

Trypanis C.A. (1981). *Greek Poetry from Homer to Seferis*. Chicago: University of Chicago Press.

Vaughan, A. T. na V. M. Vaughan (1991). *Shakespeare’s Calibean: A Cultural History*. Cambridge: Cambridge University Press.

Vonyoli, A. J. (2004). “Hadithi kama Chombo cha Maudhui katika Fasihi: Uchanganuzi wa Riwaya za Mkangi G. K. *Mafuta (1984)* na *Walenisi (1995)*.” Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Wafula, R.M. (1992). “Nadharia kama Mwongozo wa Utunzi na Uhakiki katika Fasihi”, Makala ya Semina. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijchapishwa).

Wafula, R.M. na K. Njogu (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: The

Jomo Kenyatta Foundation.

Wagner, G. (1975). *The Novel and the Cinema*. New Jersey: Associated

University Presses Inc.

Walibora, K. (1996). *Siku Njema*. Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.

Walibora, K. na S. A. Mohamed (2007) (Wahr). *Damu Nyeusi na Hadithi*

Nyingine. Nairobi: Moran Publishers Ltd.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Phoenix Publishers.

_____ (2003). *Kichocheo cha Fasihi*. Nairobi: Focus Publications Ltd.

_____ (Mhr.) (2004). *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine*. Nairobi:

Focus Publishers Ltd.

_____ (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus

Publications Ltd.

_____ (2008). *Kanzi ya Fasihi I: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*.

Nairobi: Vide-Muwa.

Wiley, J. (2002). *A Short History of Adaptations*.

media.johnwiley.com.au/product_data/excerpt/52/...

/0471225452.pdf

Wilson, E. na A. Goldfarb (1991). *Theater: The Lively Art*. New York:

McGraw-Hill, Inc.

Wolf, W. (1999). *The Musicalization of Fiction: A Study in the Theory and*

History of Intermediality. Atlanta: Editions Rodopi B.V.

SCAFM (2008). "High Fidelity: Issues of Authenticity in Contemporary

Adaptations of Jane Austen.

Bi. Kagani (6/3/2012). "Mahojiano Kuhusu Usimilisho wa Riwaya na Hadithi

Fupi." Kenya Institute of Curriculum Development.

VIAMBATISHO

KIAMBATISHO 1

HOJAJI KWA WALIMU KUHUSU RIWAYA

JIBU MASWALI YAFUATAYO KWA USAHIHI KADRI UWEZAVYO

1) Je, umeisoma riwaya iliyoigizwa? (pigia mkwaju jibu lako)

NDIO	LA
------	----

2) Kadiria usahihi wa uwasilishaji wa riwaya katika uigizaji. (pigia mkwaju jibu lako)

VIZURI SANA	VIZURI	WASTANI	VIBAYA	VIBAYA SANA
-------------	--------	---------	--------	-------------

3) Ni matatizo yapi uliyobaini katika uigizaji huo?

4. Tathmini umuhimu wa maigizo haya kwa maandalizi ya mtihani wa KCSE.

(Pigia mkwaju jibu lako).

MUHIMU SANA	MUHIMU	SI YA LAZIMA	HAYANA UMUHIMU	POTOVU
-------------	--------	--------------	----------------	--------

5. Pendeza jinsi ya kuyaboresha maigizo haya ili yawafaidi wanafunzi wanaotahiniwa.

KIAMBATISHO 2

HOJAJI KWA WALIMU KUHUSU HADITHI FUPI

JIBU MASWALI YAFUATAYO KWA USAHIHI KADRI UWEZAVYO

1) Je, umeisoma hadithi fupi iliyoigizwa? (pigia mkwaju jibu lako)

NDIO	LA
------	----

2) Kadiria usahihi wa uwasilishaji wa hadithi fupi katika uigizaji. (pigia mkwaju jibu lako)

VIZURI SANA	VIZURI	WASTANI	VIBAYA	VIBAYA SANA
-------------	--------	---------	--------	-------------

3) Ni matatizo yapi uliyobaini katika uigizaji huo?

4. Tathmini umuhimu wa maigizo haya kwa maandalizi ya mtihani wa KCSE.

(Pigia mkwaju jibu lako).

MUHIMU SANA	MUHIMU	SI YA LAZIMA	HAYANA UMUHIMU	POTOVU
-------------	--------	--------------	----------------	--------

5. Pendeza jinsi ya kuyaboresha maigizo haya ili yawafaidi wanafunzi wanaotahiniwa.

KIAMBATISHO 3

HOJAJI KWA WASIMILISHAJI

JIBU MASWALI YAFUATAYO KWA USAHIHI KADRI IWEZEKANAVYO

1. Je, ulianza kusimilisha tungo za riwaya na hadithi fupi mwaka upi? _____

2. Taja kiwango cha juu ulichoafikia katika somo la fasihi _____

3. Uliupata vipi ujuzi wa kusimilisha na kuigiza tungo za riwaya na hadithi?

A	<i>Kusoma chuoni</i>	
B	<i>Kuwa kwenye kikundi cha uigizaji</i>	
C	<i>Kutazama yakifanywa na wengine</i>	
D	<i>Maarifa na ubunifu wako</i>	

4. Huenda ikawa umeyapokea malalamishi yoyote kutoka kwa watazamaji kuhusu maigizo ya kikundi chako?

NDIO	LA
------	----

5. Taja aina ya malalamishi haya:

6. Je, kuna matatizo yoyote unayopitia katika:

<i>Kugeuza riwaya kuwa matini ya drama</i>	NDIO	LA
<i>Kugeuza hadithi fupi kuwa matini ya drama</i>	NDIO	LA
<i>Kuigiza matini ya drama ya riwaya</i>	NDIO	LA
<i>Kuigiza matini ya drama ya hadithi fupi</i>	NDIO	LA

7. Taja matatizo hayo kama yapo:

a) Yanayotokana na kuigeuza riwaya kuwa matini ya drama.

b) Yanayotokana na kuigeuza hadithi fupi kuwa matini ya drama.

c) Yale yanayohusu uigizaji wa matini ya riwaya:

d) Yale yanayohusu uigizaji wa matini ya hadithi fupi:

8. Je, umeyatatua vipi baadhi ya matatizo haya?

a) Yanayotokana na kuigeuza riwaya kuwa matini ya drama:

b) Yanayotokana na kuigeuza hadithi fupi kuwa matini ya drama:

c) Yale yanayohusu uigizaji wa matini ya hadithi fupi:

d) Yale yanayohusu uigizaji wa matini ya riwaya:

9. Pendekeza mambo muhimu yanayoweza kuyaboresha maigizo haya ya riwaya na

hadithi fupi.

KIAMBATISHO 4

MWONGOZO WA MAHOJIANO NA WASIMILISHAJI

1. Je, ulianza kusimilisha tungo za riwaya na hadithi fupi mwaka upi?
2. Je, maigizo ya riwaya yalianza mwaka upi?

3. Ni riwaya ipi ilikuwa ya kwanza kusimilishwa?
4. Je, unaweza ukavitaja baadhi ya vikundi vilivyoisimilisha riwaya hiyo?
6. Ni riwaya zipi za Kiswahili ambazo umezisimilisha kufikia sasa?
7. a) Je, umewahi kushirikisha ama kutafuta ushauri kutoka kwa mtu yoyote kuhusu usimilisho wa riwaya na hadithi fupi?
 - b) Nani? Kazi yake?
 - c) Kwa nini ulimshirikisha?
8. a) Je, uliisimilisha diwani ya hadithi fupi ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* mwaka upi?
 - b) Taja changamoto ulizokumbana nazo ukiisimilisha.
9. Usimilisho wa hadithi fupi na riwaya una changamoto zipi?
10. a) Je, kikundi chako kimesajiliwa?
 - b) Nani anavisajili vikundi vya uigizaji?
 - c) Je, kikundi chako kimeidhinishwa kuigiza tungo zinazotahiniwa na Wizara ya Elimu?
 - d) Ni mambo yapi unayohitajika kutimiza ili kikundi kisajiliwe na kiidhinishwe kuigiza?

KIAMBATISHO 5

PICHA KUONYESHA UTENDAJI, USAWIRI WA WAHUSIKA, NA WAHUSIKA (SIKU NJEMA)



Picha 1 na 2



Picha 3



Picha 4

Picha kuonyesha utendaji, usawiri wa mandhari, na wahusika. Picha ya kwanza kutoka juu na ya mwisho zinaonyesha uteuzi wa waigizaji wazee na vijana. Baadhi ya wazee walitiwa uzee bandia ili kuigiza nafasi hizo. Picha ya pili inaonyesha namna mwigizaji Amon mwenye asili ya Kimaasai alivyovikwa maleba yanayoashiria utamaduni wa jamii yake. Picha ya tatu inaonyesha mavazi ya kitamaduni ya wanawake Waswahili katika pwani ya Kenya. Hawa hupendelea kujifunga kanga, lesa, mtandio, na kuvaa buibui.


**KIAMBATISHO 6: USAWIRI WA MANDHARI NA WAHUSIKA
(RIWAYA YA *SIKU NJEMA*)**



Kutoka kushoto: Kongowea na mjombake Kitwana. Mandhari katika picha hii yanaonyesha umaskini wa Kitwana. Mwigizaji mzee ameteuliwa kuigiza nafasi ya mzee, huku kijana akimwigiza mhusika kijana Kongowea. Mwigizaji mjomba Kitwana alisawiriwa kama Muislamu kutokana na maleba aliyovalia katika maigizo hayo. (Kutoka filamu ya K.I.C.D. ya *Siku Njema*)

**KIAMBATISHO 7: USAWIRI WA MANDHARI, WAHUSIKA, NA
UTENDAJI (RIWAYA YA *UTENGANO*)**

Picha 1: Kuonyesha uangazaji jukwaani katika chumba kilichojaa giza totoro.



Picha 2: Kuonyesha jinsi maleba ya waigizaji wa kike yalivyoteuliwa kuashiria utamaduni wa Waswahili.



**KIAMBATISHO 8: USAWIRI WA WAHUSIKA, MANDHARI, NA
UTENDAJI (RIWAYA YA *UTENGANO*)**


Picha 3: Kuonyesha waigizaji katika utendaji jukwaani na maandalizi ya mandhari.



KIAMBATISHO 9: KIBALI CHA KUFANYA UTAFITI

CONDITIONS

- 1. You must report to the County Commissioner and the County Education Officer of the area before embarking on your research. Failure to do that may lead to the cancellation of your permit without prior appointment.**
- 2. Government Officers will not be interviewed**
- 3. No questionnaire will be used unless it has been approved.**
- 4. Excavation, filming and collection of biological specimens are subject to further permission from the relevant Government Ministries.**
- 5. You are required to submit at least two(2) hard copies and one(1) soft copy of your final report.**
- 6. The Government of Kenya reserves the right to modify the conditions of this permit including its cancellation without notice.**

REPUBLIC OF KENYA

NACOSTI
 National Commission for Science, Technology and Innovation

RESEARCH CLEARANCE PERMIT
Serial No. A 3125
CONDITIONS: see back page

THIS IS TO CERTIFY THAT:
MR. TITUS MUSYOKA KAUI
of KENYATTA UNIVERSITY, 0-90200
Kitui, has been permitted to conduct research in Kitui , Nairobi Counties
on the topic: USIMILISHO WA RIWAYA NA HADITHI FUPI KWA WANAFUNZI WA SEKONDARI NCHINI KENYA.
for the period ending:
31st December, 2014

Permit No : NACOSTI/P/14/1357/3138
Date Of Issue : 8th September, 2014
Fee Recieved :Ksh 2,000


Applicant's Signature


Secretary
National Commission for Science, Technology & Innovation

